

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 17 Mei, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Ishirini na Moja, kama Spika kwanza niwapongeze kwa kazi nzuri ya jana maana jana ukumbi huu uligeuka kuwa Guantanamo. Kuna Kamati yangu moja inajiita Guantanamo, lakini ndilo Bunge au sivyo jamani? Ahsante sana.(Kicheko)

Naomba tuendeleee, Katibu.

NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha mezani.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

MHE. MOSHI S. KAKOSO – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

MHE. QAMBALO W. QULWI - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu!

NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI: Maswali.

SPIKA: Kama ilivyo ada tunaanza na maswali kwa ofisi ya Mheshimiwa Rais, TAMISEMI, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 175

Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu

MHE. STANSLAUS H. NYONGO aliuliza:-

Mkoa wa Simiyu ulianzishwa kisheria na Makao Makuu yake kuwa kwenye Mji Mdogo wa Bariadi badala ya Mji wa Maswa:-

(a) Je, ni vigezo gani vilitumika kuamua Makao Makuu ya Mkoa na shughuli zake yawe Bariadi badala ya Maswa ambako kuna majengo ya kutosha ya Serikali; badala yake Serikali inaingia kwenye matumizi makubwa ya kupanga ofisi toka nyumba za watu binafsi huko Bariadi?

(b) Je, Serikali inaweza kufikiria kubadilisha maamuzi haya kwa manufaa ya Taifa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu kuwa Bariadi Mjini siyo Maswa yalipitishwa na wananchi wenyewe kupitia vikao vya kisheria ambavyo ni Mkutano Mkuu wa Vijiji, Kamati za Maendeleo ya Kata,

Mabaraza ya Madiwani, Kamati za ushauri za Wilaya (DCC) na Mkoa (RCC). Uamuzi wa mwisho ulifanyika katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa tarehe 10 Mei, 2010 ambapo Wajumbe wote waliridhia pendekezo la Bariadi Mjini kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu. Hivyo, kigezo kikubwa kilichotumika kuamua Makao Makuu kilikuwa ni maamuzi ya pamoja kupitia vikao halali vilivyoshirikisha wadau kutoka Wilaya zote, wakiwemo kutoka sekta binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu ya (a) ya jibu hili, maamuzi hayo yalifanywa na vikao halali vya kisheria, ikiwahusisha Wajumbe wa vikao hivyo, hivyo kitendo cha Serikali kubadilisha maamuzi hayo itakuwa ni kuwanyang'anya madaraka wananchi yaliyowekwa kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 145.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua ushirikishwaji wa vikao vya Wilaya ya Maswa, kwa sababu jibu lake la mwanzo ameeleza kwamba vijiji vilishirikishwa, lakini nina hakika kabisa ushirikishwaji wa vijiji hivi na Kamati hizi zilizo rodheshwa hapa sina hakika navyo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuniridhisha kwa kunionesha vikao hivi vilifanyika lini na wapi ili watu wa Maswa waweze kulitambua hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mwenyekiti wa RCC ni Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Mkoa wa wakati ule alikuwa ni Dkt. Balele ambaye naye anatokea Bariadi, huoni naye alikuwa labda ni sehemu ya kufanya Serikali iingie kwenye matumizi makubwa, kupeleka sehemu ambapo hakuna majengo mengi ikilinganishwa na Maswa ambayo ni Wilaya kongwe iliyozaa Bariadi na Meatu?

MBUNGE FULANI: Siyo kweli!

SPIKA: Kumbe hilo la pili ndilo msingi wa swali lenyewe hasa. Mheshimiwa Said Jafo majibu. Huu ugomvi wa wenyewe kwa wenyewe, Wasukuma!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali, kwa sababu suala la michakato ya kuanzisha Wilaya, kuanzisha Halmashauri, kuanzisha Mkoa mpya yote haya hayaanzii katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, haya ni maoni ya wadau ambao wameona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo, wanakaa katika vikao halali na kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, nimesema pale awali kwamba kikao hiki kilipitishwa na wajumbe, tarehe 10 Mei, ndiyo walifanya maamuzi hayo. Sasa nikisema nirejee kuthibitisha vikao kwa sababu suala hili nadhani DCC zote kabla hujafika katika

maeneo mbalimbali; kuna vikao vya Mabaraza ya Madiwani, kuna Vikao vya Ushauri vya Wilaya, *then* kuna Vikao vya Ushauri vya Mkoa.

Kwa hiyo, nasema kwamba tukitaka kupata *reference* vizuri, tunapokutana katika RCC yetu inayokuja hapo tuitishe mihtasari ambayo ilipitisha, haya naamini tutayaona na ninyi ni wajumbe wa Kamati ya RCC. Kwa hiyo nadhani hili halina shaka.

Mheshimiwa Spika, suala la kusema kwamba Mwenyekiti wa Kikao hicho ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa lakini asili yake alikuwa anatokea Bariadi. Naomba niwaambie ndugu zangu, tunapofanya maamuzi siku zote tuisukumwe na maamuzi ya mtu mmoja. Mimi kwa akili yangu siamini kama mtu mmoja ataburuza Kamati yote ya RCC na Wilaya yote na yakafuatwa maamuzi yake. Kikubwa zaidi tunapojipambanua katika mikutano yetu ni lazima tuwe imara kujenga hoja kujua jambo hilo linafanyika vipi.

Naamini kama kulikuwa na upungufu RCC yenu mtakaa na kufanya maamuzi sasa kwa mujibu wa sheria. Jambo hili bahati nzuri watu walileta pingamizi, lakini kutokana na vigezo vilivyoletwa, pingamizi lile baadaye ikaonekana kwamba kwa sababu maamuzi hayo yalifanyika halali kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 145, kurudisha madaraka kwa wananchi, ikaonekana ni halali. Ndipo jambo hili limekuja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikaona kwamba ni sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge najua kwamba hoja yake ina msingi, lakini inawezekana wakati huo yeye hukuwepo katika RCC, lakini wenzake waliokuwepo kipindi hicho waliona kwamba jambo hilo lifanyike hivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Chenge, mnatakiwa mrudi Maswa. Swali la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ndilo linalofuata.

Na. 176

Umeme Kuathiri Uzalishaji Viwandani

MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. SALOME W. MAKAMBA) aliuliza:-

Tatizo la kukatika umeme mara kwa mara katika Jimbo la Kahama Mjini linaathiri sana uzalishaji viwandani hasa ukizingatia Serikali imepiga marufuku kwa baadhi ya viwanda kama vile vya kukoboa mpunga na kusaga mahindi kutofanya kazi usiku:-

Je, Serikali ipo tayari kuruhusu viwanda Wilayani Kahama kufanya kazi masaa 24 ili kufidia uzalishaji unaokuwa haufanyiki kipindi umeme unapokuwa umekatika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa hakuna zuio lolote la Halmashauri ya Mji wa Kahama kwamba mashine za kukoboa mpunga na mahindi zisifanye kazi wakati wa usiku au saa 24. Changamoto iliyopo ni kwamba viwanda hivyo vinatumia umeme wa jenereta ambao hautoshelezi kuendesha mashine wakati wote, hivyo kumekuwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara. Halmashauri imewasiliana na Meneja wa TANESCO Kahama na tayari tatizo hilo limeanza kushughulikiwa ili kupata umeme wa uhakika kutoka gridi ya Taifa ambapo tayari kituo cha usambazaji kimeanza kujengwa Kahama.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri inahamasisha wawekezaji wa viwanda vidogo, vikiwemo vya kukoboa mpunga, mahindi na mazao mengine ili kupanua wigo wa mapato kupitia ushuru wa huduma (*service levy*) na ajira kwa vijana, hivyo hakuna sababu yoyote kwa Serikali kuzuia wawekezaji katika viwanda vidogo na vikubwa. Azma ya Serikali ni kupanua uwekezaji wa viwanda kadri iwezekanavyo kwa kuzingatia fursa zilizopo. Tunachofanya ni kuboresha mazingira yatakayosaidia uwekezaji huo ufanyike kwa faida, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha umeme wa uhakika unakuwepo.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri. Kama majibu yalivyo yanadhihirisha kabisa kwamba kuwataka au watu wa Kahama kuendelea na umeme wa jenereta wakati Watanzania wote na yeye mwenyewe anafahamu kwamba Wilaya ya Kahama ni kati ya Wilaya ambazo ni kitovu cha uzalishaji wa chakula *especially* mchele na kwa jinsi hiyo kuwazuia kwa namna moja au nyingine wasifanye uzalishaji wenye tija. Nimeshukuru amesema kwamba utaratibu umeanza wa kuwapatia umeme wa uhakika. Ningetamani sana kuona kuwa hili linapatiwa ufumbuzi haraka na ningetaka sasa aseme ni lini ambapo umeme huo utapatikana kwa uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tatizo la kukatika kwa umeme siyo la Kahama peke yake, ni la maeneo mengi sana Tanzania, likiwepo eneo la Kigamboni, Dar es Salaam, ambapo kule mnaamka mnaulizana kwenu upo? Leo umeme upo? Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI anaweza kutusaidia

kujua kwamba eneo la Kigamboni sasa litaacha kukatiwa umeme kila siku, kila mara especially siku za Jumapili kuanzia lini? Ahsante.(Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge maswali mengine hayo kweli ni ya Wizara ya TAMISEMI? Mheshimiwa Waziri nimekuona.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, Kahama imeunganishwa kwenye lane ya Shinyanga ambayo msongo wake ni wa KV 33 na sisi tunajua kwamba umeme huo ni mdogo, ulitoshwa kwa wakati huo lakini siyo kwa sasa. Kwa hiyo kinachofanyika, nadhani hata kabla ya bajeti yangu kwisha, Ijumaa atawaona watu wa TANESCO wako pale, wameondoka leo, wamekubaliana na Mgodini wa Buzwagi, Buzwagi ndiyo iko karibu sana na Kahama. Kwa hiyo, umeme utavutwa kutoka Buzwagi 33 KV kwenda Kahama. Kwa hiyo, huku watakuwa na wa Shinyanga, huku watakuwa na wa Buzwagi, tatizo hilo litakwisha.

Mheshimiwa Spika, mbali ya hilo la umeme kukatika katika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote lazima tufanye maamuzi. Tukiwa tunajenga hii miundombinu kuna wakati lazima tuzime umeme. Watu wa upande wa Ziwa Victoria kila Jumapili umeme unakatika, lakini wanatangaziwa kwamba tunajenga miundombinu ya kusafirisha umeme mwingi kutoka Iringa mpaka hapa Dodoma, tunatoka kwenye KV 220 mpaka KV 400. Tunatoka hapa Singida, Shinyanga mpaka Nyakanazi KV 400. Sasa hii tunaizindua Septemba.

Mheshimiwa Spika, sehemu zingine Tanzania nzima, hata ndugu zangu wa Arusha waliokuwa wanasema umeme unakatikakatika, tunajenga kutoka Singida kwenda Arusha KV 400, halafu kutoka Da es Salaam kupitia Tanga kwenda Arusha KV 400. Hiyo ndiyo TANESCO mpya. Ahsante.

SPIKA: Imejibu maswali yote mawili, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkambia Mbunge wa Chemba.

Na. 177

Wakulima Waliofukuzwa Kiteto

MHE. JUMA S. NKAMIA aliuliza:-

Wakulima wengi wa Wilaya ya Chemba wamefukuzwa katika mashamba yao Wilayani Kiteto licha ya kufuata taratibu na kudaiwa kuwa eneo hilo ni hifadhi.

Je, Serikali ipo tayari kufuta uamuzi uliotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara wa kuwazuia wakulima hawa ili kuondoa mgogoro huu wa muda mrefu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tamko lililotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara liliwahusu wakulima waliokuwa wavamizi katika eneo la Hifadhi ya Wanyamapori Makame kutoka Wilaya ya Kiteto, Babati, Chemba, Kondo na Mkoa wa Iringa, waliokuwepo wakiendesha shughuli za kilimo katika hifadhi kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo ulitolewa kufuatia Azimio la kikao cha pamoja cha Kamati ya Ulinzi na Usalama za Wilaya ya Kiteto na Chemba kilichokaa tarehe 12 Novemba, 2015. Kikao hicho kiliwashirikisha viongozi wa Vijiji vitano vinavyounda Mamlaka ya Hifadhi (WMA) ambavyo ni Ngobolo, Katikati, Ndedo, Ikshubo na Makame, pamoja na wawakilishi wa wakulima 10 kutoka kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hairuhusiwi shughuli yoyote ya kibinadamu, iwe kilimo, ufugaji au makazi kuendeshwa katika hifadhi. Naomba kutoa wito kwa wananchi kuzingatia sheria za nchi ili kuepuka migogoro katika jamii. Aidha, Serikali za vijiji zinakumbushwa kusimamia vizuri sheria ya ardhi namba tano ya mwaka 1999 ambayo imeweka utaratibu wa kufuata kwa mtu atakayehitaji kupata ardhi kwa matumizi mbalimbali. Lengo ni kuzuia migogoro ya ardhi isiyokuwa ya lazima ambayo kwa sehemu kubwa inatokana na kutozingatia Sheria ya Ardhi.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba unisamehe tu, maswali yangu yatakuwa marefu kidogo kwa mara ya kwanza katika historia yangu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri anachosema humu ndani ni majibu aliyoandikiwa kutoka huko huko kwenye matatizo, waliomwandikia ndiyo chanzo cha mgogoro huu. Sasa swali la kwanza; je, yuko tayari kwenda mwenyewe badala ya kusubiri majibu anayoandikiwa kutoka huko Kiteto?

Swali la pili, hivi sasa wapo wakulima kutoka Chemba, Kongwa, Kondo na maeneo mengine ambayo wafugaji wameamua kwenda kuchunga mashamba yao wakati yakiwa na mazao shambani na hakuna chochote kinachofanywa na mamlaka ya utawala wa Kiteto. Je, kama ninyi

Waheshimiwa Mawaziri mmeshindwa kutatua tatizo hili, mko tayari sasa kuturuhusu tumwombe Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli akamalize tatizo hili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini kwamba majibu haya tumeandikiwa na hao hao ambao wamesababisha mgogoro huo ni tuhuma nzito na nataka nikubaliane na ombi la Mheshimiwa Mbunge la kwenda kuuona ukweli ukoje sisi wenyewe. Kwa hiyo, tutajitahidi, tutajipanga ili tuweze kwenda. *(Makofi)*

Pili, ni kwamba migogoro ya ardhi nchini ya mwingiliano kati ya shughuli za kilimo na shughuli za ufugaji inachochewa sana na maendeleo, kwamba wananchi sasa kila mmoja anatafuta namna ya kupata maendeleo. Hivyo sidhani kama kuna namna ya muujiza unaoweza kufanyika kuimaliza kama tu wadau wote, Serikali, wakulima, wafugaji, hawatatumia busara na hekima zilizokuwa zinatumika na wazee wetu wa zamani wakati hakuna hata sheria nyingi kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kuthamini mali ya mtu mwingine ni jambo jema sana. Kinachotokea sasa hapa ni watu kuacha maadili na utaratibu wa kimila na desturi zetu. Zamani huko ilikuwa migogoro kama hii wanaimaliza kule, lakini unapokwenda kule unakuta kuna makundi na wanaochangia wengine ni sehemu ya watu wanaotakiwa kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sitaki nibishane na Mheshimiwa Mbunge hapa, ninachosema kesi zinatofautiana kati ya kesi moja na kesi nyingine, tutajaribu kwenda na tutakapokwenda tutajaribu kutatua tatizo hili kwa mazingira yake na kwa namna lilivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kusema ukweli, nikiri na nikubali kwamba liko tatizo kubwa na ni lazima sisi Serikali tulishughulikie na tuko tayari kufanya hivyo na nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitakapokwenda huko nitajaribu kushughulikia tatizo hili kwa namna lilivyo, bahati nzuri nalifahamu sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana! Nilikuona Mheshimiwa Kakoso!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Migogoro ya ardhi hasa ya WMA imekuwa ya muda mrefu katika nchi yetu. Jimboni kwangu vipo vijiji ambavyo vina migogoro ya WMA wakati vijiji hivyo ardhi hiyo ni mali yao, lakini kumekuwa na tatizo la wakulima kusumbuliwa, kufukuzwa, kuchomewa nyumba kwenye maeneo yao. Je, ni lini Serikali itakomesha tabia hii ya kuwachomea wananchi kwenye Vijiji husika vya Kabage, Sibwesa, Kapanga na eneo la Kagobole?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Spika, tukifanya rejea ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi katika majibu yake alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Juma Nkamia, alisema kwamba ni maeneo mbalimbali. Hata hivyo, katika suala la kutaka Wabunge kuuliza swali la nyongeza, Wajumbe wengi wamesimama kuonesha kwamba jambo hilo linagusa siyo sehemu ya Mheshimiwa Kakoso peke yake au sehemu ya Mheshimiwa Nkamia peke yake isipokuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tukifanya rejea, Waziri Mkuu alipokuwa akitembelea katika Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine katika Kanda ya Ziwa, alipofika kule Geita miongoni mwa matatizo yalikuwa ni ya wakulima na wafugaji hasa sehemu za hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu alitoa maelekezo katika Wizara ambazo kwa njia moja au nyingine zinashirikiana hasa Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii hali kadhalika na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba, Mheshimiwa Kakoso, sitaki kuweka *commitment* hapa ambayo maelekezo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshayatoa ni kwamba, timu itaundwa kuangalia maeneo yote ya mgogoro na kuangalia mbinu gani ya kuweza kutatua *case by case* kutoka na hali halisi ya mgogoro husika.

Mheshimiwa Spika, jambo hili Mheshimiwa Kakoso tumelisikia kama Serikali, ni miongoni mwa maeneo ambayo yatajumuishwa kufanyiwa kazi kwa pamoja kuondoa migogoro hii katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi, nimekuona!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naongezea majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli kuna matatizo mengi sana katika WMAs nyingi, siyo hii tu anayotoka Mheshimiwa Kakoso. WMAs zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria, ni maeneo ya hifadhi ambayo yanamilikiwa na wanavijiji, kandokando mwa hifadhi za Serikali, lakini WMAs hizi zimepewa mipaka na zimepewa majukumu na mamlaka ya kumiliki maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nadhani Wilaya au kwa makusudi au kwa kutokujua wanaingilia mipaka hiyo. Kwa sababu wanaotakiwa kusimamia kuweka mipaka ya WMAs hizi ni Viongozi wa Wilaya. Sasa nitashangaa Viongozi wa Wilaya kuingia kuchoma! Hata hivyo, kinachotakiwa Mheshimiwa Kakoso hapa, kila

WMA iweke matumizi bora ya ardhi katika eneo lake wanalomiliki ili ijulikane wazi sehemu ya kilimo ni ipi na sehemu ya mifugo ni ipi na mipaka hiyo na ramani hizo zinasajiliwa kwenye ngazi zote kuanzia Wilaya, Mkoa na Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Kakoso arudi kule akaangalie je, mipaka hii ya WMAs imesajiliwa katika ngazi zote hizo na mipango ya matumizi bora ya ardhi imefanyika? Kwa sababu ikifanyika mipango ya matumizi bora ya ardhi na wanaofanya ni watalaam wa ardhi na viongozi wa Wilaya haitatokea hata siku moja kuwa na *contradiction* kati ya Viongozi wa Wilaya na WMAs.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tumekusudia kama Serikali wote kwa pamoja, Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI, Maliasili na watumiaji wakubwa wa ardhi kilimo na mifugo, kukaa pamoja, kuainisha migogoro yote hii hata hiyo migogoro ambayo inasababishwa na hifadhi, wafugaji na wakulima ili kwa pamoja tukae tuweze kuitatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, najua hapa wakisimama, kila mmoja ameguswa na migogoro kama hii. Kwa hiyo, ni kweli kwamba tumeamua kama Serikali tutakaa pamoja na nitaleta kwenye bajeti yangu sehemu ya migogoro kwa uchokozi, ambayo mmeshatuletea Waheshimiwa Wabunge, kama bado mingine ipo tutaendelea kujazilizia ili Wizara hizi zote zinazohusika tuweke utaratibu wa namna ya kupitia mgogoro mmoja baada ya mwingine ili tuweze kuitatua. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lukuvi, naomba turidhike! Ni kweli alivyosema tukiendelea kwenye migogoro tutasimama wote, hata Spika atasimama! (Kicheko)

Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini.

Na. 178

Kujenga Kiwanda cha Tumbaku Tabora

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

Mkoa wa Tabora hauna viwanda kabisa na kwa sababu mkoa huu hulima tumbaku kwa wingi:-

Je, Serikali inasaidiaje kupata Kiwanda cha Tumbaku mkoani humo?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia TAMISEMI na hata kwenye Bunge lako Tukufu, Serikali imetoa mwongozo juu ya uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda na bayana tumeeleza wajibu wa kila mdau. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila mkoa una viwanda. Mkakati wa Serikali ni kuhamasisha uwekezaji katika viwanda kwa nia ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo yanayopatikana katika maeneo husika. Lengo ni kuongeza tija kwenye shughuli za wakulima ili kuongeza ajira na kipato.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mkoa wa Tabora hulima tumbaku na msimu wa mwaka 2015 Tabora ilizalisha tumbaku tani 39,502 ambayo yote ilipelekwa Mkoani Morogoro kwa ajili ya kusindikwa. Tumbaku hiyo pamoja na nyingine kutoka Mikoa ya Nyanda za Juu husindikwa katika Viwanda vya *Tanzania Tobacco Processing Limited- TTPL* kinachosindika tumbaku asilimia 50 na *Alliance One Tanzania Tobacco-AOTT* asilimia 40 ya tumbaku inayolimwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mazungumzo na wawekezaji mahiri katika sekta ya kusindika tumbaku na kuzalisha sigara. Nirudie kueleza kuwa mpaka sasa tunaendelea kufuatilia wawekezaji kutoka Vietnam na China ambao tutawashawishi waje kusindika tumbaku na au kutengeneza sigara. Lengo letu ni kupata mwekezaji anayeweza kutengeneza sigara Tabora kwa “*brand* maalum” duniani na kwenda kuuza sigara hizo nje ya nchi yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka swali la nyongeza.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumuuliza Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mazungumzo na hawa wawekezaji mahiri wa kusindika tumbaku na mambo ya sigara yanaendelea. Je, mazungumzo hayo yakifanikiwa, ana uthibitishia Mkoa wa Tabora kwamba utapata upendeleo kwa kujengwa Kiwanda cha Tumbaku? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameonesha nia ya Serikali kuwashirikisha mashirika ya kijamii kama *NSSF* kushiriki kwenye ujenzi wa viwanda na biashara, je, ni lini mazungumzo hayo, Serikali itaanza na haya mashirika ya kijamii? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Waziri, utajenga Kiwanda cha Tumbaku, Tabora?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ujenzi wa Kiwanda cha Tumbaku Tabora ni la wadau wa Tabora ambao walikaa pamoja na ninyi Wabunge. Nimewaeleza kwamba tunahangaika kutafuta wawekezaji, siku ya Jumapili mwekezaji kutoka China atafika Tabora. Kwa hiyo, Wabunge wa Tabora tukimaliza kikao tukutane kusudi ninyi mtangulie kumpokea Jumamosi halafu tujadiliane. Masharti ni yale yale, kama mtatoa eneo bila kuweka vikwazo vya fidia za ajabu mtapata upendeleo, hali ndivyo ilivyo, utakavyotoa vivutio utapata upendeleo. Ujumbe wa China unakwenda Tabora na *Precision* Jumapili, tangulieni, Jumamosi tukakutane kule tuweze kuwakaribisha wawekezaji. Kwa hiyo, Tabora nimewafanyia kazi, ni jukumu langu pia ni jukumu lenu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, uwekezaji wa hizi *Social Securities*, maelekezo ya Mheshimiwa Rais nimeyasikia, nilichofanya nimemwagiza Katibu Mkuu anayeshughulikia biashara na uwekezaji Wizarani kwangu, akutane na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Kazi inayosimamia haya mashirika, akutane na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Kilimo, wote wakae, wabainishe ni wapi kwenye shughuli zenye tija ambako hizi *Social Securities* zinaweza kuwekeza na kuweza kurudisha pato lake. Kwa hiyo, watalaam watafanya kazi hiyo na nimewaambia kabla ya tarehe 26 wanilettee orodha na nitaitangaza hapa Bungeni kwako.

SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mchemba, hujaridhika tu! Ndiyo pale nyuma pale.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, ahsante...

SPIKA: Siyo wewe yule pale nyuma!

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Naitwa Genzabuke.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa viwanda katika Mkoa wa Tabora ni sawa na ukosefu wa viwanda katika Mkoa wa Kigoma. Kwa muda mrefu sana Mkoa wa Kigoma umekuwa kama uko kisiwani kwa maana ya ukosefu wa miundombinu ya barabara za lami na umeme. Hata hivyo, kwa juhudi zinazofanywa na Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, mkoa ule umeanza kufunguka na siyo muda mrefu utafunguka kabisa. Je, Waziri yuko tayari sasa kuwahamasisha wawekezaji kuja kuweka viwanda katika Mkoa wa Kigoma? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, Kigoma viwanda namna gani?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maeneo ambayo nimepewa maelekezo mahsusi kushughulikia ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Napenda kutambua mchango wa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma kwa ujumla wenu namna mnavyonipa ushirikiano katika kushughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi iliyoko mbioni kwenda ni Kigoma *Sugar*, nimemomba Mkurugenzi Mtendaji wa *TIC* anipe *update* kama ilivyokuwa jana, Kigoma *Sugar* tumefikia wapi. Ameniletea taarifa, nimesema arudie anieleze kwa maandishi yule mwekezaji anasema nini nataka *update* ya jana, Kigoma *sugar* iko njiani.

Mheshimiwa Spika, simenti watalaam wa *cement* wamebainisha kwamba, katika Mkoa wa Kigoma ndiko kuna chokaa nyingi. Kwa hiyo, nakwenda kuwashawishi wenye viwanda, wanaotengeneza *clinker* Dar es Salaam, itengenezwa *clinker* Dar es Salaam iletwe Kigoma tuweze kutengeneza *cement*.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu mawese; mpango wa kaya moja kulima heka moja, kaya laki moja, tulime heka laki moja tutengeneze shamba kubwa la mawese nalifanyia kazi na mwekezaji ameshakubali na kiwanda kitagharimu bilioni 15, ni kazi yangu, ni kazi yenu. Atakayenichangamkia ndiyo nitakwenda kwake! *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa ni kuchangamka tu! Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, Mheshimiwa Mapunda.

Na. 179

Kuwalinda Wakulima Wadogo wa Kahawa

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la Kampuni kubwa kuanzisha mashamba ya kahawa katika maeneo ya Wilaya ya Mbinga na sehemu za Songea Vijijini jambo linalotishia uzalishaji na soko kwa wakulima wadogo wadogo wa kahawa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda wakulima wadogo wasimezwe na wakulima wakubwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na ongezeko la kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya kahawa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya za Mbinga na Songea Vijijini. Hali hii inachangiwa na sera na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo nchini. Aidha, uwepo wa uanzishwaji wa mashamba makubwa nchini hautishii uzalishaji na soko la kahawa kwa wakulima wadogo wa kahawa bali una manufaa yafuatayo:-

Kwanza, uanzishwaji na uwepo wa mashamba makubwa unawezesha wakulima wadogo walio karibu na mashamba hayo kujifunza teknolojia mbalimbali zinazotumiwa na mashamba hayo katika kuongeza tija na uzalishaji wa kahawa.

Pili, baadhi ya mashamba makubwa yanaendesha miradi ya kuwasaidia wakulima wa kahawa walio karibu na mashamba hayo katika maana ya (*outgrowers schemes*) kwa kuwapa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za ugani, ukoboaji na masoko ya kahawa yao. Kwa mfano, Shamba la Aviv lililopo Lipokela, Halmashauri ya Songea limekuwa likitoa huduma za ugani kwa wakulima wanaolizunguka. Aidha mpaka sasa kiasi cha miche 550,000 imekwisha gawanywa kwa wakulima tangu shamba hilo lianzishwe miaka minne iliyopita.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa hayo, Serikali ilifanya marekebisho ya Kanuni zinazoongoza tasnia ya kahawa ili kuwalinda wakulima wadogo wanaoingia makubaliano ya uzalishaji wa Kahawa na makampuni binafsi pamoja na mashamba makubwa.

SPIKA: Mheshimiwa Mapunda Sixtus, swali la nyongeza.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuvishirikisha Vyama vya Msingi na AMCOS kwenye hiyo *contract farming* badala ya ku-*deal* na wafanyabiashara binafsi ambao wale hawamgusi moja kwa moja mkulima, wao wako zaidi kwa ajili ya ununuzi wa kahawa siyo uzalishaji wa kahawa.

Mheshimiwa Waziri huoni sasa ni wakati muafaka kwa ile AMCOS ya Kimuli ya kule Utili sasa ishirikishwe na zile 'AMCOS' nyingine za Miyangayanga, Utili na sehemu nyingine? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kama alivyosema, ni kweli kwamba kama AMCOS zingekuwa zinashirikishwa ingeweza ikawa na manufaa kwa wakulima wengi. Nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha wakulima katika *contract farming*, tayari Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa ilishaifanyia marekebisho Sheria ya Kahawa ya mwaka 2001 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2012, ili kuweka utaratibu kwa yeyote yule ambaye anataka kuingia katika kilimo cha mkataba katika maana ya *contract farming* aweze kuingia katika namna ambayo haitamnyonya wala kumuumiza mzalishaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, zile AMCOS ambazo zinataka kuingia katika mkataba wa kilimo na wazalishaji wakubwa, tayari kuna utaratibu wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, ni suala la wenyewe kujiweka sawa na Bodi ya Kahawa itawahakikishia kwamba wanaingia katika mikataba ambayo haitawanyonya.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selasini ulikuwa umepotea hebu tupe taarifa bwana, swali la nyongeza! (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na kesi nimeshinda...! Kwa hiyo nipo tena kazini kama kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tofauti na Mbinga, wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kilimanjaro hususani Jimbo la Rombo wanaelekea kukata tamaa, wengi wao wanang'oa kahawa wakibadilisha na mazao mengine. Tatizo ni kwamba gharama ya uzalishaji wa kahawa ni kubwa sana wakati bei ya kahawa ni ndogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku katika zao la kahawa ili kuwapa motisha wakulima wa kahawa tena kahawa ile tamu ya *Arabica* ndiyo inayong'olewa, ili kahawa isije ikafa katika Mkoa wa Kilimanjaro? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la mwenzetu aliyerejea kundini, Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kwa miaka ya karibuni zao la kahawa limepata changamoto nyingi sana, hususan bei kwa wakulima wetu. Serikali imechukua hatua kadhaa ili kukabiliana na changamoto hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa

Kahawa (CDTF) ili uweze kusimamia zao la kahawa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanatoa pembejeo kwa wakulima kwa bei ambayo ni nafuu.

Mheshimiwa Spika, tayari katika mazao mengine, hususan zao la korosho, tumegundua kwamba kwa kuanzisha Mfuko ni rahisi Mfuko ule kuwasaidia wakulima kupata pembejeo kwa bei ambayo ni nzuri na hivyo basi kuwaondolea gharama ambazo katika mjengeko wa bei zinawafanya wapate bei ambayo siyo nzuri. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, tayari Mfuko huu upo, umeanza kazi na mtaji bado unaendelea kujengwa ili uweze kuwasaidia sasa wakulima wa kahawa waweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

Na. 180

Ujenzi Kituo cha Polisi Liwale

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Wilaya ya Liwale ilipandishwa hadhi kuwa Wilaya kamili tangu mwaka 1975, lakini ni Wilaya ya pekee ambayo haina Kituo cha Polisi wala nyumba za watumishi wa kada hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la kituo cha Polisi Wilaya ya Liwale sambamba na nyumba za watumishi ambao wanaishi uraiani kwa sasa?

(b) Je, ni lini Tarafa ya Kibutuka itapata kituo kidogo cha Polisi ili kulinda wafanyabiashara wa mazao ya ufuta wanaokuja Tarafani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Wilaya ya Liwale ndiyo Wilaya pekee nchini ambayo haina Kituo cha Polisi na nyumba za watumishi. Liwale ni miongoni mwa Wilaya 65 nchini ambazo bado hazijajengewa vituo vya Polisi.

Hata hivyo, Serikali itajitahidi kujenga vituo vya Polisi awamu kwa awamu kadri hali ya kibajeti itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kusogeza huduma za Polisi kwa wananchi ni azma ya Serikali kujenga Kituo cha Polisi kila Tarafa, sanjari na kupeleka Wakaguzi wa Polisi kuongoza vituo hivi, hata hivyo, Kata nne ikiwemo Kibutuka, Mirui, Kiangala na Nangano za Tarafa ya Kibutuka, kuna Askari Kata ambao wanatoa huduma kwa wananchi. Aidha, katika kutekeleza azma hii tayari Jeshi la Polisi limeshapeleka Wakaguzi katika baadhi ya Tarafa. Tunaomba Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira kwani hali ya fedha itakaporuhusu mpango huu utafika kila Tarafa ikiwemo Kibutuka.

SPIKA: Jamani, maswali ya Polisi siyo tuliyamaliza jana jamani! Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nasikitika sana kwa majibu ya kukatisha tamaa yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Wilaya ya Liwale ina umri wa miaka 41 leo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasema haina mpango wowote wa kujenga Kituo cha Polisi pale, anaposema kwamba ni zaidi ya Wilaya 65, sidhani kama hizi Wilaya nyingine ambazo anazi-include yeye zina umri wa miaka 40. Wilaya ya Liwale ina jumla ya kilometa 66,000 na hizi tarafa anazosisema zipo umbali wa kilometa zaidi ya 60 kutoka Liwale Mjini... (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka, swali sasa!

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, najenga hoja. Wilaya ya Liwale mpaka leo, nimetembelea kile kituo, mafaili yale wanafunika na maturubai, lile jengo walilopanga la mtu binafsi linavuwa. Sasa ninachoomba, nipewe *time frame*, ni lini Kituo cha Polisi Liwale kitajengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Tarafa ya Kibutuka, ndiyo tarafa inayoongoza kwa ufuta na wafanyabiashara wakubwa wako pale na Kata ya Lilombe sasa hivi kuna machimbo na wafanyabiashara wengi wako pale, ni lini Kata hizi zitajengewa vituo vya Polisi? (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kifupi.

MBUNGE FULANI: Hana majibu mengine huyo, hawezi kujibu huyo!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue *concern* ya Mheshimiwa Mbunge Kuchauka kuhusiana na unyeti na umuhimu wa kujenga kituo pale Liwale, lakini kama nilivyomwambia

kwamba vituo hivi pamoja na vingine ambavyo tumepanga kuvijenga, tutavijenga kadri ya fedha zitakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kwa uchungu kuhusiana na matatizo makubwa yaliyopo katika Wilaya yake, basi niseme tu kwamba pale ambapo tutapata fedha tutatoa kipaumbele kwenye kituo cha Liwale.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, anauliza kwamba, katika Tarafa ya Kibutuka, ninachoweza kusema ni kwamba kama nilivyojibu katika jibu la msingi, kwamba tumejaribu kupeleka Askari katika Tarafa ile ili waweze kusaidia ulinzi kwa wakati huu, wakati tunajjandaa na ujenzi wa kituo pale ambapo fedha zitapatikana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa vyovyote vile naomba tuendelee na swali linalofuata la Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, linaulizwa na Mheshimiwa Mwamoto kwa niaba yake.

Na. 181

Kuunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya

MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. DKT. NORMAN A. SIGALLA KING) aliuliza:-

Je, ni lini Mkoa wa Njombe utauunganishwa na Mkoa wa Mbeya kilomita 205 kutoka Njombe – Makete – Isionje - Mbeya?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe – Makete – Kikondo - Isionje (Mbeya) yenye urefu wa kilometa 205.6 ni barabara inayosimamiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Njombe kwa sehemu ya kilometa 183.4 kutoka Njombe hadi Kikondo na sehemu iliyobaki ya kilometa 22.2 kutoka Kikondo hadi Isionje inasimamiwa na *TANROADS* Mkoa wa Mbeya. Ili kutekeleza azma ya kuunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya, Serikali itatekeleza ujenzi wa mradi wa barabara ya Njombe – Makete – Isionje - Mbeya kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo kwa sehemu ya Njombe – Ndulamo - Makete, yenye urefu wa kilometa 109.4 umefanyika na kukamilika mwezi Machi, 2014. Aidha, Serikali inafanya maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya Makete – Kikondo - Isionje yenye urefu wa kilometa 96.2.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Ndulamo - Makete, yenye urefu wa kilometa 109.4 unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2016/17.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa barabara iliyotajwa ya kuunganisha Mbeya na Makete bado imechukua muda mrefu na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ana mpango wa kwenda Mkoa wa Njombe, haoni sasa kuna sababu kubwa ya kupita na kuangalia, kutokana na majibu aliyojibu kuona kama kweli itajengwa kwa wakati ambao amehidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa barabara hizi zipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ikiwemo hii ya kuunganisha Wilaya ya Kilolo na Iringa Mjini. Je, haoni sasa ni muda muafaka wa kufika na kutembelea barabara ambayo inaanzia Ipogolo – Ndiwili - Kilolo ambayo kwa miaka saba imejengwa kilometa saba na kilometa zilizobaki ni 28, haoni kwamba itachukua miaka 28 pia kumalizia hicho kipande kilichobaki?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, nitakagua kama ambavyo amependekeza ili kuthibitisha kwamba eneo hilo tunalokusudia kulijenga kweli litajengwa.

Pili, kuhusu barabara ya kutokea Kilolo hadi Iringa, ni barabara ambayo ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 na hata hiyo barabara nyingine nayo ni sehemu ya Ilani. Namhakikishia, barabara zote zilizopo ndani ya kitabu cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tutazishughulikia na kuzikamilisha kwa awamu kadri tutakavyokuwa tunapata uwezo mwaka hadi mwaka.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali la Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Sabreena.

Na. 182

Upatikanaji wa Tiketi za Usafiri wa Treni Kigoma

MHE. SABREENA H. SUNGURA aliuliza:-

Shirika la Reli Kigoma linawahudumia wakazi wa Kigoma, Burundi, Congo, Zambia na kadhalika na inawalazimu wakazi hao kulala stesheni au waamke alfajiri ili kuwahi tiketi na wakati mwingine hukosa tiketi hizo:-

Je, ni kwa nini Shirika la Reli Tanzania (TRL) wasianzishe mfumo wa uwakala wa tiketi ili kupunguza adha hiyo wanayopata wakazi hao?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya usafiri wa treni katika Mkoa wa Kigoma, uzaji wa tiketi katika Stesheni ya Reli ya Kigoma umekuwa na changamoto kubwa kutokana na ubaguzi na ulanguzi wa tiketi. Ili kudhibiti ulanguzi huo, Kampuni ya Reli Tanzania iliamua kubadilisha utaratibu wa kuuza tiketi siku za safari na kwa kutumia vitambulisho, jambo ambalo limesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti ulanguzi wa tiketi. Hata hivyo, utaratibu huo umekuwa na changamoto zake kwa kusababisha wasafiri kulala Stesheni au kuwalazimu kuamka alfajiri ili kuwahi tiketi hizo.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo siyo kuanzisha mfumo wa wakala ambao utaiongezea *Tanzania Railway Limited* gharama za uendeshaji. Tatizo kubwa lililopo ni idadi ndogo ya safari za treni ambapo huduma inayotolewa hivi sasa haikidhi mahitaji halisi ya wananchi na hivyo kuwa na uhaba wa tiketi kwa abiria. Hivyo ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inatarajia kuongeza idadi ya treni za abiria kwa njia ya Kigoma ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa mkoa huo.

SPIKA: Mheshimiwa Sabreena, swali la nyongeza.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa masikitiko makubwa nasikitishwa sana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, hii Serikali inajijita ni Serikali ya hapa kazi tu na kila siku imekuwa ikija na majibu mepesi kwa maswali mazito. Wamiliki wa mabasi ambao ni wananchi wa kawaida wenye uwezo wa kawaida wana uwezo wa

kuwa na mawakala katika Wilaya mbalimbali nchini, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inashindwaje kuwa na mawakala ili kusaidia wananchi waweze kuzipata tiketi hizi kwa urahisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mtu anatoka Kasulu, mtu anatoka Kibondo, mtu anatoka Ilagala anatumia sh. 10,000, sh. 8,000, sh. 7,000, anakwenda na kurudi, anakaa saa kumi usiku mpaka nne asubuhi, tiketi zinaanza kuuzwa na anakosa tiketi anarudi kijijini. Hizo gharama kwa mwananchi anazona ni ndogo kuliko Serikali kuweka mawakala katika maeneo husika? *(Makofi)*

SPIKA: Sasa swali!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, swali ni kwamba anaona gharama ya Serikali kuweka mawakala katika Wilaya husika ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa usafiri ni kubwa kuliko gharama wanazozipata wananchi kuamka saa kumi ya usiku na kukosa tiketi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ...

SPIKA: Hee! Bado!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, bado, hilo ni swali la kwanza. Swali la pili, amekiri kwamba kuna ulanguzi wa tiketi. Tiketi ya daraja la tatu ambayo inauzwa sh. 24,000 katika soko la ulanguzi inauzwa sh. 35,000 mpaka sh. 40,000. Daraja la pili kwa bei ya sh. 56,000 inauzwa sh. 75,000 mpaka sh. 85,000 na daraja la kwanza kwa bei ya sh. 76,000 inauzwa sh. 100,000 mpaka sh. 110,000. Je, Serikali, ni lini sasa mtaondoa kero hii na kutoa ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili? *(Makofi)*

SPIKA: Eeh, hapa kazi tu! Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, ulanguzi wa tiketi ulikuwa kwa kiwango kikubwa sana kabla ya utaratibu huu ambao Serikali tumesema tumeubadilisha haujafanyika, baada ya utaratibu huu kufanyika tatizo hili la ulanguzi wa tiketi sasa halipo kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama ambazo wananchi wanazipata tutaangalia uwezekano mwingine, badala ya kuanzisha wakala, tutaanzisha huduma ya wateja katika stesheni ile ile, upate uhakika wa tiketi kabla hujakwenda stesheni kulipa fedha na tunakokwenda TRL itaanzisha huduma ya kutoa tiketi ukiwa nyumbani huko kwa kutumia simu. Hatutaleta mawakala kwa

sababu kuleta mawakala kunaongeza gharama zaidi kwa *TRL* na vilevile ni gharama kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu suala la...

SPIKA: Umesikia Mheshimiwa Sabreena, Serikali hii ya hapa kazi tu inaleta *digital!* Mheshimiwa Waziri endelea! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, namhakikishia kwamba tukishaanzisha utaratibu huo, hilo tatizo la pili ambalo analiongelea halitakuwepo tena.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri. Sasa Mbunge wa Kigoma Mjini naye amesimama, haya mzee!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, alichokiuliza Mheshimiwa Sabreena ni kwa nini Serikali haitumii mawakala. Mawakala hawana gharama ni kama leo unaposema kwamba *TANESCO* iuze *LUKU* yenyewe badala ya kutumia ma-*agent* wa *LUKU*. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri na Mkurugenzi Mkuu wa *TRL* wakae, kwa sababu mimi na Mkurugenzi Mkuu wa *TRL* na Waziri tumekutana Kigoma, tumekwenda Stesheni, tumeona hali ilivyo na tumekubaliana kwamba *the best way* ni kuruhusu mawakala kuuza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu yupo Ilagala, yupo Kibondo, yupo Kasulu, kama alivyosema Mheshimiwa Sabreena, mawakala wauze, tunakuwa tunajua idadi ya mabehewa yatakuwepo Kigoma, abiria watakuoondoka, tiketi zitolewe ziweze kuuzwa. Nashindwa kuelewa Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumzia gharama gani hapa, sielewi kabisa, inabidi ujifunze kwa watu wa Nishati na Madini, *TANESCO* wanafanyaje kwenye *LUKU*.

Mheshimiwa Waziri tunaomba umsaidie Naibu wako bwana! (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa!

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikwenda pamoja na Mheshimiwa Zitto kule Kigoma na tuliona hali halisi na kupitia kampuni yetu ya *TRL* tuliamua kuanzia sasa hivi tunakwenda kufanya mfumo wa elektroniki ambao watu wanaweza kununua tiketi kwa simu popote pale walipo Tanzania. Tunaanzia na *trial* ya kwanza kuanzia Mpanda mpaka Tabora wakati wowote kuanzia sasa hivi, halafu tunakwenda Kigoma na Tabora. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa, angalieni muda, mtaona tunaishiwa muda. Swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe.

Mheshimiwa Hongoli!

Na. 183

Barabara kutoka Njombe - Morogoro

MHE. JORAM I. HONGOLI aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ilani ya CCM iliahidi kutengeneza barabara ya kutoka Njombe - Lupembe - Madeke - Morogoro - kwa lami katika mwaka 2015/2016:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kutengenezwa hasa ikizingatiwa kuwa imebaki miezi mitano katika mwaka wa fedha 2015/2016?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika ni kweli kuwa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 imeweka katika mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kibena – Lupembe - Madeke.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara *TANROADS*, imeshaanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Njombe (Kibena) – Lupembe - Madeke yenye urefu wa kilometa 126.2 kwa kiwango cha lami. Maandalizi haya yalianza kwa kusaini mkataba kati ya *TANROADS* na Mhandisi Mshauri *M/S Howard Humphreys (T) Limited* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo. Kazi ya usanifu ilikamilika mwezi Machi 2014 kwa gharama ya shilingi milioni 503.55, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Lupembe - Madeke unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2016/2017.

SPIKA: Mheshimiwa Hongoli, swali la nyongeza.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kunithibitisha juu ya kuanza ujenzi huo kwa mwaka 2016/2017, kwa kuwa kwenye vitabu vya bajeti sijaona bajeti iliyotengwa au fedha iliyotengwa kwa ajili ya barabara hiyo.

Swali la pili, barabara ya Lupembe kwa sasa hivi imefungwa, magari yote yanayoanzia tani kumi na kuendelea hayaruhusiwi kuingia, wakati wananchi wa Lupembe, hasa kata nane, wanategemea barabara hii kusafirisha mbaao, wanategemea barabara hii kusafirisha nguzo na vifaa vya ujenzi kama mchanga na tofali, sasa hivi imefungwa hawawezi kusafirisha, hivyo kuathiri uchumi wa wananchi hawa. Naomba Serikali iniambie, ni utaratibu gani ambao itauweka kwa sasa hivi ambapo tunasubiri ujenzi wa barabara hii ili wananchi wasiendelee kuathirika kwa uchumi wao?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kwa swali lake dogo la kwanza, naomba asubiri hotuba ya Waziri wangu wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili apate tafsiri sahihi ya randama ambayo ameiangalia. Namhakikishia ujenzi huo unaanza mwaka 2016/2017 kama tulivyoeleza katika jibu la swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuharibika na kukatika kwa barabara hiyo, naomba nichukue fursa hii kuwakumbusha tena *TANROADS* mikoani wote pamoja na *Chief* wao, kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo zimekatika kutokana na mvua kubwa iliyopita zinafunguliwa, wasimamie suala hilo ili wananchi waendeleo kupata huduma ya usafiri na maisha yaendeleo kama kawaida.

SPIKA: Mheshimiwa Stephen Ngonyani nilikuona, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga barabara ya lami kilometa 1.5 katika Mji wa Mombo na Rais wa Awamu ya Tano ameahidi vilevile kujenga barabara hiyo kilometa moja, lakini cha kushangaza mpaka leo hii hela hazijaingia katika Mfuko wa Mkoa. Je, ile barabara ambayo imeahidiwa na Marais wawili itajengwa lini kwa kiwango cha lami kule Mombo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Ngonyani!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia kwamba ahadi za viongozi wetu, Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne na Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano, tuliopewa dhamana tutaitekeleza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona muda hauko upande wetu, kwa hiyo, tuendeleo na mambo mengine.

Naomba niwatambue wageni walioko katika ukumbi wetu kwa siku ya leo.

Tunaanza na wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni *Engineer* Joseph Nyamuhanga, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Katibu Mkuu usimame, ahsante sana. Profesa Faustine Kamuzora, Katibu Mkuu wa Mawasiliano; *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho, Katibu Mkuu Uchukuzi, eeh, hii Wizara ina Makatibu Wakuu watatu; Dkt. Maria Sasabo, Naibu Katibu Mkuu Mawasiliano. *(Makofi)*

Nitambue Wenyeviti wa Bodi na Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara, wawakilishi kutoka Umoja wa Ulaya (*European Union*) mliopo karibuni sana. Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakurugenzi, Maofisa Waandamizi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 80 toka Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam ambao ni wageni wa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Wanafunzi wa kutoka *NIT* simameni pale mlipo, karibuni sana. Mpendeza kweli, karibuni sana Bungeni, karibuni Dodoma, mjifunze vizuri namna mambo ya mawasiliano yanavyokwenda. Leo msitoke hapo, msikilize mwanzo mwisho. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni kama ifuatavyo:

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ambao ni wanafunzi wanaosoma katika Chuo Kikuu cha *UDOM*, wanafunzi hao ni wakazi wa Nzega. Wale wanafunzi wa Nzega mlioko *UDOM*, aisee! siku hizi hata Wanyamwezi mnasoma! Karibuni sana, Mbunge wenu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Makambako, Mkoa wa Njombe, wakiongozwa na Mheshimiwa Nolasco James Mlowe na Ndugu Ola Mhema, Diwani na Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Juma Nkamia wa Jimbo la Chemba ambao ni Walimu wa Shule za Sekondari Feza kutoka Dar es Salaam, wageni wa Mheshimiwa Nkamia, watatu wale, karibuni pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango, wanaotokea Jimboni kwake Liwale, Mkoa wa Lindi. Wanafunzi 24 waliotoka Liwale. Eeh! Jamani ninyi ndiyo mnasema CCM haifanya kazi! Liwale inakuwa na wanafunzi 24, jamani hongereni sana, CCM kweli inachapa kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Ghasia ambao ni Maafisa uhusiano MOAT kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, ndugu Beatrice Singano, Ndugu Rasaline Moria na Ndugu Shabu Maurus, karibuni. *(Makofi)*

Pia kuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye ni Ndugu Francisca Shirima, Makamu wa Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA). Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Bilago, Mbunge wa Jimbo la Buyungu wakiongozwa na ndugu Piesa Bilago, Mke wake, karibuni sana, Mama watoto yuko wapi, mbona hatujamwona, ehee! Karibu sana shemeji yetu. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni mmoja na Mheshimiwa Doto Biteko, Jimbo la Bukombe ambaye ndiyo Ndugu Inyasi Kalusanga, Mjumbe wa Umoja wa Vijana kutoka Jimbo la Bukombe, karibu sana Mjumbe. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Susan Kiwanga ambao ni wakulima kutoka Jimbo la Mlimba, Ndugu Lenifrid Magundula, Mjumbe wa Serikali ya Kijiji na Ndugu Gundram Ligonja, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkangawalo, karibuni sana kutoka Mlimba mpaka hapa ni shughuli nzito, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni kwa ajili ya mafunzo ni Wenyeviti 185 wa Serikali za Mitaa na Vijiji wa Manispaa ya Dodoma kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi kwa leo hatuna, kwa hiyo, tunaendelea na shughuli za Bunge.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Nitajieni majina yenu! Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Doto Biteko, Mheshimiwa Kasuku Bilago. Inaelekea mnawasha *microphone* wengi kwa hiyo mnakuwa mnavuma. Naomba mzime. Mheshimiwa Julius Laizer, Mheshimiwa Hussein Bashe.

Tuanze na Mheshimiwa Julius, naomba tufanye kifupi Wizara hii ya leo ni kubwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri asubuhi anajibu swali kuhusu migogoro ya WMA alisema Waziri Mkuu ametoa maagizo ya kuunda Tume kwa ajili ya kupitia migogoro hiyo, lakini tunakumbuka katika Bunge lililopita kulikuwa na Kamati iliyoongozwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mheshimiwa Ole-Sendeka kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini. Mpaka leo Serikali haikuteteleza ripoti ile, je, unaona ni sahihi kuendelea kuunda Tume badala ya kwenda kwenye kutekeleza yale ambayo tayari Kamati kadhaa zilishayafanyia kazi?

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba mwongozo wako, ni namna gani Bunge hili linabariki kuendelea kuunda Tume badala ya kutekeleza yale ambayo Tume zilizopita zilishapendekeza. *(Makofi)*

SPIKA: Mbona Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana labda urudie kidogo kwa kifupi Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Mheshimiwa Mbunge wa Monduli hakuwepo humu wakati inaundwa Tume ile. Wakati ile Tume ya Mheshimiwa Jenista inasema hukuwepo, lakini ile taarifa ya Mheshimiwa Jenista imeshaanza kufanyiwa kazi na taarifa mbalimbali zimeanza kutolewa, haikuwa na *deadline*. Nimpe taarifa tu kwamba ile Kamati haina unyumbufu wa migogoro yote nchi nzima, ilitoa mwongozo wa namna ya kutatua migogoro, lakini haikupata nafasi ya kujifunza na kujua migogoro yote ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema nilipoingia hapa nimemwandikia kila Mbunge aniandikie anavyoona, maana ninyi wote mnapambana na maswali ya migogoro. Niandikieni kila mmoja habari ya migogoro mliyonyayo na wewe umeleta na nimekuja kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimeagiza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wameleta wote, faida niliyosema, kwa sababu sisi tumeelekezwa na Mheshimiwa Rais kwamba katika miaka mitano hii lazima tuondoe migogoro. Faida niliyosema, nitagawa kile kitabu cha migogoro mliyoniandikia wote ninyi kwenye bajeti yangu ili mthibitisha hii ndiyo yenyewe na ile waliyoleta Wakuu wa Mikoa muone kwa sababu migogoro siyo siri, kuna nyongeza mtaongeza ili itusaidie Mawaziri tunaohusika na sekta hizi tujipange vizuri na tuanze ratiba ya kutekeleza utatuzi wa migogoro hiyo. Utaratibu wangu nafikiri Mheshimiwa Mbunge aukubali, ni mzuri zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Doto Biteko!

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba mwongozo wako, jana kwenye kipindi cha dakika 45, *ITV*, Serikali ilitoa maelezo ambayo kwa maoni yangu nadhani yamesababisha usumbufu mkubwa. Kwanza, Serikali ilisema ufugaji wa ng'ombe Tanzania kwa maoni ya msemaji hauna faida ya kuupatia uzito wa kutosha. Jambo la pili lililosemwa ni kwamba nyama ya ng'ombe wa Tanzania imejaa magonjwa mengi na kwa hiyo ni hatari kwa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako, hivi Serikali haioni au iseme hapa kwamba ufugaji wa ng'ombe Tanzania sasa tusimamisha tufanye biashara nyingine. Vilevile Serikali itupe maelezo ya kutosha, ni msimamo wa Serikali kwamba nyama ya Tanzania ina athari kubwa kwa afya za Watanzania?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Hilo kwa kuwa Wizara ambayo unadai imesema jana bado haijawasilisha bajeti yake hapa, watakapokuja hapa mtawakumbusha watafafanua wenyewe. Nadhani unamaanisha Wizara ya Maliasili na Utalii!

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Spika, ndiyo!

SPIKA: Si ndiyo!

MHE. DOTO M. BITEKO: Ndiyo, lakini jambo hilo linasababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi kwa sababu...

SPIKA: Swali langu ni kwamba waliosema ni Wizara gani?

MHE. DOTO M. BITEKO: Alisema Waziri wa Maliasili na Utalii.

SPIKA: Ndiyo nasema kwamba kwa sababu watakuja hapa baadaye watapata nafasi ya kufafanua, Serikali imesikia. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba mwongozo wako, jana usiku baada ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, kulikuwa na hoja ya kutoa shilingi kwenye Wizara hii ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Riziki Shahari na mwisho wa siku, Wabunge kama Wabunge tuliunga mkono ile hoja tukajadili lakini cha ajabu ni kwamba kiti chako tulivyofikia mwisho wa majadiliano, kwa utaratibu wa Bunge hili ni kwamba inatakiwa Bunge liweze kuamua, kupiga kura, lakini mpaka mwisho wa majadiliano yale Kiti chako kilikaa kimya na tukaingia kwenye *guillotine*, sijui ni utaratibu gani.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, ambao tumefikia mpaka mwisho wa majadiliano na hatukupiga kura juu ya Mashekhe ambao wanadhaliushwa, wamewekwa kizuizini takribani miaka mitatu hivi sasa bila kupelekwa Mahakamani, tukafikia hatua ya kujadiliana. Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Maftaha, samahani sana! Sijakuelewa kabisa maana ni masuala ya taratibu.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze tena.

SPIKA: Ndiyo mwongozo ninaokupa huu!

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze tena. Jana usiku kulikuwa kuna mjadala juu ya Mashekhe waliowekwa ndani takribani miaka mitatu hivi sasa ambao hawajapelekwa Mahakamani, kulitolewa hoja ambao hawajapelekwa Mahakamani na kutolewa hukumu. Ikatolewa hoja na Mheshimiwa Riziki Shahari ya kutoa shilingi katika Wizara ya Mambo ya Ndani, mwisho tulijadiliana kama Wabunge, lakini tulitarajia sasa mwisho wa ule mjadala tuweze kupiga kura Bunge liweze kuamua, kwamba kuunga mkono ile hoja ya Mheshimiwa Riziki Shahari, lakini Kiti chako hakikuamua kupiga kura sambamba na kwamba tulishamaliza mjadala ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba mwongozo wako, ni utaratibu upi unatumika kwamba tunajadiliana hoja ya kutoa shilingi na shilingi imetolewa lakini kura hazijapigwa bila kuhojiwa Wabunge...

SPIKA: Mheshimiwa Maftaha naomba nishukuru kwa swali lako, sikuweza kufuatilia kwa ukaribu wa kilichoendelea, lakini niseme tu baadhi ya mambo yanatugawa sana kidini kwa hiyo inabidi twende taratibu kidogo. Niseme tu kwamba nitafuatilia kwenye *Hansard* halafu nione ilikuwaje. Mheshimiwa Bilago! *(Makofi)*

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Naomba Mwongozo wako kufuatia wageni wanaoingia kwenye jengo hili, kama wageni wa Waheshimiwa au wageni wa kwako wewe mwenyewe. Leo kumetokea utaratibu ambao hatujawahi kuuona sisi ambao tunaleta wageni hapa Bungeni. Walipofika mahali pa mapokezi wageni wameombwa vitambulisho au kuacha dhamana ya simu, au kitu chochote chenye thamani ndiyo waweze kuingia ukumbini.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, utaratibu huu umeanza lini? Huoni kwamba umeleta bugudha kwa wageni hawa ambao wameingia ukumbini humu, naomba mwongozo wako umeanza lini na kwa nini hatujajulishwa Wabunge? Ahsante.

SPIKA: Naomba nilichukue kama taarifa ili tuweze kufuatilia wakati mwingine tutawapa maelezo kuhusu hilo kwa sababu hata meza yangu bado haina taarifa ya hilo, nakushukuru kwa taarifa. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, mimi naomba ufute jina langu kwa sababu majibu ya Waziri Lukuvi yamenitia moyo kidogo.

SPIKA: Nakushukuru sana, ahsante sana, Katibu sasa.

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, karibu sana utoe hotuba yako. *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha

2015/2016. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu ambao ni wa kwanza wa Bajeti tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2015. Kwa kipindi kifupi alichokaa madarakani, Watanzania kwa ujumla wetu tumefarijika na uongozi wake mahiri ambao unaonesha nia ya dhati ya kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa kasi inayotakiwa. Naungana na Watanzania kumwomba afya njema ili aweze kuikamilisha kazi hii kubwa aliyoianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniadini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu kuwa sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Nampongeza pia Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuchaguliwa kuiongoza Bunge letu Tukufu. Napenda pia kuwapongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kuteuliwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwao kuwakilisha wananchi katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliundwa mwezi Novemba mwaka jana, baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. Wizara hii inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nitaeleza kwa kifupi majukumu ya kila sekta.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ujenzi imekabidhiwa majukumu ya kusimamia Sera ya Taifa ya Ujenzi ya mwaka 2003 na utekelezaji wake pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani ya 2009 na utekelezaji wake; ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko na kusimamia taasisi zilizo chini ya sekta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya uchukuzi, majukumu ni pamoja na kusimamia Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 na utekelezaji wake; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi; usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli, anga na viwanja vya ndege; utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji na hali ya hewa na pia kusimamia taasisi zilizo chini ya sekta.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano ina majukumu ya kusimamia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003; Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997; na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003.

Aidha, sekta ya mawasiliano ina dhamana ya kuhakikisha kuwa teknolojia ya habari na mawasiliano vinachangia katika maendeleo ya nchi yetu, pamoja na usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na mpango na bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mtiririko wa kisekta nikianza na sekta ya ujenzi, uchukuzi na hatimaye mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2015/2016. Katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020, malengo ya MKUKUTA II; ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera nyinginezo za kisekta, Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi; Bajeti ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2015/2016, sekta ya ujenzi ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 40.023 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hadi Aprili, mwaka huu shilingi bilioni 29.934 zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, sekta ya ujenzi ilitengewa shilingi bilioni 883.83 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi bilioni 191.619 na shilingi bilioni 85.572 zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara zilitengwa shilingi bilioni 606.64. Hadi Aprili, 2016 fedha zilizotolewa ni shilingi trilioni 1.08. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 607.35 ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, shilingi bilioni 149.502 ni fedha za nje na shilingi bilioni 323.952 ni fedha za Mfuko wa Barabara. Sehemu kubwa ya fedha za ndani zilizotolewa imetumika kulipa madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja; hadi kufikia Aprili, 2016, jumla ya kilometa 414.3 kati ya kilometa 523 za barabara kuu zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami zimekamilika. Aidha, kilometa 82.4 kati ya kilometa 113 za barabara kuu zilizopangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha lami zimekamilika. Vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi wa madaraja makubwa 11 ambapo madaraja ya Nyerere Kigamboni na Lukuledi namba mbili yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya kilometa 52.19 kati ya kilometa 77 zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami zimekamilika na jumla ya kilometa 676 za barabara za mikoa zimefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe, kati ya kilometa 1,252 zilizopangwa kufanyiwa ukarabati katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kwa matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa yalikusishia matengenezo ya kawaida kilometa 31,883, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi kilometa 6,096 na matengenezo ya madaraja 3,332. Hadi kufikia Aprili, 2016, jumla ya kilometa 5,968.5 na madaraja 772 yalifanyiwa matengenezo katika barabara kuu. Kwa upande wa barabara za mikoa jumla ya kilometa 12,777 na madaraja 648 yalifanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara inatekeleza mradi wa ujenzi wa Barabara ya Juu yaani *flyover* ya TAZARA, *Interchange* ya Ubungo na maandalizi ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya barabara katika maeneo ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu na Morocco. Kuhusu *flyover* ya TAZARA, mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 15 Oktoba, mwaka jana na ujenzi ulizinduliwa tarehe 16 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya juu *Interchange* katika makutano ya Ubungo umekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Zabuni kwa ajili ya ujenzi zilitangazwa tarehe 20 Januari, 2016 na zinatarajiwa kufunguliwa Juni, 2016. Aidha, ujenzi wa *flyovers* za Chang'ombe na Uhasibu utafanyika katika Awamu ya Pili ya mradi wa ujenzi wa miundombinu wa mabasi yaendayo haraka utakaogharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa *flyovers* katika makutano ya barabara katika maeneo ya Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA na Morocco zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2015/2016 yamo katika ukurasa wa nane hadi ukurasa 45 wa kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya vivuko; kuhusu miradi ya vivuko, hadi kufikia Aprili mwaka huu, kazi zilizokamilika zimeelezwa kwa kina kwenye kitabu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 46 mpaka ukurasa 49.

Mheshimiwa Spika, katika kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha miradi mbalimbali kama ilivyoelezwa kwenye kitabu cha Bajeti kuanzia ukurasa wa 51 mpaka ukurasa wa 53.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha biashara na usafirishaji kati ya bandari ya Dar es Salaam na nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imeamua kupunguza vizuizi barabarani, hivyo magari makubwa yanayosafiri kupitia Ukanda wa Kati yanapima uzito katika vituo vitatu tu vya mizani ambavyo ni Vigwaza-Pwani, Njuki-Singida na Nyakahura-Kagera. Vilevile, magari makubwa yanayosafiri kwenda nchi jirani za Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za SADC kupitia Ukanda wa Dar es Salaam yaani barabara ya Dar es Salaam-Tunduma na Uyole-Kasumulu yanapima uzito katika vituo vinne tu vya mizani ambavyo ni Vigwaza-Pwani, Mikumi-Morogoro, Makambako-Njombe na Mpemba-Songwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu utendaji wa taasisi zilizo chini ya sekta ya ujenzi yameoneshwa kwa kina katika Kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 53 hadi 63.

Sekta ya uchukuzi; katika mwaka 2015/2016, sekta ya uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 389.437. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 276.032 ni fedha za maendeleo na shilingi bilioni 113.404 ni fedha za matumizi ya kawaida. Hadi Aprili mwaka huu, fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni 147.043, sawa na asilimia 53 zilikuwa zimetolewa na fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 63.464 sawa na asilimia 56 zilikuwa zimetolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016; udhibiti wa huduma za usafiri wa mijini na uchukuzi kwa njia ya barabara, msongamano wa magari katika usafiri kwenye majiji na baadhi ya miji umeendelea kuwa changamoto. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeiagiza SUMATRA ifanye utafiti kuhusu vyanzo, madhara na namna bora ya kukabiliana na msongamano wa magari katika miji na majiji nchini.

Mheshimiwa Spika, Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti huo katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza ataanza kazi mwaka wa fedha 2016/2017. SUMATRA imeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri kwa nchi nzima na kutoa elimu ya usalama kwa umma ili kupunguza wimbi la ajali na vifo vitokanavyo na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, usafiri na uchukuzi kwa njia ya reli; Kampuni hodhi ya Rasilimali ya Reli RAHCO. Sekta ya uchukuzi kupitia RAHCO imeendelea utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa njia za reli ya kati na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa miradi ya reli ya sehemu mbalimbali hapa nchini kwa kiwango cha *standard gauge*. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 69 hadi 75.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Reli Tanzania; Kampuni ya Reli kwa sasa ina vichwa vya treni 25 ikilinganishwa na vichwa 14 vilivyokuwepo mwaka 2014/2015. Mabehewa ya mizigo yameongezeka kutoka mabehewa 530 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 hadi kufikia mabehewa 704 mwaka 2015/2016. TRL inaendelea na utaratibu wa kuunda upya vichwa vya treni na kufikia Aprili, 2016 jumla ya uundaji wa vichwa vya treni vinne umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia TAZARA; Serikali za Tanzania na Zambia zimeendelea na juhudi za uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu na huduma za reli ya TAZARA kupitia Itifaki ya 15. Miradi iliyotekelezwa na kukamilika kupitia Itifaki hii imeelezwa kwa kina kwenye cha kitabu cha hotuba yangu ya bajeti kuanzia ukurasa wa 75 hadi 77.

Mheshimiwa Spika, usafiri na uchukuzi majini; huduma za uchukuzi katika Ziwa. Katika mwaka 2015/2016, huduma za uchukuzi katika ziwa zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) pamoja na sekta binafsi. Katika kipindi hicho, MSCL iliendelea kukabiliwa na tatizo la ubovu

wa meli za MV Victoria, MV Liemba, MV Songea na MV Clarias. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa meli hizo.

Mheshimiwa Spika, huduma za bandari; katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Mamlaka ya Bandari ilihudumia jumla ya tani milioni 11.73 za shehena ikilinganishwa na tani milioni 12.28 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, kitengo cha makasha kilihudumia makasha 355,730 ikilinganishwa na makasha 344,517 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Maelezo ya kina kuhusu utendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 79 hadi 88.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuanza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo yanaendelea vizuri chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Vipengele vya Mikataba ya mradi baina ya Serikali na Wawekezaji vilisainiwa tarehe 16 Oktoba, 2015. Aidha, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa bandari hii wapatao 2,211 wa Vijiji vya Pande na Mlingotini ikiwa ni pamoja na sehemu ya Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi cha Mbegani lilianza Septemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga; Udhhibiti wa usalama wa usafiri wa anga. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea kusimamia uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini ili viendeele kukidhi matakwa ya viwango vya Kimataifa. Aidha, viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Abedi Amani Karume na Kilimanjaro vilikaguliwa tena na kupewa vyeti vya ubora baada ya kukidhi vigezo vya Kimataifa vya viwanja vya ndege vya kuweza kupokea ndege kubwa.

Mheshimiwa Spika, huduma za viwanja vya ndege; Wizara kupitia mamlaka inaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Kwa sasa mradi huu umekamilika kwa asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2016. Awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere itaongeza uwezo wa jengo kuhudumia abiria hadi milioni sita kwa mwaka. Ujenzi wa awamu ya pili unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA), Mwanza, Songwe, Bukoba na maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege kumi na moja (11) vya Lake Manyara, Musoma, Iringa, Tanga, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe, Simiyu na Singida kwa kiwango cha lami yanapatikana katika Kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 95 hadi 100.

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri wa ndege; Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, ATCL ilitoa huduma ya usafiri wa anga kati ya Dar es Salaam na Mwanza, Mtwara, Kigoma na Moroni - Comoro kwa kutumia ndege yake aina ya *Dash 8-Q300* na ndege ya kukodi aina ya *CRJ 200*. Katika kipindi hicho, ATCL ilisafirisha abiria 32,434 ikilinganishwa na abiria 30,246 waliosafirishwa mwaka wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, huduma za hali ya hewa; katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ilikamilisha kazi ya uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na uchambuzi wa *data* za hali ya hewa katika Kituo Kikuu cha Taifa cha Utabiri pamoja na vituo vilivyo katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Zanzibar, Mwanza na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano, bajeti ya matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, sekta ya mawasiliano ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 43.195 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili mwaka huu shilingi bilioni 29.081 zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016; katika mwaka wa fedha 2015/2016, sekta ya mawasiliano ilitengewa shilingi bilioni 15.798 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 2.766. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni mbili ni fedha za ndani na shilingi milioni 766.062 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya mawasiliano; Sekta ya mawasiliano imekua kwa kasi kubwa ambapo ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano. Mafanikio ya sekta yameelezwa kwa kina kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 105 mpaka ukurasa wa 107.

Ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano; sekta ya mawasiliano inasimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano awamu ya II, III na IV. Awamu ya III sehemu ya kwanza inajumuisha ujenzi wa kituo mahiri cha kutunzia kumbukumbu *Internet Data Centre* kilichopo Dar es Salaam, miundombinu ya mtandao wa itifaki na uunganishaji wa Zanzibar katika mkongo wa Taifa wa mawasiliano na utekelezaji wake umekamilika mwezi Aprili mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Nne inayohusu ujenzi wa mikongo ya mijini (*Metro Fibre Rings Networks*) na *Missing Links* ya mkongo wa Taifa imeanza na inatekelezwa kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano nchini. Jumla ya Dola milioni 80 zitatumika katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Kampuni ya VIETTEL ya Vietnam inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano vijijini. Hadi Aprili, mwaka huu 2016 kazi zifuatazo zimetetekezwa:-

- (i) Kukamilisha ujenzi wa kilometa 18,000 za Mkongo katika Wilaya zote Tanzania;
- (ii) Ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano katika vijiji 2,208;
- (iii) Kuendelea kuunganisha kwenye mkongo Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya, Hospitali za Wilaya, Ofisi 65 za Posta na Ofisi zote za Polisi za Wilaya nchini; na
- (iv) Kuzipatia intaneti Shule za Sekondari 431 za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa anwani za makazi na misimbo ya Posta ili kuboresha shughuli za kijamii na kiuchumi. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa mpango wa anwani za makazi na misimbo ya Posta yanapatikana katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 111 mpaka 112.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanakua hasa katika ofisi za Serikali, Sekta ya Mawasiliano imekamilisha ufungaji na usimikaji wa mitambo ya *Video Conference* ambayo tayari imeanza kutumika kwenye Makao Makuu ya Mikoa 22 ya Tanzania Bara, Ofisi tatu za Serikali Kuu na Ofisi tano za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano umeoneshwa kwenye ukurasa 116 hadi 123 wa Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na mikakati ya kukabiliana nazo zimeoneshwa kwenye ukurasa 142 hadi 146 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Fungu 98 – Ujenzi, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni shilingi bilioni 38.936. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 34.287 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 1.649 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2016/2017, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.176 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.248 ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi bilioni 344.838 ni fedha za nje. Aidha, shilingi bilioni 582.644 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara. Mgawanyo huo umeonesha kwenye kiambatanisho Na.1 katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Maelezo kuhusu miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya vivuko imetengewa Shilingi bilioni 15.50 kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatanisho Na.1.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya shilingi milioni saba zimetengwa kwa ajili ya miradi ya nyumba na majengo ya Serikali kama ilivyooneshwa kwenye ukurasa wa 148 mpaka 151 wa kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya shilingi trilioni 1.569 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuu zenye urefu wa kilometa 592 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja 14 pamoja na ukarabati wa kilometa 146.5 kwa kiwango cha lami. Aidha, shilingi bilioni 30 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za mikoa zenye urefu wa kilometa 63.8 pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa kilometa 712.40. Orodha ya miradi ya barabara za mikoa inayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2016/2017, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri waliokamilisha miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inayoendelea kutekelezwa, iliyotengewa fedha ambayo baadhi yake inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni pamoja na barabara za Kyaka - Bugene kilometa 59.1; Nondo - Urambo kilometa 52; Tabora - Nyahua kilometa 85; Dodoma - Babati kilometa 251.4; Tunduru - Mangaka - Mtambaswala kilometa 202.5; Tunduru - Matemanga - Kilimaseera - Namtumbo kilometa 193; Sumbawanga - Kanazi - Kizi - Kibaoni kilometa 151.6; Sumbawanga - Matai - Kasanga Port kilometa 111; KIA - Mererani kilometa 26; Uyovu - Bwanga - Biharamulo kilometa 112.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni Arusha - Moshi - Holili sehemu ya Sakina - Tengeru kilometa 14.1 na Arusha Bypass: kilometa 42.4; Nyakanazi - Kibondo kilometa 50; Kidahwe - Kasulu kilometa 50; Makutano - Natta - Mugumu kilometa 125; Nansio - Kisoriya - Bunda sehemu ya Bulamba - Kisoriya, kilometa

51; Tabora – Sikonge sehemu ya Tabora - Usesula, kilometa 30; Kikusya - Ipinda - Matema Beach sehemu ya Tenende - Matema km 34.6; Kaliua - Kazilambwa kilometa 56; Igawa - Mbarali - Ubaruku sehemu ya Mbarali - Ubaruku kilometa 8.9 na Magole - Turiani kilometa 48.8.

Mheshimiwa Spika, aidha, madaraja makubwa yatakayoendelea kujengwa na kukamilika kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni pamoja na daraja la Kilombero Morogoro, daraja jipya la Ruvu Chini Pwani, daraja la Sibiti Singida na daraja la Kavuu huko Katavi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itanza kutekeleza miradi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara zifuatazo:-

Tabora - Usesula - Ipole - Koga - Mpanda kilometa 343; Chaya - Nyahua kilometa 85.5; Uvinza - Malagarasi kilometa 51.1; Kazilambwa - Changu kilometa 40; Urambo - Kaliua kilometa 28; Mbinga - Mbamba Bay kilometa 66; Masasi - Newala - Mtwara sehemu ya Mtwara - Mnivata kilometa 50; Njombe - Ndulamo - Makete kilometa 109; barabara ya mchepuo wa Iringa kilometa 7.3; Mpanda - Mishamo sehemu ya Mpanda – Usimbili, kilometa 30; Chunya - Makongolosi kilometa 43; Makongolosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa sehemu ya Itigi - Mkiwa, kilometa 35; Sanya Juu - Kamwanga sehemu ya Sanya Juu – Elerai, kilometa 32.2; Loliondo - Mto wa Mbu, sehemu ya Wasso Loliondo - Sale Junction, kilometa 50; Njombe - Lupembe - Madeke kilometa 50; Tengeru - Holili kilometa 105; Rujewa - Madibira - Mafinga kilometa 152 na Itoni - Ludewa - Manda sehemu ya Lusitu – Mawenge, kilometa 50. Madaraja yatakayoanza kujengwa ni pamoja na daraja la Mombo; Rukwa, Songea; daraja la Ruhuhu Ruvuma, Njombe, daraja la Simiyu, Mwanza na daraja la Mara huko Mara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara itakamilisha upembuzi yakinifu wa barabara ya Dar es Salaam - Chalinze - Morogoro kilometa 200 sehemu ya Dar es Salaam - Chalinze kilometa 128 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha Expressway. Aidha, Wizara itanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za Same - Kisiwani - Mkomazi kilometa 96.7; Arusha – Kibaya - Kongwa kilometa 430; Tarime - Mugumu kilometa 86; Nanganga - Ruangwa - Nachingwea kilometa 100; Uyole - Mbalizi Songwe Bypass - kilometa 40; Isyonje - Kibondo - Makete kilometa 96.2; Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa kilometa 386; Kibada - Mwasonga - Kimbiji kilometa 19.2; Kimbiji - Tundwisongani kilometa 30.5; Tegeta-Bagamoyo km 43.2; Makofia - Mlandizi kilometa 36.7; Mbegani - Bagamoyo kilometa 7.2; Kibondo - Mabamba kilometa 45; Nyamirembe Port - Katoke kilometa 50 pamoja na daraja linalounganisha Kigongo na Busisi na daraja la Muhimbili litakalounganisha eneo la Muhimbili na Mkwajuni huko Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imetenga fedha kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ni ujenzi wa barabara za Kawawa *roundabout* - Msimbazi Valley – Jangwani - *Twiga Junction* kilometa 2.7; Tabata Dampo - Kigogo kilometa 1.6; Kimara - Kilungule - *External* kilometa 9.0; Mbezi - Malambamawili - Kinyerezi - Banana kilometa 14.0; Tegeta - Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi kilometa 20; sehemu ya Goba - Mbezi Mwisho kilometa saba; Tangi Bovu - Goba kilometa 9.0; Kimara Baruti - Msewe - Changanyikeni kilometa 2.60 pamoja na *Flyover* ya TAZARA.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazotarajiwa kuanza ni ujenzi wa *interchange* ya Ubungo, maandalizi ya ujenzi wa daraja jipya la Selander, maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili itakayohusisha barabara za Kilwa, Chang'ombe na ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu, upanuzi wa daraja la Mlalakuwa na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara ya Mwenge - Tegeta kilometa 12.9.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ni upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki, ujenzi wa barabara za Banana - Kitunda - Kivule – Msongala, sehemu ya Kitunda - Moshi Bar, kilometa 3.2; Ardhi - Makongo sehemu ya Goba - Makongo - kilometa 4.0; Maji Chumvi - Chang'ombe - Barakuda kilometa 2.5; Mjimwema - Vijibweni, Tungi - Kibada na Kibada - Mjimwema pamoja na kuanza ujenzi wa mizani ya kupima magari karibu na Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu utakaohusisha barabara ya Nyerere kuanzia Gongo la Mboto hadi katikati ya Jiji. Barabara ya Uhuru, barabara ya Bibi Titi Mohamed na Azikiwe zenye jumla ya kilometa 23.6. Mradi huu unatarajiwa kugharamiwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, yameoneshwa katika ukurasa wa 153 hadi 175 katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 832.349 zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake zimetengewa shilingi bilioni 582.644 na Ofisi ya Rais , TAMISEMI imetengewa shilingi bilioni 249.704.

Mheshimiwa Spika, kati ya shilingi bilioni 582.644 zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Sekta ya Ujenzi imetengewa shilingi bilioni 57.763 kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa katika kiambatanisho Na. 3 cha Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Aidha, miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika kiambatanisho Na. 4 cha kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara wametengewa shilingi bilioni 519.87 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya kilometa 4,749 na matengenezo ya madaraja 2,821. Muhtasari wa mpango wa matengenezo ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara umeoneshwa katika kiambatanisho Na. 5 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji kazi katika taasisi zilizochini ya Sekta ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2016/2017 yametolewa katika hotuba ya bajeti ya Wizara kuanzia ukurasa 176 hadi 187.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Sekta ya Uchukuzi Fungu 68 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, ni shilingi bilioni 91.519. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 52.430 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 39.088 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Sekta Uchukuzi na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.495 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.322 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 173.21 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi imepanga kutekeleza miradi ifuatayo:-

Kwanza, kutandika reli nzito za ratili 80 katika maeneo mbalimbali ya reli ya kati; Kujenga madaraja, makalavati na ujenzi wa stesheni na jengo la kuhifadhia mizigo; Kuboresha eneo la treni la kupakia na kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, Isaka na Ilala; Kununua vipuri vya mtambo wa kuzalisha kokoto wa Tura; na Ununuzi wa mtambo wa kukagua na kupima njia ya reli na uzalishaji wa mataruma katika karakana ya Pugu. Shilingi bilioni 202.89 zimetengwa.

Pili, kukamilishi usanifu wa kina, upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa miradi ya reli katika maeneo mbalimbali nchini kwa kiwango cha *standard gauge* ambapo shilingi bilioni 19.7 zimetengwa. Shilingi bilioni 5.0 zimetengwa kwa ajili ya kumwajiri mshauri wa uwezesaji atakayesimamia upatikanaji wa fedha pamoja na ujenzi wa reli ya Mtwara - Songea - Mbamba Bay pamoja na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga na kufanya usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge* ambapo umepangiwa shilingi trilioni moja. Kufanya usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge* ambao umepangiwa shilingi trilioni moja. Maelezo ya kina ya miradi hii yanapatikana kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 185 hadi 190.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi imetenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora, Songwe, Mwanza, Mtwara, Sumbawanga na Shinyanga na Mkoa wa Geita, Msalato, Bukoba na Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ndege ATCL imetengewa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kununua ndege mpya zisizopungua tatu. Mgawanyo wa fedha za bajeti za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Sekta ya Uchukuzi umeoneshwa katika kiambatanishi Na. 6 cha kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni shilingi bilioni 3.073. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.161 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi milioni 912.326 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano imetengewa jumla ya shilingi bilioni 92.730 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni tano ni fedha za ndani na shilingi bilioni 87.73 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imepangiwa kutekeleza mpango wa muda wa kati na muda mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo mbalimbali ambayo yameorodhesha kwenye kitabu changu cha Bajeti kuanzia ukurasa 198 hadi ukurasa 200.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa utekelezaji katika taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017, umeainishwa katika kitabu cha bajeti kuanzia ukurasa 200 mpaka 205.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kuzishukuru nchi rafiki na washirika mbalimbali wa maendeleo walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu mbalimbali katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nchi hizo na washirika wa maendeleo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Japan, Korea Kusini, Finland, Abu Dhabi Fund, Denmark, Ujerumani, Marekani, Uingereza, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Shirika la Maendeleo la Marekani, Kuwait Fund, OPEC Fund, BADEA, Shirika la Bahari Duniani, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga, Shirika la Hali ya Hewa Duniani, UNESCO, Jukwaa la Uchumi Duniani, Malaysia, Afrika Kusini, Uholanzi, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, TMEA, India, China, Norway, Belgium, Urusi, Sweden, Ufaransa, Singapore, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani SADC na wengine wengineo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, nikianza na Mheshimiwa Engineer Ngonyani - Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Engineer Joseph Nyamhanga - Katibu Mkuu; Dkt. Leonard Chamuriho - Katibu Mkuu Uchukuzi, Profesa Faustine Kamuzoro, Katibu Mkuu wa Mawasiliano; Engineer Dkt. Maria Sasabo - Naibu Katibu Mkuu Mawasiliano; Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara, Viongozi wa Taasisi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kujituma katika kutekeleza majukumu yao tuliyopewa na Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari ambavyo wametupa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa muhimu, napenda kuishukuru familia yangu hususan mke wangu na watoto wangu kwa kunifariji na kuniombea wakati nikitokeleza majukumu yangu Kitaifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu hii inapatikana katika tovuti za Sekta ya Ujenzi www.mow.go.tz, Sekta ya Uchukuzi www.uchukuzi.go.tz na Sekta ya Mawasiliano www.mst.go.tz.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla sh. 4,895,279,317,500/= . Kati ya fedha hizo, sh. 2,212,141,496,500/= ni kwa ajili ya Fungu 98 - Ujenzi. Sh. 2,587,333,762,000/= ni kwa ajili ya Fungu 62 - Uchukuzi na sh. 95,804,059,000 ni kwa ajili ya Fungu 68 - Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha miradi ya Wizara inayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kuanzia kiambatanisho Na.1 mpaka Na. 7 saba, ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatanisho hivi vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki!

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri kabisa iliyopangwa vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHESHIMIWA PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika mkutano huu ambao ni wa kwanza wa bajeti tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Tano.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kwa heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2015. Kwa kipindi kifupi dlichokaa madarakani, Watanzania kwa ujumla wetu tumefarijika na uongozi wake mahiri ambao unaonesha nia ya dhati ya kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa kasi inayotakiwa. Ninaungana na Watanzania kumuomba afya njema ili aweze kuikamilisha kazi hii kubwa aliyoianza.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kunipa dhamana ya kuongoza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu kuwa sitawaangusha.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ninampongeza pia Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb.), kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuchaguliwa kuiongoza Bunge letu Tukufu. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwao kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. Nina imani kwamba sote tutatekeleza kazi zetu za kuwatumikia wananchi kufuatana na kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya **Hapa Kazi Tu** ili tufikie malengo yetu ya kujikwamua kiuchumi.

6. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda pia kuwapongeza Mwenyekiti, Prof. Norman Sigalla King na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kuteuliwa kwao. Ninaishukuru Kamati hii kwa maelekezo, ushirikiano na ushauri iliyotupatia ambao umeboresha matayarisho ya bajeti hii ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

B. MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliundwa Novemba, 2015 baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. Wizara hii inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nitaeleza kwa kifupi majukumu ya kila sekta.

8. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi ina majukumu ya kusimamia Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003) na utekelezaji wake pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009) na utekelezaji wake; ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi; usimamizi wa masuala ya mazingira katika Sekta; uboreshaji utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Sekta na usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Sekta.

9. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, majukumu ni pamoja na kusimamia Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003) na utekelezaji wake; Ujenzi na uendelezaji wa Miundombinu ya Uchukuzi; Usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli na bandari; usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga na viwanja vya ndege (vikubwa na vidogo); Utoaji wa leseni za usafirishaji; Usalama katika usafirishaji na Hali ya Hewa; kuendeleza rasilimali watu na kusimamia Taasisi, Mashirika ya Umma na miradi iliyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

10. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano ina majukumu ya kusimamia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003; Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997; na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003 na utekelezaji wake. Aidha, Sekta ya Mawasiliano ina dhamana ya kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vinachangia katika maendeleo ya nchi yetu, pamoja na usimamizi wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano.

11. Mheshimiwa Spika, kuunganishwa kwa sekta hizi tatu kuwa chini ya Wizara moja kunatarajiwa kuwajengea Watanzania miundombinu bora na ya kisasa ili kutoa huduma zenye tija na ufanisi kwa haraka zaidi kwa kuwa majukumu ya sekta hizi yana uhusiano mkubwa. Niwaahidi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuwa kwa kushirikiana na wenzangu katika Wizara hii tutahakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi mkubwa ili kutuwezesha kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuifanya nchi yetu ifikie uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

12. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Mpango na Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mtiririko wa kisékta nikianzia na Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na hatimaye Sekta ya Mawasiliano.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2015/2016

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, Malengo ya MKUKUTA II, Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera nyinginezo za Kisekta, Kitaifa na Kimataifa.

C.1 SEKTA YA UJENZI Ukusanyaji wa Mapato

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Ujenzi ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 47,765,000** kupitia Idara zenye vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Utawala, Huduma za Ufundi na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi. Hadi Aprili, 2016, jumla ya **Shilingi 49,716,600** zilikuwa zimekusanywa.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

15. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 40,023,770,336** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 36,778,993,000** ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 3,244,777,336** ni Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2016 **Shilingi 29,934,578,171** zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 28,506,146,348** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 1,428,431,823** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 883,832,338,500** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 191,619,568,500** na **Shilingi 85,572,770,000** zilikuwa fedha za nje. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara zilitengwa **Shilingi 606,640,000,000**.

Hadi Aprili, 2016 fedha zilizotolewa ni **Shilingi 1,080,804,942,594**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 607,350,007,730** nifedhazandanikutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 149,502,934,864** ni fedha za nje na **Shilingi 323,952,000,000** ni fedha

za Mfuko wa Barabara. Sehemu kubwa ya fedha za ndani zilizotolewa imetumika kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara.

Utekelezaji wa Miradi ya Barabara na Madaraja

17. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) inasimamia mtandao wa barabara kuu na za mikoa wenye urefu wa **kilometa 35,000**. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilipanga kusimamia kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya mtandao huo wa barabara. Hadi kufikia Aprili, 2016, jumla ya **kilometa 414.3** za barabara kuu zilikuwa zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami, sawa na **asilimia 79** ya lengo la **kilometa 523** kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, **kilometa 82.4** za ukarabati wa barabara kuu kwa kiwango cha lami zilikuwa zimekamilika ambazo ni sawa na **asilimia 73** ya lengo la **kilometa 113** kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya **kilometa 52.19** zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami, sawa na **asilimia 68** ya lengo la **kilometa 77** kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Vilevile, jumla ya **kilometa 676** za barabara za mikoa zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe, sawa na **asilimia 54** ya malengo ya **kilometa 1,252** ya mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, Serikali imeendelea na ujenzi wa madaraja makubwa **11** ambapo madaraja ya Nyerere (Kigamboni) na Lukuledi II yamekamilika.

18. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matengenezo ya barabara, matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa yalikusha matengenezo ya kawaida (*routine and recurrent maintenance*) **kilometa 31,883**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi **kilometa 6,096** na matengenezo ya madaraja **3,332**. Hadi Aprili, 2016, utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya barabara ulikuwa umefikia **asilimia 47** ya malengo ya mwaka wa fedha 2015/16. Katika barabara kuu, jumla ya **kilometa 5,968.5** na madaraja **772** yalifanyiwa matengenezo. Kwa upande wa barabara za mikoa jumla ya **kilometa 12,777** na madaraja **648** yalifanyiwa matengenezo. Aidha, sehemu kubwa ya kazi za matengenezo ya barabara itafanyika katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2015/2016 baada ya mvua zinazoendelea kunyesha nchini kote kumalizika katika maeneo mengi nchini.

19. Mheshimiwa Spika, kazi ya kudhibiti uzito wa magari katika mwaka wa fedha 2015/2016 iliendelea kwa kutumia mizani **38** za kudumu na **22** zinazohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi Aprili, 2016 magari 2,594,485 yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo 676,006 sawa na asilimia 26 yalikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya fedha iliyokusanywa kutokana na tozo

ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida ilikuwa ni Shilingi 3,876,955,111. Aidha, ili kurahisisha biashara na usafirishaji kati ya bandari ya Dar es Salaam na nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imeanza kupunguza vizuizi barabarani hivyo magari makubwa yanayosafiri kupitia ukanda wa Kati (Central Corridor) yanapima uzito katika vituo vitatu tu vya mizani ambavyo ni Vigwaza (Pwani), Njuki (Singida) na Nyakahura (Kagera). Vilevile, magari makubwa yanayosafiri kwenda nchi jirani za Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia Ukanda wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Corridor) yaani barabara ya Dar es Salaam – Tunduma na Uyole – Kasumulu yanapimwa uzito katika vituo vinne tu vya mizani ambavyo ni Vigwaza (Pwani), Mikumi (Morogoro), Makambako (Njombe) na Mpemba (Songwe).

20. Mheshimiwa Spika, barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200)** sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 128) imepangwa kujengwa kwa kiwango cha “Expressway”. Mradi huu utatekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP*). Barabara hiyo itaanzia Mbagala Charambe kupitia Kisarawe, Kibamba, Kibaha, Mlandizi hadi Chalinze. Aidha, barabara hiyo itaunganishwa na bandari ya Dar es Salaam kupitia Kibada, Kigamboni. Hadi Aprili, 2016, Mshauri Mwelekezi alikuwa amewasilisha taarifa ya kitaalam kuhusu gharama za awali za ujenzi na njia mbadala za tozo kwa watumiaji wa barabara zitakazotumika ili kuwawezesha wawekezaji kwenye mradi kurudisha gharama zao na kupata faida kulingana na kipindi cha uendeshaji wa mradi. Kazi ya upembuzi yakinifu na utayarishaji wa Nyaraka za zabuni inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mei, 2016.

21. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa **barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Makofia – Msata (km 108)** kwa sehemu ya Bagamoyo – Msata (km 64) imekamilika. Aidha, ujenzi wa Daraja la Ruvu Chini pamoja na tuta la barabara lenye urefu wa km 4.16 unaendelea.

22. Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu wa kina wa barabara ya **Bagamoyo – Saadani – Tanga (km 178)** imekamilika na taratibu za kupata fedha za ujenzi kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Washirika wengine wa Maendeleo zinaendelea chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

23. Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa** (km 422) umegawanywa katika awamu tatu na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

Kyamyorwa – Buzirayombo (km 120)

Kazi za ujenzi wa barabara hii zilikamilika Februari, 2008. Hata hivyo, kutokana na mashimo kujitokeza mapema katika baadhi ya maeneo ya barabara hii mradi haukupokelewa na Serikali na Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii aliagizwa kurudia ujenzi wa sehemu zilizoharibika kwa gharama zake mwenyewe. Kazi za ujenzi zinaendelea.

Usagara – Geita (km 90) (Lot 1 na Lot 2) Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili: Geita-Sengerema (km 50) na Sengerema- Usagara (km 40). Kazi za ujenzi wa barabara hizi zimekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Uyovu – Bwanga - Biharamulo (km 112)

Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea. Hadi kufikia Aprili, 2016, ujenzi wa sehemu ya Uyovu – Bwanga (km 45) na sehemu ya Bwanga – Biharamulo (km 67) ulikuwa unaendelea.

24. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 504.7)** utekelezaji wake ni kama ifuatavyo: — Ujenzi wa barabara za **Uvinza – Kidahwe (km 76.6), Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi na Barabara Unganishi (km 48)** na **Tabora – Ndono (km 42)** umekamilika. Kwa sehemu ya **Ndono – Urambo (km 52)** utekelezaji umefikia asilimia 87 ambapo ujenzi wa kilometa 42 za lami umekamilika na kwa **Kaliua – Kazilambwa (km 56)** kazi za ujenzi zimefikia asilimia 63 ambapo kilometa 42 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za **Uvinza – Malagarasi (km 51.1), Kazilambwa – Chagu (km 40) na Urambo – Kaliua (km 33)** umekamilika na kazi za ujenzi zitaanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

25. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga na Bomang’ombe – Sanya Juu** (km 173), ujenzi umekamilika katika sehemu za Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32); Tarakea – Rombo Mkuu (km 32) na Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32). Aidha, kwa sehemu ya Bomang’ombe – Sanya Juu – Kamwanga (km 100), hadi kufikia Aprili, 2016 majadiliano ya kimkataba na Mkandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya

Sanya Juu–Alerai (km 32.2) yalikuwa yamekamilika. Utiaji saini wa mkataba utatekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

26. Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga kwa kiwango cha lami kwa njia nne barabara ya **Arusha – Moshi – Holili pamoja na Arusha Bypass (km 140)**, mkataba wa ujenzi umesainiwa Februari, 2015 kwa sehemu ya Sakina – Tengeru, km 14.10 na barabara ya mchepuo ya Arusha (Arusha Bypass), km 42.41 na Mkandarasi anaendelea na kazi. Uzinduzi wa ujenzi wa mradi huu ulifanywa na Marais wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 03/03/2016. Serikali ya Japan imekubali kugharamia ukarabati na upanuzi wa sehemu iliyobaki ya Tengeru – Holili na barabara ya kwenda KIA.

27. Mheshimiwa Spika, mkataba wa awali wa ujenzi wa barabara ya **KIA – Mererani (km26)** ulisitishwa Februari, 2014 kutokana na Mkandarasi kukiuka matakwa ya mkataba. Mkataba mpya wa ujenzi umesainiwa Februari, 2015. Hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi zilikuwa zinaendelea.

28. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa barabara ya **Kwa Sadala – Masama (km 12.5)** ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2016 km 9.5 za tabaka la lami zimekamilika na km 3 zilizobaki zinatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2016. Aidha, usanifu wa kina wa kilometa 3.5 kwa sehemu ya Masama – Machame Jct unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016. Kazi za ujenzi wa sehemu hii zinatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

29. Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina wa mradi wa barabara ya **Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)** umekamilika Januari, 2016. Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami inatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2016/2017.

30. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95)** ulikamilika mwaka 2008. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

31. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni (km 127)** ulikamilika Novemba, 2009. Aidha, mradi huu unahusisha kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini (km 4.8) pamoja na ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Muhalala (Manyoni) – “One Stop Inspection Station” (OSIS). Hadi Aprili, 2016, ujenzi barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini ulikuwa unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa OSIS ya Manyoni yako katika hatua ya usanifu wa kina.

32. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Mbwemkuru – Mingoyo (km 95) ulikamilika Desemba, 2007. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

33. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nelson Mandela** (km 15.6) ulikamilika 30 Juni, 2011. Maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Dar Port hadi TAZARA (km 6.0) yanasubiri upatikanaji wa fedha.

34. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Dumila – Kilosa** (km 63), kazi za ujenzi zimekamilika Desemba, 2013 kwa sehemu ya **Dumila – Rudewa (km 45)**. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi. Aidha, kwa sehemu ya **Rudewa – Kilosa (km 18)** ujenzi kwa kiwango cha lami haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha.

35. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port** (km 112), hadi kufikia Aprili, 2016, maendeleo ya mradi huu kwa ujumla ni asilimia 53 ambapo kilometa 56 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Matai – Kasesya (km 50) umekamilika.

36. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ujenzi wa madaraja makubwa hadi kufikia Aprili, 2016 ni kama ifuatavyo:-

(i) Daraja la Kirumi kwenye barabara ya Makutano – Sirari.

Uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalam wa kuchunguza hali ya cables na kupendekeza jinsi ya kuzifanyia ukarabati umekamilika. Kazi imeanza Machi, 2016 na itakamilika Septemba, 2016.

(ii) Daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru.

Ujenzi umekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

(iii) Daraja la Sibiti na Barabarazake kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti.

Ujenzi ulisimama kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo, kazi za ujenzi zimeanza kutekelezwa Aprili, 2016 baada ya Serikali kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa mradi huu.

(iv) Daraja la Maligisu kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi – Maligisu.

Ujenzi umekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

- (v) **Daraja la Mto Kilombero na Barabara zake** kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge. Ujenzi ulisimama kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo, kazi za ujenzi zimeanza kutekelezwa Aprili, 2016 baada ya Serikali kulipa sehemu kubwa ya madai ya Mkandarasi wa mradi huu.
- (vi) **Daraja la Kavuu** kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga. Hadi Aprili, 2016, ujenzi wa msingi na nguzo za daraja ulikuwa unaendelea.
- (vii) **Daraja la Mbutu** kwenye barabara ya Igunga – Manonga. Ujenzi wa daraja umekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na ujenzi wa kilometa 3 kwa kiwango cha lami.
- (viii) **Ununuzi wa Mabey Compact Emergency Bridge Parts na Crane Lorry**
Ununuzi wa Mabey Compact Emergency Bridge Parts upo katika hatua za maandalizi.
- (ix) **Daraja la Ruhekei** kwenye barabara ya Mbinga – Mbamba Bay. Ujenzi umekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.
- (x) **Daraja la Ruhuhu** kwenye barabara ya Kitai - Lituhi. Mkataba wa ujenzi wa Daraja la Ruhuhu ulisainiwa mwezi Mei, 2016.
- (xi) **Daraja la Momba** katika barabara ya Sitalike - Kibaoni – Kilyamatundu/ Kamsamba – Mlowo. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Momba imetangazwa na ujenzi umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.
- (xii) **Daraja la Lukuledi II** kwenye barabara Matama – Kitangali – Newala. Kazi za ujenzi wa daraja hili zimekamilika Januari, 2016.
- (xiii) **Daraja la Sukuma** katika barabara ya Magu- Kabila - Mahaha. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa daraja hili zinaendelea.
- (xiv) **Daraja Jipya la Wami** kwenye barabara ya Chalinze – Segera. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Ujenzi wa Daraja Jipya la Wami unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

(xv) **Darajala Simiyu** kwenye barabara ya Mwanza – Musoma.

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

37. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **New Bagamoyo (Kawawa JCT – Tegeta)** unahusu ukarabati na upanuzi wa barabara hii yenye urefu wa kilometa 17.2 kwa kiwango cha lami kutoka njia mbili za sasa kuwa njia nne (4 lane dual carriageway) kutoka Morocco (Makutano ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Kawawa) hadi Tegeta Kibaoni. Mradi unatekelezwa kwa awamu mbili: Mwenge – Tegeta (km 12.9) na Morocco – Mwenge (km 4.3). Kazi za ujenzi na upanuzi wa barabara hii katika awamu ya kwanza zilikamilika Julai, 2014 na mradi huu upo katika kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu kinachotarajiwa kumalizika Julai, 2017. Aidha, kazi ya upanuzi wa sehemu ya barabara Mwenge – Morocco toka njia tatu kuwa njia tano zinaendelea na zimepangwa kukamilika mwishoni mwa Mei, 2016.

38. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kyaka – Bugene** (km 59.1) ikijumuisha ujenzi wa daraja la **Mwisa** pamoja na makalavati, hadi kufikia Aprili, 2016 kazi za ujenzi zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 90 ambapo kilometa 50 zilikuwa zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na daraja la Mwisa limekamilika.

39. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Isaka – Lusahunga – Rusumo (km 392)**, hadi Aprili, 2016 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

(i) Sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242)

Ukarabati wa sehemu ya **Isaka – Ushirombo (km 132)** ulikamilika Machi, 2014 na kwa sehemu ya **Ushirombo – Lusahunga (km 110)** kilometa 54 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

(ii) Sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na Nyakasanza – Kobero (km 59)

Kazi za usanifu wa kina zimekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kupitia Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na kazi ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina ili kukidhi viwango vinavyotakiwa na AfDB inaendelea. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali imepanga kuifanyia ukarabati barabara ya Lusahunga – Rusumo wakati inasubiri kufanyiwa ukarabati mkubwa.

40. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Manyoni – Itigi – Tabora** hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

(i) Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)

Kazi ya ujenzi ilikamilika Oktoba, 2015 na kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja kinatarajiwa kukamilika Oktoba, 2016.

(ii) Tabora – Nyahua (km 85)

Hadi Aprili 2016, kazi za ujenzi zilikuwa zimefikia asilimia 90 ambapo kilometa 74 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

(iii) Chaya – Nyahua (km 85.4)

Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika na mapitio ya usanifu wa kina yanaendelea. Serikali ya Kuwait kupitia *Kuwait Fund* imeonyesha nia ya kugharamia ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zinatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo Serikali pia imetenga fedha za ndani kwa ajili ya mradi huu.

41. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Korogwe – Handeni** (km 65) umekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi.

42. Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa barabara ya **Handeni – Mkata** (km 54) zimekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

43. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **barabara za mikoa**, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 ni ukarabati wa jumla ya kilometa **746.5** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **60.3** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **17**. Hadi kufikia Aprili, 2016, kilometa **360** za barabara za mikoa zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe, kilometa **44.14** kwa kiwango cha lami na madaraja **5** yamejengwa.

44. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza**, iliyopangwa kufanyiwa ukarabati wa sehemu zilizoharibika yenye urefu wa kilometa 10, kazi za ukarabati wa sehemu zilizoharibika zinaendelea.

45. Mheshimiwa Spika, **Daraja la Umoja** katika Mto Ruvuma eneo la Mtambaswala/ Negomane limejengwa ili kuunganisha nchi za Tanzania na Msumbiji. Kazi za ujenzi wa daraja zimekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mwisho ya Mkandarasi.

46. Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami, upanuzi na ukarabati wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam ulitekelezwa kama ifuatavyo:

(i) Ubungo Bus Terminal – Mabibo – Kigogo Roundabout (km 6.4)

Kazi ya ujenzi ilikamilika Machi, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

(ii) Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley -Jangwani/ Twiga Jct (km 2.7)

Hadi kufikia Aprili, 2016, maendeleo ya kazi ya ujenzi, upanuzi na ukarabati wa barabara hii yalikuwa asilimia 86 ambapo kilometa 2.3 zimekamilika kwa kiwango cha lami.

(iii) Jet Corner – Vituka – Davis Corner (km 10.30)

Ujenzi, upanuzi na ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami ulikamilika Septemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/16 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

(iv) Tabata Dampo – Kigogo (km 1.60) na Ubungo Maziwa – External (km 0.65)

Hadi kufikia Aprili 2016, kazi za ujenzi zilikuwa zimekamilika kwa sehemu ya Ubungo Maziwa – External (km 0.65). Kwa sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.60) kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 72 ambapo kilometa 1.17 zimekamilika kwa kiwango cha lami.

(v) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure – BRT)

Hadi Aprili, 2016, kazi zilizokamilika ni uhamishaji wa miundombinu ya umeme ili kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara na vituo vya mabasi kwa ajili ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART); ujenzi wa miundombinu ya barabara za Kimara - Kivukoni, Magomeni - Morocco na Fire - Kariakoo zenye urefu wa jumla ya kilometa 20.9; ujenzi wa madaraja matatu (3) ya watembea kwa miguu na vituo vya mabasi 27; ujenzi wa Karakana (Depot) ya Jangwani; ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kivukoni pamoja na ujenzi wa Kituo Kikuu na Kituo Kidogo cha Mabasi eneo la Gereza Kariakoo. Aidha, kazi za ujenzi wa Vituo Vidogo vya Mabasi vya Urafiki, Shekilango, Magomeni Mapipa, Kinondoni, Mwinyijuma na Fire zilikuwa katika hatua za mwisho. Hata hivyo, kwa upande wa ujenzi wa Karakana (Depot), Kituo Kikuu na Kituo Kidogo (Ubungo) na uboreshaji wa Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo mikoani (Ubungo Up-Country Bus Terminal), hakuna kazi iliyofanyika katika mwaka 2015/16 kutokana na kutopatikana eneo la mradi kwa wakati.

(vi) Mbezi (Morogoro Road) – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14)

Hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 76 ambapo kilometa 3 kati ya kilometa 4 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

(vii) TegetaKibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi Mwisho (km 20)

Kazi za ujenzi wa sehemu ya Mbezi Mwisho hadi Goba (km 7) kwa kiwango cha lami inaendelea. Hadi kufikia Aprili, 2016, kazi za ujenzi zilikuwa zimefikia asilimia 83 ambapo kilometa 5.87 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

(viii) Tangi Bovu – Goba (km 9)

Hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi zilifikia asilimia 68 ambapo kilometa 7.10 zilikamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

(ix) Kimara Baruti – Msewe (km 2.6)

Hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi zilikuwa zinaendelea ambapo kilometa 1.0 imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

(x) Kimara – Kilungule – External/Mandela Road (km 9)

Hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi wa sehemu ya kwanza yenye urefu wa km 3.3 zilikuwa zimekamilika.

(xi) Kibamba – Kisopwa (km 12.0)

Hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi wa sehemu ya Kibamba hadi Mloganzila (km 4) zilikuwa zimekamilika.

(xii) Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7)

Hadi Aprili, 2016, mradi wa ujenzi wa barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola ulikuwa upo katika hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

(xiii) Ardhi – Makongo (km 4.0)

Hadi Aprili, 2016, mradi wa ujenzi wa barabara ya Ardhi hadi Makongo ulikuwa upo katika hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

(xiv) Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5)

Hadi Aprili, 2016, mradi wa ujenzi wa barabara ya Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda kwa kiwango cha lami ulikuwa upo katika hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

47. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Ndundu – Somanga (km 60)** umekamilika. Fedha zilizotengwa mwaka 2015/16 ni kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi huu.

48. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396),** hadi Aprili, 2016, kazi za upembuzi yakinifu zilikuwa zimekamilika na kazi za usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

49. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359),** hadi Aprili, 2016, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Tabora – Usesula (km 30)** zilikuwa zinaendelea. Aidha, kwa sehemu ya **Sikonge (Usesula) – Ipole – Koga – Mpanda (km 343)** fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zimepatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na maandalizi ya kutangaza zabuni za ujenzi yanaendelea.

50. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo (km 239) na Loliondo – Mto wa Mbu (km 213),** hadi kufikia Aprili, 2016 ujenzi wa sehemu ya **Makutano – Sanzate (km 50)** ulikuwa uncendelea. Aidha, ujenzi wa barabara ya **Loliondo – Mto wa Mbu** unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/17.

51. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Ibanda – Itungi/Kiwira (km 26),** hadi Aprili, 2016 kazi za ujenzi wa sehemu ya Kajunjumele – Kiwira Port (km 6) zilikuwa zinaendelea

52. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya **Tanga – Horohoro (km 65),** kazi ya ujenzi wa barabara hii ilikamilika Oktoba, 2012. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/16 ni kwa ajili ya kulipa fidia.

53. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya **Nzega – Tabora (km 115),** ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya **Nzega – Puge (km 58.8).** Aidha, kwa sehemu ya **Puge – Tabora (km 56.10)** ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika pamoja na barabara ya mchepuo ya Nzega (Nzega Bypass – km 7).

54. Mheshimiwa Spika, barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi (km 770.9)** inaendelea kujengwa kwa awamu. Mradi huu umegawanyika katika sehemu kuu nne ambapo hadi Aprili, 2016 utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

Sumbawanga – Kanazi (km 75)

Mradi umekamilika kwa asilimia 69, ambapo hadi Aprili, 2016 kilometa 43.47 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6)

Mradi umekamilika kwa asilimia 50.30 ambapo hadi Aprili, 2016 kilometa 23.43 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Sitalike – Mpanda (km 36.9)

Mradi umekamilika kwa asilimia 76, ambapo hadi Aprili, 2016 kilometa 19.50 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mpanda – Uvinza (km 195.4)

Ujenzi wa barabara hii utafanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza itahusisha sehemu ya Mpanda – Usimbili (km 30). Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi zimekamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

55. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nyanguge – Musoma (km 185.5)** unahusisha pia ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo ya Usagara – Kisesa (km 17), barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda (Sehemu ya Bulamba – Kisorya: km 51), barabara ya Nyamuswa – Bunda (km 55) na barabara za Mwanza Mjini kwa kiwango cha lami. Hadi Aprili, 2016 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:–

Mpakani mwa Simiyu/Mara – Musoma (km 85.5)

Ukarabati ulikamilika Novemba, 2014. Fedha zilizotengwa katika mwaka 2015/2016 ni sehemu ya malipo ya Mkandarasi.

Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17) Ujenzi umefikia asilimia 60 na ujenzi wa madaraja madogo manne (4) umekamilika.

Nansio – Kisorya – Bunda (Sehemu ya Bulamba – Kisorya: km 51)

Utekelezaji wa mradi huu unaendelea.

Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55)

Kazi za ujenzi hazikuweza kuanza katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 kutokana na ukosefu wa fedha. Kazi za ujenzi wa barabara hii zinatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

56. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Magole – Mziha (km 83.8)** umegawanyika katika sehemu kuu mbili: Magole –Turiani (km 48.8) ambapo hadi Aprili, 2016, maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 69. Kwa

sehemu ya Turiani – Mziha (km 35), usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

57. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa barabara za juu (flyovers) na maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam, lengo ni kujenga ‘Flyover’ ya TAZARA, “Interchange” ya Ubungo na maboresho ya makutano ya Chang’ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco. Hadi Aprili, 2016 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

(i) Barabara ya Juu (Flyover) ya TAZARA Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 15 Oktoba, 2015 na ujenzi ulizinduliwa tarehe 16 Aprili, 2016. Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

(ii) Barabara ya Juu (Interchange) ya Ubungo Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Zabuni kwa ajili ya ujenzi zilitangazwa tarehe 20 Januari, 2016 na zinatarajiwa kufunguliwa Juni, 2016.

(iii) Maboresho ya Makutano ya barabara katika maeneo ya Chang’ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu na Morocco

Ujenzi wa “flyovers” za Chang’ombe na Uhasibu utafanyika katika Awamu ya Pili ya Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II) chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, ununuzi wa Mhandisi Mshauri wa usanifu wa “flyovers” nyingine unaendelea.

58. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Bariadi – Lamadi (km 71.8)**, hadi Aprili, 2016 barabara hii ilikuwa imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa sehemu ya **Mwigumbi – Maswa (km 50)** Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi.

59. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Ipole – Rungwa (km 172.4)**, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza na inatarajiwa kukamilika Juni, 2017.

60. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310)**, hadi kufikia Aprili, 2016 ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Kidahwe – Kasulu (km 50)** na sehemu ya **Nyakanazi – Kibondo (km 50)** ulikuwa unaendelea. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu wa kina inaendelea kwa sehemu ya **Nyakanazi – Kasulu/Manyovu (km 258)** ambayo

utekelezaji wake unafadhiliwa na AfDB chini ya uratibu wa Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

61. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya kwenda **Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia Airport Access Road - km 14)**, mradi ulikamilika Januari, 2015. Fedha zilizotengwa mwaka 2015/16 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

62. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12)** una lengo la kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2016 utekelezaji wa mradi ulikuwa unaendelea.

63. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni)** (mita 680) na barabara unganishi za kilometa 2.5, hadi kufikia Aprili, 2016 kazi za ujenzi wa Daraja zilikuwa zimekamilika. Daraja lilifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 19 Aprili, 2016. Aidha, ujenzi wa barabara unganishi kutoka daraja la Nyerere (Kigamboni) hadi barabara ya *Ferry – Kibada* (km 1.5) umepangwa kuanza mwishoni mwa Mei, 2016.

64. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ukanda wa Kati** (Central Corridor) una lengo la kuimarisha na kuboresha barabara pamoja na kuongeza usalama kwa watumiaji barabara katika ukanda huo. Hadi Aprili, 2016 taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya utafiti wa maeneo ya kujenga njia hizo zilikuwa zinaendelea. Aidha, kazi za ujenzi zinaendelea kwenye baadhi ya barabara ambazo tayari zimeainishwa kama vile barabara ya Morogoro eneo la Kibamba.

65. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa barabara ya **Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) hadi Pugu (km 8.0)** ni kuipanua barabara hii. Hadi kufikia Aprili 2016, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina wa barabara hii zilikuwa zinaendelea.

66. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusu upanuzi wa sehemu za miinuko. Aidha, mradi unajumuisha **upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**. Kazi za upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha pamoja na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji zinaendelea.

67. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa barabara ya **Kisarawe - Maneromango – Mlandizi (km 119)** ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi Aprili, 2016 upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mlandizi – Mzenga - Maneromango (km 65) ulikuwa katika hatua za mwisho. Aidha, usanifu wa barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54) umekamilika.

68. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa **barabara ya Bandari (km 1.2), barabara ya Dockyard (km 0.7) na barabara ya Mivinjeni (km 1.0)** ni kupanua sehemu ya barabara hizi ili kukidhi mahitaji ya magari makubwa yanayoingia na kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam. Hadi Aprili, 2016 maandalizi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina yanaendelea. Ujenzi wa barabara hizo utafadhiliwa na *TradeMark East Africa* (TMEA) na utasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA).

69. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya pete ya **Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha *Expressway* ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Kazi ya kupitia (review) upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii itanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

70. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa **mizani mpya karibu na bandari ya Dar es Salaam**, unatekelezwa ili madereva wa magari makubwa wapime uzito wa mizigo waliyobeba kabla ya kuanza safari na hivyo kudhibiti uzidishaji wa mizigo kwenye malori. Kazi za usanifu wa kina zimekamilika. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mizani zinaendelea.

71. Mheshimiwa Spika, lengo la kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Tunduma – Sumbawanga (km 223.21)** ni kuboresha miundombinu ya barabara katika Ukanda wa Magharibi. Ujenzi kwa sehemu ya Tunduma - Ikana (km 63.7); Ikana - Laela (64.2) na Laela -Sumbawanga (km 95.31) umekamilika. Kuhusu barabara ya Tunduma – Ikana (eneo la Tunduma mjini - km 1.6) maandalizi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii yamekamilika na mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 4 Aprili, 2016. Aidha, kwa upande wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.20) kazi ya usanifu wa kina imekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

72. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga (km 154)**, ujenzi ulikamilika Desemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

73. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya **Arusha – Namanga (km 105)** ulikamilika Desemba, 2012. Aidha, kazi ya ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (One Stop Border Post - OSBP) imekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

74. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **barabara ya Arusha – Minjingu – Babati – Singida (km 321.5)**, ujenzi na ukarabati wa barabara ya Singida – Babati – Minjingu – Arusha umekamilika. Fedha zilizotengwa kwenye mradi huu kwa mwaka 2015/2016 niza kulipasehemu ya madai ya makandarasi.

75. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) (km 12.9)**, lengo ni kukarabati na kupanua barabara ya lami kutoka njia mbili hadi nne kati ya Bendera Tatu na Mbagala Rangi Tatu na Bendera Tatu – KAMATA. Kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 1.5) pamoja na daraja la Mzinga haikuanza kutokana na ukosefu wa fedha. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kufanya upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu – KAMATA (km 1.3) zinaendelea.

76. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Msimba – Ruaha/Ikokoto – Mafinga – Igawa (km 356.6)** kazi za ukarabati zimekamilika kwa sehemu ya Iringa – Mafinga (km 68.9); Iyovi – Kitonga Gorge (km 86.3); Ikokoto – Iringa (km 60.9) na barabara ya mchepuo kuingia Iringa Mjini (km 2.1). Aidha, kwa barabara ya Mafinga – Igawa (km 137.9) ujenzi unaendelea kwa sehemu ya Mafinga – Nyigo (km 74.1) na sehemu ya Nyigo – Igawa (km 63.8).

77. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa **Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152)** ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Kazi za ujenzi zitaanza katika mwaka wa fedha 2016/20 pamoja na barabara ya **Njombe – Ndulamo – Makete (km 109)**. Aidha, kwa barabara ya **Igawa – Mbarali – Ubaruku sehemu ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9)** kazi za ujenzi zinaendelea. Kwa barabara ya **Njombe – Lupembe – Madeke (km 125)** taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu zinaendelea.

78. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)** umegawanyika katika sehemu mbili: Korogwe – Mkumbara (km 76) na Mkumbara – Same (km 96). Mradi umekamilika kwa sehemu zote mbili.

79. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Mbeya – Makongolosi (km 115),** ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36) umekamilika. Aidha, usanifu wa kina wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 43) na Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (km 413) umekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hizi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

80. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa barabara ya **Chalinze – Segera – Tanga (km 245)** ni kuifanyia ukarabati na upanuzi. Mradi huu uligawanywa katika sehemu mbili ambazo ni Chalinze – Kitumbi (km 125) na Kitumbi – Segera – Tanga (km 120). Kazi za ukarabati kwa sehemu zote mbili zimekamilika. Aidha, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass: km 10) zimekamilika.

81. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda (km 211)** unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na zege. Hadi kufikia Aprili, 2016 taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) zilikuwa zimekamilika. Ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi kwa kiwango cha zege utanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

82. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Dodoma – Mtera – Iringa (km 260),** lengo ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni Iringa – Migori (km 95.2); Migori – Fufu Escapment (km 93.8) na Fufu Escapment– Dodoma (km 70.9). Ujenzi wa sehemu zote tatu umekamilika. Fedha zilizotengwa mwaka 2015/2016 ni kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi. Kuhusu barabara ya mchepuo wa Iringa (km 7.3) ili kupunguza msongamano wa magari katika mji wa Iringa, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Serikali itanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo ikiwa ni pamoja na malipo ya fidia kwa wananchi watakapoathiriwa na utekelezaji wa mradi huo katika mwaka wa fedha 2016/2017.

83. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya **Dodoma – Babati** (km 261), hadi Aprili, 2016, utekelezaji wa mradi huu ambao umegawanywa katika sehemu nne ni kama ifuatavyo: Dodoma – Mayamaya (km 43.65) - mradi umekamilika kwa asilimia 80; Mayamaya – Mela (km 99.35) - utekelezaji wa mradi unaendelea; Mela - Bonga (km 88.8) - utekelezaji wa mradi unaendelea na Bonga – Babati (km 19.2) - ujenzi kwa kiwango cha lami ulikamilika Aprili, 2013.

84. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 659.7)** na **Masasi – Newala– Mtwara (km 209)** unatekelezwa kwa awamu. Hadi Aprili, 2016, utekelezaji ni kama ifuatavyo: Kwa sehemu ya **Mangaka – Nakapanya (km 70.50)** utekelezaji ulifikia asilimia 50 ambapo kilometa 30 zimejengwa kwa kiwango cha lami; sehemu ya **Nakapanya – Tunduru (km 66.50)** utekelezaji ulifikia asilimia 54 ambapo kilometa 38 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami; sehemu ya **Mangaka – Mtambaswala (km 65.50)** utekelezaji ulifikia asilimia 50 ambapo kilometa 30 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu ya **Tunduru–Matemanga (km 58.7)** utekelezaji ulifikia asilimia 52 ambapo kilometa 22 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami; sehemu ya **Matemanga – Kilimasera (km 68.2)** utekelezaji ulifikia asilimia 24 ambapo kilometa 9 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami na sehemu ya **Kilimasera – Namtumbo (km 60.7)** utekelezaji ulifikia asilimia 82 ambapo kilometa 48 zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa barabara ya **Mbinga – Mbamba Bay (km 66)** na **Mtwara – Newala – Masasi (km 209)** sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) utanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

85. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo** pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho, ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

86. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi imeendelea **kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara** ikiwa ni maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara hizo. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, ukarabati wa barabara kwa kiwango cha changarawe na kujenga uwezo. Hadi Aprili, 2016 utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:

- (i) **Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/ Benaco (km 183.1) – Sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco (km 124)**
Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika na usanifu wa kina unaendelea.
- (ii) **Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwamtoro – Singida (km 460)**
Upembuzi yakinifu umekamilika. Aidha, hadi Aprili, 2016 usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni ulikuwa katika hatua ya mwisho ya utekelezaji.
- (iii) **Malipo ya Fidia kwa Barabara za Juu za TAZARA na Ubungo**
Kazi ya uhamishaji wa miundombinu kwa TAZARA imekamilika.
- (iv) **Barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldeani Jct (km 328)**
Kazi za upembuzi yakinifu zimekamilika na kazi za usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zinaendelea.
- (v) **Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Barabara ya Ipole – Rungwa (km 172)**
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii inaendelea na inatarajiwa kukamilika Juni, 2017.
- (vi) **Kuimarisha Uwezo wa Maabara Katika Ufuatiliaji na Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara (Central Materials Laboratory)**
Mkataba wa ununuziwa vifaa vya maabara umesainiwa.
- (vii) **Kufanya Mapitio na Kuandaa Viwango na Miongozo ya Barabara (Standards and Specifications)**
Wizara ilipitia Miongozo na Kanuni mbalimbali za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara ikiwemo *Manual for Provision of Low Volume Roads in Tanzania*.
- (viii) **Ufuatiliaji na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Barabara Na Madaraja**
Kazi ya kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya barabaraimekuwa ikifanyika katika kila robo ya mwaka wa fedha na kazi hiyo inaendelea.
- (ix) **Ujenzi wa Maeneno ya Kupishana Magari Kwenye Milima na Barabara Mbadala ya Kupanda Milima**
Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

(x) Malipo ya Awali na Fidia kwa Miradi ya Maendeleo

Malipo ya fidia iliyotolewa yamefikia asilimia 63.

(xi) Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika.

(xii) Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zipo katika hatua za mwisho.

(xiii) Kupunguza Msongamano wa Magari katika Barabara za Jiji la Dsm (Decongestion of DSM Roads)

Hatua za utekelezaji wa mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami barabara sita za kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara za Jiji la Dar es Salaam ni kama ifuatavyo: Barabara ya Goba – Mbezi Mwisho (asilimia 83); Barabara ya Tangi Bovu – Goba (asilimia 68); Barabara ya Kimara Baruti – Msewe (asilimia 40); Barabara ya Kifuru – Kinyerezi (asilimia 63); na Barabara ya Tabata – Dampo – Kigogo (asilimia 72). Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara ya Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda kwa kiwango cha lami ulikuwa upo katika hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

(xiv) Daraja la Kigongo/Busisi katika Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 424)

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Kigongo – Busisi zinaendelea.

(xv) Barabara ya Kazilambwa – Chagu (km 40)

Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika.

(xvi) Barabara ya Urambo – Kaliua (km 33)

Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika.

(xvii) Barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 96.7)

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina zinaendelea.

(xviii) Upembuzi Yakunifu na Usanifu wa Barabara Zinazounganisha Bandari Mpya ya Bagamoyo (km 87.9)

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakunifu na usanifu wa kina wa barabara za Wazo Hill – Bagamoyo (km 44), Makofia – Mlandizi (km 36.7) na Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) zinaendelea.

(xix) Kuwajengea Uwezo Watumishi wa Sekta ya Ujenzi

Lengo la mradi huu ni kujenga uwezo wa ndani wa wataalam kwenye Sekta ya Ujenzi ili kupunguza utegemezi wa wataalam kutoka nje pamoja na kurasimisha vyuo vilivyo chini ya Wizara ambavyo ni Chuo cha Ujenzi Morogoro (MWTI) na Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (ATTI). Hadi Aprili, 2016, Timu ya Wataalam (Special Team of Experts) ilikuwa imeundwa kutoka Taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya ujenzi; majukumu ya vyuo vya ATTI na MWTI yamaeainishwa; na maandalizi ya Hadidu za Rejea za kumpata Mshauri wa kuandaa mapendekezo ya kuviunganisha vyuo hivi kuwa chuo kimoja yanaendelea.

(xx) Barabara ya Mchepuo ya Uyole – Mbalizi – Songwe (km 40)

Ukaguzi wa awali kwa ajili ya kupata njia (site reconnaissance) umefanyika. Wizara kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) inaendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakunifu na usanifu wa kina wa barabara ya mchepuo ya Uyole – Mbalizi - Songwe.

(xxi) Kuweka Mifumo ya Kompyuta (Software) kwa ajili ya Usanifu wa Barabara na Kuandaa Mipango ya Usafiri (Highway /Transport Planning)

Mifumo miwili ya kielektroniki kwa ajili ya kuandaa mipango ya usafiri na kufanya usanifu wa barabara (design software) imenunuliwa na mafunzo kwa wataalam yamefanyika.

(xxii) Kupunguza Msongamano wa Magari katika Jiji la Mwanza (Daraja la Waenda kwa Miguu la Furahisha)

Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi.

(xxiii) Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Mikoa

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa jumla ya kilometa 505.5, ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa 28.7 na ujenzi wa madaraja 20 katika barabara za mikoa katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara. Aidha, kilometa 833.4 zilipangwa

kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Hadi Aprili, 2016 kazi zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa jumla ya kilometa 316, ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa 8.05 na ujenzi wa madaraja mawili (2).

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho ya Vivuko na Matengenezo ya Magari

87. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ilipanga kununua vivuko vitatu (3) vitakavyofanya kazi kati ya Magogoni – Kigamboni, Kigongo – Busisi na Pangani - Bweni; kukarabati vivuko sita (6) vya MV Nyerere, MV Magogoni, MV Mwanza, MV Kome I, MV Geita na MV Pangani II na kuendelea na ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo. Kazi nyingine ni kujenga majengo ya abiria kwa maeneo ya Kirumba, Igogo, Mkuyuni, Butimba, Sweya, Luchelele na Busisi katika jiji la Mwanza; kukamilisha ujenzi wa maegesho katika vivuko vya Iramba – Majita, Bukondo – Zumacheli, Ilagala-Kajeje, Msangamkuu – Msemu, Kilombero, Bugolora, na Kahunda – Maisome; upanuzi wa sehemu ya maegesho ya Kigamboni pamoja na ujenzi wa majengo ya abiria kwa kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo.

88. Mheshimiwa Spika, Wakala ulipanga kufanya ununuzi wa mashine za kisasa za kukatia tiketi kwa ajili ya vivuko vya Kisorya -Rugezi, Ilagala - Kajeje na Pangani - Bweni; ununuzi wa vitendea kazi vya karakana za TEMESA; ukarabati wa Karakana za MT. Depot Dar es Salaam na Dodoma; kuhuisha mfumo wa mashine za kukatia tiketi katika vituo vya Magogoni na Kigamboni pamoja na kutoa ushauri wa kibandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozzi na majokofu katika nyumba za Serikali.

89. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016 Wizara kupitia TEMESA imeendelea na ujenzi wa vivuko vya Magogoni – Kigamboni na Pangani – Bweni. Usanifu wa kivuko cha Kigongo – Busisi umekamilika na hatua za ununuzi zinaendelea na ukarabati wa kivuko cha MV Mwanza unasubiri upatikanaji wa fedha. Kazi zilizokamilika ni ukarabati wa MV Nyerere; ujenzi wa maegesho ya Msangamkuu – Msemu (Mtwara) na Ilagala – Kajeje (Kigoma), Majita – Iramba (Mara), Kahunda – Maisome (Mwanza), Kilombero (Morogoro) na Mwanza mjini; ujenzi wa vituo vitatu vya kivuko kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari jijini Mwanza ambavyo ni Luchelele, Igogo na Sweya; awamu ya I ya ukarabati wa karakana ya MT Depot na usimikaji wa mashine za kielektroniki za kukatia tiketi katika Kivuko cha Ilagala – Kajeje. Aidha,

ukarabati wa MV Kilombero II umekamilika kufuatia ajali ya kivuko hicho iliyotokea Januari, 2016.

Mkataba wa ukarabati wa MV Magogoni umesainiwa na kazi zimeanza mwanzoni mwa Mei, 2016. Uhuishaji wa mfumo wa mashine za kieletroniki kwa kivuko cha Magogoni – Kigamboni, ukarabati wa MV Pangani II na ujenzi wa maegesho ya kivuko kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo uko katika hatua ya zabuni. Hata hivyo, maegesho ya muda yamejengwa Magogoni na Mbegani (Bagamoyo) ili kuwezesha kuanza kufanya kazi baada ya ujenzi wa maegesho ya Jangwani Beach kuchelewa kukamilika.

90. Mheshimiwa Spika Awamu ya II ya ukarabati wa karakana ya MT. Depot imefikia asilimia 55, ukarabati wa karakana ya Dodoma awamu ya I umefikia asilimia 95 na ujenzi wa karakana mpya ya mkoa wa Manyara awamu ya II umefikia asilimia 75 ya kazi nzima. Wakala umenunua viwanja vitatu katika mikoa mipya ya Njombe, Katavi na Simiyu kwa lengo la kujenga karakana katika mikoa hiyo.

Wakala pia umeendelea kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali. Jumla ya miradi 128 imetekelezwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, TEMESA imetengeneza jumla ya magari 7,102 katika karakana zake pamoja na kukodisha mitambo na magari maalum ya viongozi wa Serikali.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

91. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilipanga kuendelea kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea pamoja na mpango maalum wa ujenzi wa nyumba 10,000 za watumishi wa Umma. Vilevile, Wakala wa Majengo ulipanga kuendelea na ujenzi wa nyumba 149 za TAMISEMI pamoja na kuendelea kufanya matengenezo ya nyumba za Serikali ikiwa ni pamoja na kununua samani kwa ajili ya nyumba za Serikali. Kazi zingine zilizopangwa ni kuimarisha Kikosi chake cha Ujenzi kwa kununua vifaa pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi wake ili kuwaongezea uwezo wa kutumia vifaa vya kisasa katika utendaji wao wa kazi. Aidha, Wakala ulipanga kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi za Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

92. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2016, Wakala wa Majengo Tanzania umeendelea kukamilisha miradi ya ukarabati wa jengo la ofisi ya iliyokuwa Benki ya Posta katika kiwanja namba 487 eneo la Kilimani, Dodoma, ujenzi wa nyumba 57 za Daraja 'B' Mikoani, Jengo la Kitega uchumi Kitegauchumi lililopo barabara ya Simioni/Goliondoi (Arusha) na Jengo la Ghorofa 6 lililopo Mtaa wa Moshi (Dodoma). Aidha, Wakala umeendelea na ujenzi wa nyumba 149 za TAMISEMI katika mkoa 20 ya Tanzania Bara pamoja na kufanya matengenezo ya nyumba 29 za Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Tano na Ikulu Ndogo za Chamwino na Arusha. Wakala wa Majengo umesimamia jumla ya miradi 198 ya Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za umma. Usanifu wa miradi hii umezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Kuhusu mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 za watumishi wa umma, Wakala umekamilisha ujenzi wa nyumba 219. Awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 256 inaendelea katika eneo la Bunju B, Dar es Salaam. Aidha, Wakala umeendelea na kununua viwanja katika sehemu mbalimbali nchini na kufanya Wakala kuwa na jumla ya viwanja 2,947 na maeneo 9 yenye jumla ekari 2,489.5 kwa ajili ya mpango maalum wa ujenzi wa nyumba 10,000 za watumishi wa umma.

Wakala umeendelea kuimarisha Kikosi chake cha ujenzi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya "Tunnel Formwork System" ili kuongeza kasi ya ujenzi na kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma. Katika kutimiza azma hiyo, Wakala umewapeleka wataalam wake nchini Uturuki ili kujifunza matumizi ya teknolojia hiyo na tayari imenunua vifaa hivyo kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wa nyumba zake katika maeneo mbalimbali nchini.

Usalama Barabarani na Mazingira

93. Mheshimiwa Spika, katika kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara, katika mwaka 2015/16 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipanga kuanzisha Mamlaka ya Usalama Barabarani, ukaguzi wa usalama wa barabara pamoja na uandaaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani (*Road Accident Information System*). Kazi nyingine ni ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (One Stop Inspection Stations), ujenzi wa mizani ya kisasa inayopima uzito wa magari yakiwa katika mwendo (*Weigh In Motion*) eneo la Mikese (Morogoro) na kufanya mapitio ya Sheria ya Usalama Barabarani. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara ilipanga kuendelea kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kwa miradi inayotekelezwa katika Sekta ya Ujenzi.

94. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2016 ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa katika mwendo (Weigh-In-Motion) katika eneo la Mikese mkoani Morogoro umekamilika. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kujenga mizani inayopima magari yakiwa kwenye mwendo katika maeneo ya Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe) zinaendelea. Vilevile, Mtaalam Mshauri amekamilisha usanifu wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi vitakavyojengwa katika Ukanda wa Kati katika maeneo ya Manyoni na Nyakanazi. Vilevile, usanifu unaendelea katika Ukanda wa Dar es Salaam (barabara za Dar es Salaam – Tunduma na Uyole – Kasumulu) maeneo ya Vigwaza, Mikumi, Makambako na Mpemba. Taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Usalama Barabarani itakayokuwa na mamlaka ya kisheria kusimamia majukumu ya usalama barabarani zinaendelea. Aidha, Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani umekamilika na umeanza kazi kwa mikoa minane ya majaribio ambayo ni Tanga, Mtwara, Dar es Salaam, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Singida na Mwanza. Maandalizi ya kuunganisha mfumo huu kwa mikoa ambayo haijaunganishwa yapo katika hatua za mwisho. Vilevile, mfumo wa kutoa vibali vya usafirishaji wa mizigo isiyo ya kawaida (*abnormal load permits*) kwa njia ya kielektroniki (e-permits) umekamilika na umeanza kutumika.

95. Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya usimamizi wa mazingira, katika mwaka 2015/16 Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika Sekta ya Ujenzi. Maandalizi ya Kabrasha la Mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hifadhi ya mazingira katika Sekta ya Ujenzi kwa wahandisi na mafundi sanifu kutoka TEMESA na TBA yamekamilika na maandalizi ya Programu za Udhhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira (*Pollution Control Programme*) ikiwa ni pamoja na kuandaa machapisho na matangazo yanayohusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa umma yapo katika hatua za mwisho.

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI

Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)

96. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mfuko wa Barabara ulipanga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 866.63** na kuzigawa kwa taasisi zinazofanya kazi za barabara ambazo ni Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi); Wakala wa Barabara (TANROADS) na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Aidha, Bodi ilipanga kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi za Bodi – Dodoma, kukamilisha tafiti mbalimbali zinazoendelea na kuwasilisha mapendekezo ya tafiti hizo Serikalini pamoja na kushirikiana na TANROADS, EWURA na TRA kufuatilia na kuweka mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato kwenye vyanzo vya mapato ya Mfuko.

Bodi pia ilipanga kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Mfuko kwa kuendelea na ukaguzi wa kiufundi wa ubora wa kazi (Value for Money Audit) katika mikoa yote nchini wakati miradi ya matengenezo ya barabara inaendelea; kuchapisha nakala za Kanuni za Matumizi ya Fedha za Mfuko na kuzigawa kwa watekelezaji wote ikiwa nipamojani Halmashauri zote nchini ili zisaidie kuwaelimisha watendaji na wananchi kwa ujumla pamoja na kununua vifaa 120 vya kupima ubora wa kazi kwa Halmashauri nchini.

97. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016 jumla ya **Shilingi bilioni 432.55** zilikuwa zimepokelewa na Bodi ya Mfuko wa Barabara sawa na asilimia 50 ya malengo ya mwaka wa fedha 2015/2016 na kuzigawanya kwa Bodi yenyewe, TANROADS, TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) iliendelea na taratibu za ununuzi wa mtaalam mwelekezi atakayefanya utafiti wa kina kuhusu vyanzo vya mapato ya Mfuko kwa kuzingatia uzoefu wa kimataifa. Vilevile, Bodi iliandaa na kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya kuongeza vyanzo vya mapato ya Mfuko ambayo yalijumuisha tozo ya leseni za magari makubwa pamoja na kurekebisha kiwango cha tozo ya mafuta ili kufidia mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya Shilingi. Bodi pia iliendelea kugharamia uimarishaji wa uboreshaji wa mifumo ya ukusanyaji na ufuatiliaji wa mapato yatokanayo na tozo za uzidishaji mizigo na vibali vya mizigo yenye vipimo visivyo vya kawaida ili iwe ya kielektroniki; ilinunua na kugawanya vifaa 120 vya kupima ubora wa kazi kwa ajili ya Halmashauri nchini pamoja na kuendelea kufanya utafiti kuhusu kiwango cha mafuta ya ndege na ya taa kinachohitajika nchini ili kubaini iwapo kuna uchakachujaji ili iweze kuishauri Serikali ipasavyo. Ujenzi wa jengo la Ofisi za Bodi Dodoma unaendelea na umekia asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2016.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

98. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilijiweka malengo ya kusajili wahandisi **800**, mafundi sanifu **200** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **25**; kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri; kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 981 pamoja na kukagua shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

99. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2016, Bodi ilisajili wahandisi **714** na makampuni ya ushauri wa kibandisi **4** na kufikisha jumla ya wahandisi **16,032** waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali na makampuni ya ushauri wa kibandisi **283**. Kati ya jumla ya wahandisi waliosajiliwa **14,525** ni wazalendo, na **1,507** ni wageni, makampuni ya ushauri wa kibandisi **203** ni ya kizalendo na **80** ni ya kigeni. Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi watalaamu **304**, Wahandisi Washauri **26** na kampuni za ushauri wa Kibandisi **37** kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Katika kipindi hiki, jumla ya miradi **256** ilikaguliwa. Wahandisi wa kigeni **23** walibainika kufanya kazi bila usajili ambapo kati yao **13** walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa, na **10** walikataliwa usajili kwasababu hawakuwa na sifa za kutosha na hivyo kurejeshwa kwao.

100. Mheshimiwa Spika, Bodi pia iliandaa warsha **3** katika Kanda **3** kati ya kanda **5** kwa Wahandisi Wataalam wanaosimamia mafunzo ya wahandisi wahitimu kwa vitendo. Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (*Professional Oath*) ambapo jumla ya wahandisi **2,193** waliapishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu **933**. Jumla ya wahandisi wahitimu **3,222** wameshapitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Aidha, Wahandisi wahitimu zaidi ya **312** toka Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali za Serikali wameshahitimu mafunzo hayo na kusajiliwa na Bodi kama wahandisi watalaam.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

101. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili wataalam **64**, ambapo Wabunifu Majengo ni **31** na Wakadiriaji Majenzi ni **33** pamoja na kusajili Kampuni **16** za Wabunifu Majengo na Kampuni **14** za Wakadiriaji Majenzi. Aidha, Bodi ilipanga kuendelea na mpango wa kuwajengea uwezo wahitimu katika fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi kupitia mafunzo kwa vitendo pamoja na kufanya ukaguzi wa miradi inayotakiwa kukaguliwa nchini.

102. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili wataalam **65**, ambapo Wabunifu Majengo ni **19** na Wakadiriaji Majenzi **46** na kufanya jumla ya Wabunifu Majengo waliosajiliwa kufikia **421** na Wakadiriaji Majenzi **326**. Aidha, bodi ilisajili kampuni za Ubunifu Majengo **15** na Ukadiriaji Majenzi **8** na kufanya jumla ya Makampuni ya Ubunifu Majengo yaliyosajiliwa kuanzia Bodi ilipoanzishwa hadi sasa kufikia **216** na Makampuni ya Ukadiriaji Majenzi **112**. Vilevile, Bodi ilifanya ukaguzi wa shughuli za wataalam kwenye miradi **2,101** katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kazi nyingine iliyofanyika ni kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu **62** katika

fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na kutoa elimu kuhusu taaluma za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi kwa TAMISEMI, Askari Polisi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi. Bodi pia iliendesha mashindano ya Insha kwa wanafunzi wa Sekondari kuhusiana na taaluma ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi ambapo zawadi mbalimbali zilitolewa. Aidha, Bodi iliendesha mashindano ya kubuni nyumba ya gharama nafuu ambapo mshindi atatangazwa Juni, 2016.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi **915** wa fani mbalimbali na kukagua miradi ya ujenzi **2,350** ambayo ina thamani ya kuanzia Shilingi milioni 10 na kuendelea. Bodi pia ilipanga kuendesha kozi tano za mafunzo katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dar es Salaam.

Hadi Aprili, 2016 Bodi ilisajili Makandarasi wapya **808** wa fani mbalimbali. Aidha, Bodi ilisajili miradi **2,967** na kukagua miradi **2,735** ya ujenzi, ambapo miradi **862** ilikutwa na kasoro. Makandarasi katika miradi yenye upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili. Aidha, Bodi iliendesha kozi **5** za mafunzo zenye lengo la kukuza uwezo wa makandarasi ambapo jumla ya makandarasi **233** walishiriki mafunzo hayo.

Baraza la Taifa la Ujenzi

104. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Baraza la Taifa la Ujenzi lilipanga kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria iliyoanzisha Baraza (CAP 162 R.E.2008), kuandaa majarida ya kiufundi kuhusu Sekta ya Ujenzi, kufanya tafiti mbalimbali za masuala yanayohusiana na sekta pamoja na kuendelea na uboreshaji wa ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za sekta ya ujenzi.

Vilevile, Baraza lilipanga kuendelea na jitihada za kukuza Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund*), kuratibu mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji (*Construction Sector Transparency Initiative - CoST*) ikiwa ni njia mojawapo ya kupambana na rushwa katika Sekta pamoja na kuratibu na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri wa kiufundi na utatuzi wa migogoro. Aidha, Baraza lilipanga kuendelea na ukamilishaji wa jengo la ghorofa 23 la ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na mwekezaji binafsi (Lindi Express Limited).

105. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016 Baraza la Taifa la Ujenzi liliendesha mafunzo yaliyohusu usimamizi na menejimenti ya mikataba ya ujenzi, usuluhishi wa migogoro na ununuzi wa huduma ya ushauri wa kitaalam. Baraza pia lilifanya ukaguzi wa kiufundi (*technical auditing*) wa miradi 85, kutoa ushauri wa kiufundi kwa wadau 20 pamoja na kushughulikia usuluhishi wa migogoro 50 ya miradi ya ujenzi.

106. Mheshimiwa Spika, Baraza linashirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi katika kushauri matumizi ya teknolojia ya bei nafuu na ya haraka kwa ujenzi wa nyumba za Mahakama za Mwanzo. Kwa sasa miradi ya majaribio inatekelezwa kwa ujenzi wa majengo ya mahakama Kibaha, Kigamboni, Mkuranga, Bagamoyo na Kawe. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Baraza limeendelea kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) ili kuharakisha uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*) ili uweze kutoa huduma kwa wadau (washauri na makandarasi) wa Sekta ya Ujenzi.

107. Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kushirikiana na U.K. Department for International Development (DFID) liliratibu uanzishwaji wa mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji (*Construction Sector Transparency (CoST) Initiative*). Hivi sasa mradi wa CoST unahifadhiwa na Baraza la Taifa la Ujenzi. Uanzishwaji wa mfumo wa kuongeza uwazi na uwajibikaji (transparency and accountability) ni mojawapo ya jitihada za kukabiliana na rushwa katika Sekta ya Ujenzi. Kwa sasa CoST imeandaa mpango wa kutoa taarifa ya miradi inayofadhiliwa na DFID katika Halmashauri 14 hapa nchini.

Vikosi vya Ujenzi (Corporation Sole Works Superintendent)

108. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Vikosi vya Ujenzi vilipanga kufanya ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi pamoja na nyumba za viongozi wa Serikali, ujenzi wa maegesho ya vivuko, kufanya ukarabati wa ofisi na maghala ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Ruvuma na Mbeya pamoja na kufanya ukarabati na ujenzi wa ofisi ya Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoa wa Dar es Salaam.

109. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016 Vikosi vya Ujenzi vilifanya ukarabati wa majengo, nyumba za viongozi wa Serikali na maghala ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Ruvuma na Mbeya. Aidha, Vikosi vya Ujenzi vilifanya kazi ya ujenzi wa ofisi na ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe pamoja na ujenzi wa nyumbayalidara ya Uhamiaji mkoa wa Mwanza. Aidha, Vikosi vya Ujenzi vimeendelea na utekelezaji wa mradi wa utengenezaji wa vifaa vya ujenzi (*blocks and pre-cast concrete elements*) jijini Dar es Salaam. Viwanja 38 vinavyomilikiwa na

Vikosi vya Ujenzi mjini Dodoma havikuweza kuendelezwa kutokana na ukosefu wa fedha. Vikosi vimepanga kutafuta mbia wa kushirikiana kviendeleza viwanja hivi kwa ajili ya vitega uchumi.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

110. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Kituo kilipanga kusambaza taarifa zinazohusu teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji hapa nchini. Kituo pia kilipanga kusambaza majarida yanayohusu teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi na usafirishaji pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maktaba ya Kituo. Aidha, Kituo kilipanga kuendelea kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji hapa nchini. Vilevile, Kituo kilipanga kuendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Morgan cha Marekani na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto za msongamano wa magari katika miji mbalimbali hapa nchini kwa kuanzia na jiji la Dar es Salaam.

111. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016 Kituo kilisambazamajaridanamachapishoyanayohusu teknolojia ya Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji; kilishiriki katika mradi unaotekelezwa na Umoja wa Mamlaka za Barabara Katika Nchi za SADC (ASANRA) unaolenga kutambua mapungufu ya ujuzi na hivyo kutoa mapendekezo ya kujenga uwezo kwa watendaji wa Mamlaka za Barabara pamoja na kufanya maandalizi ya Mkutano wa Kimataifa wa Kikanda Barani Afrika kuhusu utumiaji wa kandarasi za muda mrefu za usimamizi na matengenezo ya barabara ambapo mkandarasi hupimwa na kulipwa kwa matokeo ya ubora wa barabara badala ya kupimwa na kulipwa kwa kazi alizofanya.

Vilevile, Kituo kiliendelea kutoa huduma za maktaba kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji; kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo na njia za utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji wa habari pamoja na kukamilisha maandalizi ya mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji nchini.

C.2 SEKTA YA UCHUKUZI

112. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 389,437,277,000**. Kati ya hizo, **Shilingi 276,032,592,000** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi 113,404,685,000** ni fedha za Matumizi ya Kawaida.

113. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2016, fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi 147,043,610,000**, sawa na asilimia 53 zilikuwa zimetolewa na fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 63,464,787,364** sawa na asilimia 56 zilikuwazimetolewa.

HALI YA UTENDAJI WA SEKTA YA UCHUKUZI

114. Mheshimiwa Spika, hali ya utendaji wa Sekta ya Uchukuzi katika kipindi cha 2015/2016 ni kama ifuatavyo:

HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI

Usafiri kwa Njia ya Barabara

115. Mheshimiwa Spika, sekta binafsi imeendelea kutoa huduma za usafiri katika majiji na miji hapa nchini kwa ushindani mkubwa. Ni matarajio yangu kuwa kukua kwa ushindani kutasaidia wananchi wa mijini kuendelea kupata huduma hizo kwa urahisi zaidi na gharama nafuu. Hata hivyo, utoaji wa huduma hii unakabiliwa na changamoto ya msongamano wa magari hasa katika Miji mikubwa nchini hivyo kupunguza ufanisi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ziliendelea kuboresha huduma hizo kwa kukarabati na kuboresha barabara mbalimbali kwa lengo la kupunguza msongamano, kuboresha usafiri wa abiria katika majiji na kuanza kwa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT).

Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam

116. Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam zimeendelea kutolewa na TRL kutoka stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa (km 12) na TAZARA kutoka Mwakanga hadi stesheni kuu ya Dar es Salaam (km 34.5) kwa siku 5 za wiki. Wastani wa abiria 14,000 wanasafirishwa kwa treni kwa siku hivi sasa. Idadi hii ingehitaji jumla ya mabasi zaidi ya 467 kwa siku yenye uwezo wa kubeba abiria 30 kila moja. Kutokana na umuhimu wa usafiri wa reli katika kupunguza msongamano jijini Dar es Salaam, Wizara kupitia RAHCO ilimwajiri Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya GIBB) kutoka Afrika Kusini ili kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Kerege. Kazi hii ilianza Desemba, 2015 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2016.

Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Mijini

117. Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri katika majiji nchini imeendelea kutolewa kwa kiasi kikubwa na Sekta binafsi. Vyombo vinavyotumika kutoa huduma hiyo ni mabasi, taxi, bajaji na pikipiki. Wengi wa vyombo hivyo hasa vile vyenye uwezo wa kubeba abiria wachache umeendelea kuwa changamoto hasa maeneo ya katikati ya majiji. Wizara kwa kutambua changamoto ya msongamano wa magari katika majiji, imeiagiza SUMATRA ifanye utafiti kuhusu vyanzo, madhara na namna bora ya kukabiliana na msongamano wa magari katika miji na majiji nchini. Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti huo katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza atanza kazi mwaka 2016/2017. Utafiti huo utawezesha upatikanaji wa taarifa na takwimu muhimu katika kuelewa changamoto ya msongamano wa magari na hivyo kufikia mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hiyo.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA BARABARA

118. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na SUMATRA iliendelea kudhibiti huduma za usafirishaji kwa njia ya barabara kwa kuzingatia Sheria ya SUMATRA ya mwaka 2001 (*The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, 2001*). Katika kutekeleza jukumu hilo, SUMATRA ilipokea na kuyafanyia kazi malalamiko ya wamiliki wa mabasi yaendayo mikoani kuhusu uboreshaji wa ratiba za mabasi. Ili kupata suluhisho la kudumu la malalamiko hayo, iliundwa Kamati maalum ya kushughulikia changamoto zinazowakabili wasafirishaji ikiwa ni pamoja na ratiba hizo. Kamati hiyo ilijumuisha wajumbe kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; SUMATRA; TANROADS; Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani; Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) na Chama cha Madereva (TADWU). Tathmini ya Kamati hiyo ilibaini kuwepo kwa tofauti kati ya muda wa safari ya ratiba za sasa na muda halisi wa safari. Aidha, iliabainika kuwa muda halisi wa safari ni mrefu ikilinganishwa na muda wa ratiba. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati.

119. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuimarisha usalama na ubora wa huduma za uchukuzi kwa njia ya barabara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan Jeshi la Polisi – Kikosi cha usalama barabarani. Pamoja na Usafiri wa barabara kuwa tegemeo la wananchi walio wengi, umeendelea kukabiliwa na changamoto za ajali barabarani. Ili kukabiliana na changamoto za ajali barabarani, SUMATRA imeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri kwa nchi nzima na kutoa elimu ya usalama kwa umma. Kupitia kaguzi hizo na elimu kwa

umma wimbi la matukio ya ajali limepungua kutoka ajali 20,936 kwa mwaka 2013/2014 hadi ajali 10,034 kwa mwaka 2014/2015. Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya vifo vitokanavyo na ajali hizo imepungua kutoka vifo 7,630 kwa mwaka 2013/2014 ikilinganishwa na vifo 3,764 kwa mwaka 2014/2015.

Katika mwaka 2015/2016, SUMATRA pia iliendesha mafunzo ya kuzuia ajali zinazotokea katika vivuko vya barabara na reli. Mafunzo hayo yalijumuisha madereva wa treni, magari ya abiria wa masafa marefu na magari ya mizigo kutoka katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya, Tabora, Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Singida na Dodoma. Mafunzo ya aina hii yatafanyika katika mikoa iliyobaki katika mwaka 2016/2017.

120. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, SUMATRA ilipanua matumizi ya mifumo maalum ya TEHAMA kwa ajili ya utoaji leseni za usafirishaji (SUMATRA Road Licensing Information System - SURLIS) na mfumo wa kahasibu (*Epicor 9 – Integrated Financial Management Systems - IFMS*) katika mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma, Manyara na Rukwa ili kuboresha utendaji wake. Upanuzi wa matumizi ya mifumo hii umeiwezesha Mamlaka kudhibiti mapato na matumizi yake mikoani.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA RELI

121. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha na kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri wa reli nchini. Lengo likiwa ni kutoa huduma bora ya usafirishaji kwa njia ya reli na hivyo kuongeza tija katika ufanyaji biashara na kukuza uchumi wa nchi. Aidha, Serikali kupitia taasisi zake imeendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa reli mpya, kukarabati njia ya reli iliyopo na kununua na kukarabati vifaa mbalimbali vya kutoa huduma ya reli. Uboreshaji na uandaaji wa ujenzi wa njia mpya za reli ya Kati imeendelea kufanywa na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) na huduma za uchukuzi wa reli hiyo zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL). Aidha, huduma na miundombinu ya reli ya Tanzania na Zambia zimeendelea kutolewa na kusimamiwa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO)

122. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia RAHCO imeendelea na kazi ya kuboresha miundombinu ya reli ili kuongeza uwezo wa njia zilizopo katika reli ya Kati kubeba mizigo mizito zaidi, kuhimili mwendokasi wa juu na kupunguza ajali za treni. Hatua hii itafanya usafiri wa reli ya Kati uwe wa kuaminika na salama kwa watumiaji. Aidha, maandalizi ya

mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu na Huduma za Reli ya Kati (*Tanzania Intermodal and Rail Development Project – TIRP*) yameendelea. Kazi ya uandaaji wa Makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kutandika reli ya Dar es Salaam - Munisagara (km 269) na Igalula - Tabora (km 37) itakamilika Juni, 2016. Zabuni ya kuanza ukarabati wa maeneo hayo zitatangazwa Agosti, 2016. Ukarabati huo utakaohusu utandikaji wa reli mpya na nzito zaidi; uimarishaji wa tuta, mifereji na tabaka la kokoto utaanza mwanzoni mwa mwaka 2017 na kukamilika Juni, 2019.

123. Mheshimiwa Spika, kazi za kufanya usanifu wa kina wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa madaraja yaliyo katika hali mbaya (*Condition E*) kati ya stesheni za Dar es Salaam na Isaka ili kufikia uwezo wa kubeba tani 25 kwa ekseki ilikamilika Machi, 2016. Madaraja yanayopaswa kukarabatiwa kati ya Dar es Salaam na Isaka ni 38. Zabuni za kukarabati madaraja hayo zilitangazwa Aprili, 2016 na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Novemba, 2016.

124. Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharibifu wa miundombinu ya reli kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe linalojirudia kila msimu wa mvua kubwa, inafanywa kwa msaada kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la JICA na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mei, 2016. Kutokana na matokeo ya awali ya upembuzi huo, JICA inatarajia kuanza ujenzi wa reli katika eneo hilo mwaka 2020 na kukamilika mwaka 2022. Kazi hizi sasa zinafanywa na JICA kwa njia ya msaada na kazi ya ujenzi katika eneo hili itafanywa baada ya Serikali ya Japan kuridhia ufadhili kwa njia ya mkopo.

125. Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa reli ya Kati, na utafiti wa JICA kuchukua muda mrefu kukamilika, Serikali kupitia RAHCO imeamua kufanya usanifu wa kina ili kuanza ujenzi wa mabwawa ya kupunguza kasi ya maji kwa lengo la kuondoa tatizo la mafuriko katika eneo la Kilosa na Gulwe. Mshauri Mwelekezi *Inros Lackner* akishirikiana na *H.P Gauff* kutoka Ujerumani anatarajia kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa mabwawa hayo katika mwaka 2016/2017.

126. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa katika mwaka 2015/2016 ni pamoja na:

- (i) Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – Mbamba Bay na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga (km 1000) kwa *standard gauge* Februari, 2016. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hii; Kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha (km 438) na

kuunganisha na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (km15) kwa *standard gauge*. Kazi hii awali ilikuwa ikamilike Desemba, 2015 lakini baada ya kuongeza tawi la kuelekea KIA, sasa kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2016;

- (ii) Kuendelea kukamilisha kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora - Kigoma na Kaliua - Mpanda. Kazi hii iliyoanza Februari, 2015 inaratajiwa kukamilika Agosti, 2016;
- (iii) Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali mradi wa ujenzi wa njia mpya ya reli ya Mpanda – Karema (km150) kwa *standard gauge* inaendelea na inatarajiwa kukamilisha Juni, 2016;
- (iv) Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Arusha hadi Musoma (km 600) kwa *standard gauge* ambao umeongezewa matawi yatakayounganisha reli ya Tabora - Mwanza (km 120), tawi kuelekea Engaruka (km 53), tawi kuelekea Minjingu (km 35) na tawi kuelekea Dutwa (km 2.8) unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016; na
- (v) Kuendelea na usanifu wa kina wa reli ya Tabora – Kigoma na Kaliua – Mpanda kwa *standard gauge*. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2016/2017.

127. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza makubaliano baina yake na nchi za Rwanda na Burundi kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya Dar es Salaam-Isaka-Kigali (km 1,464) na Keza - Musongati (km 197) kwa *standard gauge*. Mshauri wa Uwekezaji (Transaction Advisor) mwenye jukumu la kunadi mradi na kuandaa nyaraka za zabuni kwa mfumo wa Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) hususan kwa Serikali kuwekeza kwenye miundombinu na sekta binafsi kwenye uendeshaji/utoaji huduma za treni (Affermage) ulibainika kuwa na changamoto kiutekelezaji na kusitishwa Februari, 2016 baada ya kupokea mapendekezo ya wawekezaji waliojitokeza kupitia zabuni iliyotangazwa. Baada ya matokeo hayo, Mawaziri wenye dhamana ya reli wa nchi tatu wanachama wa mradi walikutana Februari, 2016 na kuamua kwamba sasa utumike mfumo wa Sanifu, Jenga, Endesha, Kabidhi (DBOOT). Kutokana na hali hiyo, Mshauri wa Uwekezaji ameajiriwa tena kuendelea na awamu ya pili ya mradi huu kutafuta wawekezaji kwa kutumia mfumo huo wa DBOOT. Kazi ni kama imeanza upya baada ya mfumo wa PPP kubadilishwa. Hivyo, inatarajiwa kuchukua muda wa miezi 23 kabla ya ujenzi kuanza.

128. Mheshimiwa Spika, Mshauri Mwelekezi wa kufanya usanifu wa kina ili kuanza ujenzi wa daraja (km 349/5c) kati ya stesheni za Godegode na Gulwe anatarajiwa kuanza kazi Agosti, 2016. Ujenzi wa daraja hili utasaidia kukabiliana na tatizo la kujaa mchanga kwenye makalavati yaliyopo kati ya stesheni za Gulwe na Godegode kila mara mvua inaponyesha.

129. Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Burundi zinatarajia kujenga reli mpya ya *standard gauge* kati ya stesheni za Uvinza na Musongati (Burundi) yenye urefu wa Km 200. Serikali za Tanzania na Burundi zimetiliana saini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) ili kushirikiana katika kuendeleza reli hiyo. Kazi ya usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli hii kwa *standard gauge* inatarajiwa kukamilika Juni, 2016. Reli hii inalenga kusafirisha madini ya *nickel*, mazao ya kilimo, mafuta na bidhaa mbalimbali.

Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

130. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Reli (TRL) imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kwa kiwango cha wastani. Utendaji wa TRL umeanza kuonesha mafanikio baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi wa kununua vifaa mbalimbali vya utoaji wa huduma za uchukuzi kwa njia ya reli. Hivi sasa Kampuni ina vichwa vya treni 25 ikilinganishwa na vichwa 14 vilivyokuwepo mwaka 2014/2015. Hili ni ogezeko la asilimia 71.43. Mabehewa ya mizigo yameongezeka kwa asilimia 32.83 kutoka mabehewa 530 kwa mwaka 2014/2015 hadi kufikia 704 mwaka 2015/2016. Upatikanaji wa mabehewa ya mizigo kwa siku ni 634. TRL inaendelea na utaratibu wa kuunda upya vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo. Hadi Aprili, 2016, jumla ya uundaji wa vichwa vipya vya treni 4 kati ya 8 vya awamu ya pili ilikuwa imekamilika.

131. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza idadi ya vichwa vya treni ili kuiwezesha Kampuni kuwa na vichwa vya treni 44, vichwa vya sogeza 13 na mabehewa ya mizigo 1,500. Upatikanaji wa idadi hiyo ya vifaa pamoja na watumishi wenye ari ya kufanyakazi kutaiwezesha TRL kujiendesha kiabiashara kwa kusafirisha mizigo ya tani milioni 1.2 kwa mwaka.

132. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Kampuni ilisafirisha tani 156,104 za mizigo ikilinganishwa na tani 154,150 ziliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 1.2. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 abiria 248,819 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 310,334 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2014/2015. Hii ni pungufu ya asilimia 19. Sababu ya upungufu huo inatokana na kusitishwa kwa huduma

ya usafiri wa treni za abiria kulikotokana na athari ya mafuriko katika eneo la Kilosa – Gulwe hivyo kusababisha kufungwa kwa njia.

133. Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Kanda ya Ziwa na nchi jirani, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imekubali kugharamia uundwaji upya wa vichwa 5 vya treni kwa ajili ya kuanzisha treni maalum (block trains) itakayokwenda Kigoma na Mwanza ili kuhudumia wafanyabiashara wa Kigoma, DR Congo, Burundi; Mwanza, Uganda na Rwanda.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

134. Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Zambia zimeendelea na juhudi za uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu na huduma za reli ya TAZARA. Uboreshaji unaoendelea umeiwezesha TAZARA kusafirisha tani 95,379 za mizigo katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, ikilinganishwa na tani 54,537 zilizosafirishwa katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015. Utendaji huu ni ongezeko kwa asilimia 57. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, TAZARA ilisafirisha abiria 489,680 ikilinganishwa na abiria 454,380 waliosafirishwa kati ya Julai, 2014 na Machi, 2015. Utendaji huu ni ongezeko kwa asilimia 7.7. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa uwezo wa utendaji wa vichwa vya treni (reliability) na wastani wa upatikanaji wake kwa siku (availability) baada ya idadi ya vitendea kazi kuongezeka kutokana na utekelezaji wa Itifaki ya 15 kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi kati ya Tanzania, Zambia na China. Serikali za Tanzania, Zambia na China zimekamilisha utekelezaji wa miradi iliyoainishwa katika Itifaki ya 15 ya ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi iliyosainiwa Machi, 2012 yenye mkopo wenye thamani ya Shilingi bilioni 67.2.

135. Mheshimiwa Spika, miradi iliyotekelezwa na kukamilika kupitia Itifaki hii ni pamoja na ununuzi wa vichwa vipya 4 vya treni ya njia kuu, vichwa vipya 4 vya treni ya sogeza, mabehewa ya abiria mapya 18, mashine za okoa 2 pamoja na mitambo na vifaa vya usalama; mitambo 5 ya kufanyia kazi ngumu za marekebisho ya njia ya reli; mitambo ya kunyanyua mizigo; Seti 1,600 za “SKF Bearings” za mabehewa ya tani 30; vipuri kwa ajili ya matengenezo ya vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo, njia ya kudumu ya reli, kiwanda cha kutengeneza mataruma ya zege; na ununuzi wa mataruma 30,000 ya mbao yanayotumika kwenye sehemu za kawaida, madaraja na vibadilisha njia ya reli.

USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI

136. Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji zimegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni uchukuzi baharini, huduma za bandari na uchukuzi katika maziwa. Katika mwaka 2015/2016, huduma za uchukuzi katika maziwa zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) pamoja na sekta binafsi. Aidha, huduma ya uchukuzi katika bahari zimeendelea kutolewa na Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (SINOTASHIP) pamoja na kampuni nyingine kutoka nje ya nchi. Kuhusu bandari, huduma zimekuwa zikitolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Serikali imefanya juhudi za kuimarisha na kuboresha miundombinu ya huduma za uchukuzi majini na kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma hizo.

Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

137. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Kampuni ya MSCL ilisafirisha abiria 84,173 ikilinganishwa na abiria 159,699 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Huu ni upungufu wa asilimia 47. Sababu za upungufu huo ni pamoja na meli za MV Victoria, MV Liemba, MV Songea na MV Clarias kusimama kutoa huduma. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa meli hizo. Kuhusu usafirishaji wa mizigo, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Kampuni ilisafirisha tani 33,015 za mizigo ikilinganishwa na tani 31,013 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Hili ni ongezeko la asilimia 6. Sababu za ongezeko hilo ni pamoja na kukamilika kwa matengenezo ya meli ya MV. Serengeti.

138. Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaendelea na mpango wake wa kujenga meli 4 mpya katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Awamu ya kwanza itakayohusu ujenzi wa meli moja (1) mpya katika Ziwa Victoria, ukarabati wa meli za MV Butiama na MV Victoria katika ziwa Victoria na ukarabati wa MV Liemba katika Ziwa Tanganyika utanza mwaka 2016/2017. Katika mwaka huu, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa meli mpya katika ziwa Victoria, Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa MV Victoria, Shilingi bilioni 5.9 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa MV Liemba na Shilingi bilioni 3.6 zimetengwa ili kufanya ukarabati wa MV Butiama.

139. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha matengenezo ya meli ya MV Serengeti na kuanza tathmini ya kufunga mfumo mpya wa kielektroniki wa kukata tiketi melini.

Huduma za Uchukuzi Baharini

140. Mheshimiwa Spika, SINOTASHIP inamiliki meli kubwa moja yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja. Meli hii inatoa huduma ya uchukuzi wa mizigo wa masafa marefu baharini. Katika mwaka 2015, Kampuni hii iliweza kusafirisha tani 437,000 ikilinganishwa na tani 350,000 zilizosafirishwa katika mwaka 2014. Aidha, Kampuni imekamilisha utafiti wa awali wa kununua meli ya kusafirisha gesi ndani na nje ya nchi. SINOTASHIP inaendelea kufanya kazi kwa karibu na Kampuni ya Meli ya China (COSCO) katika kutafuta fedha za ununuzi wa meli hiyo.

Huduma za Bandari

141. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kupata mafanikio makubwa katika kuziendeleza bandari za mwambao wa Bahari ya Hindi na zile za Maziwa Makuu kwa kuziboresha na hivyo kuziwezesha kuhimili ushindani wa kibiashara kikanda.

142. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Mamlaka ya bandari ilihudumia jumla ya tani milioni 11.73 za shehena ikilinganishwa na tani milioni 12.28 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 4.4. Katika shehena hiyo, bandari ya Dar es Salaam ilihudumia jumla ya tani milioni 10.61 za shehena na bandari nyingine tani milioni 1.13. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Kitengo cha Makasha (TICTS) kilihudumia makasha 355,730 ikilinganishwa na makasha 344,517 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Hili ni ongezeko la asilimia 3.2.

143. Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yanatokana na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa katika kuboresha huduma za bandari. Jitihada hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA; kufungua ofisi katika miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DR Congo) na Lusaka - Zambia; kuimarisha usalama wa mizigo na kutoa huduma za bandari kwa saa 24 kwa siku kwa wiki.

144. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, shehena iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi za Burundi, DR Congo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia ni tani milioni 4.7 ikilinganishwa na tani milioni 4.41 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2014/2015. Hili ni ongezeko la asilimia 6.6 wa mizigo iliyosafirishwa.

145. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, Wizara kupitia TPA iliendelea kuhakikisha kuwa ujazo wa mafuta yanayoingia nchini ni sahihi kutokana na vipimo sahihi na vinavyokubaliwa Kimataifa. Katika kutekeleza azma hii, Novemba, 2015 Mamlaka iliingia mkataba na Mkandarasi (Woolgate Trademark Co. Ltd) kwa ajili ya ufungaji wa mita za kupima ujazo wa mafuta (flow meters) yanayoshushwa melini katika boya la kushushia mafuta (SPM) lililoko katika Bandari ya Dar es Salaam. Kazi ya ufungaji ilikamilika Aprili, 2016 na mita hizo zimeanza kutumika.

146. Mheshimiwa Spika, kazi ya uboreshaji na uongezaji wa kina katika gati Na. 1 hadi 7 na ujenzi wa gati jipya la kushushia magari eneo la Gerezani Creek katika bandari ya Dar es salaam kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, TMEA na DfID zinaendelea. Nyaraka za zabuni kwa hatua ya pili na ya mwisho ya kupata mkandarasi wa kazi ya ujenzi zilitolewa Machi, 2016 kwa Wakandarasi sita waliofuzu katika hatua ya kwanza ya zabuni, na zinatarajiwa kufunguliwa Juni, 2016. Aidha, kampuni ya M/S Inros Lackner Ag kutoka Ujerumani tayari imeteuliwa kuwa Msimamizi wa kazi za ujenzi (Consultant for Works Supervision).

147. Mheshimiwa Spika, Mkataba kati ya TPA na Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa namna bora ya kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli (entrance channel and turning basin) ulisainiwa Desemba, 2015. Mshauri Mwelekezi alianza kazi Januari, 2016 na atakamilisha Julai, 2016. Aidha, kazi za kupanua, kuchimba na kuongeza kina zinatarajiwa kuanza Oktoba, 2016 nakukamilika Novemba, 2017.

148. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ilipanga kujenga gati Na.13 na 14 kwa kushirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga, Endesha na Rejesh (Design, Build, Operate and Transfer - DBOT). Hata hivyo, kazi hiyo haikutekelezwa kutokana na kutokamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali utakaoonesha hali halisi ya mradi na gharama zake. Ujenzi wa gati hizi unatarajiwa kuanza mwaka 2017 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, TMEA na DfID baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kukamilika. Ni matarajio yetu kuwa sekta binafsi itawekeza katika utoaji huduma na ujenzi wa maghala katika magati hayo.

149. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuanza Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo, yanaendelea vizuri chini ya uratibu wa ofisi ya Waziri Mkuu. Vipengele vya Mikataba ya Mradi (Heads of Agreements) baina ya Serikali na Wawekezaji (Kampuni ya CMH ya China na Taasisi ya Reserve Fund ya Serikali ya Oman) vilisainiwa tarehe 16 Oktoba, 2015. Aidha, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa bandari hii wapatao 2,211 wa vijiji vya Pande na Mlingotini ikiwa ni pamoja na sehemu ya Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi cha Mbegani (FETA) lilianza Septemba, 2015.

150. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2015, jumla ya wananchi 2,185 sawa na asilimia 98.8 ya wafidiwa wote walishalipwa jumla ya Shilingi bilioni 45.27. Fedha hizi ni sawa na asilimia 79.32 ya malipo yote. Wananchi 85 pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani bado hawajalipwa fidia zao. Sababu za kuchelewa kulipwa ni pamoja na kasoro zilizojitokeza katika kumbukumbu zao, kutojitokeza kuhakikiwa kwa ajili ya malipo, kutowasilisha taarifa kamili za kibenki na kutokamilisha taratibu za mirathi. TPA kwa kushirikiana na Mamlaka za Wilaya ya Bagamoyo wanaendelea kuwasiliana na wahusika ili waweze kukamilisha taratibu stahiki za malipo. Ni matarajio yangu kuwa ifikapo Juni, 2016, malipo yote yatakuwa yamekamilika. Ujenzi wa bandari hii utaongeza uwezo wa kuhudumia shehena ziingiazo nchini na ziendazo nchi jirani za Burundi, DR Congo, Rwanda, Uganda na Zambia.

151. Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa reli ya uhakika inayoiunganisha Bandari ya Mwambani, Tanga na maeneo mengine zikiwemo nchi jirani, kumesababisha wawekezaji kushindwa kujitokeza kuwekeza katika ujenzi wa bandari hii. Kwa kuwa sasa taarifa za awali za upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya Tanga – Arusha – Musoma, unaonesha kuwa kuna urari wa kutosha wa mradi wa reli, Mamlaka imerejea upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa ujenzi wa bandari hii kwa kushirikiana na Taasisi za taaluma za ndani ya nchi. Lengo ni kufanya utafiti utakaozingatia ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma.

152. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Bunge lako lilitaarifiwa juu ya kukamilika kwa majadiliano baina ya Mamlaka na mkandarasi wa mradi wa kupanua Bandari ya Mtwara kwa kujenga gati mpya nne kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga na Gharamia. Napenda kulitaarifu tena Bunge lako kuwa majadiliano hayo hayakufanikiwa baada ya Mkandarasi Kampuni ya *Hyundai Company* (HEC-DBS- SANY) kudai hana fedha za kugharamia mradi badala yake aikutanishe Mamlaka na benki itakayotoa mkopo. Suala hili lilikuwa ni kinyume na makubaliano pamoja na matakwa ya zabuni ya mradi huo.

153. Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa bandari ya Mtwara ni muhimu hususan katika uendelezaji wa uchimbaji wa gesi na mafuta katika mwambao wa Bahari ya Hindi; uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe katika maeneo ya Mchuchuma, Liganga na Ngaka, Mbinga; uimarishaji Ukanda wa Mtwara pamoja na uhudumiaji wa shehena za nchi jirani za Malawi, Msumbiji na Zambia. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imepanga kutekeleza mradi huu kwa awamu. Awamu ya kwanza itakayoanza mwaka 2016/2017 itahusu ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 350 ili kuhudumia shehena mchanganyiko. Mamlaka inaendelea kuwasiliana na Vyuo vya ndani ya nchi ili kupata Mtaalam Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakini na Usanifu wa gati zote nne na kuandaa nyaraka za zabuni za ujenzi wa gati moja. Kazi hii inatarajiwa kuanza Juni, 2016.

154. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeingia makubaliano ya awali (MoU) na kampuni ya *Dangote* kwa ajili ya kukodisha ardhi yenye ukubwa wa hekta 25 katika eneo la Kisiwa/Mgao Oktoba, 2015. Eneo hili litatumika kujenga Gati la kuhudumia shehena ya Kiwanda cha Saruji kinachomilikiwa na Kampuni hiyo. Mamlaka itaendelea kusimamia Makubaliano hayo na kufuatilia kwa karibu ujenzi wa gati hilo. Aidha, kuhusu uendelezaji wa Eneo Huru la Uwekezaji (Free Port Zone) katika bandari ya Mtwara, lenye ukubwa wa hekta 10 ambalo limekodishwa kwa EPZA Agosti, 2015, Kampuni ya *Bandari Gas and Oil Terminal Ltd* inaendelea kuandaa *Business Plan and Design* kwa ajili ya ujenzi wa Gati moja mpya kwa ajili ya kuhudumia Kampuni zinazojihusisha na utafiti wa mafuta na gesi katika mwambao wa bahari ya Hindi.

155. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeendelea kuboresha bandari ndogo za Lindi na Nyamisati katika Bahari ya Hindi; Lushamba na Ntama katika Ziwa Victoria; Kagunga, Lagosa na Kalya katika Ziwa Tanganyika; na Ndumbi katika Ziwa Nyasa. Hatua ya utekelezaji wa uboreshaji wa bandari hizi ni kama ifuatavyo:

- (i) Ukarabati wa gati la Lindi ulioanza Machi, 2015, unatarajiwa kukamilika Juni, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 3.1;
- (ii) Kazi ya ujenzi wa gati la Ntama katika Ziwa Victoria inaendelea na inatarajiwa kukamilika Juni, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.039;
- (iii) Ujenzi wa gati la Lushamba, unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.124;
- (iv) Ujenzi wa gati la Kagunga ulianza Agosti, 2015 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 3.356;
- (v) Ujenzi wa gati la Kalya/Sibwesa ulianza Desemba, 2015 na utakamilika Desemba, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 3.452;

- (vi) Ujenzi wa gati la Nyamisati, Rufiji utakaofanywa kwa kutumia wataalam wa ndani unatarajiwa kuanza Julai, 2016 na kukamilika Juni, 2017 kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.5;
- (vii) Ujenzi wa gati la Ndumbi ulianza Februari, 2016 kwa kutumia wataalam wa ndani ya Mamlaka na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.8;
- (viii) Ujenzi wa magati ya Lagosa, Kibirizi na Kabwe utanza Julai, 2016 kwa kutumia wataalam wa ndani. Aidha, vifaa (water master, dredging and piles) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa magati hayo viliwasili Februari, 2016;
- (ix) Ujenzi wa gati la Kyamkwikwi katika Ziwa Victoria ulianza Aprili, 2015 kwa kutumia wataalam wa ndani wa Mamlaka na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2016 kwa gharama ya Shilingi milioni 290;
- (x) Ujenzi wa gati la Pangani ulianza Julai, 2015 kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.27 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016.

156. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa gati la Karema, mpango wa awali ulikuwa ni kujenga gati dogo kwa ajili ya abiria. Kutokana na umuhimu wa bandari hii kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Bandari yake ya Kalemie na kwa kuzingatia mpango uliopo wa kujenga reli ya Mpanda - Karema, Wizara imeamua kujenga bandari kubwa ili kukidhi mahitaji ya shehena inayotarajiwa. Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari hii ameanza kazi Machi, 2016 na unatarajiwa kukamilisha Novemba, 2016.

157. Mheshimiwa Spika, katika Bunge la mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Mamlaka ya Bandari iliahidi kuboresha usafirishaji wa mizigo na abiria katika Ziwa Nyasa kwa kujenga meli moja na matishari mawili. Napenda kutoa taarifa kuwa ujenzi wa Meli hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo ulianza Juni, 2015 na unatarajiwa kukamilika Februari, 2017 kwa gharama ya Shilingi bilioni 9.12. Kuhusu matishari mawili (Self-Propelled cargo Barges) zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja, ujenzi ulianza Juni, 2015 na unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 11.25. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha huduma za usafirishaji wa mizigo katika ziwa Nyasa husasan shehena za makaa ya mawe, mbolea na saruji kutoka na kwenda katika masoko ya Mbeya, Njombe, Ruvuma na nchi jirani za Malawi na Msumbiji.

158. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) waliendelea na kazi ya kuwezesha mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato kutoa huduma za *electronic Single Window System (eSWS)* kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza imekamiliwa, ambapo thamani ya mzigo (CIF Value) hutumwa kielektroniki kutoka mfumo wa TANCIS wa TRA kwenda mfumo wa *Billing system*

wa TPA. Awamu ya pili itakamilika tarehe 1 Julai 2016, ambapo makusanyo yote ya *Wharfage* yatafanywa na mfumo wa TANCIS badala ya mfumo wa *Billing System*. Awamu ya mwisho, itakamilika tarehe 1 Julai 2017 ambapo mfumo wa TANCIS utatoa huduma zote za *electronic Single Window System*.

159. Mheshimiwa Spika, kazi ya kufanya Upembuzi Yakinifu wa kuboresha miundombinu katika bandari za Ziwa Victoria (Mwanza, Musoma na Bukoba) na Ziwa Tanganyika (Kigoma) itakamilika Juni, 2016. Mpango uliopo ni kuzijengea uwezo bandari hizi wa kuhudumia shehena kubwa itakayosafirishwa kwa njia ya reli ya Kati.

Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Majini

160. Mheshimiwa Spika, SUMATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority - ZMA*) imeendelea kudhibiti huduma za usafiri wa majini nchini. Aidha, Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi wa ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini kwa kuzingatia Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003 (*Merchant Shipping Act, 2003*) na kusimamia viwango vya huduma na sheria za kimataifa zinazosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Bahari (IMO).

161. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Shirika la Kimataifa la Bahari, kuhusu kupima makasha yote yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia bandari zote kuanzia Julai, 2016, SUMATRA imewapa taarifa wadau wote wa bandari zetu ndani na nje ya nchi kupitia balozi zetu. Utaratibu huu una lengo la kuwawezesha wenye meli kujua na kuzingatia uzito anaotakiwa kuubeba ili kuhakikisha usalama wa vyombo vya usafiri. SUMATRA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kuandaa kanuni za kupima uzito wa makasha yanayosafirisha mizigo kwenda nje ya nchi kupitia katika bandari zetu. Mkutano wa wadau kwa lengo la kukusanya maoni kuhusu rasimu ya kanuni za udhibiti wa uzito wa makasha yanaposafirishwa kwenda nje kupitia bandarini ulifanyika tarehe 22 Desemba, 2015. Kuanza kutumika kwa kanuni hizo kutaimarisha usalama wa vyombo vya usafiri majini kwani kutakuwa na uhakika wa uzito sahihi wa mizigo inayosafirishwa kwenye meli. Aidha, kanuni hizo pia zitaimarisha usalama wa shughuli za upakuaji na upakiaji Bandarini.

162. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuimarisha udhibiti wa ulinzi, usalama na ubora wa huduma ya usafiri majini kwa kufanya ukaguzi wa vyombo vya majini mara kwa mara. Pamoja na ukaguzi huo, usafiri wa majini uliendelea kukabiliwa na changamoto ya ajali. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, ajali za majini zilipungua hadi kufikia

ajali 14 ikilinganishwa na ajali 16 za mwaka 2014/2015. Aidha, Kituo cha Ukoaji na Utafutaji (MRCC) kilichoko Magogoni, Dar es Salaam kimeendelea kuboresha mfumo wa upashanaji wa taarifa kuhusu matukio ya ajali katika eneo la maji ya Tanzania.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga

163. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kusimamia uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini ili viendeleo kukidhi matakwa ya viwango vya Kimataifa. Aidha, viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Amani Abedi Karume na Kilimanjaro vilikaguliwa tena na kupewa vyeti vya ubora baada ya kukidhi vigezo vya kimataifa vya viwanja vya ndege vya kuweza kupokea ndege kubwa. Mamlaka pia imeendelea kudhibiti ubora wa viwanja vya ndege vya Arusha, Mwanza, Kigoma, Tabora, Bukoba, Mtwara, Tanga, Lindi na Iringa.

164. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kuhakikisha kwamba matukio na ajali za vyombo vya usafiri wa anga zinapungua mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2015/2016, matukio matatu (3) pamoja na ajali mbili (2) zilitokea ikilinganishwa na mwaka 2014/2015 ambapo matukio manne (4) na ajali mbili (2) zilitokea. Ajali zilizotokea zilihusu ndege moja ya helikopta aina ya BELL 206 yenye usajili Na. 5H-MWK iliyoanguka katika kijiji cha Legaruki, Arusha. Watu wote waliokuwemo kwenye ndege hiyo walisalimika. Ajali ya pili ilihusisha ndege ya helikopta aina ya Eurocopter AS 350 B3 yenye usajili Na. 5Y-DKK ambayo ilianguka katika mbuga ya wanyama ya Selous na kuwa watu wote wanne waliokuwamo kwenye ndege hiyo. Uchunguzi wa ajali za ndege hizo bado unaendelea. Mungu azilaze roho za marehemu hao mahala pema peponi- Amen.

165. Mheshimiwa Spika, usalama wa anga ni suala la kimataifa na husimamiwa kwa karibu na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (International Civil Aviation Organization- ICAO). Ili kuhakikisha usalama katika usafiri wa anga Duniani unaimarika, ICAO imekuwa ikifanya kaguzi za mara kwa mara ili kupima ni kwa kiwango gani nchi inatekeleza viwango vya usalama wa anga vya kimataifa (*International Security Standard*). Kwa mara ya mwisho, nchi yetu ilikaguliwa Septemba, 2015 katika aina ya ukaguzi unaojulikana kama *ICAO Universal Security Audit Program- Continuous Monitoring Approach* (ICAO USAP-CMA). Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba katika ukaguzi huu, Tanzania ilifanya vizuri kwa kupata asilimia 86.20. Tutaendelea kuhakikisha kunakuwa

na usalama katika viwanja vya ndege ikiwa ni pamoja na huduma zinazotolewa kwenye viwanja hivyo.

166. Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma za usafiri wa anga nchini umechangia katika kukua kwa sekta ya uchukuzi nchini. Katika mwaka 2015/2016, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga imeongezeka hadi kufikia abiria 5,065,184 ikilinganishwa na abiria 4,895,833 waliotumia usafiri huo mwaka 2014/2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 3.5. Aidha, idadi ya abiria wa ndani ilikuwa 3,134,663 katika mwaka 2015/2016 ikilinganishwa na abiria 2,808,270 katika mwaka 2014/2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 16.

167. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, jumla ya safari za ndege 283,097 zilifanyika ikilinganishwa na safari 212,259 za mwaka 2014/2015. Hili ni ongezeko la asilimia 33.4. Kati ya safari hizi, safari za kimataifa zilipungua kutoka safari 36,534 mwaka 2014/2015 hadi kufikia safari 34,086 mwaka 2015/2016, kupungua kwa safari hizi kulitokana na mashirika mengi yanayofanya safari za kimataifa kati ya nchi yetu na nchi zingine kupunguza safari za kuja na kutoka nchini, huu ni upungufu wa asilimia 6.7. Safari za humu nchini ziliongezeka kutoka safari 175,725 mwaka 2014/2015 hadi kufikia safari 249,011 mwaka 2015/2016, sawa na ongezeko la asilimia 41.7.

168. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, mizigo ya kwenda na kutoka nje ya nchi ilifikia tani 30,417 ikilinganishwa na tani 29,629 zilizosafirishwa mwaka 2014/2015. Hili ni ongezeko la asilimia 2.7. Ongezeko hili linatokana na kukua kwa shughuli za kibiashara na kiuchumi ndani na nje ya nchi. Ufanisi uliopatikana katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga kwa kiasi kikubwa umechangiwa na ongezeko la Kampuni zinazotoa huduma hizo. Hadi sasa kuna kampuni 51 zinazotoa huduma za usafiri wa anga za ratiba (scheduled) na zisizo za ratiba (non-scheduled air services). Hii ni ongezeko la asilimia 4.

169. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha kuwa sekta binafsi inaimarika na kuendelea kukua katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga, katika mwaka 2015/2016, Serikali ilisaini Mikataba ya Usafiri wa Anga kati ya Tanzania na nchi nyingine (Bilateral Air Services Agreements – BASA) na nchi saba (7) za Sri Lanka, Serbia, Ghana, Morocco, Curacao, Malta na Kuwait. Hatua hii imeifanya Tanzania kuingia mikataba ya usafiri wa anga (BASA) na jumla ya nchi 60, ikilinganishwa na nchi 53 zilizokuwa katika Mikataba mwaka 2014/2015. Kati ya mikataba hiyo, ni mikataba ya nchi 19 tu ambayo kampuni/mashirika yake ya ndege yanatoa huduma kati ya Tanzania na nchi husika. Aidha, katika

mwaka 2015/2016, mashirika ya ndege ya kimataifa yaliyoendelea kutoa huduma nchini kwa utaratibu wa BASA yalikuwa 29.

170. Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyotekelezwa katika mwaka 2015/2016 ni pamoja na:

- (i) Ukamilishaji wa utengenezaji wa mifumo ya ramani za kutua ndege katika viwanja vya ndege vya Zanzibar na Mwanza. Ramani hizi zimeanza kutumika Februari, 2016;
- (ii) Kukamilisha Mradi wa kubadilisha alama (Coordinates) za viwanja vya ndege vya Arusha, Mafia, Lindi, Kigoma na Tabora. Uwepo wa alama hizi unaziwezesha ndege kutumia mfumo wa Satelaiti wakati wa kutua na kuondoka;
- (iii) Kukamilisha kazi ya kubadilisha mfumo wa mawasiliano ya ufuatiliaji safari za ndege ya angani kutoka katika mfumo unaotumika sasa wa analogia kwenda mfumo wa kisasa wa teknolojia ya digitali. Mfumo huu umefungwa katika viwanja vya ndege vya Mtwara, Songea na Kigoma. Ufungaji wa mfumo huu katika kituo cha Pemba utakamilika Juni, 2016.
Mfumo huu utapunguza gharama za mawasiliano na kuleta uhakika wa mawasiliano kati ya kituo na kituo;
- (iv) Kukamilisha kazi ya kufunga Mtambo wa kisasa aina ya *Air Traffic Message Handling System (AMHS)* wenye uwezo wa kupitisha na kusambaza taarifa za mawasiliano ya angabadala ya ule uliokuwepo (*Aeronautical Fixed Telecommunication Network - AFTN*) ambao ufanisi wake nimdogo;
- (v) Kuendelea na Mradi wa kufunga kifaa kitiwacho *VHF area cover relay station* ili kuboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani wakiwa angani katika vituo vya Lolkisale, Arusha na Changarawe, Iringa. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mei, 2016; na
- (vi) Kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa kufunga mitambo ya ufuatiliaji wa mienendo ya ndege angani ujulikanao kama *Automatic Dependent Surveillance - Broadcast (ADS-B)* na Mtambo wa usambazaji wa taarifa za usafiri wa anga (*Air Traffic Services Message Handling System – AMHS*). Mtambo wa ADS-B umehusisha upande wa Mashariki hadi juu ya bahari ya Hindi.

Huduma za Viwanja vya Ndege

171. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kwa kuzingatia Sera ya kuwezesha viwanja vya ndege kujijendesha kibiashara, kujitosheleza na kujitegemea. Aidha, Mamlaka iliendelea na

ununuzi wa mitambo, matengenezo ya miundombinu na mitambo mbalimbali katika viwanja inavyoendesha ili kuboresha huduma, kuimarisha usalama na kutambua vitu vya hatari.

172. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka inaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria (Terminal III Building) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa msingi, nguzo, mihimili ya jengo na uezekaji wa paa. Aidha, kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa kuta za ndani ya jengo; usimikaji wa madaraja ya kupandia ndege abiria, viyoyozi, miundombinu ya umeme, mifumo ya maji safi na taka pamoja na mifumo ya zimamoto. Ujenzi wa maegesho ya ndege umefikia hatua ya matabaka ya lami. Mradi huu umekamilika kwa asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2016. Awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA itaongeza uwezo wa jengo kuhudumia abiria hadi milioni 6 kwa mwaka. Ujenzi wa awamu ya pili unatarajiwa kukamilika Desemba, 2017.

173. Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi zinazoendelea za ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika jengo la pili la Abiria (TB II) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), kazi zilizokamilika katika Kiwanja cha ndege cha JNIA kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na:

- (i) Ufungaji wa Mitambo 4 mipya ya kufua umeme wa dharura na usimikaji wa seti tatu (3) za vivuko vya abiria;
- (ii) Usimikaji wa mashine 2 kwa ajili ya kubaini milipuko na madawa ya kulevya (Explosive and Narcotics trace Detectators) yaliyofichwa kwenye mizigo ya abiria; na
- (iii) Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la pili la abiria. Serikali inaendelea na majadiliano na Taasisi ya Fedha ya Ufaransa (AFD) kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa kazi hizo.

174. Mheshimiwa Spika, kazi za ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) zilianza Septemba, 2015 na zinatarajiwa kukamilika Mei, 2017. Kukamilika kwa ukarabati huu wa kiwanja utaongeza uwezo wa barabara ya kuruka na kutua ndege kuhudumia ndege nyingi zaidi na pia jengo la abiria ambalo lina uwezo wa kuhudumia abiria 500,000 kwa mwaka litaweza kuhudumia abiria Milioni 1.2 kwa mwaka.

175. Mheshimiwa Spika, kazi ya ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mwanza inaendelea. Kazi zilizokamilika mpaka mwaka 2015/2016 ni ujenzi wa tabaka la mwisho la lami kwenye maegesho ya ndege za abiria, kuweka tabaka la pili la lami katika barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa kingo na sakafu za zege katika jengo la mizigo, ujenzi

wa boma (super structure) na kuta za ndani katika jengo la kuongozea ndege. Kukamilika kwa ukarabati huu kutaifanya Serikali kutimiza azma yake ya kukifanya kiwanja hiki kuwa kitovu cha usafiri wa anga katika Ukanda wa nchi za Maziwa Makuu.

176. Mheshimiwa Spika, kiwanja cha ndege cha Songwe ni muhimu katika uendelezaji na uboreshaji wa biashara na uchumi wa wakazi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Katika mwaka 2015/2016, Mamlaka iliendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa maegesho ya ndege na miundombinu yake. Aidha, kazi ya kusimika mifumo maalum (Special Systems) katika jengo jipya la abiria inaendelea. Ili kuhakikisha kuwa ndege zinatua kwa usalama kiwanjani, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imesaini mkataba na Mkandarasi atakayesimika taa za kuongozeandegewakati inapotaka kutua (PAPI).

177. Mheshimiwa Spika, kazi ya kukarabati kiwanja cha ndege cha Bukoba imekamilika na kiwanja kilianza kutumika rasmi Septemba, 2015. Mkataba wa kazi za awamu ya pili zinazohusisha ukarabati wa barabara ya pili ya kutua na kuruka ndege (secondary runway), eneo la maegesho ya ndege (apron), barabara ya maungio (taxiway) kwa kiwango cha lami, usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege (NavAids, DME na VOR) na AGL chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ulisainiwa tarehe 22 Septemba, 2015. Kazi zitaanza mara majadiliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia yatakapokamilika. Zabuni kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) zitatangazwa Juni, 2016 na ujenzi unatarajiwa kuanza Oktoba, 2016.

178. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka inaendelea na maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege kumi na moja (11) vya Lake Manyara, Musoma, Iringa, Tanga, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe, Simiyu na Singida kwa kiwango cha lami. Kazi inayoendelea ni kukamilisha Upembuzi Yakunifu, Usanifu wa Kina pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2016. Aidha, Wizara inaendelea kufanya majadiliano na Taasisi za kifedha kwa ajili ya utafutaji fedha za kuanza ujenzi na upanuzi wa viwanja hivyo.

179. Mheshimiwa Spika, zabuni kwa ajili ya kuanza ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) zitatangazwa Juni, 2016 na ujenzi unatarajiwa kuanza Oktoba, 2016. Uboreshaji wa viwanja hivi utawezesha viwanja kutoa huduma kwa majira yote ya mwaka na kwa saa ishirini ya nne (24).

180. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TAA inaendelea kuandaa Usanifu na Mpango Kabambe (Concept Design & Master Plan) kwa ajili ya kukarabati na kupanua kiwanja cha ndege cha Mtwara. Lengo ni kukiwezesha kiwanja hicho kiendane na kasi ya maendeleo ya kiuchumi yanayotokana na ugunduzi wa gesi na mafuta katika mikoa ya Kanda ya Kusini. Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi hii na anatarajiwa kukamilisha Julai, 2016.

181. Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipyaa cha ndege cha Msalato kwa kiwango cha lami. Mradi wa ujenzi wa kiwanja hiki utahusisha ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara za kiungio, maegesho ya ndege na magari, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, mfumo wa maji ya mvua, jengo la abiria na zimamoto, mnara wa kuongozea ndege pamoja na Kituo cha kupokea na kusambaza umeme. Usanifu wa Kina wa miundombinu ya kiwanja hiki ambacho kitahuisha shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo kukuza utalii katika Makao Makuu ya Nchi yetu unatarajiwa kuanza Desemba, 2016.

Huduma za Usafiri wa Ndege

182. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) pamoja na sekta binafsi zimeendelea kutoa huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Napenda kuzipongeza kampuni binafsi za *Precision Air, Fastjet, Auric* na *Coastal Air* kwa kuendelea kutoa huduma za usafiri wa anga nchini na nje ya nchi.

183. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Serikali imeendelea kuiwezesha ATCL ili itoe huduma ya usafiri wa anga kati ya Dar es Salaam na Mwanza; Mtwara; Kigoma na Moroni, Comoro kwa kutumia ndege yake aina ya Dash 8-Q300 na ndege ya kukodi aina ya CRJ 200. Hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kusimamia ukamilishaji wa ukaguzi wa hesabu za Kampuni katika kipindi cha miaka 7 iliyopita hadi 30 Juni, 2015; kurejea katika IATA Clearing House, hivyo kufanya viti vya ndege zake kuuzwa popote duniani; kuunda Bodi ya Wakurugenzi pamoja na kuimarisha uendeshaji wa Kampuni kwa kuwekeza katika mifumo mbalimbali ya mawasiliano ya TEHAMA.

184. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, ATCL ilisafirisha abiria 32,434 ikilinganishwa na abiria 30,246 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2014/2015. Utendaji huu umesaidia kukua kwa mapato ya Kampuni kutoka Shilingi bilioni 7.8 katika mwaka 2014/2015 hadi shilingi bilioni 10.9 katika mwaka 2015/2016. Kuongezeka kwa mapato kumechangiwa na kuongezeka kwa idadi ya safari zinazolipa zaidi kutoka Dar es Salaam kwenda Comoro na Kigoma kutoka safari 4 kwa juma hadi safari 6 kwa juma.

185. Mheshimiwa Spika, kazi inayoendelea ni kukamilisha taratibu za ununuzi wa ndege mbili mwaka 2016. Wizara kwa kushirikiana na ATCL na wadau wengine imekwishaainisha ndege zinazofaa kununuliwa baada ya kukutana na wawakilishi wa viwanda vya ndege vya Boeing ya Marekani, Airbus ya Ufaransa, Embraer ya Brazil na Bombardier ya Canada. Ndege mbili za awali zinazotarajiwa kununuliwa zitakuwa na uwezo wa kubeba abiria 78 kila moja. Ndege ya tatu na ya nne zitakazonunuliwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 zitakuwa na uwezo wa kubeba abiria 155.

HUDUMA ZA HALI YA HEWA

186. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kuhakiki, kuratibu na kutoa huduma za hali ya hewa nchini. Katika mwaka 2015/2016, Mamlaka iliendelea kutoa huduma za utabiri wa hali ya hewa pamoja na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa. Lengo ni kuhakikisha usalama wa watu na mali pamoja na kuongeza mchango wa huduma za hali ya hewa katika kuendeleza sekta za kiuchumi na kijamii. Aidha, kwa kiasi kikubwa huduma za hali ya hewa zinachangia katika kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi. Mamlaka pia imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuiwakilisha nchi kikanda na kimataifa.

187. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ilikamilisha kazi ya uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na uchambuzi wa data za hali ya hewa katika Kituo Kikuu cha Taifa cha Utabiri pamoja na vituo vilivyo katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Zanzibar, Mwanza na Kilimanjaro. Kukamilika kwa mradi huu kumesaidia kuongeza usahihi wa utabiri wa hali ya hewa na kuimarisha uwezo wa kutuma data na taarifa za hali ya hewa ndani na nje ya nchi. Aidha, Tanzania kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imefanikiwa kupata fursa ya kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Utendaji la Shirika ya Hali ya Hewa Duniani.

188. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya kushindwa kutoa taarifa zenye usahihi kwenye maziwa makuu, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka imeanza kutumia kompyuta yenye uwezo mkubwa katika kuchambua data za hali ya hewa na hivyo kutoa utabiri hadi wa maeneo madogo madogo. Uwepo wa Mtambo huu umesaidia kuimarisha usalama wa usafiri majini na ufanisi wa shughuli za kiuchumi zinazofanyika kwenye maziwa ya Victoria na Nyasa. Taratibu za kuanza kutoa huduma kama hizo kwa Ziwa Tanganyika zinaendelea.

189. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imekamilisha kazi ya kufanya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa awali wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri. Kazi inayoendelea ni kufanya usanifu wa kina.

C.3 SEKTA YA MAWASILIANO Ukusanyaji wa Mapato

190. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 12,011,000** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali. Hadi Aprili, 2016 Sekta ilikusanya jumla ya **Shilingi 10,021,900**, sawa na asilimia **83.4** ya makisio.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

191. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi 43,195,303,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 38,072,072,000** ni Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Mawasiliano na Taasisi na **Shilingi 5,123,231,000** ni Matumizi Mengineyo. Hadi Aprili, 2016 **Shilingi 29,081,693,638** zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,229,022,904** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Mawasiliano na Taasisi na **Shilingi 2,852,670,734** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

192. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa **Shilingi 15,798,888,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni Shilingi 13,400,000,000 na Shilingi 2,398,888,000 zilikuwa fedha za nje. Hadi Aprili, 2016 fedha zilizotolewa ni **Shilingi 2,766,062,001.60**. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 766,062,001.60 ni fedha za nje.

Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano

193. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi kubwa na kuwa moja ya nguzo muhimu ya kukuza uchumi kwa Taifa letu. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano. Sekta hii huchangia katika uchumi moja kwa moja na kupitia sekta zingine zote kama nyenzo ya uwezeshaji katika kuongeza ufanisi wa utendaji kupitia jamii habari. Takwimu zinaonyesha kuwa laini za simu zinazotumika zimeongezeka kutoka 34,251,801 mwaka 2014 hadi kufikia laini 39,808,419 mwaka 2015 na idadi ya Watumiaji wa intaneti waliongezeka kutoka 14,217,311 kwa mwaka 2014 hadi kufikia 17,263,523 kwa mwaka 2015. Zaidi ya asilimia 64 ya kaya nchini zinamiliki simu za mikononi. Aidha, vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 91 mwaka 2014 hadi kufikia vituo 116 mwaka 2015 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vilipungua kutoka vituo 28 mwaka 2014 na kushuka hadi kufikia vituo 26 mwaka 2015. Vilevile, *teledensity/ penetration rate* ni kiasi cha asilimia 90 ya nchi kufikiwa na huduma za mawasiliano ikiwemo simu, intaneti na utangazaji. Pia watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenye tija na ufanisi nchini kwa sekta zote.

194. Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yamewezesha kukua kwa kasi kwa sekta ya Mawasiliano kutoka asilimia 8.0 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 12.1 mwaka 2015 na hivyo kuwa sekta ya kwanza katika sekta za huduma na kuwa ya pili kwa sekta zote katika ukuaji hapa nchini. Sekta hii imechangia katika Pato Ghafi la Taifa kwa asilimia 3.6 mwaka 2015. Matokeo haya ya ukuaji na mchango katika teknolojia ya habari na mawasiliano kwa sehemu kubwa kilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za mawasiliano zikiwemo zile za muda wa maongezi kwa simu za viganjani na mezani, intaneti na utangazaji. Pia, ufanisi huu ulichangwiwa na kukua kwa matumizi ya miamala ya kielektroniki ambayo ni pamoja na uzaji na ununuzi wa bidhaa na utoaji wa huduma kwa njia za kielektroniki. Utafiti kupitia tathmini ya *Global Microscope* umebaini kuwa Tanzania ipo nafasi ya sita kati ya nchi 55 Ulimwenguni na inaongoza katika Bara la Afrika kwa kuwa na mazingira mazuri ya huduma za kifedha kupitia simu za kiganjani. Vilevile, kwa mujibu wa ripoti ya *Fiscope Survey* ya mwaka 2015, huduma za kifedha zimewafikia watanzania kwa asilimia 76 kutoka asilimia 44 mwaka 2009 ikiwa imechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa Mawakala wa Kibenki (Agent Bankings) pamoja na huduma za kifedha kupitia kampuni ya simu kiasi cha kufikia akaunti za miamala ya kifedha (mobile money accounts) kuwa 17,639,349 hadi Desemba 2015.

195. Mheshimiwa Spika, Tanzania inaripotwa kuwa nchi ya kwanza duniani kwa kampuni za simu za viganjani kuwa na makubaliano ya kutengamanisha (interoperability) miamala ya huduma ya fedha. Hii imewezesha kupunguza gharama za kutuma fedha kutoka mtandao mmoja kwenda mitandao mingine. Jambo hili limewezesha Tanzania kuongoza duniani katika kutumia huduma ya *Mobile Money Banking* kwa kiasi cha fedha zinazozunguka kwenye mtandao kwa wastani wa Shilingi trilioni 4.5 kwa mwezi.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

196. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano inaratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini, ambao kwa sasa upo katika Awamu ya III na IV ya utekelezaji. Awamu ya III imegawanyika katika sehemu mbili (Awamu ya III Sehemu ya I na Awamu ya III Sehemu ya II). Awamu ya III Sehemu ya I inajumuisha ujenzi wa kituo mahiri cha kutunzia kumbukumbu (Internet Data Centre) Dar es Salaam, utekelezaji wa miundombinu ya Mtandao wa Itifaki-Internet Protocol-Multilayer Label Switching (IP/MPLS service) na uunganishaji wa Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na utekelezaji wake umekamilika mwezi Aprili 2016. Aidha, Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Awamu ya III sehemu ya II ambayo itahusisha kufikisha Mkongo katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini, ujenzi wa vituo Mahiri vya Kutunza Data (Internet Data Centres) za Dodoma na Zanzibar na ujenzi wa Miundombinu ya *Public Key Infrastructure (PKI)*.

197. Mheshimiwa Spika, Awamu ya IV inayohusu ujenzi wa Mikongo ya Mijini (Metro Fibre Ring Networks) na *Missing Links* ya Mkongo wa Taifa imeanza na inatekelezwa kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano (operators) nchini. Hadi April, 2016 Kilometa 300 zimekamilika katika jiji la Dar es Salaam na mkongo huo unatumika. Aidha, ujenzi wa Mikongo ya Mijini katika mikoa ya Mwanza (km 36) na Arusha (km 58) tayari umekamilika. Pia, ujenzi katika mikoa ya Morogoro (km 18), Dodoma (km 42), Tanga (km 43.28), Moshi (km 35.08), Mbeya (km 6.9), Shinyanga (km 2.3), Musoma (km 2.1) na Biharamulo (km 0.2) tayari umeanza na unategemewa kumalizika mwezi Juni, 2016. Pia inahusisha ujenzi wa *Missing Links* kupitia njia za reli ya kati na kaskazini: Dodoma – Tabora – Mwanza (km 762), Tabora–Kigoma (km 410) na pia kupitia barabara kuu kutoka Dar es Salaam hadi Arusha na Korogwe hadi Tanga (km 820), Morogoro hadi Ifakara (km 309), Arusha–Babati–Dodoma (km 390), Babati – Singida – Isaka (km 418) na Moshi hadi Rombo (km 67). Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 80 zitatumika katika mradi huu.

Ushirikishaji wa Sekta Binafsi katika ujenzi wa miundombinu katika jiji la Dar es Salaam umerahisisha utekelezaji wa miradi mingine kama vile Mradi wa Kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti na Mradi wa Serikali Mtandao. Miradi hiyo miwili imetumia njia (duct) zilizojengwa na mradi wa Metro. Maandalizi ya Awamu ya Tano kuhusu ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha watumiaji wa mwisho (*Last Mile Broadband Connectivity*) yanaendelea.

198. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanaongezeka hasa katika taasisi za Serikali, shule, hospitali na vyuo vya elimu, Sekta ya Mawasiliano inafanya juhudi za kuwezesha taasisi za Serikali kutumia intaneti kwa bei nafuu kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma za *broadband* na kuongeza ufanisi na uwazi wa Serikali kupitia matumizi ya Serikali Mtandao. Wizara imekamilisha ujenzi wa Mtambo wa *Internet Bandwidth* na ununuzi wa *Internet Bandwidth* yenye ukubwa wa *1.55 Gbps* ambayo tayari imeanza kutumika na hadi hivi sasa zaidi ya taasisi za Serikali 170 zinatumia huduma hiyo.

Juhudi za Serikali Kufikisha Huduma ya Mawasiliano Vijijini

199. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Kampuni ya VIETTEL (Viettel Joint Stock Company – VIETTEL) ya Vietnam inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mawasiliano Vijijini. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu, 2015-2017 ambapo hadi Aprili, 2016 kazi zifuatazo zimetekelwa:

- i) Kukamilisha ujenzi wa kilometa 18,000 kati ya kilometa 20,000 za Miundombinu ya Mkongo katika Wilaya zote nchini;
- ii) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano katika vijiji 4000 visivyokuwa na mawasiliano kwa kipindi cha Oktoba, 2014 hadi Novemba, 2017. Ujenzi huu umefanyika katika vijiji 2,208 katika kipindi cha Oktoba, 2014 hadi Aprili, 2016.
- iii) Kuendelea kuunganisha Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya, Hospitali za Wilaya na Ofisi zote za Polisi za Wilaya nchini pamoja na Ofisi 65 za Posta nchini. Wizara inaendelea kupokea mapendekezo ya taasisi mbalimbali zinazoomba kuunganishwa katika mtandao huo; na
- iv) Kuzipatia intaneti shule za sekondari 431, Ofisi za Wilaya 101, Hospitali za Wilaya 93, Ofisi za Polisi 118, Ofisi za Posta 63 na Mahakama 11.

200. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na ushirikiano wa Serikali na Viettel, yamevutia kampuni kubwa za mawasiliano hapa nchini kutaka kushiriki kikamilifu katika juhudi za Serikali za kupeleka mawasiliano vijijini. Ili kuweka mfumo mzuri, Sekta ya Mawasiliano imetoa Mwongozo wa kushirikisha kampuni za simu ambao utaongeza kasi ya kufikisha huduma bora za mawasiliano kwa wananchi na hivyo kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Taifa letu.

Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi

201. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 inayoelekeza kuwepo kwa Anwani za Kitaifa zitakazoweza ufikishaji wa barua, nyaraka na vipeto nyumbani, mahali pa biashara na ofisini. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kunakuwepo na Anwani za Kitaifa ambazo zitaainisha makazi, mahali pa kazi au pa biashara. Anwani za Makazi na Postikodi sio tu kwa ajili ya kufikisha barua, nyaraka na vipeto majumbani bali pia zitarahisisha na kuboresha utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi, kwa mfano: Afya, Elimu, Sensa, Uokoaji, Biashara Mtandao na Ukusanyaji wa Mapato.

202. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo Postikodi za nchi nzima zimeandaliwa na zimeanza kutumika; Hifadhi – Data imeundwa; kazi ya uwekaji wa miundombinu wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi unaendelea Dar es Salaam na Zanzibar ambapo katika awamu ya kwanza na ya pili Dar es Salaam zimekamiliwa kata 32 na Zanzibar zimekamiliwa wadi nane. Utekelezaji wa awamu ya tatu ya utekelezaji katika jiji la Dar es Salaam ambao utahusisha kata zilizobaki umeanza na taarifa za maeneo yaliyokamilika zinaendelea kuingizwa kwenye Hifadhi - Data.

203. Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha utekelezaji na matumizi ya miundombinu ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi zimeandaliwa nyaraka tatu. Nyaraka hizo ni Mwongozo wa Anwani za Makazi, Mwongozo wa Postikodi na Sheria Ndogo. Nyaraka hizi zimekamiliwa kwa ajili ya kuridhiwa na kutolewa kwa matumizi. Aidha, katika kuwezesha matumizi ya mfumo huu, zimeandaliwa ramani kwa ajili ya kurahisisha usambazaji wa barua, nyaraka na vifurushi. Sambamba na ramani zilizoandaliwa, tarehe 5 Aprili, 2016 Serikali kupitia Shirika la Posta ilizindua huduma iitwayo "Posta Mlangoni" ambayo itatumia mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi kufikisha barua, nyaraka na vifurushi hadi mahali alipo mteja (nyumbani au ofisini). Huduma ya Posta Mlangoni itaanza kutolewa katika maeneo ambayo miundombinu ya Mfumo huu imekamiliwa. Pia, kwa kushirikiana na wadau wengine, hasa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mkakati wa kutekeleza mpango

wa miaka miwili wa kuhakikisha kila mtaa mijini, vijijini na ngazi ya kitongoji vinapewa majina na nyumba zinapewa namba umekubaliwa kutekelezwa.

Mradi wa Video Conference

204. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano katika kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanakua hasa katika ofisi za Serikali; imekamilisha ufungaji na usimikaji wa mitambo ya Video Conference ambayo tayari imeanza kutumika kwenye Makao Makuu ya Mikoa 22 ya Tanzania Bara, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na TAMISEMI. Wizara inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kufunga vifaa husika katika Mikoa mipya minne iliyobaki ya Njombe, Geita, Songwe na Simiyu. Aidha, Wizara imekamilisha ufungaji wa mitambo ya video conference katika Ofisi tano za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ofisi hizo ni Ofisi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Chuo cha Amali Mkokotoni kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Chakechake na Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyopo Wete. Pia, Wizara imefanya mafunzo kwa waendesha mitambo husika kwa mikoa yote iliyonufaika na mradi huu. Katika kuhakikisha kuwa mitambo hiyo inatumiwa kikamilifu, Serikali imeandaa mwongozo wa matumizi ya Video Conference. Vilevile, Serikali inaendelea na kazi ya ufungaji wa bridge ambayo pamoja na mambo mengine itawezesha vituo vyote kuwasiliana kwa wakati mmoja au kuwezesha vituo husika kuunganishwa katika mikutano tofauti tofauti.

Mradi wa Elimu Mtandao (e-Schools)

205. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA katika shule yanaongezeka kwa kasi na kuweka mazingira ya kutumia elimu mtandao, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Ofisi ya Rais –TAMISEMI zimeainisha shule 300 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa majaribio wa shule mtandao (e-schools) ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kutekeleza Mpango wa Taifawa Kuunganisha Shule. Hadi Aprili, 2016 vituo 129 zikiwemo shule 123, vituo vya posta vitatu na vyo vya afya vitatu vimepelekewa na kufungiwa vifaa vya TEHAMA. Aidha, mafunzo kwa walimu 258 yametolewa juu ya TEHAMA ili kuwapa uwezo wa kutumia TEHAMA na kufundisha wanafunzi. Pia, maudhui kwa ajili ya ufundishaji wa somo la TEHAMA yametengenezwa kwa kufuata mitaala ya shule za sekondari. Sekta ya Mawasiliano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inatekeleza Mradi wa Kuunganisha Mtandao wa Intaneti katika Shule za Umma kwa ushirikiano na kampuni ya mawasiliano kwa njia ya Setelaiti ya

Avanti ambapo imeweza kuziunganisha shule 224 kati ya shule 250 katika mtandao wa intaneti.

Ununuzi wa Mtambo wa Internet Bandwidth na Ununuzi wa Internet Bandwidth

206. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha ujenzi wa Mtambo wa Internet Bandwidth na ununuzi wa Internet Bandwidth yenye ukubwa wa 1.55 Gbps ambayo tayari imeanza kutumika na zaidi ya taasisi za Serikali 170. Lengo ni kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanaongezeka ili kuwezesha taasisi za Serikali kutumia intaneti kwa bei nafuu, kuongeza ufanisi na uwazi wa Serikali kupitia matumizi ya Serikali mtandao.

Kuimarisha Uwezo wa Wizara katika Kuongoza Sekta (Strengthening of the Institutional Capacity of MWTC)

207. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuendana na mabadiliko ya ukuaji kasi wa TEHAMA ambapo watumishi 83 wamenufaika na mafunzo. Aidha, katika kuhakikisha mifumo ya ndani ya Sekta inaimarika, Sekta ya Mawasiliano imeanzisha mifumo ya kielektroniki ya utumaji na upokeaji wa mafaili (Document Management Information System – DMIS) pamoja na mfumo wa kielektroniki wa mahudhurio (Electronic Attendance Register) lengo likiwa ni kuimarisha na kurahisisha utendaji kazi.

Kuimarisha Mfumo wa ubunifu (Tanzania Innovation Program)

208. Mheshimiwa Spika, eneo hili limelenga kujenga na kukuza mfumo wa ubunifu utakaowezesha kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kutumia TEHAMA katika kukuza ujasiriamali (entrepreneurship) na ubunifu kuanzia ngazi ya chini (grassroot innovation). Pia, kubadilishana uzoefu wa Kikanda na Kimataifa kwa wasimamizi wa Sera za TEHAMA na Ubunifu. Katika mwaka wa fedha 2015/16, mradi umetumia jumla ya Shilingi 30,000,000 kupitia Mfuko wa Ubunifu (innovation Fund) kwa ajili ya kuwezesha wabunifu huko Zanzibar. Eneo la ubunifu linaendelea kuwakutanisha wabunifu katika kuendeleza shughuli zao (innovation space), Programu ya kubadilishana uwezo ya TaFin inatekelezwa, pia usimamizi wa vituo vya kijamii vya ubunifu (*living labs*) unafanyika. Aidha, programu ya *Team Academy* imeanzishwa katika chuo kikuu cha Iringa. Vilevile, mradi umeweza mchakato wa uwekaji wa Mfumo wa Ubunifu (National Innovation System) kwa utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

209. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na wanaotoa huduma za mawasiliano katika mwaka wa fedha 2015/2016, wameendelea na ufikishaji wa huduma ya mawasiliano vijijini ambapo jumla ya kata 103 kati ya kata 443 zenye vijiji 634 na wakazi 1,107,585 zimekwisha pata huduma ya mawasiliano. Mfuko unatekeleza miradi sita ya kufikisha huduma ya mawasiliano ambayo ni mradi wa Awamu ya Kwanza ambao kata 51 kati ya kata 52 zimekwisha pata huduma ya mawasiliano, mradi wa Awamu ya kwanza "A" ambapo kata 15 kati ya kata 77 zimepata huduma ya mawasiliano, mradi wa maeneo ya mipakani na kanda maalum ambapo kata mbili kati ya kata 10 zimekwisha pata huduma ya mawasiliano, mradi wa Awamu ya pili "B" ambao kata 35 kati ya kata 86 zimeshapata huduma ya mawasiliano. Aidha, watoa huduma wanahimizwa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyobaki ya mawasiliano kabla ya mwezi Juni, 2016 ili kuepuka hatua kali kutoka Serikalini ikiwemo kulipishwa gharama za kuchelewesha mradi (*Liquidated Damages*).

210. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetekeleza mradi wa kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule za umma 250 pamoja na kutoa vifaa vya TEHAMA vikiwemo projekta na kompyuta. Sambamba na mtandao wa intaneti na vifaa vya TEHAMA, vituo 25 vya kufundishia TEHAMA vimeanzishwa kwa ajili ya kuwapatia walimu elimu ya jinsi ya kutumia TEHAMA katika kufundishia. Jumla ya walimu 500 watapata elimu ya TEHAMA kutoka katika shule hizo. Mafunzo haya ya TEHAMA yalianza tarehe 1 Aprili, 2016 na yatakamilika mwezi Mei, 2016.

211. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, inatekeleza mradi wa kuanzisha vituo vya TEHAMA kwa upande wa Zanzibar, ambapo hadi kufikia mwishoni wa mwezi Juni, 2016 itakamilisha ujenzi wa vituo hivyo. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Miundombinu ya Zanzibar ambayo ilifanikisha zoezi la kuainisha maeneo ya ujenzi wa vituo hivi. Jumla ya vituo 10 vya TEHAMA vitajengwa katika wilaya za Pemba na Unguja.

212. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetekeleza mradi wa kufikisha huduma za matangazo ya runinga ya kidigitali katika mikoa minne ambayo ni Geita, Simiyu, Katavi na Njombe kwa kusambaza ving'amuzi vya runinga kwa njia ya satelaiti (Direct to Home – DTH decoders) kupitia ruzuku ya Mfuko. Ving'amuzi hivyo vilisambazwa na kuuzwa na kampuni ya Star Media kwa bei ambayo ni nusu ya bei ya sokoni ili kuwanufaisha wananchi wengi kupata matangazo ya runinga ya kidigitali.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (Telecommunication Traffic Monitoring System - TTMS)

213. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea kutekeleza Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (TTMS) ili kuwezesha usimamizi wenye ufanisi zaidi kwa watoa huduma za mawasiliano ya simu nchini. Mfumo huu unaonyesha takwimu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapato halisi yanayopatikana kutokana na miamala ya kifedha. Mfumo huu wa uangalizi wa miamala ya fedha za simu za kiganjani pia utaiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kujua mapato yatokanayo na huduma hii hivyo kukusanya kodi stahiki.

214. Mheshimiwa Spika, faida za kuwa na TTMS na mifumo mingine iliyotekelezwa ndani yake ni pamoja na: kuweza kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hivyo kudhibiti vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia hizo na Kuimarisha usalama nchini. Mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia ya ulaghai yameweza kudhibitiwa na sasa yamepungua kabisa na Kusimamia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano (Quality of Service) na hivyo kuboresha viwango vya huduma hizo. Aidha, Mtambo huu umechangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (HAZINA) kiasi cha **Shilingi 45,218,484,735.06** ikiwa ni makusanyo ya kuanzia Oktoba, 2013 hadi Desemba, 2015.

Usalama wa Mitandao ya Mawasiliano - (Tanzania Computer Emergency Response Team - TZ-CERT)

215. Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) umekuja na fursa nyingi na unakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinaathiri maendeleo ya TEHAMA. Athari hizo ni pamoja na uhalifu kimitandao (cyber Crime), ugaidi kwenye mifumo wa mitandao (cyber terrorism) na uharibifu wa mila na desturi (mfano picha zisizo na maadili kwenye mitandao).

216. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 TZ-CERT imekuwa ikikusanya na kuchambua taarifa mbalimbali za kiusalama katika mtandao wa intaneti hapa nchini, Taarifa hizi zinajumuisha matishio katika mitandao (Cyber threats) kama vile usambazaji wa *Malicious Software – Malware, Web defacement, Phishing, Spam, Hacking*. Aidha, faida za TZ-CERT ni pamoja na: kusaidia kutafuta na kuhifadhi ushahidi wa uhalifu katika mitandao kwa lengo la kusaidia vyombo vya usalama; Kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya usalama mtandaoni; kufuatilia maendeleo ya nchi katika nyanja ya usalama mitandao (Cyber security development) na kuwa na uhakika wa kiusalama wa taarifa mitandao nchini na pia kujenga utamaduni wa jamii kufahamu na kufanyia kazi usalama wa mitandao na taarifa mitandao.

Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Uhalifu wa Matumizi Mabaya ya Mtandao.

217. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuwajenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu na matumizi mabaya ya mitandao kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Vilevile, Mamlaka imelipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi ili kuwawezesha kukabiliana na uhalifu na matumizi mabaya ya mtandao.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

218. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza na kuimarisha huduma za usambazaji wa barua, nyaraka na vipeto kwa haraka mijini, Shirika limeanzisha huduma za *Courier and Express Mail Service* pamoja na *Posta City Urgent Mail (pCUM)* ili kurahisisha usambazaji huo. Aidha, utaratibu huu umerahisisha huduma za usambazaji wa barua kwa wananchi kwa kutumia miundombinu ya Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta.

219. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 249 katika nyanja zifuatazo:- Uendeshaji: 179; Uongozi: 9; Kumjali Mteja 48; Semina za uongozi na Utawala Bora 5; na Semina na Mafunzo ya Kimataifa 8. Vilevile, Shirika la Posta limekamilisha kuweka mfumo mpya wa kielektroniki ujulikanao kama *Postglobal Netsmart* katika Ofisi za Posta 120 kutoka ofisi 52 za mwaka 2014/2015. Kwa kuwa Tanzania ndio makao makuu ya Umoja wa Posta wa Afrika (Pan African Postal Union - PAPU) jijini Arusha, Shirika la Posta kwa kushirikiana na TCRA na Wizara vinaratibu ujenzi wa jengo litakalochangiwa na wabia wawili yaani PAPU na TCRA. Matatizo ya umiliki wa kiwanja cha PAPU yanashughulikiwa kati ya sekta hii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

220. Mheshimiwa Spika, Mpango mahsusi wa TTCL wa huduma za simu za kiganjani zinazotumia teknolojia ya kisasa na bora zaidi ya data ya 4G LTE na Data (ADSL) zikiwa na vifurushi vilivyoboreshwa zaidi ulizinduliwa tarehe 23 Desemba 2015 katika Mkoa wa Dar es Salaam kama hatua ya awali (soft launch). Hadi April, 2016 huduma hii ya 4G LTE inapatikana kikamilifu katika maeneo 11 ya Dar es Salaam ya Uwanja wa Ndege, Nyerere Road, Posta Mpya, Kinondoni, Ubungo, Oysterbay, Mwenge, Mbezi Tangibovu, Mbezi, Kunduchi Salasala na Wazo Hill Tegeta. Hatua za kupanua huduma hii katika maeneo mengine ya Dar es Salaam zinaendelea. Usambazaji wa mtandao wa teknolojia ya 4G LTE unatarajiwa kufanyika katika mikoa mingine mitatu ambayo ni Dodoma, Arusha na Mwanza kwa mwaka 2016.

221. Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Kituo cha *Internet Protocol Point of Presence - (IP PoP)* Kijitonyama umetekelezwa na TTCL kwa kushirikiana na Kampuni ya Sparkle ya Italia. Kituo hiki chenye hadhi ya daraja la juu la mtandao wa intaneti na uwezo mkubwa wa kutoa huduma za mawasiliano ya Intaneti kitaifanya Tanzania kuwa kitovu cha mtandao wa intaneti katika eneo la Pwani ya Afrika Mashariki na ukanda wa nchi za Maziwa Makuu ambazo zimekwisha fikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (National ICT Broadband Backbone, NICTBB). Vilevile, kituo hiki kina uwezo mkubwa wa kumuunganisha mteja kwenye mtandao wa intaneti moja kwa moja bila kupitia kwa watoa huduma (ISP) wengine wa kati huko Ulaya, hivyo kuongeza kasi kwa kupunguza urefu wa njia ya mawasiliano kwa mteja kufikia mahitaji kwa watumiaji. Hadi Aprili, 2016 Kituo cha IP PoP Kijitonyama tayari kimekwishauunganisha kampuni za Malawi Telecom, Roke Telekom ya Uganda pamoja na TTCL yenyewe.

Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

222. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Tangazo la Gazeti la Serikali la tarehe 20 Novemba, 2015. Majukumu ya msingi ya Tume hii ni pamoja na kusimamia mifumo mbalimbali kupitia TEHAMA; kutambua, kusajili, kusimamia na kuendeleza weledi katika TEHAMA yaani *ICT Professional development, registration and certification*; kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji wa miundombinu na huduma za TEHAMA kitaifa ikiwemo masuala ya *Information Technology Enabled Business Process Outsourcing* na Kusimamia mfumo utakaowezesha wabunifu na wajasiriamali kuendeleza sekta ya TEHAMA.

223. Mheshimiwa Spika, Nimeteua Kamati ya Usimamizi ya Tume ya TEHAMA na kuunda menejimenti ya mpito (interim) itakayofanya kazi chini ya Kaimu Mkurugenzi Mkuu. Ofisi za muda za Tume ya TEHAMA zipo katika jengo la Posta ya zamani katika mtaa wa Sokoine, Dar es Salaam.

D. TAASISI ZA MAFUNZO

224. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasimamia vyo vya mafunzo vifuatavyo:

Chuo cha Ujenzi Morogoro

225. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo kilipanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,390** katika fani za ufundi sanifu na ukaguzi wa barabara, madaraja, majengo, umeme na mitambo pamoja na mafunzo kwa madereva wa umma (*Public Professional Drivers*), madereva wa awali (*Basic Driving Course*) na madereva wa magari ya abiria (*PSV*). Chuo kilipanga kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la maabara ya vifaa vya ujenzi (*materials laboratory*), kuendeleza ujenzi wa karakana ya ufundi, kukarabati majengo 3 na mitambo 3 ya kufundishia na kununua vitendea kazi vya kufundishia.

Hadi Aprili, 2016 jumla ya wanafunzi wa fani za ujenzi **1,520** walipata mafunzo ya fani mbalimbali. Aidha, Chuo kiliendelea na ujenzi wa jengo jipya la karakana ya ufundi, mitambo **3** ya kufundishia imepatikana pamoja na ukarabati wa majengo ya ofisi, madarasa na kumbi.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATTI)

226. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo kilipanga kuendesha mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe na mafunzo ya uwekaji wa tabaka la lami kwa kutumia nguvukazi; kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake kushiriki katika kazi za barabara pamoja na kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Kazi nyingine ni kufanya ziara ya tathmini ya mafunzo yaliyotolewa katika mikoa ya Rukwa, Tabora, Singida, Dodoma na Mbeya pamoja na kuendelea kutoa ushauri na mafunzo maalum kwa viongozi wa vikundi mbalimbali vya ujenzi kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvukazi.

227. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2016 Chuo kilitoa ushauri wa matumizi stahiki ya teknolojia ya nguvukazi kupitia mradi wa (*Rural Maintenance System Development (RMSD)*) unaoafadhiliwa na JICA chini ya TAMISEMI pamoja na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya nguvukazi hapa nchini kupitia maonyesho ya Nane Nane yaliyofanyika Mkoani Mbeya. Aidha, Chuo kilifanya tathmini ya mafunzo yaliyofadhiliwa na TAMISEMI yaliyotolewa katika mikoa ya Rukwa, Tabora, Singida, Dodoma na Mbeya. Hadi sasa mikoa minne (4) imeshatembelewa kwa ajili ya kutathimini matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi pamoja na kuona utekelezaji wa mafunzo haya yaliyofanyika kuanzia mwaka 2008 – 2011. Chuo pia kiliendesha mafunzo yaliyoratibiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya kuwajengea uwezo wanawake katika kushiriki kazi za barabara nchini ambapo wanawake ishirini (20) walishiriki pamoja na kutoa mafunzo ya awali ya ushiriki wa wananchi katika kukarabati na kutengeneza barabara za vijijini kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa washiriki 45 ambao ni viongozi wa vijiji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

228. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kimeendelea kutoa mafunzo katika fani za uhandisi wa meli na unahodha, pamoja na utaalum kwenye masuala ya uchukuzi na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya maji.

229. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo kilidahili wanafunzi 528 wa ngazi ya shahada, diploma, cheti na vyeti vya ujuzi (certificate of Competency). Kati yao, wanawake ni 23, wanaume ni 505 na kutoka nchi za nje ni 61. Aidha, Wanafunzi 3,413 walihitimu kozi fupi za aina 46 kwa kuzingatia matakwa ya Shirika la Bahari la Kimataifa (IMO). Kati yao, wanawake ni 140 na wanaume ni 3,273 ambapo watahiniwa 422 walitoka katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pia maafisa wa meli 92 walihitimu, kati yao 9 kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kupitia wafadhili na wadau wa sekta ya Bahari, Chuo kimefanikiwa kupata meli moja kwa ajili mafunzo kama inavyotakiwa na sheria zinazosimamia mafunzo ya ubaharia. Kwa niaba yangu mwenyewe na Wizara, tunatoa shukrani za dhati kwao kwa kuendelea kutoa michango yenye lengo la kuboresha mafunzo katika sekta ya Bahari. Tunawaomba waendelea na wadau wengine wajitokeze katika kuboresha sekta hii.

230. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.871 kwa ajili ya kuboresha majengo ya Chuo, kununua mitambo ya kufundishia (engine room simulator) na kununua ardhi ya ukubwa wa ekari 500 Wilayani Mkuranga kwa ajili ya upanuzi wa Chuo. Napenda kutoa taarifa kuwa ulipaji wa fidia kwa wananchi walio chukuliwa maeneo yao Wilayani Mkuranga na ununuzi na usimikaji wa Mtambo wa kufundishia umekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na upimaji na uandaji wa michoro ya matumizi bora eneo hilo.

231. Mheshimiwa Spika, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na upembuzi yakinifu wa eneo kilipo Chuo kwa sasa unaotarajiwa kukamilika Julai, 2016, kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa eneo lake lililopo Kiparan'ganda, Wilayani Mkuranga na ukamilishaji wa maandalizi ya kozi mpya kwa kiwango cha shahada katika fani ya lojistiki za usafirishaji wa mizigo (Port & Shipping Logistic Management) pamoja na sheria na bima za uchukuaji na usafirishaji wa mizigo (Maritime Law & Insurance). Uanzishaji wa kozi utaongeza udahili wa wanafunzi kwa kozi zote kutoka 528 waliopo hivi sasa hadi kufikia 800.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

232. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji ili kiendeleo kuwa kituo bora kinachokidhi mahitaji ya mafunzo, utafiti na ushauri elekezi katika Sekta ya Uchukuzi. Aidha, Chuo kiliendesha kozi za muda mrefu kuanzia Astashahada ya awali hadi Stashahada ya Uzamili katika taaluma za Uongozi katika usafirishaji, uondoshaji na usafirishaji mizigo na uhandisi wa mitambo na magari. Katika mwaka 2015/2016, Chuo kilidahili wanafunzi 2,516 ikilinganishwa na wanafunzi 1,688 waliodahiliwa mwaka 2014/2015. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 40. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kwa asilimia 88 kutoka wanafunzi 3,248 waliokuwepo mwaka 2014/2015 hadi wanafunzi 6,118 waliopo hivi sasa.

233. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu Chuo kimechukua hatua mbalimbali ili kuanza kutoa mafunzo yatakayoimarisha huduma za usafiri wa anga. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka 2015/2016, Chuo cha NIT kimeanzisha rasmi kozi ya Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Matengenezo ya Ndege (Aircraft Maintenance Engineering) na kudahili wanafunzi 38. Aidha, Chuo kinaendelea na ujenzi wa karakana ya ndege kwa ajili ya mafunzo. Napenda kutumia fursa hii kuwasihahi Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kupeleka vijana wao katika Chuo cha NIT kwa ajili ya kuchukua kozi mbalimbali ikiwemo hii ya uhandisi wa matengenezo ya ndege ili kuboresha sekta ya usafiri wa anga na kupunguza gharama za mafunzo nje ya nchi.

234. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mwaka 2014/2015, Chuo kilikamilisha ujenzi wa Kituo Cha Kisasa Cha Ukaguzi wa Magari na kusimika Mtambo mmoja wa ukaguzi wa magari. Aidha, Chuo kiliingia mkataba wa kukagua magari yaliyotumika na kuingia nchini bila kukaguliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa, katika kipindi cha Agosti, 2015 hadi Aprili, 2016, Kituo hiki kimekagua jumla ya magari 368. Chuo kinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufunga mashine zingine tatu za ukaguzi wa magari.

Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)

235. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usafiri wa Anga (*Civil Aviation Training Centre - CATC*) kimeendelea kutoa mafunzo yanayohusu usafiri wa anga katika fani za uongozaji ndege, mawasiliano ya taarifa za anga, usambazaji wa taarifa za safari za ndege, usalama na upekuzi wa viwanja vya ndege na utafiti na ushauri kuhusu usalama wa usafiri wa anga. Aidha, katika mwaka 2015/2016, jumla ya wanafunzi 513 walihitimu mafunzo hayo ikilinganishwa na wanafunzi 557 walihitimu katika kipindi cha mwaka 2014/20, upungufu huu unatokana na ushindani unaojitokeza kutoka vyuo vingine kama vile vya Afrika ya Kusini na Nairobi, Kenya. Kati yao wanafunzi 460 ni watanzania na 53 ni kutoka nje ya nchi.

Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma

236. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutoa mafunzo ya kati ya hali ya hewa kupitia Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya wanafunzi 33 wanaendelea na mafunzo ya ngazi ya awali (certificate) na wanafunzi 24 ngazi ya Diploma. Chuo kimeendelea kutoa wataalam wanaopunguza changamoto ya uhaba wa wafanyakazi katika vituo vya haliyahewanchini.

Chuo cha Reli Tabora (TIRTEC)

237. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Reli Tabora pamoja na Kampasi yake ya Morogoro kimeendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi. Katika mwaka 2015/2016, Chuo kilidahili wanafunzi 226 ikilinganishwa na wanafunzi 187 waliidahiliwa mwaka 2014/2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 21. Aidha, jumla ya watahiniwa 179 walihitimu mafunzo katika mwaka 2015/2016 ikilinganishwa na wahitimu 53 mwaka 2014/2015. Hadi sasa Chuo kina jumla ya Wanafunzi 365. Kati yao wanafunzi 230 wako kampasi ya Tabora na wanafunzi 135 kampasi ya Morogoro.

238. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Chuo kilichukua hatua zifuatazo ili kukamilisha upungufu uliopo kwa ajili ya kupata ithibati ya kudumu (full Accreditation). Hatua hizo ni pamoja na kukamilisha maabara inayokidhi viwango, kuajiri walimu wenye sifa stahiki, kuanza kulipa ada za mafunzo NACTE na kujenga uzio wa Chuo. Baada ya kukamilisha upungufu huu, Chuo kinatarajia kupata Ithibati ya kudumu katika mwaka 2016/2017.

E. MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara

239. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa wanawake wanashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilikamilisha rasimu ya Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara na mafunzo kwa Makandarasi wanawake yalifanyika mwezi Desemba, 2015. Aidha, Wizara ilifanya vikao na wanafunzi wa shule kumi na moja (11) za sekondari za wasichana katika Wilaya za Mkuranga, Bagamoyo na Kisarawe katika mkoa wa Pwani ili kuwashawishi waweze kusoma masomo ya hisabati na sayansi yatakayowasaidia kusomea fani za uhandisi. Wizara pia inaandaa mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu (database) kwa wanawake wanaoshiriki kazi za ujenzi wa miundombinu.

Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa

240. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imeendelea kushiriki katika masuala yanayohusu Sekta ya Usafirishaji, Mawasiliano na hali ya hewa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

241. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara imeshiriki katika kutunga Kanuni za Udhhibiti wa Uzito wa Magari ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Udhhibiti wa Uzito wa Magari katika Jumuiya (EAC Vehicle Load Control Act, 2013). Kanuni hizo zimeidhinishwa na Mkutano wa 33 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya. Aidha, uzinduzi wa ujenzi wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Sakina – Tengeru (km 14.1) na ujenzi wa Arusha Bypass (km 42.4) ulifanywa na Marais wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 03/03/2016. Mradi huu ni sehemu ya mradi wa kikanda wa Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi (Tanzania/Kenya). Vilevile, usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Saadani – Tanga (km 178) umekamilika chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Barabara hiyo itaungana na barabara ya Tanga –

Horohoro iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na Lunga Lunga – Mombasa – Malindi kwa upande wa Kenya. Aidha, mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakanazi (Kibondo) – Kasulu – Manyovu (km 258) inayoungana na nchi ya Burundi na barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92) inayoungana na nchi ya Rwanda unaendelea chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

242. Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Wizara inaendelea kushiriki katika majadiliano ya biashara ya huduma katika maeneo yanayohusu Wizara katika mikutano ya kikanda kwa nchi za SADC. Baadhi ya maeneo yanayopendekezwa kufunguliwa ni: Utoaji wa huduma za uchukuzi kwa njia ya maji, anga, reli, barabara, mawasiliano ya simu na usafirishaji wa vipeto na vifurushi. Huduma nyingine ni ujenzi (*general construction works*), huduma za kihandisi kwa kazi za ujenzi (*general construction works engineering*), “*installations and assembly works*”, kazi za umaliziaji wa majengo (*building completion and finishing works*), na kazi za ujenzi za ufundi maalum (*special trade construction works*). Masuala mengine yanahusisha utambuzi wa taaluma (*mutual recognition agreement*) za uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi katika makubaliano hayo. Aidha, Wizara iliandaa miradi ya barabara, reli, bandari, mawasiliano na viwanja vya ndege iliyojumuishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa SADC (SADC Revised Regional Indicative Strategic Plan –RISDP) wa mwaka 2015-2020.

243. Mheshimiwa Spika, Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Mawasiliano Kimataifa (International Telecommunication Union, ITU) ilishiriki Mkutano Mkuu wa Dunia kuhusu Masafa (World Radiocommunication Conference) na kufanikiwa kutetea masafa yanayotumika kwa huduma mbalimbali ikiwemo utangazaji hapa nchini yasipangiwe matumizi mengine na hivyo kufanya huduma mbalimbali hapa nchini kuendelea kupatikana kwa wananchi. Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya kubadilisha teknolojia ya utangazaji kutoka analogia kwenda dijitali, ilipigania upangaji wa masafa yaliyopatikana ili yatumike kwa huduma za mawasiliano ya *broadband* kupitia simu za kiganjani ambayo yatasaidia juhudi za kufikisha huduma za “*broadband*” hadi vijijini kwa ubora zaidi.

Maendeleo ya Watumishi

244. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka watumishi 28 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 147 katika mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi 14 walijajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo yauzeeni na 9 walithibitishwa kazini, watumishi 7

walibadilishwa vyeo na watumishi 31 walipandishwa vyeo. Wizara pia imekamilisha mpango wa miaka mitatu wa urithishanaji madaraka (3 years succession plan). Lengo la mpango huu ni kukabiliana na changamoto za kuwepo kwa rasilimali watu walioandaliwa kujaza nafasi za juu.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

245. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imeboresha miundombinu ya mawasiliano inayotumia TEHAMA (Local Area Network - LAN) pamoja na kuweka mfumo wa e-permits ambao unawezesha wasafirishaji kupata vibali vya kusafirisha mizigo isiyo ya kawaida (*abdonomal load permit*) kwa njia ya mtandao na hivyo kumrahisishia msafirishaji kupata kibali popote alipo. Mfumo huu umeshaanza kutumiwa na wasafirishaji. Aidha, Tovuti ya Wizara imeboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata taarifa mbalimbali zinazohusu Wizara.

Sera na Sheria za Wizara

246. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imeendelea namapitio ya Sera ya Ujenzi, Sera ya Uchukuzi, Sera ya Taifa ya Posta na Sera ya Taifa ya TEHAMA za mwaka 2003 ili kuziboresha ziweze kuendana na mazingira ya sasa. Aidha, Sera Mpya ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji zinatokana na kuhuishwa kwa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 vimekamilika na kuidhinishwa na Baraza la mawaziri katika kikao chake cha tarehe 2 Mei, 2016.

247. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha usalama wa Mtandao uncimarika, Wizara inaendelea na utoaji wa elimu kuhusu Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya Mwaka 2015. Hadi Aprili, 2016 Wizara imetoa elimu kuhusu Makosa ya Kimtandao kwa viongozi wa Jeshi la Polisi, Waendesha Mashtaka, Vyuho Vikuu, Wachunguzi, Wapelelezi, Mahakimu na Majaji. Aidha, elimu kuhusu sheria hizo inaendelea kutolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya Habari. Vilevile, Wizara inaendelea na taratibu za kukamilisha Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi (Personal Data Protection).

248. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya sekta ya mawasiliano yanahitaji mfumo madhubuti wa usimamizi (regulatory) ili kuimarisha ushindani, kuvutia uwekezaji na kuwalinda watumiaji wa huduma za mawasiliano. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Serikali imetunga Kanuni za Huduma za Ziada katika mitandao ya simu (Value Added Services (VAS) Regulations,

GN. No. 320) za mwaka 2015 zilizotangazwa katika Gazeti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 7 Agosti, 2015.

Usalama katika Utoaji wa Huduma za Uchukuzi

249. Mheshimiwa Spika, Vikao vya Wakuu wa Mikoa ya Mwambao wa Bahari ya Hindi na Zanzibar kuhusu Ulinzi na Usalama wa Bandari zisizo rasmi vimeendelea kufanyika. Kikao cha hivi karibuni kilifanyika Mtwara tarehe 26 Februari, 2016 na maazimio ya kikao hicho ni kurasimisha baadhi ya Bandari zisizo rasmi na kuimarisha Kamati za ulinzi na usalama wa maeneo husika. Bandari zisizo rasmi kumi na mbili zilipendekezwa zirasimishwe kama ifuatavyo: Tanga ni bandari ya Jasini, Kigombe, Kipumbwi, Mkwaja na Pangani; Dar es Salaam ni Mbweni; Pwani ni Mlingotini, Kisiju na Nyamisati; Lindi ni Rushungi na Kilwa Kivinje na Mtwara ni Kilambo. Bandari hizo zimependekezwa kurasimishwa baada ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kubaini kiwango cha biashara na mizigo inayopita kwenye bandari hizo. Lengo ni kuziendeleza na kusimamiwa rasmi na TPA.

250. Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua na kupendekeza Bandari zisizo rasmi kurasimishwa pia Kamati za Ulinzi na Usalama za maeneo yenye bandari zisizo rasmi zimeimarishwa kwa kufanya mikutano na Mamlaka ya Udhubiti wa Usafiri nchi kavu na majini (SUMATRA) na TPA kuhusu utaratibu mzuri wa kusimamia bandari hizo katika mikoa ya Tanga mikutano ilifanyika Jasini, Moa, Mwaboza, Monga, Kwale na Kasera, Mkoa wa Dar es Salaam mikutano ilifanyika Pemba Mnazi, Buyuni Mtoni, Kimbiji, Kigamboni, Kunduchi, Ununio na Mbweni na Pwani mikutano ilifanyika Nyamisati, Salele, Mlingotini, Kasiki, Kaole/ Magambani, Jito Kuu na Sadani. Mamlaka zitaendelea kufanya mikutano kama hiyo katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

251. Mheshimiwa Spika, sambamba na kuimarisha usimamizi katika bandari zisizo rasmi, pia Mamlaka ya Usimamizi wa bandari kwa kushirikiana na SUMATRA imefanya taratibu za kurasimisha bandari binafsi tisa (9) zilizopo katika Ziwa Victoria. Utaratibu huu unalengo la kuwatambua rasmi waendeshaji binafsi wa bandari hizo ili kusimamia vema ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuimarisha ulinzi na usalama. Zoezi hili la kurasimisha bandari binafsi litaendelea pia katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa katika mwaka huu wa fedha.

252. Mheshimiwa Spika, ulinzi katika bandari na viwanja vya ndege umeimarika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wengine. Wasafiri wanaojaribu kupita na nyara za Serikali katika bandari na viwanja vya ndege wamekuwa wakibainishwa na kuchukuliwa hatua. Vifaa vya kutambua nyara, madini na silaha katika

Viwanja vya ndege vimeimarishwa. Jeshi la Polisi limeanza kutoa huduma ya ulinzi katika bandari kuu za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Kyela. Aidha, ulinzi katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na Bandari ya Dar es Salaam umeimarika zaidi kwa kutumia Mbwa waliofunzwa kutambua Nyara za Serikali na madawa ya kulevya. Kumekuwepo pia na udhibiti wa usafirishaji wa Fedha nyingi za kigeni kwenda nje ya nchi.

253. Mheshimiwa Spika, Bandari zetu kuu za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mtwara zimeendelea kuhudumia meli za kimataifa kwa kufuata na kutekeleza taratibu mahususi za kiusalama kwa meli na bandari kama zilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa ya Usalama wa meli ambayo Tanzania ni Mwanachama na kufaulu kaguzi zinazofanyika kila mwaka na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization - IMO).

254. Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kilio cha muda mrefu kwa Watanzania kufanya kazi katika Sekta ya mafuta na gesi. Pamoja na kuwepo vijana wenye weledi wa kufanya kazi katika mitambo hiyo, wengi wamekosa sifa juu ya mafunzo ya usalama (*Safety emergency training in maritime and petroleum industry*) ambayo ni muhimu kwa mfanyakazi yeyote yule awe mpishi au mhandisi ili aruhusiwe kufanya kazi hizo. Hatimaye, Chuo cha Bandari kinachosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya mafuta na Gesi kutoka hapa nchini na Norway, kinakamilisha maandalizi ya kuanza kutoa mafunzo na kujenga miundombinu inayotakiwa ili kuendesha mafunzo hayo ambayo hadi sasa mafunzo kama hayo hutolewa nje ya nchi tu. Kwa Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara; mafunzo kama hayo yanatolewa nchini Afrika kusini, Angola na Nigeria. Kutolewa kwa mafunzo hayo hapa nchini kutaongeza fursa ya ajira kwa Wahitimu wetu kufanya kazi katika sekta ya mafuta na gesi, lakini pia kupata wanafunzi kutoka nchi jirani zenye Viwanda vya mafuta na Gesi kama Uganda, Sudan na Kenya. Tunategemea ifikapo Desemba, 2016 mafunzo hayo yatakuwa yameanza. Mafunzo yatatolewa kwa kufuata mitaala ya kimataifa na hivyo, Wahitimu watapewa vyeti vinavyotambuliwa kimataifa.

Usimamizi wa Mazingira

255. Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa Mazingira ya uchukuzi tumeandaa rasimu ya Mpango wa Taifa wa kukabiliana na Mafuta yaliyomwagika Baharini. Mpango huo tayari umewasilishwa katika Kamati ya Taifa ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu na kupata idhini ya utekelezaji.

256. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2004 tunafanya tathmini ya athari za mazingira (EIA) katika utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi. Pia katika kuandaa Sera, Mipango na Programu za maendeleo ya sekta ya Uchukuzi, tunafanya Tathmini ya Athari za Mazingira Kimkakati (SEA). Aidha, tunatoa elimu ya utunzaji wa Mazingira ya Uchukuzi kwa wadau mbalimbali wakiwemo Wananchi wanaoishi karibu na miundombinu ya uchukuzi ili kuimarisha na kuboresha mazingira ya miundombinu hiyo.

257. Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali tunazochukua katika kuhakikisha kuwa mazingira ya Miundombinu ya Sekta ya Uchukuzi yako salama, tunakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo athari za mabadiliko ya tabianchi mfano; mafuriko yanayosababisha uharibifu wa miundombinu ya Uchukuzi mfano reli ya kati katika eneo kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe, Viwanja vya ndege (kiwanja cha ndege cha Mwanza) na madaraja ya reli. Aidha, changamoto nyingine ni baadhi ya wananchi kutupa takataka katika miundombinu ya usafiri.

Udhibiti wa UKIMWI

258. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima ili kujua afya zao. Watumishi waliotambuliwa kuwa na maambukizi ya UKIMWI na wanaoishi na virusi vya UKIMWI waliendelea kupatiwa huduma kwa kuzingatia mwongozo uliopo. Suala la kukabiliana na UKIMWI limekuwa agenda mojawapo katika mikutano ya Wafanyakazi. Hii imesaidia kuwakumbusha wafanyakazi kuhusu umuhimu wa kuchukua tahadhari. Aidha, Wataalam wa afya wameendelea kualikwa ili kutoa elimu ya kujikinga pamoja na jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI.

F. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

259. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo pamoja na mikakati ya kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:

260. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara ilikabiliwa na changamoto ya **upungufu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.** Katika kutatua changamoto hii, Wizara imeendelea kushawishi Sekta Binafsi na Taasisi za Umma kuwekeza katika uendelezaji wa miundombinu. Juhudi nyingine ni kuendelea kuinadi miradi ya Wizara katika mikutano mbalimbali ya wawekezaji Duniani.

261. Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni **uzidishaji wa uzito wa magari ya mizigo unaosababisha uharibifu wa barabara.** Wizara kupitia Wakala wa Barabara imeendelea kudhibiti uzito wa magari barabarani kupitia mizani iliyopo katika Mikoa yote hapa nchini. Mkakati mwingine ni kufunga mfumo wa Kamera (CCTV Cameras) katika vituo vya mizani ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi.

262. Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya **msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam,** mkakati uliopo ni pamoja na kujenga barabara za juu (*flyovers/Interchanges*) katika makutano ya TAZARA, Ubungo, Uhasibu, Chang'ombe na Kurasini. Serikali pia inaendelea kujenga kwa kiwango cha lami barabara za mlিশo (*feeder roads*). Aidha, Wizara inaendelea kufanya utafiti wa kupanua na kuboresha huduma za usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam.

263. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa changamoto ya **uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Barabara na Reli.** Ili kutatua changamoto hii, Wizara imeendelea kuelimisha umma juu ya ufahamu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Sheria ya Reli Na. 4 ya mwaka 2002. Sheria hizi zinazuia aina yoyote ya uendelezaji wa eneo la hifadhi ya barabara na reli. Aidha, alama za kuonesha mipaka ya eneo la hifadhi zimeendelea kuwekwa katika maeneo husika.

264. Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni **kujenga uwezo wa Makandarasi Wazalendo katika kutekeleza miradi ya maendeleo.** Mkakati uliopo ni kuendelea kuwajengea uwezo Makandarasi na Wahandisi Washauri nchini. Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Baraza la Taifa la Ujenzi zimeendelea kutoa mafunzo hayo. Pia, Wizara imeanzisha Mfuko wa kuwasaidia makandarasi wazalendo (*Contractors Assistance Fund - CAF*) kwa lengo la kutoa dhamana za zabuni au malipo ya awali. Aidha, Serikali kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 inawapa upendeleo maalum (*exclusive preference*) Makandarasi wazalendo kufanya ujenzi wa miradi yenye thamani ya chini ya Shilingi bilioni 10.

265. Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya **ajali za barabarani,** Wizara imeanzisha mfumo wa kutambua maeneo hatarishi ya ajali barabarani na kushauri hatua stahiki za kuchukua. Vilevile, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi salama ya barabara kupitia vyombo vya habari. Aidha, Serikali inakusudia kuanzisha Mamlaka ya Usalama Barabarani ili kusimamia kikamilifu masuala ya usalama barabarani.

266. Mheshimiwa Spika, Changamoto nyingine ni **wizi wa miundombinu ya uchukuzi kutokana na biashara ya chuma chakavu.** Mikakati iliyopo ili kukabiliana na changamoto hii ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya uchukuzi kwa lengo la kupunguza Uharibifu/ hujuma ya miundombinu hiyo na kuendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wanaoharibu miundombinu ya uchukuzi.

267. Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya **ushindani wa kibiashara kutoka katika taasisi zilizo nje ya nchi,** Wizara imeendelea kuelekeza taasisi zake kuboresha miundombinu na huduma, kujitangaza, kufungua ofisi katika nchi jirani na kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha ili kukabiliana na changamoto hii.

268. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto ya **tishio la ugaidi na uharamia katika utoaji wa huduma za uchukuzi.** Kwa kuwa changamoto hii inahusisha mataifa mbalimbali Duniani, Wizara imeendelea kujenga uwezo wa kitaalamu na vifaa pamoja na kuimarisha ushirikiano na taasisi za kimataifa katika kukabiliana na masuala ya kigaidi na uharamia.

269. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano inakabiliwa na changamoto ya **miundombinu isiyo rafiki kwa ujenzi wa mitambo ya mawasiliano, inayojumuisha ukosefu wa nishati muhimu ya umeme katika maeneo mengi ya vijijini.** Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini inahakikisha inatumia fursa ya usambazaji wa nishati ya umeme vijijini ili kuondoa changamoto zinazowakabili watoa huduma katika ujenzi wa Mitambo ya Miundombinu.

270. Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuongeza juhudi za kushawishi kampuni binafsi kupeleka mawasiliano vijijini ambapo mwitikio kwa mwaka wa fedha 2015/16 umekuwa ni mzuri, bado kuna **maeneo ambayo hayavutii kibiashara** kutokana na gharama kubwa za uendeshaji. Katika kulipatia ufumbuzi suala hili, Serikali inaangalia uwezekano wa kutumia teknolojia rahisi na muafaka kwa maeneo ya vijijini ili kufikia azma yake ya kufikisha mawasiliano vijijini. Vilevile, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka mawasiliano maeneo yote hususan maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara.

271. Mheshimiwa Spika, uelewa mdogo kuhusu **Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta umesababisha ushiriki hafifu katika kutekeleza mpango huo.** Vilevile, baadhi ya barabara na mitaa kutokuwa na majina yaliyorasimishwa, pia kukosekana kwa takwimu halisi za idadi ya barabara na mitaa katika kata pamoja na kukosekana kwa taarifa halisi za makazi

na wakazi katika kata na uharibifu wa miundombinu ya Mfumo kwa maeneo ambayo mradi huu umetekelezwa (Nguzo za Mitaa na Vibao vya Namba za Nyumba). Kwa kulitambua hili, Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeandaa mkakati wa kuwajengea uwezo wadau mahususi kuhusu manufaa yatokanayo na Mpango huu wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta.

G. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

G.1 SEKTA YA UJENZI Makadirio ya Mapato

272. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **58,004,000.00** kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Ufundi na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi.

Matumizi ya Kawaida

273. Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi **35,936,939,500.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **34,287,474,500.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **1,649,465,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara (Sekta ya Ujenzi) na Taasisi zake.

Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

274. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 2,176,204,557,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,248,721,422,000.00** ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 344,838,635,000.00** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi 582,644,500,000.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara.

Vipaumbele vya miradi ya Sekta ya Ujenzi itakayotekelezwa ni miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo na miradi iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.1**. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL SUPPORT)

275. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 500** fedha za ndani kwa ajili ya kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali kwa Watumishi wa Sekta ya Ujenzi. Aidha, fedha hizo zitatumika kununua vitendea kazi na vifaa vingine vya ofisi.

MIRADI YA VIVUKO NA UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI **Vivuko na Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

276. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,500.00**. Maelezo ya kila mradi ni kama ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko

277. Mheshimiwa Spika, mradi huu una lengo la kujenga maegesho ili vivuko viweze kuegushwa na kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko kwa urahisi nyakatizote za mwaka. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 9,029.24** kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo, upanuzi wa maegesho ya Kigamboni, ujenzi wa maegesho ya Bwina ya kivuko cha Chato – Nkome, ujenzi wa maegesho ya Lindi – Kitunda na kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.

ii) Ununuzi wa Vivuko Vipya

278. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 6,059.00** kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni; ununuzi wa kivuko kipya cha Kigongo - Busisi; ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA; ununuzi wa boti ya abiria ya kivuko cha Kilambo - Namoto, ununuzi wa boti ya abiria ya kivuko cha Mkongo – Utete na kazi za ufuatiliaji wa miradi hii.

iii) Ukarabati wa Vivuko

279. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 411.76** kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II (Tanga), ukarabati wa kivuko cha MV Sengerema (Mwanza) na kazi ya ufuatiliaji wa miradi hii.

Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

280. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,000.00**. Maelezo ya kila mradi ni kama ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi na Ofisi za Serikali

281. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,796.20** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Urambo na ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mikoa ya Shinyanga (1), Kagera (1), Mtwara (1), Kilimanjaro (1), Dar es Salaam (1), Dodoma (1), Iringa (1), Mwanza (1), Tanga (1), Tabora (1) na Ruvuma (1). Kazi nyingine ni kujenga nyumba za makazi Ikulu (Dar es Salaam) na kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bariadi.

ii) Huduma za Ushauri, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Majengo na Nyumba za Serikali

282. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya **Shilingi milioni 359.99** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya huduma za ushauri, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali.

iii) Ukarabati wa Nyumba, Ofisi, Karakana, na Ununuzi wa Samani kwa Nyumba za Viongozi

283. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,843.81** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa uzio, kuweka mfumo wa ulinzi na kukarabati nyumba za viongozi wa Serikali zilizopo Mikocheni, Kijitonyama na Msasani Peninsular. Kazi nyingine ni ukarabati nyumba ya Jaji iliyopo Iringa; kukarabati Ikulu Ndogo za Chamwino na Arusha pamoja na kukarabati karakana za Serikali chini ya Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na Dodoma. Vilevile, fedha hizi zitatumika kufanya maboresho ya kiutendaji kwa kufanya ukarabati wa karakana za Vikosi vya Ujenzi (Carpentry Workshops) zilizopo Dar es Salaam na Dodoma; kukarabati ofisi za Vikosi vya Ujenzi zilizopo Dar es Salaam, Dodoma na Arusha pamoja na kuongeza vifaa na vitendea kazi. Aidha, utafanyika ununuzi wa samani kwenye Ikulu Ndogo za Serikali.

iv) Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

284. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 140** kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors).

MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA

Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 128)

285. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,626.00** kwa ajili ya kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze (km 128) kwa kiwango cha “Expressway” kwa utaratibu wa kushirikisha Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Aidha, kazi zingine ni kufanya ukarabati wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24).

Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 107) na Bagamoyo (Makurunge) – Saadan–Tanga (km 178)

286. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 31,352.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Bagamoyo – Msata (km 64), daraja la Ruvu Chini pamoja na ujenzi wa kilometa 4.2 za barabara za maingilio ya daraja hilo. Aidha, mradi utahusisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge) – Saadani–Tanga (km 178).

Barabara ya Usagara – Geita – Kyamyorwa (km 422)

287. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 34,735.00** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Uyovu – Bwanga – Biharamulo (km 112) na ukarabati wa barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo (km120). Aidha, fedha hizi zitahusisha sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi kwa sehemu ya Geita – Usagara (lot 1 na 2) (km 90) na kulipa fidia ya mali zilizoathiriwa na ujenzi wa barabara ya Buzirayombo – Geita (km 100).

Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 491)

288. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 69,915.26** kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya malipo ya mwisho ya Makandarasi waliojenga miradi ya Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi, barabara ya Kidahwe – Uvinza na barabara ya Tabora–Ndono. Kazizingine ni kukamilisha ujenzi wa sehemu ya Ndono – Urambo na Kaliua – Kazilambwa. Aidha, Wizara itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Uvinza – Malagarasi na barabara ya Urambo - Kaliua.

Barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/ Bomang’ombe – Sanya Juu (km 173), Arusha – Moshi – Holili (km 140), KIA - Mererani (km 26), Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16.0) na Kiboroloni – Kikarara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)

289. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 96,419.95.** Fedha hizo ni kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya mwisho ya Makandarasi wa barabara ya Rombo Mkuu – Tarakea, barabara ya Marangu – Rombo Mkuu na Mwika – Kilacha. Aidha, fedha hizo zitatumika kuendelea na ujenzi wa njia nne kutoka njia mbili za sasa za barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.10) na njia mbili kwa sehemu ya Arusha Bypass (km 42.41) pamoja na kuendelea na ujenzi wa barabara ya KIA – Mererani. Vilevile, Makandarasi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama - Machame Jct na barabara ya Kiboroloni – Kikarara – Tsuduni – Kidia watalipwa. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Sanya Juu – Kamwanga kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95)

290. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 85.00** fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Makandarasi.

Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127)

291. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,150.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini na malipo ya sehemu ya gharama za usuluhishi (Arbitration) kwa sehemu ya Dodoma – Manyoni. Aidha, mradi utahusisha kulipa sehemu ya madai ya fidia kwa ajili ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (*One Stop Inspection Station - OSIS*) cha Muhalala

(Manyoni) na kununua mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion - WIM*) utakaojengwa kwenye mizani iliyopo Nala (Dodoma).

Ukarabati wa Barabara ya Port Access (Nelson Mandela) (km15.6)

292. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,995.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi pamoja na kuanza maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Dar Port – TAZARA (km 6).

Barabara ya Dumila – Kilosa (km 63)

293. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,838.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyejenga sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45), kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 18) pamoja na maandalizi ya ujenzi wa mizani ya kisasa (*Weigh in Motion - WIM*) ya Dakawa.

Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)

294. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 43,624.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai Kasanga Port (km 112) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50).

Ujenzi wa Madaraja Makubwa

295. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 47,236.00** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madaraja ya Kirumi (Mara), Sibiti (Singida), Sukuma (Mwanza), Kilombero (Morogoro), Kavuu (Katavi), Mbutu (Tabora), Momba (Songwe/Rukwa), Simiyu (Simiyu), Lukuledi II (Lindi) pamoja na Daraja Jipya la Wami (Pwani). Kazi zingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa Daraja Jipya la Selander, Daraja la Mlalakuwa, Daraja la Ruhuhu na Daraja la Mara pamoja na ununuzi wa vyuma vya Madaraja ya Dharura (*Emergency Bridge Parts*).

Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta - km 17)

296. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 1,148.00** zimetengewa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Kawawa Jct – Mwenge.

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 170)

297. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 17,925.00** zimetengewa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1).

Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero (km 150)

298. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 56,445.22** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi wa barabara ya Isaka – Ushirombo (km 132), kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110) na ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero (km 58) pamoja na madai ya Mkandarasi wa Rusumo OSBP. Kazi nyingine ni maandalizi ya ujenzi wa mizani inayopima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion - WIM) ya Mwendakulima (Shinyanga).

Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7)

299. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 79,528.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85) na sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.3). Kazi nyingine ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4).

Barabara ya Korogwe – Handeni (km 65)

300. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 10,794.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyejenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Barabara za Mikoa

301. Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 30,000.00** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya **kilometa 712.40** kwa kiwango cha changarawe, kujenga **kilometa 63.8** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa **madaraja 15**. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 10)

302. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya **Shilingi milioni 1,574.00** zitatumika kuendelea na ukarabati wa sehemu zilizoharibika katika barabara hii.

Barabara ya Handeni – Mkata (km 54)

303. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 barabara hii imetengewa **Shilingi milioni 3,655.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 111.85)

304. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 38,966.00** kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara za Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga Jct (km 2.7), Tabata Dampo – Kigogo (km 1.6), Kimara – Kilungule – External (km 9.0), Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14.0), Tegeta – Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi (km 20) sehemu ya Goba – Mbezi Mwisho (km 7), Tangi Bovu – Goba (km 9.0), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeneni (km 2.60), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (sehemu ya Kitunda – Moshi Bar - km 3.2), Ardhi – Makongo (sehemu ya Goba – Makongo - km 4.00) na Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5). Aidha, Makandarasi waliojenga barabara za Ubungo Terminal – Kigogo Roundabout (km 6.4), Jet Corner – Vituka – Davis Corner (km 10.3), Kibamba – Kisopwa (sehemu ya Kibamba – Mloganzila - km 4) na Ubungo – Maziwa – External (km 0.65) watalipwa madai yao. Kazi zingine ni upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki, ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara ya Mwenge – Tegeta (km 12.9).

Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)

305. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 5,029.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga na Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa Daraja la Mkapa katika mto Rufiji.

Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396)

306. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,144.00** kwa ajili ya kukamilisha usanifu na maandalizi ya nyaraka za zabuni. Kazi nyingine ni maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mikumi - Kidatu – Ifakara (km 103.3).

Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359)

307. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 120,931.09** kwa ajili ya kuanza ujenzi na kulipa fidia kwa watakaopisha ujenzi wa barabara sehemu ya Mpanda – Koga – Ipole - Usesula (km 343) pamoja na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora – Sikonge (sehemu ya Tabora – Usesula, km 30).

Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/ Loliondo – Mto wa Mbu (km 338)

308. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 20,000.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Loliondo – Mto wa Mbu (km 213).

Barabara ya Ibanda – Itungi/Kajunjumele – Kiwira Port (km 26)

309. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,157.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara ya Ibanda – Kiwira Port sehemu ya Kajunjumele – Kiwira Port na barabara ya Ibanda – Itungi Port. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (sehemu ya Tenende – Matema: km 34.6).

Barabara ya Nzega – Tabora (km 114.7)

310. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 51,661.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Makandarasi wa sehemu ya Nzega – Puge (km 58.6) na sehemu ya Puge – Tabora (km 56.10).

Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 768)

311. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 77,561.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga – Kanazi (km 75), sehemu ya Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6) na sehemu ya Sitalike – Mpanda (km 36.9) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Mpanda – Mishamo sehemu ya Mpanda – Usimbili (km 30).

Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17) na Bulamba – Kisorya (km 51)

312. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 70,922.00** kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 80), malipo ya madai ya Mkandarasi wa mradi wa Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5), kuendelea na kazi ya ujenzi wa sehemu ya barabara ya Usagara – Kisesa Bypass (km 17), kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 50), kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55) na Musoma – Makojo – Busekela (km 92). Aidha, fedha zilizotengwa zinajumuisha malipo ya madai ya mradi wa barabara za Mwanza mjini na ukarabati wa barabara ya Makutano – Sirari (km 83).

Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 154)

313. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 32,525.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Magole – Turiani (km 48.8).

Ujenzi wa Flyovers Jijini Dar es Salaam na Barabara za Maingilio

314. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 36,712.545** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa 'Flyover' ya TAZARA; malipo ya awali ya Mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo pamoja na usanifu wa makutano ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata na Morocco. Kazi nyingine ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya TAZARA – JNIA (km 6).

Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171)

315. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 46,961.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi wa barabara ya Bariadi – Lamadi (km 71.8) na kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50).

Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Ipole – Rungwa - km 172)

316. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 861.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 350)

317. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 39,856.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50), sehemu ya Nyakanazi – Kibondo (km 50) pamoja na kukamilisha mapitio ya usanifu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Nyakanazi/Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 258).

Barabara ya Kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia Airport Access Road, km 16)

318. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Barabara ya Dodoma University (km 12)

319. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi za Daraja

320. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 27,233.00** kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara unganishi za Mjimwema – Vijibweni (km 1.5), Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.6).

321. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara pia itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo: **Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu za Ukanda wa Kati** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** kwa ajili ya kuendelea na kazi ya usanifu wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ukanda wa Kati.

Upanuzi wa Barabara ya JNIA – Pugu (km 8) ambao umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya JNIA – Pugu (km 8).

Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara na madaraja hayo.

Ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii.

Upanuzi wa Barabara ya Bandari (km 1.2), Ujenzi wa Barabara ya Dockyard (km 0.7) na Mivinjeni (km 1.0) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya ufuatiliaji. Mradi huu unatekelezwa na Mamlaka ya Bandari kwa ufadhili wa *TradeMark East Africa (TMEA)*.

Ujenzi wa Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34.0) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 950.00** kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na barabara ya Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3). Lengo ni kupunguza msongamano wa magari kwa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami (njia 6).

Ujenzi wa Mizani Karibu na Bandari ya Dar es Salaam umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mizani ya kupima uzito wa magari karibu na Bandari ya Dar es Salaam.

Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (km 276.01) ambayo imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 17,972.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Mpemba – Isongole (km 51.2) na Tunduma – Sumbawanga eneo la Tunduma Mjini (km 1.6).

Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 154) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,457.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

Barabara ya Arusha – Namanga (km 105) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

Barabara ya Singida – Babati – Minjingu (km 223.5) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,047.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Singida – Katesh (km 65.1), Katesh – Dareda (km 73.8) na Dareda – Babati – Minjingu (km 84.6).

Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (sehemu ya KAMATA – Bendera Tatu, km 1.3) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,586.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi kwa kupanua barabara ya Gerezani (Sehemu ya KAMATA – Bendera Tatu) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe pamoja na Daraja la Mzinga.

Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/ Ikokoto Mafinga (km 445.8) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 69,567.910** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyekarabati barabara ya Iringa – Mafinga (km 68.9), kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Mafinga – Igawa (km 137.9), maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152), ujenzi wa barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete (km 109), maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Njombe – Lupembe – Madeke (km 50) na ujenzi wa barabara ya Igawa – Mbarali – Ubaruku (sehemu ya Mbarali – Ubaruku km 8.9).

Barabara ya Korogwe – Mkumbara – Same (km 172) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,609.670** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarsi wa barabara za Korogwe – Mkumbara (km 76) na Mkumbara – Same (km 96).

Barabara ya Mbeya – Makongolosi - Mkiwa (km 528) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 45,107.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu za Chunya – Makongolosi (km 43) na Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (sehemu ya Itigi – Mkiwa: km 35).

Barabara ya Chalinze – Segera – Tanga (km 245) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,100.00** kwa ajili kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Kitumbi – Segera – Tanga (km 120) na Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass: km 10).

Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 35,375.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50).

Daraja Jipya la Ruvu limetengewa jumla ya **Shilingi milioni 350.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mwisho ya Mkandarasi.

Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,460.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Iringa – Migori (km 95.1), Migori – Fufu Escarpment (km 93.8) na Fufu Escarpment – Dodoma (km 70.9). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass, km 7.3).

Barabara ya Dodoma – Babati (km 251.4) ambayo imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 81,068.270** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35) na Mela – Bonga (km 88.80). Aidha, Mkandarasi wa sehemu ya Bonga – Babati (km 19.6) atalipwa madai yake.

Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 623.3) ambayo imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 125,718.140** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Mangaka – Nakapanya (km 70.5), Nakapanya – Tunduru (km 66.5), Mangaka – Mtambaswala (km 65.5), Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimatera (km 68.2) na Kilimatera – Namtumbo (km 60). Aidha, kazi za ufuatiliaji wa mradi wa barabara ya Namtumbo – Songea (km 72) katika kipindi cha uangalizi wa ufanisi wa mradi zitafanyika. Kazi zingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Masasi – Newala – Mtwara (sehemu ya Mtwara – Mnivata, km 50) na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea – Nanganga (km 91).

Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Ofisi za Mikoa umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,866.00** kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) pamoja na Ofisi za mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

Ujenzi wa Barabara ya Kwenda Chuo cha Uongozi Bagamoyo umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,211.00** katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Dar es Salaam - Bagamoyo kuingia Chuo cha Uongozi pamoja na barabara zilizoko ndani ya Chuo hicho.

MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA

322. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,407.10** kwa ajili ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani nchini, mapitio ya Sheria ya Usalama Barabarani, ukaguzi wa usalama wa barabara, uendeshaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani, kuanzisha mfumo wa kudhibiti mwendokasi wa vyombo vya usafiri barabarani, ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi na ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo. Aidha, mradi wa **Kujenga Uwezo wa Mfumo wa Usalama na Mazingira** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 283.587** kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutoa elimu ya usalama barabarani kwenye shule za msingi na kwa umma.

323. Mheshimiwa Spika, mradi wa **Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 309.314** kwa ajili ya kutoa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hifadhi ya mazingira katika Sekta ya Ujenzi kwa wataalam mbalimbali kutoka Taasisi za Wizara. Kazi zingine ni kuandaa Mfumo wa Kusimamia Mazingira, kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira na kuandaa program za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta.

FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA

324. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi **832,349,290,000.00** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake imetengewa Shilingi **582,644,500,000.00** na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetengewa Shilingi **249,704,790,000.00**.

325. Mheshimiwa Spika, kati ya Shilingi **582,644,500,000.00** zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), TANROADS imetengewa Shilingi **519,870,381,570.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara (Sekta ya Ujenzi) imetengewa Shilingi **57,763,375,730.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi

hiyo. Aidha, Shilingi **5,010,742,700.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara. Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 3 - 5.**

Miradi ya Barabara Kuu

326. Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/17 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya Barabara Kuu ni **Shilingi 16,580,803,000.00.** Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina **kilometa 3,184** na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kupunguzamsongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam **kilometa 28** pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe barabara za **kilometa 10.** Orodha ya Miradi ya Barabara Kuu itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3.**

Miradi ya Barabara za Mikoa

327. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, kiasi cha Shilingi **29,773,307,730.00** kitatumika kutekeleza miradi ya Barabara za Mikoa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (**Kiambatisho Na. 3**). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya ukarabati wa jumla ya kilometa **584.30** kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometa **36.9** kwa kiwango cha lami. Aidha, madaraja **14** yatajengwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Orodha ya miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4.**

Miradi ya Vivuko

328. Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka wa 2016/17 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya miradi ya vivuko ni **Shilingi 4,781,440,000.00.** Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3.**

Miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira

329. Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka wa 2016/17 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira ni **Shilingi 2,545,152,000.00.** Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.3 . Kazi zinazohusu Shughuli za Barabara**

330. Mheshimiwa Spika, usimamizi na ufuatiliaji pamoja na kazi zinazohusu shughuli za barabara umetengewa **Shilingi 4,082,673,000.00.** Mchanganuo wa kazi hizo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3.**

MPANGO WA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17

331. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 519,870,381,570.00** fedha za Mfuko wa Barabara zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja, uendeshaji wa mizani, gharama za usimamizi na uendeshaji wa Wakala wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2016/17. Mchanganuo wa mpango huo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5A hadi 5E.**

MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

Wakala wa Barabara

332. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wakala wa Barabara (TANROADS) umepanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometa 592** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **14** pamoja na ukarabati wa **kilometa 146.5** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Aidha, Wakala umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 22,839**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya **kilometa 4,749** na matengenezo ya madaraja **2,821**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za utawala na usimamizi wa kazi, udhibiti wa uzito wa magari, kazi za dharura, mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu (Performance Based Management and Maintenance of Roads) na kazi zinazosimamiwa toka makao makuu za mipango, usalama barabarani na hifadhi ya barabara.

333. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala utajenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometa 100.7** ambapo **kilometa 63.8** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 36.9** zitajengwa kwa fedha kutoka Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 1,296.70** zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo **kilometa 712.40** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 584.30** zitakarabatiwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara pamoja na kukarabati madaraja **29.**

Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA)

334. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara kupitia Wakala wa Majengo ya Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa jengo lenye Ghorofa 6 (Mtaa wa Moshi Plot Na.5) – Dodoma; kununua viwanja mikoani; kufuatilia upatikanaji wa hati za viwanja vya Wakala mikoani na Makao Makuu; kufanya upembuzi yakinifu kwenye viwanja vya TBA kwa ajili ya miradi ya uwekezaji pamoja na kumaliza ujenzi wa jengo la TBA Makao Makuu na Ofisi ya TBA Mkoa wa Manyara. Kazi nyingine ni kukarabati majengo mbalimbali nchini; kuanza ujenzi wa maghorofa mawili ya flat 8 kila moja katika jengo la EX NMC Mbezi Beach - DSM na maghorofa mawili katika kiwanja Na. 276- Ukonga, DSM; kumaliza nyumba 57 daraja 'B' mikoani; ujenzi wa nyumba 100 za Watumishi mikoani pamoja na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuendeleza karakana za samani mikoani.

335. Mheshimiwa Spika, Wakala pia utaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba za Makazi za Majaji mikoani; ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Urambo; kujenga nyumbaza makazi Ikulu – Dar es Salaam; ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bariadi; kufanya matengenezo ya nyumba za makazi ya Viongozi; ujenzi wa nyumba 256 kati ya nyumba 851 zitakazojengwa Bunju DSM na nyumba 300 kati ya nyumba 600 eneo la Gezaulole, DSM; kukamilisha ukarabati wa jengo la ofisi lililokuwa la Benki ya Posta katika kiwanja Na. 487 eneo la Kilimani, Dodoma pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la kibiashara, Goliondoi – Arusha.

Wakala wa Ufundi na Umeme

336. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara kupitia TEMESA itaendelea na ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo, upanuzi wa maegesho ya Kigamboni, ujenzi wa maegesho ya Bwina ya kivuko cha Chato – Nkome na ujenzi wa maegesho ya Lindi – Kitunda. Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa vivuko vipya vya Pangani – Bweni, Kigongo - Busisi na Magogoni – Kigamboni; ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa karakana za TEMESA; ununuzi wa boti ya abiria ya kivuko cha Kilambo – Namoto na Mkongo – Utete pamoja na ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II na MV Sengerema. Aidha, TEMESA itafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozzi kwenye majengo ya Serikali pamoja na kutoa ushauri wa kibandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozzi na majokofu katika nyumba za Serikali.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

337. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Bodi ya Mfuko wa Barabara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 832,349,290,000.00** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 582,644,500,000.00** zitapelekwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) na **Shilingi 249,704,790,000.00** zitapelekwa Ofisi ya Rais –TAMISEMI. Bodi pia inatarajia kupokea Dola za Kimarekani milioni 10 kutoka Shirika la Misaada la Marekani (USAID) kwa ajili ya ukarabati wa barabara katika Halmashauri nne nchini.

338. Mheshimiwa Spika, Bodi pia imepanga kuimarisha na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mfuko kuwa ya kielektroniki na kushirikiana na TANROADS na Wizara imeweka mfumo wa pamoja wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo vya mizani. Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kupima magari na kutoza faini kutoka Ofisi za Bodi kupitia Mfumo wa Taarifa (Management Information System). Aidha, Bodi imepanga kufanya utafiti kuhusu matokeo ya kiuchumi na kijamii yatoakanayo na matengenezo ya barabara pamoja na kufanya tathmini ya mtandao wa barabara (road inventory and condition survey) ili kubaini taarifa sahihi za thamani, urefu na hali ya barabara kwa ujumla na kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini. Bodi pia itaendelea na ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini. Vilevile, Bodi imepanga kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Bodi na kuhamia Dodoma ifikapo Desemba, 2016.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

339. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Bodi imepanga kusajili wahandisi **950**, mafundi sanifu **150** na kampuni za ushauri wa kihandisi **20** na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu **1,133**. Idadi hii inahusisha wahandisi wahitimu **933** wanaoendelea na mafunzo na **200** wapya wanaofadhiliwa na Serikali na sekta binafsi. Aidha, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi pamoja na kutembelea na kukagua miradi yote ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri. Bodi pia itaendelea kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaam na washauri wote, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi kwa ujumla pamoja na kuwashawishi wahandisi wataalam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogeza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

340. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Bodi inategemea kusajili wataalam wa Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi 95. Aidha, Kampuni 20 za Wabunifu Majengo na 14 za Wakadiriaji Majenzi zimepangwa kusajiliwa katika kipindi hicho.

Bodi pia itaendelea kuwajengea uwezo wahitimu katika taaluma inazosisimamia kwa kupitia mpango wa kutoa mafunzo kwa vitendo. Aidha, katika kuhakikisha kuwa ukaguzi wa miradi ya ujenzi unaboreshwa, Bodi itaimarisha ofisi zake za kanda nchi nzima.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

341. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Bodi imepanga kusajili jumla ya makandarasi wapya 900 pamoja na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi 2,800. Aidha, Bodi imepanga kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wawekezaji wanaokiuka na kuvunja sheria za ujenzi. Bodi pia imepanga kuendesha kozi tano za mafunzo kwa makandarasi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma. Aidha, Bodi itaendelea kuboresha Mfuko wa kuwawezesha Makandarasi Wazalendo (Contractors Assistance Fund) ili waweze kupata dhamana mbalimbali.

Baraza la Taifa la Ujenzi

342. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Baraza limepanga kuendelea kuratibu mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi (Construction Sector Transparency Initiative - CoST) ili kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ikitilia mkazo kujenga uwezo wa taasisi husika kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria zilizopo; kuratibu utatuzi wa migogoro; kuboresha ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za sekta ya ujenzi kwa kuboresha kituo cha rasilimali ya habari na kukipatia nyaraka muhimu pamoja na kutathmini, kuhuisha na kuchapisha nyaraka zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi; kuchapisha matokeo ya tafiti zikiwemo bei za vifaa vya ujenzi na ukokotoaji wa bei kwa kipimo cha mraba; kuanzisha database ya gharama za ujenzi pamoja na kuchambua upya kanuni za ukokotoaji wa mabadiliko ya bei za ujenzi.

Baraza pia litaendelea na jitihada za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*) kwa kushirikiana na Taasisi inayoshughulikia Sekta Binafsi (*Tanzania Private Sector Foundation - TPSF*) na wadau wengine wa maendeleo, Baraza litaendelea kuratibu maendeleo ya wajenzi katika sekta isiyo rasmi kwa kukiimarisha Chama cha Wajenzi wa Sekta Isiyo Rasmi (*Tanzania Association of Informal Construction Workers - TAICO*) na kuwashawishi wajenzi wa sekta isiyo rasmi waliopo Dar es Salaam na mikoani kujiunga na chama hiki.

Vikosi vya Ujenzi

343. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Vikosi vya Ujenzi vimepanga kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za viongozi wa Serikali pamoja na maghala. Aidha, Vikosi vinatarajia kuimarisha mradi wa utengenezaji na uuzaji wa vifaa vya ujenzi (*Building Materials Centre*) Dar es Salaam na Dodoma, pamoja na kviendeleza viwanja 38 vinavyomilikiwa na Vikosi vya Ujenzi mjini Dodoma.

Vikosi vitaendelea na ukarabati wa karakana zake zilizopo Dar es Salaam na Dodoma, ukarabati wa ofisi za Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha pamoja na kuongeza vitendea kazi.

Chuo cha Ujenzi Morogoro

344. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 Chuo cha Ujenzi Morogoro kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi **945** wa fani za Barabara na Ukaguzi wa Madaraja, Majengo, Magari, Mfumo wa Umeme na Elektroniki. Mafunzo ya Madereva wa Umma, fani za ufundi mbalimbali (*Basic Artisans*), Madereva wa awali, Madereva wa Magari ya Abiria, Ufundi Mitambo (*Plant Mechanics*) na uendeshaji wa mitambo (*Plant Operation*). Aidha, Chuo kitaendelea na mipango ya kutoa mafunzo kwa makandarasi wanaotekeleza shughuli za ukarabati wa barabara, majengo na umeme, hasa kwa wale makandarasi wa kazi maalum (*Specialized Contractors*) daraja la I – III na wale waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi wa madaraja ya chini.

Chuo pia kimejipanga kuendeleza ukarabati wa majengo yake matatu na kujenga karakana mpya ya ufundi bomba, kuendeleza ujenzi wa karakana ya ufundi, kukarabati mitambo **3** ya kufundishia na kununua vitendea kazi vya kufundishia masomo ya ufundi. Chuo kinatarajia kununua gari moja kwa ajili ya kufundishia madereva, kukarabati magari yaliyopo na kununua kifaa cha kielektroniki cha kukagulia magari.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATTI) - Mbeya

345. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Chuo kinatarajia kuendesha mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe; mafunzo ya uwekaji tabaka la lami (*Surface Dressing*) kwa Wahandisi (10), Mafundi Sanifu (30) na wasimamizi wa barabara (30); kuboresha mitaala ya Chuo ya utoaji wa mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvukazi pamoja na kuanzisha mafunzo mapya. Chuo pia kitaendelea kutoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa vitendo. Aidha, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo na kuhamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa umma, kwa njia ya makongamano na kuendelea kutoa ushauri wa matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa wadau mbalimbali.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

346. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na uchukuzi hapa nchini. Kituo kitasambaza taarifa zinazohusu teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maktaba ya Kituo. Aidha, Kituo kimepanga kuandaa na kuendesha mafunzo kupitia warsha na semina kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi, na kuendelea kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji hapa nchini. Vilevile, Kituo kitaendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Morgan cha Marekani na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto za msongamano wa magari katika miji mbalimbali hapa nchini kwa kuanzia na jiji la Dar es Salaam.

MASUALA MTAMBUKA

Maendeleo ya Rasilimali Watu

347. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara itaendelea kuwaendeleza watumishi wake ili kuwaongezea uzoefu wa kikazi na kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Watumishi watapandishwa vyeo kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na taarifa za Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi (OPRAS).

Habari, Elimu na Mawasiliano

348. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara itaendelea kutoa taarifa na kuelimisha umma kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) kupitia tovuti (www.mow.go.tz), vipindi vya radio, televisheni pamoja na machapisho.

Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara

349. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara imepanga kutekeleza kazi mbalimbali zenye lengo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Wizara kupitia Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara itaendelea kuhamasisha wasichana wa shule za sekondari wasome masomo ya sayansi ili kuongeza idadi ya wanawake katika fani ya uhandisi. Vilevile, mafunzo kwa makandarasi wanawake kuhusu kutumia teknolojia ya nguvukazi pamoja na namna ya kuandaa zabuni yatafanyika. Aidha, Wizara itachapisha na kugawa miongozo ya namna ya kufanikisha ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara na kutoa elimu kwawadau kuhusu matumizi ya miongozo hiyo kupitia warsha.

Mapitio ya Sera ya Ujenzi

350. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara imepanga kukamilisha maboresho pamoja na kuandaa mikakati ya Sera ya Ujenzi itakayolenga zaidi kuwajengea uwezo wadau wa Sekta ya Ujenzi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

G.2 SEKTA YA UCHUKUZI Matumizi ya Kawaida

351. Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Sekta ya Uchukuzi) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi **91,519,632,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **52,430,658,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **39,088,974,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara (Sekta ya Uchukuzi) na Taasisi zake.

Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

352. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 2,495,814,130,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,322,603,400,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 173,210,730,000.00** ni fedha za nje (Kiambatisho Na 6).

MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

353. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara (Sekta ya Uchukuzi) imepanga kutekeleza miradi ifuatayo:

- (i) Kutandika reli nzito za ratili 80 kwa yadi katika umbali wa km 61 kati ya Lulanguru na Tabora, km 283 kati ya Dar es Salaam – Kilosa, Igalula – Tabora na Tabora – Isaka, kununua vipuri vya Mtambo wa kuzalisha kokoto wa Tura, ununuzi wa Mtambo wa kukagua na kupima njia ya reli na uzalishaji wa mataruma katika karakana ya Pugu, Shilingi bilioni 105.16 zimetengwa;
- (ii) Kutandika reli katika njia ya Kaliua – Mpanda, kujenga daraja moja (km 185), makalavati matatu (km 154,162, na km 174 Kaliua – Mpanda), na ujenzi wa stesheni na jengo la kuhifadhia mizigo katika stesheni ya Mpanda, Shilingi bilioni 5.5 zimetengwa;
- (iii) Ukarabati wa njia kuu ya reli. Kazi zitakazohusika ni pamoja na kuendelea na matengenezo ya maeneo yaliyoathiriwa na mvua kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe, Ujenzi wa madaraja 10 kati ya 38 yaliyo katika hali mbaya (condition E) katika njia ya Tabora – Kigoma, usanifu na ujenzi wa madaraja na makalavati 38 yenye uwezo wa tani 25 yaliyo katika hali mbaya (Condition E) kati ya Dar es Salaam – Isaka na kuboresha mfumo wa mawasiliano, Shilingi bilioni 81.78 zimetengwa;
- (iv) Kukamilisha usanifu wa kina, upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli kati ya Tabora – Kigoma na Kaliua – Mpanda, Uvinza – Msongati, Mpanda - Karema, kulipa fidia eneo la Buhongwa na mradi wa reli ya Mpanda – Karema, Shilingi bilioni 15 zimetengwa;

- (v) Shilingi bilioni 5.0 zimetengwa kwa ajili ya kumwajiri Mshauri wa Uwekezaji (Transaction Advisor) atakayesimamia upatikanaji wa fedha pamoja na ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – Mbamba Bay pamoja na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga (km 1000) na kulipa deni la usanifu wa kina wa reli hiyo;
- (vi) Kukamilisha usanifu wa kina wa njia ya reli kati ya Tanga – Arusha na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli *standard gauge* ya Arusha – Musoma, pamoja na matawi yake kwenda Engarukana Minjingu, Shilingi bilioni 9.7;
- (vii) Kufanya usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa reli ya Kati kwa *standard gauge* ambapo Shilingi trilioni 1.0 zimetengwa;
- (viii) Kuboresha eneo la treni kupakia/kupakua mizigo katika bandari ya DSM, pamoja na kukarabati vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka, Shilingi bilioni 5.0;
- (ix) Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam, zikiwemo zile za kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Bagamoyo na ujenzi wa mchepuo wa njia ya reli kutoka “Ilala block post” hadi Stesheni ili kuepusha mwingiliano wa treni ya abiria kutoka Stesheni kwenda Ubungo na ile ya mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam, Shilingi bilioni 7.5 zimetengwa.

354. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) imetengewa Shilingi bilioni 50.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

- (i) Kuanza ujenzi wa meli moja (1) mpya katika Ziwa Victoria ambapo shilingi bilioni 21.0 zimetengwa;
- (ii) Kufanya ukarabati wa meli 2 katika Ziwa Victoria ambazo ni MV Butiama (Shilingi bilioni 3.6) na meli ya MV Victoria (Shilingi bilioni 20.0); na
- (iii) Kufanya ukarabati wa MV Liemba katika Ziwa Tanganyika ambapo shilingi bilioni 5.9 zimetengwa.

355. Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza na kuboresha bandari nchini, katika mwaka 2016/2017, katika Bajeti yake, Mamlaka ya Bandari imetenga Shilingi bilioni 510.677 ili kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kazi ya ujenzi na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na. 1-7; kujenga gati jipya la Ro-Ro; kukamilisha ujenzi wa jengo la kituo kimoja cha huduma kwa wateja (one stop centre); kuhamisha gati la mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga gati jipya la kisasa la kushushia mafuta aina zote; kujenga gati la Nyamisati na kituo cha mafuta na gesi; kuongeza maeneo ya kuhudumia shehena, ukarabati wa 'flow meters'; kujenga uzio wa gati la bandari ya mafia na ghala na kuboresha mifumo ya kazi za mamlaka kutoka katika mifumo ya kawaida na kuingia katika mifumo ya kielektroniki (automation). Kazi hizo zimetengewa jumla ya Shilingi bilioni 342.18;
- (ii) Kuboresha na kupanua bandari ya Mtwara, shilingi bilioni 59.32;
- (iii) Kukarabati maegesho ya meli na sehemu ya kupakulia shehena, kukarabati miundombinu ya barabara ya kuingilia bandarini, kuimarisha ulinzi katika maghala na mnara wa kuongozea meli pamoja na sehemu ya kushuka abiria, ujenzi wa jengo la abiria na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mwambani, Tanga. Shilingi bilioni 7.6 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo;
- (iv) Kuboresha bandari za Maziwa Makuu shilingi bilioni 24.05; na
- (v) Kununua vifaa na mitambo ya kuhudumia shehena na meli shilingi bilioni 77.53.

356. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi imetenga Shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege:

- (i) Kuanza awamu ya pili ya ukarabati wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora, jumla ya shilingi bilioni 14.65 zimetengwa;
- (ii) Usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege cha Songwe (Mbeya) ambapo shilingi bilioni 10 zimetengwa;
- (iii) Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza, ambapo shilingi bilioni 30.15 zimetengwa;
- (iv) Kukamilisha usanifu na Mpango Kabambe (Concept Design & Master Plan) na kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake, maegesho ya ndege, usimikaji wa taa pamoja na mitambo ya kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, ambapo shilingi bilioni 10 zimetengwa;

- (v) Kuanza ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga na Shinyanga, jumla ya shilingi bilioni 19.43 zimetengwa;
- (vi) Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, ambapo shilingi bilioni 50 zimetengwa;
- (vii) Kufanya Usanifu na ujenzi wa kiwanja cha mkoa wa Geita, shilingi bilioni 2 zimetengwa;
- (viii) Kuanza usanifu wa kina wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, shilingi bilioni 2.07 zimetengwa;
- (ix) Ulipaji wa fidia katika kiwanja cha ndege cha Bukoba na eneo la Omukajunguti, shilingi bilioni 3 zimetengwa; na
- (x) Kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha JNIA, shilingi bilioni 58 zimetengwa.

357. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kampuni ya Ndege (ATCL) imetengewa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kununua ndege mpya zisizopungua 3. Idadi kamili ya ndege zitakazonunuliwa na bei ya kila ndege itajulikana baada ya uchambuzi wa suala hili kukamilika.

358. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ya Usafiri wa Anga itatekeleza miradi ifuatayo kupitia bajeti yake:

- (i) Kuanza kazi ya kubadilisha Mtambo mkuu wa VHF katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.0;
- (ii) Kuendelea na taratibu za manunuzi ya rada mbili kwa ajili ya kuongozea ndege za kiraia nchini ambapo Shilingi bilioni 8.8 zimetengwa;
- (iii) Kukarabati mnara wa kuongozea ndege katika kituo cha Pemba, Shilingi milioni 500;
- (iv) Kununua *Simulator* ya kufundishia kwa ajili ya Chuo cha Usafiri wa Anga Shilingi milioni 768;
- (v) Kuendelea na uboreshaji wa mawasiliano katika vituo vya Pemba, JNIA na Chuo cha Usafiri wa Anga kilichopo katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere Shilingi milioni 190.5; na
- (vi) Kuendelea na ufuatiliaji wa eneo la kujenga Chuo cha Usafiri wa Anga nchini huko Fukayose, Bagamoyo Shilingi milioni 200.

359. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Reli (TRL) imeendelea kuboresha huduma zake ili kuvutia wateja na wawekezaji na kuwa na hisa kubwa katika soko la usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi. Ili kufikia malengo hayo, katika mwaka 2016/2017, TRL itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kusafirisha tani 537,500 za mizigo na abiria 541,000;
- (ii) Kuendelea kufanyamatengenezo ya kawaida ya njia; na
- (iii) Kuendelea na ukarabati wa mabehewa ya abiria na mizigo.

360. Mheshimiwa Spika, Ili kufikia malengo yake, katika mwaka 2016/2017, SUMATRA imetenga fedha katika bajeti yake ili kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuendelea na ujenzi wa Jengo la ofisi Makao Makuu, Dar es Salaam ambapo Shilingi bilioni 8.5 zimetengwa;
- (ii) Kuanza usanifu na ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa ya Dodoma na Mbeya, Shilingi bilioni 9.30 zimetengwa;
- (iii) Kununua vifaa maalum vya udhibiti (*Technical and Specialized Regulatory Equipment*) ili kuboresha utekelezaji wa shughuli za Mamlaka, Shilingi bilioni 5.37 zimetengwa; na
- (iv) Kununua viwanja katika maeneo mbalimbali nchini ili kuanza ujenzi wa majengo ya ofisi za Mamlaka na kukarabati ofisi za SUMATRA zinazotumika sasa kwa kuboresha vitendea kazi, Shilingi bilioni 6.0 zimetengwa.

361. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali inatarajia kuwasilisha Bungeni Sheria mpya ya TAZARA ili kuboresha utendaji wake.

362. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa imetenga fedha zifuatazo ili kuendelea kuboresha huduma za sekta ya hali ya hewa nchini. Miradi itakayotekelezwa katika mwaka 2016/2017 ni:

- (i) Kuanza ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa, ambapo Shilingi bilioni 1.0 imetengwa;
- (ii) Kununua vifaa na mitambo ya kupima hali ya hewa, Shilingi milioni 520.0 zimetengwa;

- (iii) Shilingi milioni 27.75 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kutoa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Tanganyika; na
- (iv) Shilingi milioni 100.0 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma.

363. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kinatarajia kuanzisha program za mafunzo katika sekta ya mafuta na gesi (mobile offshore training). Lengo ni kuwapatia Watanzania ujuzi na utaalumu utakao wawezesha kuajiriwa katika sekta hii. Aidha, Chuo kinatarajia kuanzisha kozi za *shipping and logistics management, Maritime Law and Insurance*, kuendelea na upimaji na uchoraji wa ramani kwa ajili ya matumizi ya kampasi ya Mkuranga; kuendelea na ujenzi wa madarasa katika eneo la Barabara ya Sokoine.

364. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimepanga kuendelea na ujenzi wa kituo cha rasilimali mafunzo (Maktaba), ujenzi wa kituo cha kisasa cha ukaguzi wa magari pamoja na ujenzi wa karakana ya mafunzo ya matengenezo ya ndege. Aidha, Chuo kitanunua kiwanja mkoani Dodoma kwa ajili ya kujenga kituo cha mafunzo ya marubani pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwemo magari na 'simulators' za ndege na kuanzisha mafunzo ya *Logistics and Transport management* ngazi ya shahada ya uzamili.

G.3 SEKTA YA MAWASILIANO

Makadirio ya Mapato

365. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Sekta ya Mawasiliano inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **11,011,000** kutokana na mauzo ya Nyaraka za zabuni mbalimbali.

Matumizi ya Kawaida

366. Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Sekta ya Mawasiliano) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi **3,073,949,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,161,623,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **912,326,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara (Sekta ya Mawasiliano).

Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

367. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano imetengewa jumla ya **Shilingi 92,730,110,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 87,730,110,000.00** ni fedha za nje (Kiambatisho Na 7).

368. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano, imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

- (i) Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta, 2003 na Mpango Mkakati wake wa utekelezaji na kuanza kuhuisha Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu (*National Telecommunications Policy, 1997*);
- (ii) Kupitia Sheria ya Kampuni ya Simu Tanzania na Sheria ya Shirika la Posta Tanzania ili kubaini maeneo ya kurekebishwa na hatimaye kuyaimarisha mashirika hayo yaweze kuhimili ushindani;
- (iii) Kuimarisha udhibiti katika sekta ili kuongeza ushindani katika sekta ya mawasiliano kwa lengo la kupunguza gharama za mawasiliano na kuwalinda walaji;
- (iv) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta Dar es Salaam na Zanzibar na kuanza utekelezaji katika miji ya Morogoro, Mwanza na Mbeya ikiwa ni pamoja na kuhimiza matumizi ya mfumo husika;
- (v) Kuimarisha utendaji wa taasisi tano za TCRA, UCSAF, TTCL, TPC na Tume ya TEHAMA;
- (vi) Kuendelea kuratibu miundombinu ya TEHAMA nchini (National ICT infrastructure development programme) ikiwa ni pamoja na ushiriki, utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi makao makuu ya Wilaya zote nchini (Awamu ya III-V);
- (vii) Kuratibu matumizi ya huduma za TEHAMA nchini (*National IT systems and services/applications*);
- (viii) Kusimamia uanzishwaji wa miundombinu wa matumizi salama ya Miamala ya Kielektroniki "Public Key Infrastructure - PKI";

- (ix) Kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (*National Cyber Security Strategy*); na
- (x) Kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (*National Broadband Strategy*).

MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

369. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Shirika la Posta Tanzania litatekeleza kazi zifuatazo:

- (i). Kuimarisha na kuboresha huduma ya *Posta Mlangoni* itakayotoa huduma ya kusambaza barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kwa kupitia Misimbo ya Posta na anwani za makazi kuwafikia wateja hadi majumbani/ofisini kwao. Huduma hii inatolewa katika mikoa ya Dar es salaam, Arusha na Dodoma. Miundombinu ya kuanzisha huduma hii Zanzibar inakamilishwa;
- (ii). Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ofisi 35 zilizounganishwa katika mtandao wa kielektroniki wa *Postglobal Netsmart* ili kufikia ofisi 140 na hivyo, kuwezesha kutoa huduma za kufuatilia (*Track and Trace*) nyaraka, vifurushi na vipeto vinavyotumwa kupitia mtandao wa Posta;
- (iii). Kuanzisha huduma ya Posta (*One Stop Centre*) pamoja na kupatikana kwa *Payment Switch* kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uwakala na huduma za kifedha sehemu za vijijini;
- (iv). Kuimarisha na kuendeleza maduka ya kununua na kuza fedha za kigeni (*Bureau de Change*) katika Ofisi za Posta kwa kufungua maduka Arusha, Mwanza na Tunduma baada ya Dar es Salaam na Tawi la Shangani Zanzibar kuonesha maendeleo mazuri;

Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

370. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/17 Kampuni ya Simu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (i). Kuongeza idadi ya wateja hai (*Active Customers*) wa huduma mbalimbali za simu (voice na data) kutoka 74,790 mwaka 2015 hadi 851,000 mwaka 2018;
- (ii). Kuanzisha na kuendesha mtandao wa kisasa wa simu za kiganjani wa 2G/3G, 4G LTE;

- (iii). Kuboresha mtandao wa *data* na simu za waya/mezani (*fixed network*) ili kuleta ufanisi katika huduma za wateja; na
- (iv). Kuongeza ufanisi katika taratibu za utoaji huduma kwa wateja na nyanja za kuwafikia wateja.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

371. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu sheria, haki na wajibu wa watumiaji, kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa anwani za makazi na misimbo ya posta, uhakiki wa usajili wa laini za simu za kiganjani, haki na wajibu wa watumiaji na masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao;
- (ii) Kuendelea kutekeleza usimamizi wa usalama wa mitandao ya mawasiliano (TZ- CERT);
- (iii) Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kumbukumbu za simu za kiganjani kwa kushirikiana na watoa huduma wa simu za kiganjani (CEIR);
- (iv) Mamlaka itaendelea na utekelezaji wa *Mobile Number Portability* (MNP) kwa kuhamasisha wamiliki wa mitandao na kumpata msimamizi wa *Number Portability Clearing House*;
- (v) Kuratibu ukamilishaji wa kituo cha taifa cha Uokozi na kukabiliana na majanga kwa Kushirikiana na Ofisi ya waziri Mkuu, ikiwa ni pamoja na kuwezesha kutumika kwa namba za kuokoa na za dharura ambazo ni 110, 115 na 118. Pia, kufuatilia utendaji wa namba 111 na 112;
- (vi) Kuweka mfumo wa malipo ya matumizi ya mkongo wa taifa ambao utazingatia Gharama;
- (vii) Kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa taasisi za Ulinzi na Usalama;
- (viii) Kusimamia mfumo wa kumbukumbu, takwimu na taarifa zinazohusu mfumo wa kitaifa wa anwani za makazi na misimbo ya posta; na

- (ix) Kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za huduma za mawasiliano.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (Universal Commucation Service Access Fund - UCSAF)

372. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuendelea kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara nchini kwa lengo la kuyajumuisha katika miradi ya Mfuko;
- (ii) Kuendelea na uangalizi na utekelezaji wa miradi ya kufikisha mawasiliano ya simu katika Kata mia nne na arobaini na tatu (443) ili kuona huduma iliyokusudiwa inawafikia wananchi katika viwango vinavyokubalika;
- (iii) Kutoa Mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 300 kutoka katika shule zilizonufaika na mtandao wa intaneti na vifaa vya TEHAMA kutoka katika Mfuko;
- (iv) Kutathmini na kutoa ruzuku ya ving'amuzi vya matangazo ya kidigitali ya runinga katika mkoa mmoja ambao haujafikiwa na huduma hiyo;
- (v) Kutekeleza mradi wa Wawezeshe Walimu wa Kesho kwa kutoa ruzuku ya kompyuta mpakato kwa wanafunzi 100 wa chuo kikuu cha Dodoma wanaosoma diploma ya ualimu;
- (vi) Kutekeleza mradi wa kuanzisha Vituo 10 vya TEHAMA nchini Tanzania; na
- (vii) Kuendeleza ushirikiano na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano kwa hospitali zote za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa madaktari bingwa katika hospitali zisizo na madaktari bingwa.

Tume ya TEHAMA

373. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume ya TEHAMA itatekeleza mambo yafuatayo:

- (i) Kuandaa muundo, kukusanya rasilimali na kutafuta/kuajiri watumishi;
- (ii) Kuandaa mapendekezo ya muswada wa Sheria ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
- (iii) Kuandaa Mpango Mkakati wa Tume ya TEHAMA;
- (iv) Kuanzisha mfumo wa kutambua na kuendeleza wataalam na utalam wa TEHAMA; na
- (v) Kufanya utafiti katika maeneo ya usalama wa TEHAMA, miundombinu muhimu ya TEHAMA (*critical ICT infrastructure*) na muundo na mahitaji muhimu ya kuanzisha kituo mahiri cha TEHAMA (ICT Park).

SHUKURANI

374. Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kulingoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu na kwa nafasi ya pekee kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushauri wao wenye tija katika kuendeleza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

375. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu katika kuendeleza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini, Finland, Abu Dhabi Fund, Denmark (DANIDA), Ujerumani (KfW), Marekani (MCC), Uingereza (DFID), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait Fund, OPEC Fund, BADEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC.

376. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani (Mb.), Naibu Waziri; Eng. Joseph M. Nyamhanga, Katibu Mkuu (Ujenzi), Dkt. Leonard M. Chamuriho, Katibu Mkuu (Uchukuzi), Prof. Faustin R. Kamuzora, Katibu Mkuu (Mawasiliano), Eng. Dkt. Maria L. Sasabo, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano); Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kujituma katika kutekeleza majukumu tuliropewa na Taifa.

377. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari ambao wametupa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Nitumie fursa hii pia kuishukuru Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

378. Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda niishukuru familia yangu hususan mke wangu na watoto kwa kunifariji na kuniombea wakati nikitokeleza majukumu yangu ya kitaifa.

379. Mheshimiwa Spika, hotuba yangu hii inapatikana katika tovuti za Sekta ya Ujenzi (www.mow.go.tz), Sekta ya Uchukuzi (www.uchukuzi.go.tz) na Sekta ya Mawasiliano (www.mst.go.tz).

MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILANO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/20

380. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/20, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,895,279,317,500.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,212,141,496,500.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi 2,587,333,762,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 95,804,059,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)

381. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 2,212,141,496,500.00** za Sekta ya Ujenzi zinajumuisha **Shilingi 35,936,939,500.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 34,287,474,500.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,649,465,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 2,176,204,557,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,248,721,422,000.00** ni fedha za ndani, **Shilingi 582,644,500,000.00** ni za Mfuko wa Barabara na **Shilingi 344,838,635,000.00** ni fedha za nje.

SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)

382. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 2,587,333,762,000.00** za Sekta ya Uchukuzi zinajumuisha **Shilingi 91,519,632,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 52,430,658,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 39,088,974,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 2,495,814,130,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,322,603,400,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 173,210,730,000.00** ni fedha za nje.

SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)

383. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 95,804,059,000.00** za Sekta ya Mawasiliano zinajumuisha **Shilingi 3,073,949,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 2,161,623,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 912,326,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 92,730,110,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 87,730,110,000.00** ni fedha za nje.

384. Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 (**Kiambatisho Na. 1 - 7**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

385. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Maftaha aliniomba mwongozo, nafikiri niutolee majibu sasa hivi tu. Ni kwamba nilipofuatilia nimeona, hoja ile wakati imetolewa wakati mjadala unaendelea ilifika wakati ambao zimebakia dakika kumi kabla ya muda wa Bunge kwisha. Kwa utaratibu wa kanuni zetu ni kwamba, inapobakia dakika kumi kabla ya muda wa Bunge kwisha, Mwenyekiti anayekuwa anaendesha kikao hicho, anaahirisha mijadala yote na tunaingia kwenye kitu kinachoitwa *guillotine*. Kwa hiyo, haijalishi kuna kitu gani mezani, vyote vinasimama, tunaingia kwenye *guillotine* tunaendelea na utaratibu. Kwa hiyo, utaratibu ule uliotumika jana na Mheshimiwa Zungu ni sahihi kabisa. *(Makofi)*

Naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia masuala hayo ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

(Hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu alichelewa kidogo kufika mbele kwa ajili ya kuwasilisha Maoni ya Kamati)

SPIKA: Kamati wamejisahau! itabidi nimwite msemaji wa upinzani kwanza. *(Makofi)*

Msemaji wa Upinzani kuhusu...

MBUNGE FULANI: Ameshafika.

SPIKA: Ameshafika! Aaah, karibu sana. Kidogo uchelewe Profesa! Ahsante sana.

MHE. DKT. NORMAN A. S. KING - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha mimi pamoja na Kamati yangu kutekeleza jukumu hili.

Pili, napenda kumshukuru Mungu kwa kutupa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambaye kipekee kabisa amewezesha kwa namna moja Bajeti ya Wizara ambayo Kamati hii inasimamia kuongezeka hadi kufikia 17% ambazo siyo kawaida, ni mara ya kwanza kwa mujibu wa utekelezaji wa miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kuwasilisha kwako utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba taarifa yangu ichukuliwe yote kama ilivyoandikwa. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari mwaka 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, maoni yatakayotolewa katika taarifa hii ni kutokana na majukumu ya Kamati kama yalivyobainishwa katika kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6(8) ambayo imeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na cha (2) Kamati ilifanya ukaguzi na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na vikao, kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha unaoishia 2015/2016 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata yaani 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati imechambua mafungu yafuatayo:-

Fungu la 62 - Sekta ya Uchukuzi, Fungu la 98 - Sekta ya Ujenzi na Fungu la 68 - Sekta ya Mawasiliano. Mtiririko wa taarifa hii umezingatia maeneo makubwa matatu ambayo ni mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2015/2016 ikiwemo utekelezaji wa maoni ya Kamati ya

mwaka 2015/2016. Masuala mengine muhimu yalijitokeza wakati wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti hiyo, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile nimesimama hapa nikitambua kwamba mwenye hoja ameshawasilisha na hivyo Kamati yangu nayo inaomba iungwe mkono kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya undani juu ya utekelezaji wa mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016, imeainishwa katika aya ya saba mpaka ya 10 ya taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kulipa madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri ambayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka; katika kutekeleza ushauri huu Serikali imeendelea kulipa madeni kadri fedha zinavyopatikana ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Serikali imelipa shilingi bilioni 635.35. Lengo ni kukamilisha madeni ya miaka ya nyuma ifikapo Juni, 2016. Kamati inasisitiza umuhimu wa kukamilisha ulipaji madeni hayo mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuchukua mikopo kwenye taasisi mbalimbali za fedha ili kuweza kujenga nyumba nyingi na kwa haraka, Kamati imeelekezwa kuwa Wakala imefanikiwa kukopa fedha kutoka benki mbalimbali za CRDB kwa maana ya shilingi bilioni 25 na TIB kwa maana shilingi bilioni 6.9 na shilingi bilioni 3.5 kutoka PSPF kwa ajili ya kujenga nyumba mbalimbali zenye bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizopatikana kwa njia ya mkopo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi 475 eneo la Bunju Dar es Salaam, kumalizia jengo la ghorofa 10 lililopo Goliondoi Mkoa wa Arusha pamoja na jengo la ghorofa nne lililopo Mtaa wa Kilimani, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa matengenezo ya Kivuko cha Magogoni, Kamati imeelekezwa kuwa kazi ya ukarabati inatarajiwa kuanza Mei, 2016 na kwa ujumla Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kudhirishiwa shilingi trilioni 4.2 kama zilivyowasilishwa ama sh. 4,229,408,685,900. Bajeti hii ni sawa na asilimia 16.7 ya bajeti yote ya Serikali, yaani ya shilingi trilioni 29.353.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati ambao umetolewa katika vikao pamoja na ziara mbalimbali zilizofanywa na Kamati. Ushauri huu wa Kamati umezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Tunatambua maendeleo ni vita, kwa hiyo,

maamuzi juu ya maendeleo ni lazima yafanyike mapema na kwa wakati unaotakikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo kwa mara ya kwanza Sekta hii imeweza kupata asilimia 16.7. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba ni muhimu sana Serikali kuongeza bajeti hii miaka ijayo kufika asilimia 20 kwa sababu Wizara ya Miundombinu ndiyo kichochezi cha sekta nyingine zote. Huwezi kujenga miundombinu yote ile isipokuwa kama barabara zinapitika, kama reli inapitika, kama viwanja vya ndege viko sawasawa.

Mheshimiwa Spika, reli ya kati inanufaisha takriban mikoa 15 ya Tanzania. Kwa lugha nyingine, zaidi ya nusu ya Watanzania wanategemea reli ya kati. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa reli ya kati na matawi yake ambayo ni kutoka Dar es Salaam – Kigoma, Uvinza – Msongati kwa ajili ya mzigo wa Burundi, Tawi la Tabora kwa ajili ya mizigo ya DRC na Tawi la Tabora – Shinyanga – Mwanza kwa ajili ya Ukanda wa Ziwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali pia kuanza kufanya utafiti wa kutanua matawi ya reli kutoka bandari kavu ya Isaka, Shinyanga hadi Rusumu Mkoa wa Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya *nickel* huko Kabanga kutekelezeka. Serikali pia ichunguze uwezekano wa kuweka tawi la reli sambamba na bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Isaka ili kupanua uwezekano wa uwekezaji wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maendeleo ni vita, hivyo ni lazima Serikali itambue kuwa nchi nyingine Wanachama za Afrika Mashariki zinaendelea na ujenzi kwa kasi kubwa sana kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Mombasa - Nairobi, Kampala hadi Kigali. Ni vizuri kujulikana kwamba itakuwa vigumu kwa bandari za Tanzania kushindana na bandari za Kenya kwa mizigo ya Uganda na Rwanda kama reli yetu ya kati itachelewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea reli ya *standard gauge* liyojengwa na kampuni ya CRCC ya Serikali ya China pale Soga Kibaha yenye urefu wa kilometa 1.5. Kamati inashauri Serikali kukamilisha hatua zake za ujenzi wa reli ya aina ile ili kuleta maendeleo ya haraka katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ikiwa mababu zetu wakati wa ukoloni waliweza kujenga reli hii ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, yaani mwaka 1906 mpaka mwaka 1911 kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma bila kuwa na teknolojia ambayo tunayo sasa, ni wazi kuwa Serikali ya Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli ina uwezo wa kukamilisha mradi huu kwa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali itangaze rasmi muda wa kuanza na kukamilisha ujenzi wa reli ya kati ili kuwapa matumaini wananchi wa zaidi ya mikoa 15 wanaotegemea reli hii.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea na uimarishaji wa mitandao ya reli nchini, Kamati inashauri uimarishaji huu uende sambamba na kutafuta suluhisho la kudumu katika maeneo korofi ya *station* ya Kilosa, Gulwe Morogoro kwani tatizo la kuharibika eneo hili kwa reli kusombwa na maji limekuwa linajirudia mara kwa mara na linagharimu fedha nyingi bila kupata suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali iimarishe karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu. Vilevile Kamati imebaini kwamba lengo zuri la Serikali la kutenganisha mashirika ya RAHCO na TRL pamoja na TPA na MSCL limeshindwa kufanikiwa kwa sababu ushindani uliotegemewa haukupatikana (*market failure*).

Kamati inashauri mashirika haya yaunganishwe ili mashirika yale yasaidiane na mashirika ya kudumu ambayo mpaka sasa yanatengeneza hasara, yaani *cross stabilization* na yanahitaji kusaidiwa na shirika mama. Ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kukamilisha utaratibu mpya waliokubaliana kati yake na Zambia juu ya uendeshaji wa Shirika la TAZARA. Vilevile Serikali iendelee kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha kwenye shirika hili. Aidha, Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi pamoja na kuhakikisha mapato ya wafanyakazi yanayopelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuepuka usumbufu kwa wafanyakazi wanaostaafu.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam ndiyo bandari kubwa kuliko zote Tanzania. Inahudumia asilimia 90 ya shehena ya aina mbalimbali ya nchi zaidi ya 10, yaani Tanzania, Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Uganda, Zimbabwe, Malawi, Comoro na Sudan Kusini.

Kamati ilibaini kwamba, ili kukabiliana na changamoto ambazo zimesababisha kushuka kwa shehena ya mizigo Bandari ya Dar es Salaam, Serikali haina budi kuchukua hatua za haraka na madhubuti kutafuta ufumbuzi wa masuala yafuatayo:-

Kwanza, hofu ya wateja kutokana na kuanzishwa kwa sheria ya *Value Added Tax* kwa huduma zitolewazo na Mawakala kwenye nchi jirani, yaani *VAT on transit*.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa sheria hii unafanya wateja kutotumia bandari ya Tanzania kwa sababu ya kuhofu gharama. Mgongano wa tozo za hifadhi ya mizigo (*custom warehouse rent*) inayotozwa na mamlaka ya mapato Tanzania TRA na *storage charges* zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA), malipo haya yanafanana isipokuwa yametofautiana majina tu. Mtunzaji wa mizigo ni TPA, kwa hiyo, Kamati inashauri kodi ibaki moja ya TPA (*storage charges*) na kodi inayotunzwa na TRA iachwe.

Mheshimiwa Spika, tozo ya barabara, yaani ambapo tozo ya Dola za Kimarekani 16 ukilinganisha na Dola nane kwa kilomita zinazotozwa na nchi jirani, ni vizuri pia zianganaliwe ili tuweke kodi zinazolandana au zinazofanana na nchi za wenzetu jirani.

Mheshimiwa Spika, pia muda mfupi, (*short grace period of transit bulk liquid*) vimiminika vinavyopitia katika bandari yetu kama mafuta kwa Bandari ya Dar es Salaam vinapewa siku 30 za kukaa bila kutozwa kodi, lakini nchi jirani; Bandari za Beira pamoja na Durban na Walvis Bay zina *grace period* ya siku 60 mpaka 90, hivyo kufanya wanaoagiza mafuta mengi kupendelea bandari hizo. Kamati inashauri Serikali kuangalia, kuongeza muda wa *grace period* ili kuongeza ushindani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba bandari kavu ICD zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mizigo bandarini, bandari hizi zimeendelea kulalamikiwa kwa ucheleweshwaji na upotevu wa mizigo pamoja na ukwepaji kodi. Ili kuondokana na matatizo haya, kuongeza ushindani, Kamati inashauri Serikali kuondoa zuio kwa Wakala wa Bandari Tanzania (TPA), kufungua bandari kavu yake Kisarawe kama ilivyokuwa imepangwa, ombi hili lina zaidi ya miaka mitatu Serikalini kwa ajili ya kuweka bandari kavu pale Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri maombi mengine ya ujenzi wa bandari kavu ICDs, nje ya Dar es Salaam yapewe kipaumbele kama mkakati wa kuimarisha ushindani hasa na ICDs zinazojinufaisha au zinazojihusisha na udanganyifu. Kamati imebaini kuwa, hapa kuna udanganyifu unaofanywa na mamlaka yaani *freight forwarders* kwa kuongeza gharama kwenye hati za madai zinazotumwa kwa wateja. Kamati inashauri adhabu kali zitolewe kwa mawakala wanaobainika kuongeza gharama hizi ikiwezekana wafutiwe leseni zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili Mamlaka za viwanja vya Ndege (TAA) iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia ushauri ufuatao:-

Kwanza, kuwa Mamlaka hii inatoa mchango mkubwa katika mapato yatokanayo na Viwanja vya Ndege na kwa kuwa bado kuna changamoto ya uboreshaji wa ujenzi wa viwanja mbalimbali Tanzania, Kamati inashauri Serikali kuipa Mamlaka hii angalau asilimia 50 ya Maduhuli (*retention*) yanayotokana na viwanja vya ndege ili kusaidia kuongeza kasi ya shughuli za Mamlaka ya viwanja hivi.

Mheshimiwa Spika, ijulikane kwamba Mamlaka hii inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 80 kwa mwaka, ni ushauri wa Kamati yangu kwamba asilimia 50 angalau zibaki kwenye mamlaka hii kuweza kuhudumia viwanja hivi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kabla ya mwaka wa fedha 2015/2016, kwisha imalize malipo ya fedha zilizoainishwa kwa ajili ya viwanja vya ndege hususan viwanja vya ndege vya Mwanza, Songwe, Mtwara na Bukoba.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kupewa fedha zote zilizotakiwa kwa ajili ya ulipaji wa fidia ambazo kwa sasa inafikia shilingi bilioni 80. Vilevile Kamati inashauri Serikali kuharakisha kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu (*terminal free*) la abiria katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa, yaani Desemba, 2017. Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili mwonekano wake uwe wa kuleta taswira nzuri.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kusema aya ya 108 kwa vitabu mlivyonavyo Waheshimiwa Wabunge, isomeke shilingi bilioni 500 na siyo bilioni tano. Kuhusu Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*), Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 500 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya nne. Kamati inashauri fedha hizi zitolewe kwa wakati ili shirika hili liweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara zilitengewa fedha mwaka 2016/2017, Kamati inashauri kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha mikoa yetu na nchi jirani hususan Mikoa ya Kagera, Mkoa wa Kagera kwa maana Kagera Rwanda na Uganda, Mkoa wa Kigoma kwa maana ya Kigoma na Burundi, Katavi kwa maana DRC-Congo na Zambia, Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Ruvuma na nchi ya Msumbiji na Mkoa wa Mtwara kwa maana ya Mtwara na nchi ya Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ushauri, Serikali izingatie vigezo muhimu vya kiuchumi na hasa huduma za afya pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais Mstaafu na Rais aliyepo madarakani wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2015. Ni muhimu sana lizingatiwe ili miradi pia ipewe kipaumbele kufuata fursa ilizonazo kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuunga mkono kwa juhudi zake za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kupitia miradi mbalimbali inayofanywa ikiwemo mradi wa *DART* chini ya TAMISEMI, Ujenzi wa *Flyovers* barabara za Dar es Salaam – Chalinze, yaani *express way* na ukarabati wa Miundombinu mbalimbali ya Barabara mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa kukamilisha ujenzi wa daraja la Mwalimu Nyerere, Kigamboni hatimaye kulizindua tarehe 19 mwaka 2016. Aidha Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kumpa heshima Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba daraja hilo bora Afrika Mashariki liweze kuitwa jina lake. Kamati pia inashauri Serikali kukusanya mapato yanayotokana na malipo ya watu wanaopita katika daraja hili kwa mfumo wa *electronic* ili kudhibiti ufujaji ama wizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi bora wa namna ya kupata taarifa za makusanyo ya kampuni za simu kwa kutumia mtambo wa *TTMS* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu za mkononi. Kuendelea kuchelewa kulitekeleza suala hili, kunazidi kuikoshesha nchi yetu kodi stahiki kutokana na makampuni haya kutotozwa kodi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa Kamati ilijulishwa kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) imeweza kupata takwimu za huduma za *mobile money* baada ya usimikaji wa mtambo wa *Mobile Money Monetary Solution* na kwamba kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) ilishawaandikia barua; narudia, ilishawaandikia barua Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ili ianze kutumia taarifa za kupata mapato stahiki, lakini hadi mwezi Machi, Kamati ilipotembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TRA*) ilikuwa bado haijaanza kutumia taarifa hizo na kulikosesha Taifa fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali iliambie Bunge lako Tukufu sababu zinazopelekea Mamlaka ya Mapato Tanzania, kutotumia takwimu hizi za kutoka *TCRA* na kuendelea kukosesha nchi yetu mapato. Kamati inatambua kazi nzuri ya Serikali ya kusambaza mawasiliano katika maeneo mbalimbali yenye mvuto kwa ajili ya kuboresha na kuongeza mvuto wa kibiashara. Hata hivyo, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto na sehemu ambazo ziko mbali na miji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni

ya Simu pamoja na masharti mengine ya kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni ya nchi yetu, kama mchango wake katika jamii (*cooperate social responsibility*).

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ijulikane kwamba ushauri niliowasilisha ni sehemu tu ya ushauri mrefu, nimezingatia muda.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Mhandisi Profesa Makame Mbarawa Mnyaa na Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Edwin A. Ngonyani, Mbunge pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii, yaani Mhandisi Joseph Nyamhanga ambaye anashughulikia Ujenzi; Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho ambaye anashughulikia Uchukuzi pamoja na Profesa Faustine Kamuzora ambaye anashughulikia Mawasiliano, pamoja na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Dkt. Maria Sasabo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Makaimu Wakurugenzi ambao kwa muda wote wameonesha weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, narudia, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Makaimu Wakurugenzi ambao kwa muda wote wameonesha weledi mkubwa wa kutekeleza majukumu yao. Kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kuchambua na kupitia bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kipekee kabisa kumshukuru Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi ambapo bila yeye ujasiri wangu wa kusimama hapa usingewezekana. Pili, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Makete ambao kwa vyovyote vile, dua zao na sala zao zimeendelea kumwezesha Mwenyekiti wa Kamati hii kuwa na afya njema. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kwasababu muda bado ninao.

Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso ambaye ni Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe ni Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Abbasi Ali Hasan Mwinyi, Mheshimiwa Miza Bakar Haji, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mheshimiwa Mansour Shanif Hiran, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Hawa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Chuachua Mohamed Rashid, Mheshimiwa

Mary Deo Muro, Mheshimiwa Ritha E. Kabati, Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mheshimiwa Khadija Salum Ali, Mheshimiwa Baghwanj Maganlal Meisuria, Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi, Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mheshimiwa Raphael Japhary Michael na Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nashukuru kwa ushirikiano mkubwa alionipa Mwenyekiti wakati wa kufanya hitimisho la hotuba hii na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Thomas Kashilillah pamoja na Sekretarieti ya Kamati ikiongoza na Ndugu Dickson Bisile na Watendaji wote wa Bunge kwa kufanya kazi nzuri ya kuiwezesha Kamati hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu, lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Norman Sigalla, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, tunakushukuru sana.

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2016/2017 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

2. **Mheshimwa Spika**, maoni yatakayotolewa katika Taarifa hii ni kutokana na majukumu ya Kamati kama yalivyobainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6(8) ambayo imeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.
3. **Mheshimiwa Spika**, jukumu la kuisimamia Wizara hii lilitokelezwa kwa njia ya vikao, ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo pamoja na ziara za shughuli za kawaida za Kamati katika maeneo mbalimbali yanayosimamiwa na Wizara hii. Aidha, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 7 (1) a-d inazipa Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta zinazojumuisha Kamati hii majukumu mbalimbali ikiwemo kushughulikia Bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo.
 4. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), (2), Kamati ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2015/2016) na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata (2016/2017). Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati imechambua mafungu yafuatayo:-
 - a) Fungu 62- Sekta ya Uchukuzi;
 - b) Fungu 98- Sekta ya Ujenzi; na
 - c) Fungu 68- Sekta ya Mawasiliano.
5. **Mheshimiwa Spika**, mtiririko wa Taarifa hii umezingatia maeneo makubwa matatu (3) yafuatayo:
 - a) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ikiwemo:-
 - i) Utekelezaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka 2015/2016;
 - ii) Utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2015/2016; na
 - iii) Masuala Mengine Muhimu yaliyojitokeza wakati wa Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya 2015/2016.
 - b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na
 - c) Maoni na Ushauri wa Kamati.

SEHEMU YA PILI

2. O MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

2.1 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

6. **Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inabainisha utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya zilizokuwa Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Mawasiliano 2015/2016. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya Muundo wa Serikali, taarifa hii itazingatia maoni yaliyotolewa kuhusu Sekta zinazosimamiwa na Wizara kwa sasa ambazo ni Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

2.1.1 Sekta ya Uchukuzi

7. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge*:

Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeona umuhimu wa ushirikishaji wa Sekta binafsi katika miradi ya ujenzi wa reli ambapo kupitia RAHCO imeweka mikakati mbalimbali ya kuendelea ujenzi wa reli nchini. Katika kufanikisha lengo hilo Serikali imeajiri wataalam wa kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa reli nchini ambapo itashughulikia maeneo yafuatayo:-

- i. Reli ya Kaliua-Mpanda na Tabora –Kigoma ambayo itagharimu **shilingi bilioni 5.6**. Mkataba ulisainiwa Februari 2015 na ulitarajiwa kumalizika Januari 2016. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya fedha kazi hiyo inatarajiwa kukamilika Agosti 2016;
- ii. Reli ya Mpanda –Karema na Uvinza-Msongati ambayo itagharimu **shilingi bilioni 6.0**. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali inaendelea. Mkataba ulisainiwa Machi 2015 ambapo hata hivyo kazi ilichelewa kuanza kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha. Kwa mujibu wa mkataba kazi hii ni ya miezi kumi, hivyo kwa sasa, inatarajiwa kukamilika Agosti 2016;
- iii. Reli ya Isaka-Mwanza, Mkataba wa usanifu wa kina ulisainiwa Agosti 2013 kwa thamani ya **shilingi bilioni 4.53** ambapo kazi ilikamilika Mei 2015;
- iv. Reli ya Tanga Arusha, mkataba wa kazi ya usanifu wa kina ulisainiwa Septemba 2013 kwa lengo la kukamilisha kazi Aprili, 2014. Hata hivyo kutokana na kuongezewa tawi la kuingia Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro-KIA na ukosefu wa fedha, kazi ilikamilika Februari 2015 kwa gharama ya **shilingi bilioni 5.02**;

- v. Reli ya Mtwara- Mbambabay, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ilitekelezwa kwa gharama ya **shilingi bilioni 6.54** na ilikamilika mwezi Machi 2016.
8. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu mchakato wa kurekebisha Sheria ya TAZARA Na. 23 ya Mwaka 1975: Kamati ilijulishwa kuwa katika mkutano wa Marais wa Tanzania na Zambia uliofanyika tarehe 25-26 Februari, 2015, walikubaliana kuharakisha ukamilishaji wa marekebisho ya Sheria. Kamati ya pamoja ya Wataalam kati ya Tanzania na Zambia imeshakamilisha rasimu ya sheria mpya ya TAZARA. Waraka wa Mapendekezo ya kutunga Sheria mpya hiyo umeandaliwa na Serikali inatarajia kuwasilisha waraka huo katika vyombo vya maamuzi Serikalini. Kamati inasisitiza Serikali ikamilishe mchakato huu mapema ili kupunguza migogoro ambayo mara nyingi imekuwa ikitokea na kukwamisha utendaji wa reli ya TAZARA.
9. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli jijini Dar es Salaam kwenda Pugu, Mbagala/ Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Kerege: Kamati imejulishwa kuwa kazi hiyo ilianza Disemba, 2015 na Kampuni ya *GIBB International* ya Afrika ya Kusini na inatarajia kukamilika mwezi Agosti 2016. Kamati inaona umuhimu wa kutekelezwa kwa mikakati hii mizuri kwa ustawi wa nchi yetu.
10. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu muda wa Makasha kutumika pasipo malipo (*Demurrage free period*) ambapo Kamati ilishauri kuwa muda huo uongezwe kutoka siku 30 hadi siku 60: Kamati sasa imeelezwa kuwa SUMATRA imefanya utafiti kwa kulinganisha utaratibu unaotumika kwa shehena ya DRC inayopita bandari shindani za Beira- Msumbiji na Walvis Bay- Namibia na kubaini kuwa muda unaotolewa ni siku 15 hadi 21. Aidha, Mamlaka ya Mapato katika Bandari hizo shindani zinaruhusu makasha yaendayo nchi jirani kufunguliwa (*stripping*) hivyo kuondoa ulazima wa kusafirisha kontena pamoja na mzigo. Hivyo, SUMATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania zinaangalia uwezekano wa kuruhusu usafirishaji wa shehena bila kutumia makasha. Kamati inasisitiza utekelezaji wa suala hili kwa kuangalia ushindani wenye kuleta tija kutoka nchi nyingine.

2.1.2 Sekta ya Ujenzi

11. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Serikali kulipa madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri ambayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka; Katika kutekeleza ushauri huu Serikali imeendelea kulipa madeni kadiri ya fedha zinavyopatikana ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi 2016 imetoa jumla ya **shilingi bilioni 635.35**. Lengo ni kukamilisha madeni ya miaka ya nyuma ifikapo mwezi Juni 2016.

12. Mkakati wa kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam kwa kujenga barabara za mlisho (*feeder roads*): Kamati imeelezwa kuwa jitihada za kujenga barabara za mlisho zinaendelea zikijumuisha ujenzi wa barabara za Ubungo Terminal- Kigogo Roundabout (Km 6.4), Kawawa Roundabout- Msimbazi Valley- Jangwani/ Twiga Hotel Junction (km 2.7), Jet Corner- Vituka- Davis Corner (km 10.3), Tabata Dampo- Kigogo(km1.6), Kimara Kilungule- External (km 3), Mbezi- Malambamawili- kinyerezi- Banana-(sehemu ya Kifuru- Kinyerezi km 4), Tegeta-Kibaoni-Wazo Hill- Goba- Mbezi (Morogoro Road) km 20, Tangi bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti- Msewe-Changanyikeni (km 2.6), Kibamba-Kisopwa-Mlonganzila (km 4.0), Banana- Kitunda-Kivule- Msongola (km 14.7), Ardhi-Makongo (km 4), Maji Chumvi-Changombe- Barakuda (km 2.5) na Goba- Mbezi (Morogoro Road) km 7).

Aidha, miradi mingine ya kupunguza msongamano ni pamoja na upanuzi wa barabara ya Morocco-Mwenge (km 4) ambayo inapanuliwa kutoka njia tatu hadi njia tano unaotarajiwa kukamilika Julai 2016. Vilevile, upanuzi wa barabara ya KAMATA- Bendera Tatu (km 1.3) ambao upo katika hatua ya ununuzi kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

13. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Majengo Tanzania-TBA kuchukua mikopo kwenye taasisi za fedha ili kuweza kujenga nyumba nyingi na kwa haraka: Kamati imeelezwa kuwa Wakala umefanikiwa kukopa fedha kiasi cha **shilingi bilioni 25** kutoka CRDB, **shilingi bilioni 6.9** kutoka TIB na **shilingi bilioni 3.5** kutoka PSPF kwa ajili ya miradi ya nyumba. Aidha, Wakala umefanya mazungumzo ya kukubaliana na Benki ya Afrika (BOA) ya kupata mkopo wa kiasi cha **shilingi bilioni 18**. Fedha zilizopatikana kwa njia ya mkopo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi 475 eneo la Bunju, Dar es Salaam, kumaliza jengo la ghorofa 10 lililopo Goliondoi Mkoani Arusha pamoja na jengo la ghorofa 4 lililopo mtaa wa Kilimani, Dodoma.
14. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ofisi nyingi za TEMESA kuwa chakavu: Kamati ilijulishwa kuwa ukarabati mkubwa unaendelea katika karakana za MT Depot (Dar es Salaam), Dodoma, Kigoma, Kibaha, Mbeya, Lindi na Katavi. Aidha, ujenzi wa karakana mpya katika Mkoa wa Manyara unaendelea.
15. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ukarabati na matengenezo ya Kivuko cha Magogoni: Kamati imeelezwa kuwa kazi ya ukarabati inatarajiwa kuanza Mei, 2016 na kukamilika ndani ya miezi mitatu.

2.1.3 Sekta ya Mawasiliano

16. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu ununuzi wa asilimia 35 za hisa za *Bharti Airtel*: Kamati imejulishwa kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Simu Tanzania-TTCL katika vikao vilivyofanyika tarehe 15 Januari 2016, imeridhia makubaliano ya Serikali kununua hisa asilimia 35 za *Bharti Airtel* ndani ya TTCL. Kwa sasa ukokotoaji wa mapato ya Serikali unaendelea kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na Msajili wa Hazina na kazi hiyo itakapokamilika taratibu za kurejesha hisa asilimia 35 zitakamilishwa.
17. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote- UCSAF: Kamati imejulishwa kuwa; pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya mapato vikiwemo kutoka kwa nchi marafiki na wafadhili mbalimbali, Serikali inarekebisha Kanuni za Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuongeza kiasi cha tozo kinachokusanywa kutoka kwa watoa huduma. Fedha hizi zitakapopatikana zitatumika katika kufikisha Mawasiliano vijijini kwa kushirikiana na watoa huduma ambao ni Makampuni ya Simu ya hapa nchini yenye leseni za TCRA.
18. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu matumizi sahihi ya huduma za simu na mtandao: Kamati imejulishwa kuwa inaendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu kutumia huduma za mawasiliano vizuri. Vilevile, Mamlaka ya Mawasiliano inahamasisha Kampuni za Simu kutumia mfumo wa uandikishaji wa kieletroniki ambao unamtaka anayesajili laini apigwe picha na kuweka saini kwenye eneo la usajili (*Biometric Registration*) ili kumtambua mmiliki wa simu kwa uhakika.
19. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni, ushauri na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Kamati isipokuwa katika maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ukosefu wa fedha.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2015/2016

2.2.1 Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

20. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa lengo la kujiridhisha na utekelezaji wa miradi pamoja na utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi hiyo kwa mwaka wa fedha ulioisha (2015/2016). Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikagua baadhi ya miradi kama ifuatavyo:-
 - i. Mradi wa ujenzi jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere, fungu 62, mradi namba 4289 ulioidhinishwa kiasi cha **shilingi bilioni 1 (1,000,000,000)**;

- ii. Mradi ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe fungu 62, mradi namba 4206 ulioidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 5 (5,000,000,000)**;
- iii. Mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni, fungu 98, mradi namba 4167 ulioidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 2.215 (2,215,000,000)**;
- iv. Mradi wa upanuzi wa Barabara ya Kimara-Kibaha (km 25.7) fungu 98, mradi namba 4174 ulioidhinishiwa kiasi cha shilingi **101,000,000**;
- v. Mradi wa ukarabati wa barabara ya Mlandizi- Chalinze (km 42) fungu 98, mradi namba 4108 ulioidhinishiwa kiasi cha **shilingi 2,450,000,000**; na
- vi. Mradi wa ujenzi wa barabara Mbeya-Lwanjilo (km 36) Mbeya –Makongorosi fungu 98, mradi namba 4188 ulioidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 5.405 (5,405,000,000)**.

2.2.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi

- 21. **Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Uchukuzi Kamati ilitembelea miradi ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe Mbeya.
 - i. Mradi wa Ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili: ambapo awamu ya kwanza ni ujenzi wa jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni tatu na nusu kwa mwaka na awamu ya pili itahusisha jengo la kuhudumia abiria milioni mbili na nusu kwa mwaka. Hivyo, mradi huu ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka tofauti na jengo linalotumika kwa sasa la *Terminal II* lenye uwezo wa kuhudumia watu 1,200,000 kwa mwaka.

Gharama za mradi wote ni **shilingi bilioni 560** ambapo awamu ya kwanza ni **shilingi bilioni 293** na awamu ya pili **shilingi bilioni 267**. Fedha za mradi awamu ya kwanza ni mkopo kutoka Benki ya HSBC ya Uingereza (85%) na CRDB ya Tanzania (15%). Katika kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi huu Serikali imeendelea na taratibu za kupata mkopo kutoka kwa Wabia wa Maendeleo ambapo ombi la kupatiwa mkopo limeshawasilishwa kwenye Kamati ya madeni ya Taifa kwa maamuzi.

Kwa upande wa Fedha za ndani mradi huu katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 ulioidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 1 (1,000,000,000)**. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu mwezi Aprili 2016, hakuna kiasi chochote cha fedha za ndani zilizokuwa zimetolewa.

- ii. Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe Mbeya
24. **Mheshimiwa Spika**, uwanja huu ni kati ya viwanja vya ndege muhimu sana kwani ndicho kiwanja kinachotoa fursa kwa wakazi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika huduma ya usafiri wa anga na kuchangia kukuza uchumi wa Mikoa ya nyanda za juu kusini na Taifa kwa ujumla. Ili mradi hu ukamilike unahitaji fedha kiasi cha **shilingi bilioni 16.154 (16,154,239,492.14)**. Hata hivyo, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 5** ambazo hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 hazikuwa zimetolewa.
- i) Kutokutolewa fedha za mradi huu kwa wakati kunasababisha kuwepo kwa ongezeko la madeni ya mradi kutokana na ucheleweshwaji wa hati za malipo ya Mkandarasi ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi huu Mkandarasi alikuwa anadai **shilingi bilioni 2.157 (2,157,609,013.02)** ambazo ni kwa ajili ya kazi zilizofanyika.
- ii) **Mheshimiwa Spika**, vile vile kutokutolewa fedha za mradi kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi, mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha na kutokamilika kufungwa kwa baadhi ya mitambo na taa za kuongozea ndege ambayo ingesaidia ndege kutua wakati wa ukungu na usiku jambo ambalo mara kadhaa limesababisha ndege kushindwa kutua kiwanjani hapo.

2.2.1.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi

i) **Mradi wa Ujenzi Daraja la Mwalimu Nyerere (Kigamboni)**

25. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi wa daraja la Mwalimu Nyerere ambao upo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii- NSSF.
26. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa makusanyo yote yatakayokuwa yanapatikana yatasimamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii- NSSF na yatatumika kulipia gharama ya ujenzi wa daraja hilo takribani **shilingi bilioni 214.6**. Makusanyo hayo yataendelea kuchukuliwa na Mfuko wa Hifadhi za Jamii- NSSF mpaka gharama zilizotumika kujenga daraja hilo zitakapokamilika.
27. **Mheshimiwa Spika**, pia Kamati ilikagua miradi mbali mbali ya barabara nchini ikiwemo barabara ya Kimara- Kibaha (km 25.7), Ukarabati wa barabara ya Mlandizi-Chalinze (km 42), ujenzi wa barabara ya Mbeya –Rungwe sehemu ya Mbeya -Makongorosi (km 115) pamoja na barabara nyingine ambazo Kamati imekuwa ikipita wakati wa utekelezaji wa shuguli zake.

28. **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya kuharibika kwa barabara mapema mara baada ya kujengwa. Kamati ilijulishwa kuwa uharibifu wa barabara hizi unasababishwa na wingi wa magari makubwa yanayotumia barabara, matumizi ya aina ya magari ya mizigo yanayotumia tairi moja yaani *Super single* pamoja na joto kubwa la barabara hasa mikoa yenye joto linalotokana na mabadiliko ya tabia nchi linalofikia nyuzi 62 sentigredi ambalo halioani na aina ya lami inayotumika yenye uwezo wa kuhimili joto la barabara la nyuzi joto 50 sentigredi. Pia Kamati elielezwa teknolojia ya kutengeneza imara zaidi lakini gharama kubwa.

2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

2.3.1 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

a) Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa iliyokuwa Wizara ya Uchukuzi hadi Kufikia Machi, 2016

29. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 iliyokuwa Wizara ya Uchukuzi iliidhinishwa kiasi cha **shilingi bilioni 389.4 (389,437,277,000)**.


Katika Fedha hizo, Fedha za Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 113.4 (113,404,685,000)** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 54.28 (54,288,680,000)** ni fedha za Mishahara na **shilingi bilioni 59.11 (59,116,005,000)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

30. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, kiasi cha Fedha za Matumizi ya Kawaida kilichotolewa ikijumuisha Mishahara na Matumizi Mengineyo ni **shilingi bilioni 63.46 (63,464,787,364.14)** sawa na **asilimia 56** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 35.54 (35,549,991,102.00)** ni Matumizi Mengineyo, na **shilingi bilioni 27.91 (27,914,796,262.14)** ni Mishahara.

31. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kiasi kilichoidhinishwa ni **shilingi bilioni 276.03 (276,032,592,000)** ambapo kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 143.5 (143,500,000,000)** ni Fedha za Ndani na **shilingi bilioni 132.5 (132,532,592,000)** ni Fedha za Nje. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 kiasi kilichotolewa ni **shilingi bilioni 147.04 (147,043,610,000)** sawa na **asilimia 53** ya Fedha za Maendeleo. Kati ya Fedha hizo zilizotolewa **shilingi bilioni 56.68 (56,688,240,000)** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 40** na **shilingi bilioni 90.35 (90,355,370,000)** sawa **asilimia 68** ya Fedha za nje.

32. **Mheshimiwa Spika**, kielelezo Na.1 kinaonesha Bajeti ya iliyokuwa Wizara ya Uchukuzi; Ulinganifu wa Utoaji Fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa Fedha Kwa Mwaka 2015/2016 hadi Kufikia Mwezi Machi, 2016.

33. **Mheshimiwa Spika**, kwa jumla namna ya utoaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa iliyokuwa Wizara ya Uchukuzi si yakuridhisha hasa kwa upande wa Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo. Fedha za ndani zilizotolewa ni **asilimia 40** na fedha za Wahisani zilizotolewa ni **asilimia 68** ya Bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo ya Nje iliyotengwa. Kuendelea kutegemea fedha za wahisani zaidi ambazo mara nyingi hazina uhakika au hutolewa kwa masharti ni tatizo na bila kulitatua Taifa hili halitaweza kupiga hatua za haraka katika kujiletea maendeleo.




b) Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa iliyokuwa Wizara ya Ujenzi hadi Kufikia Machi, 2016

34. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 iliyokuwa Wizara ya Ujenzi ilitengewa **shilingibilioni 39.9 (39,923,770,336.00)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 3.2 (3,244,777,336.00)** ni Fedha za Matumizi Mengineyo na **shilingi bilini 36.7 (36,778,993,000.00)** ni Mishahara.

Hadi kufikia mwezi Machi 2016, **shilingi bilioni 26.7 (26,715,033,125.00)** zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 66.92** ya kiasi chote kilichoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 25.7 (25,719,170,848.00)** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi milioni 995.8 (995,862,277.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

35. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo iliyokuwa Wizara ya Ujenzi ilitengewa **shilingi bilioni 883.8 (883,832,338,500.00)** ambapo kati ya Fedha hizo, fedha za ndani ni **shilingi bilioni 191.6 (191,619,568,500.00)** na Fedha za Nje ni **shilingi bilioni 85.5 (85,572,770,000.00.)**, Fedha za Mfuko wa Barabara ni **shilingi bilioni 606.64 (606,640,000,000.00.)** Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Fedha zilizotolewa ni **shilingi trilioni 1.080 (1,080,804,942,594.00)** sawa na **asilimia 122** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 607.35 (607,350,007,730.00)** sawa na **asilimia 317** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 149.50 (149,502,934,864.00)** sawa na **asilimia 175** ni fedha za nje. Kwa upande wa Mfuko wa Barabara zimetolewa **shilingi bilioni 323.95 (323,952,000,000.00)** sawa na **asilimia 53** ya fedha zote zilizotengwa za Mfuko wa Barabara.

36. **Mheshimiwa Spika**, kielelezo Na. 2 kinaonesha Bajeti ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi; Ulinganifu na Utoaji Fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka 2015/2016 Hadi Kufikia Mwezi Machi, 2016. Wizara inaonekana kuwa imepokea fedha nyingi hivyo kupandisha kiwango cha asilimia kutokana na fedha za miaka ya nyuma za madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri kutolewa mwaka huu wa fedha ambapo hadi kufikia mwezi April, 2016 jumla ya **shilingi bilioni 635.35** zimetolewa.



c) Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia hadi Kufikia Machi, 2016


37. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia iliidhinishiwa **shilingi bilioni 58.9 (58,994,191,000)**. Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 43.19 (43,195,303,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya hizo **shilingi bilioni 38.07**

(38,072,072,000.00) ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 5.12 (5,123,231,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Kwa upande wa Fedha za Maendeleo Wizara iliidhinishiwa **shilingi bilioni 15.7 (15,798,888,000)** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 13.4 (13,400,000,000)** ni Fedha za Ndani na **shilingi bilioni 2.39 (2,398,888,000.00)** ni Fedha za Nje.

38. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 25.6 (25,689,452,425.60)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 43.54** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa. Kati ya Fedha zilizotolewa, Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo hazikutolewa sawa na **asilimia 0** ambapo Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo zimetolewa **shilingi milioni 766.06 (766,062,001.60)** sawa na **asilimia 32** ya Fedha zote za Nje zilizoidhinishwa.

39. **Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Na. 3 kinaonesha Bajeti ya iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi Na Teknolojia; Ulinganifu wa Utoaji Fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha Kwa Mwaka 2015/2016 Hadi Kufikia Mwezi Machi, 2016. Utolewaji wa fedha kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 haukuwa wa kuridhisha. Wizara hii haikupata kiasi chochote cha fedha za Miradi ya Maendeleo wakati kwa upande wa fedha za nje za Miradi ya Maendeleo zilitolewa takribani **asilimia 31** ya bajeti yote ya nje iliyoidhinishwa. Hali hii imekuwa ni changamoto na mojawapo ya sababu ya miradi na kazi kadhaa kutokamilika kama zilizopangwa.



2.4 Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

40. **Mheshimiwa Spika**, kwa jumla Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa **shilingi trilioni 4.2 (4,229,408,685,900.00)**. Bajeti hii ni sawa na **asilimia 16.7** ya bajeti yote ya Serikali ambayo ni **shilingi trilioni 29.353**.

Jedwali lifuatalo linaonesha Fedha zilizoombwa kwa Sekta za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2016/2017

SEKTA	MATUMIZI YA KAWAIDA	MIRADI YA MAENDELEO	JUMLA
Ujenzi	35,936,939,500	2,176,204,557,000	2,212,141,496,500
Uchukuzi	90,756,253,000	1,999,778,929,000	2,090,535,182,000
Mawasiliano	3,412,635,200	5,000,000,000	8,412,635,200
JUMLA KUU	130,105,827,700	4,180,983,486,000	4,311,089,313,700

2.4.1 Mchanganuo wa Fedha zilizoombwa kwa Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2016/2017

a) Makadirio ya Sekta ya Uchukuzi

41. **Mheshimiwa spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Sekta ya Uchukuzi (fungu 62) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi Trilioni 2.09 (2,090,535,182,000.00)**. Kati ya fedha hizo:-

i) Fedha za Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 90.75 (90,756,253,000.00)** ambapo **shilingi bilioni 52.43 (52,430,658,000.00)** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi bilioni 38.32 (38,325,595,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

ii) Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **shilingi trilioni 1.9 (1,999,778,929,000.00)** ambapo **shilingi 1,811,926,400,000** ni fedha za ndani na **shilingi 187,852,529,000** ni fedha za nje.

42. **Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za ndani za maendeleo ni **shilingi trilioni 1 (1,000,000,000,000.00)** ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard Gauge*; **Shilingi bilioni 500 (500,000,000,000.00)** ni za ununuzi wa ndege mpya za abiria ATCL;

shilingi bilioni 161.42 (161,426,000,000.00) ni kwa ajili ya Mfuko wa Reli; **shilingi bilioni 21 (21,000,000,000.00)** ni kwa ajili ya malipo ya asilimia 50 ya ujenzi wa meli mpya ya ziwa Victoria; **Shilingi bilioni 20 (20,000,000,000.00)** kwa ajili ya ukarabati wa MV Victoria (MSCL); **Shilingi bilioni 5.9 (5,900,000,000.00)** ni kwa ajili ya ukarabati wa MV Liemba; **Shilingi bilioni 3.6 (3,600,400,000.00)** kwa ajili ya ukarabati wa MV Butiama na **shilingi bilioni 100 (100,000,000,000.00)** kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege.

Aidha, fedha za nje za Miradi ya Maendeleo **shilingi bilioni 187.85 (187,852,530,000.00)** ambapo kati ya hizo **shilingi bilioni 100 (100, 000, 000,000.00)** ni kwa ajili ya viwanja vya ndege (TAA) na **shilingi bilioni 87.85 (87,852,530,000.00)** kwa ajili ya miradi ya reli (RAHCO).

b) Makadirio ya Sekta ya ujenzi

43. **Mheshimiwa spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Sekta ya Ujenzi (fungu 98) inaomba kuidhinishiwa **shilingi trilioni 2.2 (2, 212,141, 496,500.00)**. Kati ya fedha hizo:-

- i) Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 35.9 (35,936,939,500.00)** ambapo **shilingi 34,287,474,500** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 1,649,465,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.
- ii) Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 2,176,204,557,000** ambapo **shilingi 1,831,365,922,000** ni fedha za ndani na **shilingi 344,838,635,000** ni fedha za nje. Aidha, **shilingi 582,644,500,000** ni fedha kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara.

c) Makadirio ya Sekta ya mawasiliano

44. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Sekta ya Mawasiliano (fungu 68) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 8.4 (8,412,635,200.00)**. Kati ya Fedha hizo:-

- i) Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 3.4 (3,412,635,200.00)** ambapo **shilingi bilioni 2.5 (2,500,309,200.00)** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi milioni 912.3 (912,326,600.00)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.
- ii) Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo ni **shilingi bilioni 5 (5,000,000,000)**. **Shilingi shilingi 3,000,000,000** ni kwa ajili ya Mradi wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta na **shilingi 2,000,000,000** ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

2.5 Mambo Mengine Muhimu yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara hii kwa Mwaka 2016/2017

2.5.1 Sekta ya Uchukuzi

a) Umuhimu wa Kuimarishwa kwa Mtandao wa Reli Nchini

45. **Mheshimiwa Spika**, katika mipango ya Sekta ya Uchukuzi ya Mwaka 2016/2017, miongoni mwa malengo yaliyowekwa kuhusu kuimarisha miundombinu ya reli nchini ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* ambapo imetengwa **trilioni 1 (shilingi 1,000,000,000,000.00)**
46. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona upo umuhimu mkubwa wa kuendelea kutenga fedha za kutosha ili kuimarisha usafiri wa reli kwa kuzingatia muelekeo wa sasa wa Taifa letu linapotaka kwenda katika Uchumi wa Viwanda na Biashara. Bila kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli nchi nzima, bado kutakuwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa barabara zetu kwa ajili ya usafirishaji wa mali ghafi pamoja na bidhaa zitakazokuwa zinatoka Viwandani. Isotoshe usafiri wa reli ndio wa bei nafuu na ni wa muhimu kuongeza ushindani wa bidhaa za nchi yetu katika masoko ya dunia. Kamati inaona umuhimu mkubwa wa kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya uimarishaji wa mtandao wa reli nchini. Hata hivyo, kutegemea fedha za ndani pekee mipango hii mizuri haitaweza kukamilika kwa wakati, hivyo ipo haja ya Serikali kuangalia vyanzo vingine ikiwezekana kushirikisha Sekta binafsi- PPP katika ujenzi wa reli kwa utaratibu wa *Build Own Operate Transfer* (BOOT) ilimradi mikataba hiyo itayarishwe kwa umakini mkubwa na uwazi ili kulinda maslai ya umma bila kuathiri motisha kwa mwekezaji.

b) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

47. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 17 ya Mwaka 2004 (*The Ports Act No.17*) na ilianza kazi zake rasmi mwaka 2006 ikirithi majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (*Tanzania Harbours Authority-THA*) na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL).
48. **Mheshimiwa Spika**, hali ya bandari nchini kwa mwaka 2015/2016 kwa jumla imekuwa si nzuri kwani shehena zimekuwa zikipungua kutokana na changamoto mbalimbali za kimiundombinu na za kiutawala. Miongoni mwa bandari ambazo zimeathirika na kushuka kwa shehena ni pamoja na Bandari ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Itungji-Kyela.

i) Bandari ya Dar es Salaam

49. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujua kwa kina mipango mikakati iliyopo kwa ajili ya kuboresha Bandari ya Dar es Salaam. Kamati imejulishwa kuwa maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam yatafanyika kupitia mpango utakaogharimu kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 690**. Fedha hizo zitapatikana kupitia vyanzo mbalimbali vifuatavyo:-
- a. Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania itachangia kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 60**;
 - b. Benki ya Dunia kupitia mfuko wa *International Bank for Reconstruction and Development (IBRD)* itatoa mkopo wa masharti nafuu kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 600**; na
 - c. DFID watatoa ruzuku ya kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 30**.
50. **Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa fedha hizo zitatekeleza miradi ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kama ifuatavyo:-
- a) Kuongeza kina cha maji kutoka mita 10 hadi kufikia mita 14 katika gati namba 1-7 inayokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani Milioni 60**;
 - b) Kuongeza kina kutoka mita 12 hadi kufikia mita 14 katika gati namba 8-11 zilizokodishwa kwa Kampuni ya TICS inayokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani Milioni 40**;
 - c) Kujenga gati mpya ya kushushia magari katika eneo la Gerezani inakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani Milioni 40**;
 - d) Uchimbaji ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli kufikia mita 14 pamoja na sehemu ya kugeuzia meli, na kupanua upana wa lango kutoka mita 140 kufikia mita 240 hadi 350 unaokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani Milioni 175**;
 - e) Uhamishaji wa gati la mafuta Kurasini Oil Jet (KOJ) pamoja na mabomba yake ya mafuta **Dola Milioni 80**;
 - f) Ufungaji wa "conveyor system" na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia nafaka **Dola za Marekani Milioni 30**;
 - g) Ujenzi na uboreshaji wa mtandao wa reli ndani ya bandari na ujenzi wa sehemu ya kupakulia na kushushia mizigo kwenye mabehewa unaokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani Milioni 15**; na

h) Maandalizi na usimamizi wa miradi yote unaokisiwa kugharimu kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 50**.

51. **Mheshimiwa Spika**, mkataba wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na namna bora ya kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la bandari ulisainiwa Disemba 2015 na kazi zimeanza tarehe 20 Januari 2016 ambapo inategemewa kuchukuwa muda wa miezi sita (6).

52. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu gati namba 13 na 14, baada ya Serikali kushauriana na wafadhili wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam mwezi Oktoba 2015, ilikubalika kujumuisha magati yote ya bandari kwenye mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Ujenzi wa magati hayo unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani Milioni 200** ambapo unatarajiwa kuanza rasmi mwaka 2018 baada ya kukamilika kwa uhamishaji wa gati la mafuta Kurasini Oil Jet (KOJ) na mabomba yake.

53. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo mazuri ya Serikali katika jitihada za kuboresha bandari ya Dar es Salaam, bado bandari hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za utendaji hafifu wa reli kufikia asilimia 1 kwa mwaka ikilinganishwa na asilimia 10 mwaka 2008; jambo linalosababisha mizigo mingi kusafirishwa kwa njia ya barabara. Aidha, msongamano katika jiji la Dar es Salaam unaoathiri uondoshaji wa mizigo kutoka bandarini pamoja na ubovu wa barabara zinazolingia na kutoka bandarini na zile zinazounganisha bandari na bandari kavu- ICD's.

Vilevile, changamoto nyingine ni kutokuwepo kwa maegesho kwa ajili ya magari yanayoenda kupakia miziya mizigo bandarini.

54. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo, bandari hii inakabiliwa na changamoto nyingine kubwa ambazo kama Serikali haitazifanyia kazi, basi kuna uwezekano mkubwa wa nchi yetu kupoteza wateja wengi waliokuwa wakitumia bandari ya Dar es Salaam na kwa sasa wanahamia katika bandari nyingine shindani za Mombasa- Kenya, Beira- Msumbiji, Durban- Afrika Kusini na Walvis Bay-Namibia ambazo zimeweka mazingira rafiki na wafanyabiashara na kuvutia wengi kukimbilia huko.

55. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya sababu ambazo Kamati imebaini kuwa zimesababisha kupungua kwa shehena za mizigo katika bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na:-

a) Kodi zinazotozwa kwa watoa huduma zitolewazo kwenye mizigo ya nje (VAT on Transit Goods);

- b) Tozo za *Port Storage* na *Customs Warehouse Rent* kutozwa kwa pamoja;
- c) Ushindani mkubwa katika kupakua na kupakia mzigo- “*dwell time*” ambapo katika banadari ya Dar es Salaam inachukuwa siku tisa (9) wakati banadari nyingine kama Durban ni siku nne (4) tu;
- d) Kuwepo kwa Mamlaka nyingi (*Regulatory Authority*) ambazo kwa kaisi zinasababisha ucheleweshwaji wa uondoshwaji wa mizigo bandarini, Mfano, SUMATRA, EWURA, Wakala wa Vipimo, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania na *Government Chemistry Laboratory-GCLA*;
- e) Kutofautiana kwa gharama za tozo za bandari (*wharfage*) baina ya nchi na nchi ambapo za Tanzania ziko juu; na
- f) Shehena inayosafirishwa nje ya nchi kupewa siku 30 tu tofauti na bandari zingine shindani bila kujali mazingira ya usafirishaji wa barabara ndani na nje ya nchi iendako.

ii) Bandari ya Mwanza

- 56. **Mheshimiwa Spika**, hali ya utendaji wa bandari ya Mwanza si ya kuridhisha kabisa kwani imekuwa ikishuka kwa muda kutokana na kuporomoka kwa ufanisi wa reli ya kati hivyo kupungua kwa mizigo. Utendaji hafifu wa reli umesababisha mizigo mingi kusafirishwa kwa njia ya barabara ambapo wateja wengine wameamua kuhama na kupitia bandari ya Mombasa. Hali hii ya kushuka kwa shehena imekuwa ikisababisha bandari ya Mwanza kutofikia malengo ya kusafirisha shehena iliyokusudiwa.
- 57. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, sababu zingine ni ushindani mkubwa kutoka kwa bandari bubu pamoja na kuharibika mara kwa mara kwa meli ya MV Serengeti na MV Victoria ambazo zimekuwa ndiyo tegemeo kubwa la usafiri wa mwambao wa Ziwa Victoria. Changamoto nyingine ni ujenzi wa vituo vya kuegesha meli ambavyo ni vya watu binafsi na baadhi siyo rasmi. Vituo kadhaa vimejengwa karibu sana na bandari ambapo pamoja na kuinyima mapato Serikali pia vinatishia usalama na utaratibu wa uendeshaji wa meli katika Maziwa.
- 58. **Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine zinazosababisha wafanyabiashara wa kitanzania kuikimbia bandari ya Mwanza ni mgogoro kati ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Bandari Mwanza kuhusu mipaka ya bandari pamoja na tozo mbalimbali za ushuru kwa magari yanayoingia na kutoka bandarini jambo linalosababisha gharama kwa wafanyabiashara na hivyo kuona usumbufu na kuamua kutumia bandari nyingine.

C) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (Tanzania Airport Authority-TAA)

59. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka hii inajukumu la kuendeleza na kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini. Katika kutekeleza jukumu hili changamoto kubwa imekuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini; kwani hadi kufikia mwezi Machi 2016, hakuna fedha zozote zilizokuwa zimetolewa kwa viwanja vya ndege isipokuwa **shilingi bilioni 5 (5,000,000,000.00)** tu, ambazo zilitolewa kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Pamoja na kutokutolewa fedha kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini, bado Mamlaka hii imeweza kukusanya **shilingi bilioni 88.5** na inatarajia kukusanya kiasi kikubwa zaidi katika mwaka ujao wa fedha 2016/2017 takribani **shilingi bilioni 105.0**.
60. **Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi kabisa na hali hii ya kutokutolewa fedha ambazo zimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu hasa ukizingatia kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inakusanya fedha nyingi na kwa hiyo usingetarajia kukosa fedha kwa ajili ya miradi yake.

i. Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

61. **Mheshimiwa Spika**, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ndicho Kiwanja kikubwa kinachotegemewa na wakazi wa Kanda ya Ziwa. Serikali imekuwa na nia ya kukiendeleza Kiwanja hiki kwa kukipanua ili kiweze kukidhi mahitaji mengi ya sasa na kuweza kutua ndege kubwa na za Kimataifa. Hata hivyo ujenzi wa mradi huu umekumbwa na changamoto ya kutotolewa kwa fedha hivyo kusababisha kuongezeka kwa madai ya mkandarasi hali iliyosababisha kushindwa kuendelea na kazi.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Kiwanja hiki kiliidhinishwa **shilingi bilioni 10.7 (10,777,975,000.00)** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2016 kilikuwa kimepewa **shilingi bilioni 5 (5,000,000,000.00)**.

62. **Mheshimiwa Spika**, mwaka huu wa fedha 2016/2017, Kamati imefarijika kuona kiwanja hiki kimetengewa **shilingi bilioni 30.1 (30,150,000,000.00)** ambazo zitatumika kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria, ujenzi wa jengo la mizigo, maegesho ya ndege na viungio vyake, kuendelea na kazi ya kurefusha na kujenga barabara ya kuruka na kutua ndege, jengo la kuongezea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege pamoja na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua.

d) Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL

63. **Mheshimiwa Spika**, katika kupitia taarifa ya utekelezaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania, Kamati ilijulishwa kwamba Kampuni hii imeendelea kutekeleza

majukumu yake ya kufanya biashara ya kusafirisha abiria, mizigo na vifurushi katika masoko ya ndani na nje ya nchi ambayo ni Kigoma, Mwanza, Mtwara na Visiwa vya Comoro. Kamati imejulishwa kuwa katika jitihada za kuikwamua ATCL, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga **shilingi milioni 500 (500,000,000.00)** kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya.

2.5.2 Sekta ya Ujenzi

64. **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya ujenzi kupitia wakala wa barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi na ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa jumla ya Kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilomita 22,214 ni barabara za Mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara zetu ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

a) Miradi ya ujenzi wa Barabara

65. **Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa katika kipindi cha 2015/16 Wakala wa barabara nchini imetekeleza na kuendelea kusimamia kazi za ukarabati, kujenga na kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa zenye urefu wa Kilometa 35,000. Matengenezo ya barabara kuu na mikoa yakihusisha matengenezo ya kawaida kilometa 31,883, matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya sehemu korofi kilomita 6,096 na madaraja 510 yalifanyiwa kazi. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kukamilisha baadhi ya miradi ya barabara katika kiwango cha lami na mengine katika kiwango cha changarawe.

66. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Kanuni zake imeweka miongozo kuhusu utaratibu wa matumizi ya barabara ikiwemo udhibiti wa watu wanaofanya uharibifu wa miundombinu ya barabara, bado uharibifu wa miundombinu unajitokeza hususan vyuma vinavyokuwa na alama za barabarani ambapo vyuma hivi hung'olewa na kwenda kuuzwa kama vyuma chakavu. Kamati imejulishwa kuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imeandaa waraka wa kupendekeza Kutungwa kwa sheria ya kudhibiti biashara ya vyuma chakavu ili kuthibiti uharibifu.

67. **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, kuwepo kwa matuta kumekuwa chanzo cha uharibifu wa barabara kwani magari yenye mizigo hulazimika kwenda mwendo mdogo hivyo uzito kuwa mkubwa na kusababisha barabara kutitia. Vilevile matuta barabarani yamekuwa yakisababisha mizigo kuhama na kuelemea upande mmoja jambo ambalo wakati mwingine limekuwa chanzo cha ajali kwa magari mengi. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)

umeendelea kurekebisha matuta makubwa ili kuyaweka katika viwango. Matuta hayo mapya yatazingatia viwango vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Wizara kuhusu usanifu wa barabara wa mwaka 2011 (*Road Geometric Design MANUAL, 2011*).

68. **Mheshimiwa Spika**, kati ya malengo ya Sekta ya Ujenzi ni pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo 2017/18. Hata hivyo, bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaweza kuunganishwa kwa barabara ya lami kama vile Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya – Makete- Njombe n.k Pia baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

b) Madeni ya Makandarasi na Waandisi Washauri

69. **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuhakikisha inalipa na kupunguza madeni ya Wakandarasi na Waandisi Washauri. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea na juhudi za kulipa madai ambapo lengo ni kukamilisha kulipa madai ya miaka ya nyuma ifikapo mwezi Juni 2016. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Serikali imekwishatoa jumla ya **shilingi bilioni 605.35** kwa ajili ya kupunguza madeni hayo. Kamati inaona hatua zilizochukuliwa na Serikali ni nzuri kwani zitaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya barabara pamoja na kupunguza gharama ya malimbikizo ya riba zitokanazo na ucheleweshwaji wa malipo.

c) Mizani ya Barabarani

70. **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inatoa pongezi kwa Serikali kwa kujenga mzani unaopima magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion Weghbridge-WIM*) uliofungwa eneo la Vigwaza Mkoa wa Pwani ambapo kuwepo kwa mzani huu kumesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano mkubwa wa magari uliokuwapo katika mzani wa Kibaha. Kamati ilielezwa kuwa **asilimia 62** ya magari makubwa yanayopita kwenye mzani huu pamoja na magari madogo yote huelekezwa kuendelea na safari.
71. **Mheshimiwa Spika**, moja kati ya majukumu ya TANROADS ni ujenzi na utunzaji wa barabara, kudhibiti uzito wa magari ili kuhakikisha barabara zinadumu kwa muda mrefu. Pamoja na kuwapo kwa vituo vingi vya mizani bado barabara zimekuwa zikiendelea kuharibika. Tatizo hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu mapema, litaendelea kuigharimu nchi yetu kwa kutenga fungu la fedha kila mara kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara zile zile kila mwaka. Changamoto nyingine kubwa inayoendelea kuikabili sekta ya barabara nchini ni ya uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kubeba mizigo yenye

uzito mkubwa. Mfano, magari mengi ya aina ya fuso kwa wastani yanatakiwa kubeba mzigo usiozidi tani 3.5 lakini mengi yanazidisha na kubeba mizigo hadi tani 8. Hali hii ni hatari sana kwani mara nyingi yamekuwa yakisababisha ajali pamoja na uharibifu wa barabara kwani matairi yake ni membamba na huchimba barabara na kusababisha mabonde.

2.5.3 Sekta ya Mawasiliano

a) Mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA)

72. **Mheshimiwa spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilianzishwa chini ya Sheria Na. 12 ya Mwaka 2003 ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Utangazaji Tanzania na Tume ya Mawasiliano Tanzania-TCC. Dhumuni la kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini ikiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuendelea kusimamia mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma ya mawasiliano (*Telecommunication Traffic Monitoring system-TTMS*) mtambo huu ulianza kazi rasmi tarehe 1 octoba, 2013 ambapo umesaidia kuboresha na kuongeza mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi ambapo Mamlaka imeshapeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali **shilingi bilioni 40.6 (40,656,865,447.03)** ikiwa ni makusanyo kuanzia mwezi Oktoba 2013 mpaka Agosti 2015.

73. **Mheshimiwa spika**, Kamati ilipoitembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilielezwa kuwa pamoja na juhudi nyingine zinazoendelea za kuweza kujua mapato yatokanayo na simu za ndani, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeweza kupata takwimu za huduma za *Mobile Money* baada ya usimikaji wa *Mobile Money Monitoring Solution* na kukamilika na mfumo huu sasa umeweza kusimamia takwimu za huduma hiyo. Hii ni taarifa nzuri ya kupanua wigo wa kuongeza mapato. Kamati ilijulishwa kuwa Mamlaka ya Mawasiliano imeshaliwasilisha suala hilo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA ili ianze kutumia taarifa hizo na kuweza kupata mapato stahiki. Hata hivyo, mpaka mwezi Machi Kamati ilipotembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,TRA ilikuwa haijaanza kutumia taarifa hizo muhimu kukusanya mapato hayo.

74. **Mheshimiwa spika** suala zima la ukusanyaji wa mapato hasa kwa simu za ndani ya nchi ni muhimu sana kwani eneo hili linaweza kuipatia nchi yetu fedha nyingi. Ikiwa kwa sasa nchi yetu inaweza kupata takwimu sahihi za simu za Kimataifa zinazolingia nchini na kuweza kukusanya mapato, kwa nini ishindikane kupata takwimu sahihi za Makampuni ya ndani ya nchi. Kuendelea kutegemea

makampuni ya simu kuleta taarifa zao za simu kuna uwezekano mkubwa kwa nchi kutokupata taarifa sahihi.

b) Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano

75. **Mheshimiwa spika**, chini ya sheria mpya ya *Electronic and Postal Communication Act- EPOCA*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuratibu zoezi zima la kusajili simu za kiganjani. Hadi kufika Disemba 2015 laini za simu zilizosajiliwa ambazo zinatumiwa zilikuwa ni 39, 808,417 kutoka laini 2,963,737 mwaka 2005. Idadi ya watumiaji wa intaneti imeongezeka na kufikia 17,263,523 kutoka watu 1,013,104 mwaka 2005, hii inazidi kuongezeka kutokana na watumiaji wa simu za kisasa (*smart Phone*) kuongezeka. Kwa jumla matumizi ya simu za mkononi yamebadilisha mfumo wa maisha ya wananchi kwani kumekuwapo na urahisi katika kupata huduma mbalimbali kama kutuma na kupokea pesa, kulipia ankra za umeme, maji, ving'amuzi na huduma nyingine nyingi bila kulazimika kuzifuata mbali.

Hata hivyo, pamoja na zoezi la usajili wa laini za simu kuendelea kwa idadi kubwa ya watu, kumekuwepo na changamoto katika zoezi zima la usajili wa laini kwani wananchi walio wengi hawana vitambulisho vya kudumu; hivyo, hupelekea kusajili kwa majina ya uongo au kutumia kitambulisho cha mtu mwingine.

c) Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta

76. **Mheshimiwa spika**, mradi wa anuani za makazi unalenga kuanzisha mfumo mpya wa anuani nchini utakaowezesha kuwapo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni kwa kutumia anuani za makazi ujulikanao kama postikodi. Mradi huu ni muhimu sana kwani utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchimi na kisiasa. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto ,magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.
77. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa mfumo huu uko tayari nchi nzima kinachosubiliwa ni serikali za miji na mitaa kutekeleza katika maeneo husika. mamlaka imeweka postikodi maeneo ya mfano katika jiji la Arusha, Dodoma na Dar Salaam ambapo imeweka namba za nyumba na majina ya mitaa. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa kutokuwa na mipango miji na ujenzi holela, na pia upatikanaji wa majina ya mitaa, kutokana na mabishano juu ya majina katika ngazi ya Halmashauri husika.

Vilevile, changamoto nyingine zinazoukabili mradi huu ni kutokuwa na bajeti ya kutosha, kutokuwepo kwa takwimu halisi za idadi ya barabara/mitaa katika

kata, kutokuwepo kwa takwimu na taarifa halisi za makazi na wakazi katika Kata na uharibifu wa miundombinu kama vile nguzo za majina ya mitaa na vibao vya namba za nyumba hata sehemu zilizopangwa.

78. **Mheshimiwa spika** kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa. Kamati ilipopata taarifa hii mwezi Machi, 2016 fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu hazikuwa zimetolewa. Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga **shilingi bilioni 3 (3,000,000,000.00)** kwa ajili ya uendelezaji wa mradi katika mji wa Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza na Mbeya.

d) Shirika la posta Tanzania

79. **Mheshimiwa spika**, shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliana na ushindani uliopo na changamoto ya soko katika sekta ya posta. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea kufanyia kazi Shirika hili ili liweze kujiendesha ikiwa ni pamoja na kulipa madeni mbalimbali. Aidha, shirika limeendelea kulipa *pension* za wastaafu wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki kwa niaba ya Serikali kwa makubaliano ya kurejeshewa fedha husika na Serikali ambapo hadi sasa Shirika linaidai serikali **shilingi billion 5**.
80. **Mheshimiwa spika**, kufuatia hali mbaya ya kifedha Shirika limeshindwa kulipa madeni ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA ilikamata akaunti za shirika mara tatu kati ya Desemba 2015 na Februari 2016 kwa wakati tofauti kwa limbikizo la **takribani bilioni 15**. Aidha, Shirika kuwekwa kwenye orodha ya mashirika yanayokusudiwa kurekebisha kumesababisha Shirika kushindwa kupata kibali cha kukopa fedha kwa taasisi za fedha kwa ajili yakuongeza mtaji na kuendeleza rasilimali za Shirika na kutoa huduma zake.

d) Mfuko wa mawasiliano kwa wote (UCSAF)

81. **Mheshimiwa spika**, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote Kamati imejulishwa kuwa mfuko huu ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2006 ukiwa na lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea kupeleka mawasiliano vijijini kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan makampuni ya simu. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya watoa huduma za simu wengi kutokushiriki kikamilifu katika zoezi hili, Serikali imeandaa Mwongozo wa kupeleka Mawasiliano vijijini kwa kushirikiana na watoa huduma ili kuongeza kasi ya kupeleka mawasiliano vijijini. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 Kata 100 zimeshapata huduma za mawasiliano. Hadi sasa Mfuko wa Mawasiliano umetekeleza miradi sita ya kupeleka mawasiliano vijijini ambapo jumla ya Kata 433 zenye jumla ya Vijiji 1939 na wakazi takribani 6,229,825 na kugharimu ruzuku kiasi cha Dola za Marekani **milioni 37**.

82. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu na muda ambao mfuko huu umekaa toka kuanzishwa kwake, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Kamati imebaini kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajaimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kama mojawapo ya uwajibikaji wao kwa jamii (*corporate social responsibility*). Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku kuyafikia maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara ili kuyafikia yote kwa haraka zaidi utaratibu wa kuzitaka Kampuni kubwa kuonekana zinasaidia ni jambo sahihi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

83. **Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati ambao **umetolewa** katika vikao pamoja na ziara mbalimbali zilizofanywa na Kamati. Ushauri huu wa Kamati umezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.
84. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuunganisha Wizara za Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano kuwa Wizara moja kwani ukiangalia kwa undani majukumu hususan ya ujenzi na uchukuzi yanaingiliana. Kuunganishwa kwa Wizara hizi kutasaidia sana katika kushughulikia mambo yote yanayohusu miundombinu ya nchi yetu kwa pamoja.
85. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo kwa mara ya kwanza Sekta hii imeweza kupata **asilimia 16.7** ya bajeti yote ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, Kamati inaona bado upo umuhimu wa kutenga fedha nyingi zaidi katika siku sijazo kwa ajili ya Miundombinu angalau kufikia **asilimia 20** ya bajeti yote ya Serikali. Ikumbukwe kuwa miundombinu hii ndiyo itawezesha tija na utendaji bora wa Sekta nyingine ziwe za Kiuchumi au Kijamii. Mbali na kuongeza bajeti kufikia asilimia 20 nia matarajio ya Kamati kuwa katika bajeti hii ya mwaka 2016/2017 fedha zitatolewa zote kwa wakati kama zilivyoidhinishwa ili kuharakisha maendeleo katika miradi mbalimbali katika sekta hii.

3.1 Sekta ya Uchukuzi

86. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuangalia bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Uchukuzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, pamoja na bajeti hii kuongezeka kila mwaka, bado kiwango kinachotengwa ni

kidogo na hakipatikani kwa wakati hivyo kushindwa kukidhi mahitaji makubwa tuliyonayo hasa ujenzi wa reli, bandari na viwanja vya ndege. Baada ya kupitia kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati imebaini pamoja na Serikali kuainisha miundombinu ya Uchukuzi kuwa ni kati ya maeneo ya kipaumbele, utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo imeshindwa kukamilika kutokana na kutotolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyotarajiwa.

87. **Mheshimiwa Spika**, Kiasi cha fedha za ndani cha **asilimia 40** iliyotolewa hadi mwezi Machi, 2016 ni kidogo sana ukilinganisha na miradi mikubwa iliyopo kwenye Sekta ya Uchukuzi kama vile ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege, ukarabati na ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya reli na uboreshaji na upanuzi wa bandari. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuweza kuwa na ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa miradi na hatimaye kufikia malengo tuliojiwekea.
88. **Mheshimiwa Spika**, pia fedha za nje zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2016 kiasi cha **asilimia 68** hakiridhishi. Ni vyema sasa katika awamu hii mpya, Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu hasa fedha za ndani za Maendeleo zinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuweza kuleta ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo na hatimaye kuyafikia kwa wakati malengo ambayo Taifa limejiwekea.
89. **Mheshimiwa Spika**, pia ni vyema Serikali ikawa inatoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kwani kucheleweshwa kwa fedha hizo kunapunguza kasi ya maendeleo ambayo wananchi wanategemea kuyapata kwa wakati.
90. **Mheshimiwa Spika**, reli ya kati inanufaisha takribani Mikoa 15 ya Tanzania. Kwa lugha nyingine, karibu zaidi ya nusu ya Watanzania wanatumia reli ya kati. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa reli ya kati na matawi yake ambayo ni kutoka Dar es Salaam – Kigoma, Uvinza - Msongati kwa ajili ya mzigo wa Burundi; tawi la Tabora- Kalemi kwa ajili ya mizigo ya DRC; na Tabora- Shinyanga- Mwanza kwa ajili ya ukanda wa ziwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali pia kuanza kufanya utafiti wa kupanua matawi (*spurs*) ya reli ya kati kutoka Bandari kavu ya Isaka (Shinyanga) hadi Rusumo Mkoani Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya *Nickel* huko Kabanga kutekelezeka. Serikali pia ichunguze uwezekano wa kuweka tawi la reli sambamba na bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Isaka ili kupanua uwekezaji katika viwanda.
91. **Mheshimiwa Spika**, maendeleo ni vita, hivyo ni lazima Serikali itambue kuwa nchi zingine wanachama wa Afrika Mashariki zinaendelea kujenga kwa kasi

kubwa sana reli kwa kiwango cha *Standard gauge* kutoka Mombasa- Nairobi-Kampala hadi Kigali. Itambulike kwamba itakuwa vigumu kwa Bandari za Tanzania kushindana na Bandari za Kenya kwa mzigo wa Uganda na Rwanda bila kuwa na reli inayoziungisha nchi hizo na reli ya Kati hadi Isaka (Shinyanga).

92. **Mheshimwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea reli ya *Standard Gauge* iliyojengwa na Kampuni ya CRCC ya Serikali ya China pale Soga- Kibaha yenye urefu wa kilometa 1.5. Kamati inashauri Serikali kukamilisha hatua zake za ujenzi wa reli ya aina ile ili kuleta maendeleo ya haraka katika nchi yetu.
93. **Mheshimiwa Spika**, ikiwa mababu zetu wakati ukoloni wa Wajerumani waliweza kujenga reli hii ya kati ndani ya miaka mitano tu (1906-1911) kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma; tena bila ya kuwa na teknolojia ya kisasa; ni wazi kuwa Serikali hii ya awamu ya tano, chini ya uongozi mahiri na kasi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inauwezo wa kukamilisha mradi huu kwa muda mfupi. Kamati inashauri Serikali itangaze rasmi muda wa kuanza na kukamilisha kazi ya ujenzi wa reli hii na matawi yake.
94. **Mheshimiwa Spika**, wakati tunaendelea na uimarishaji wa mtandao wa reli nchini, Kamati inashauri uimarishwaji huu uende sambamba na kutafuta suluhisho madhubuti katika maeneo korofi kama vile stesheni ya Kilosa- Gulwe Morogoro kwani tatizo la kuharibika eneo hili kwa reli kusombwa na maji limekuwa linajirudia mara kwa mara na kugharimu fedha nyingi bila kupata suluhisho la kudumu.
95. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati inashauri Serikali iimarisha karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu.
96. **Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati imebaini kwamba lengo zuri la Serikali kutenganisha mashirika yake ya RAHCO na TRL pamoja na TPA na MSCL limeshindwa kufanikiwa kwa sababu ushindani uliotegemewa haukapatikana (*Market Failure*). Kamati inashauri Mashirika haya yaunganishwe ili Mashirika yake mama yasaidiane na mashirika ya huduma ambayo mpaka sasa yanatengeneza hasara (*cross-subsidization*) na yanahitaji kusaidiwa na shirika mama.
97. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA; Kamati inashauri Serikali kuharakisha kukamilisha utaratibu mpya waliokubalina kati yake na Zambia juu ya uendehaji wa Shirika la TAZARA. Vilevile, Serikali iendeele kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha kwenye Shirika hili; Aidha, Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi pamoja na kuhakikisha makato ya wafanyakazi

yanayopelekwa katika mifuko ya hifadhi jamii ili kuepuka usumbufu kwa wafanyakazi wanaostaafu.

98. **Mheshimiwa Spika**, Bandari ya Dar es Salaam ndiyo bandari kubwa kuliko zote Tanzania inayohudumia asilimia tisini (90%) ya shehena za aina mbalimbali za nchi zaidi ya kumi yaani Tanzania, Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Uganda, Zimbabwe, Malawi, Comoro na Sudan Kusini.
99. **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, ili kukabiliana na changamoto ambazo zimesababisha kushuka kwa shehena ya mizigo katika bandari ya Dar es Salaam; Serikali haina budi kuchukua hatua za haraka na madhubuti katika kutafuta ufumbuzi wa masuala yafuatayo:-
- i. Hofu ya wateja kutokana na kuanzishwa kwa Sheria ya (*Value Added Tax-VAT*) kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo ya nchi jirani (*VAT on transit goods*) ambayo ni kinyume na Sheria za Kimataifa. Uwepo wa Sheria hii unawafanya wateja kutotumia bandari za Tanzania kwa sababu ya gharama;
 - ii. Mgongano wa tozo za hifadhi za mizigo "*Customs Warehouse Rent*" inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA na "*Storage Charges*" zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA. Malipo haya yanafanana isipokuwa yametofautiana majina tu, hivyo wafanyabiashara kuona kuwa wanalipa mara mbili igharama ya hifadhi za mizigo;
 - iii. Tozo za barabara (*Road Tolls*) ambapo hutozwa **Dola za Kimarekani 16** kwa Kilomita ukilinganisha na **Dola za Kimarekani 8** kwa Kilomita zinazotozwa katika nchi zenye bandari shindani;
 - iv. Tozo ya **Dola za Kimarekani 23** kwa tani kwa mzigo wa shaba ambapo bandari nyingine shindani kama Durban hutoza Dola za **Kimarekani 17.86**;
 - v. Kwa mujibu wa makubaliano ya mwanzo, tozo kubwa kwa mizigo yote inayotoka ama kwenda Zambia tofauti na tozo za nchi nyingine kama Rwanda na Burundi. Mfano, kasha la urefu wa futi 40 linatozwa **Dola za Kimarekani 530** kwa mzigo wa Zambia badala ya **Dola za Kimarekani 320** ambazo hutozwa kwa kasha hilo hilo linalokwenda Rwanda ama Burundi;
 - vi. Himaya ya forodha kwa pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mzigo wa Congo umeleta utata na kupunguza motisha kwa wafanyabiashara wan chi hiyo kwa kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Hii inatokana na kuwa mfumo wa ukusanyaji kodi ndani ya DRC unatoa mwanya kwa baadhi ya wafanyabiashara katika nchi hiyo kutolipa kodi kwa asilimia mia moja (100%) tofauti na mizigo inayopatikana kwenye mfumo wa "*Single Customs Territory*" ambayo hutozwa kodi kwa asilimia mia moja (100%) jambo linalosababisha

baadhi ya wafanyabiashara wa Congo kuona gharama kubwa kupitisha mizigo yao Tanzania;

- vii. Muda mfupi (*Short grace period of Transit Bulk liquid*) kwa mzigo wa mafuta wa nchi za jirani (Siku 30) bila kujali mazingira ya usafirisha wa barabara katika nchi yetu tofauti na nchi nyingine shindani ambazo ni siku 60 hadi 90 na utaratibu duni;
- viii. Mfumo wa TANCIS wa TRA kutokurushu kugawanya "*Bill of Lading*" ili kuruhusu kutoa mizigo ambayo haina tatizo panapokuwa na tatizo la Mzigo Moja badala ya mzigo wote kuzuiwa na kusababisha gharama za tozo za hifadhi kwa mteja ambazo sio za lazima;
- ix. Kuongezeka kwa Tozo kutokana na "*Government Chemical Agencies*" kutoza USD 1.00 Kwa Tani badala ya USD100 Kwa "*Bill of lading*" kwa bidhaa ambazo wanazikagua kama vile mbolea na hivyo kuongeza kutoka wastani wa USD 500 hadi USD 20,000 au zaidi kutokana na ukubwa wa mzigo;
- x. Idara za Serikali (OGD's) na Mabenki kutokufanya kazi masaa 24 /7. Utendaji wa bandari unategemea upatikanaji wa vibali kutoka idara za mbalimbali za serikali pamoja na huduma za kibenki;
- xi. Usalama mdogo wa mizigo inayosafirishwa kwenda nchi za jirani (wizi wa mizigo na madereva kuvamiwa) na hivyo wenye mzigo kulazimika kuingia gharama ya kuweka walinzi wa kusindikiza mizigo; na
- xii. Gharama kubwa za usafirishaji kwa njia ya barabara inayochangiwa na wingi wa vituo vya ukaguzi "*check Points*" na malipo yanayodaiwa na watendaji wasio waaminifu.

100. **Mheshimiwa Spika**, ni wakati sasa tunahitaji kuweka mazingira mazuri ya bandari yetu na kuweza kuwavutia na kuwashawishi wafanyabiashara ili kuendelea kutumia bandari ya Dar es Salaam. Ikiwa Serikali itashughulikia changamoto zilizotajwa na Kamati, pamoja na kuboresha mazingira bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina katika gati namba 1-7, upanuzi wa lango la kuingilia meli, kujenga gati namba 13 & 14 pamoja na kuimarisha usafiri wa njia ya reli, Bandari ya Dar es Salaam itaweza kushindana na bandari nyingine hivyo kutoa mchango mkubwa na hata kukuza uchumi wa nchi yetu. Kamati inashauri Serikali kuhimiza Mamlaka ya Bandari Tanzania kuwa na mkakati wa kutangaza maboresho hayo na huduma zake kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuharakisha TICS kuuza hisa **asilimia arobaini (40%)** ya hisa zote za TICS kwa wafanyakazi na wananchi wa kawaida

kupitia soko la hiza la Dar es Salaam. Pia Kamati inaishauri Serikali kujiridhisha juu uongezwaji wa mkataba wa miaka 15.

101. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba bandari kavu- ICD's zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano wa mizigo bandarini; bandari hizi zimeendelea kulalamikiwa kwa uchelewashaji na upotevu wa mizigo pamoja na ukwepaji wa kodi. Ili kuondokana na matatizo haya na kuongeza ushindani, Kamati inashauri Serikali kuondoa zuio kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA kufungua bandari kavu yake huko Kisarawe kama ilivyokuwa imepangwa. Kamati pia inashauri maombi mengine ya ujenzi wa bandari kavu -ICDS nje ya Dar es Salaam yapewe kipaumbele kama mkakati wa kuimarisha ushindani hasa na ICD's zinazojihusiha na udanganyifu.
102. **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwapo kwa udanganyifu unaofanywa na mawakala (*freight forward*) kwa kuongeza gharama kwenye hati za madai zinazotumwa kwa wateja. Kamati inashauri adhabu kali zitolewe kwa mawakala wanaobainika kuongeza gharama hizo ikiwezekana wafutiwe leseni zao.
103. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Temeke zilishaanza mchakato wa kuwa na eneo Kurasini- Shimo la Udongo ambalo litatumika kama maegesho ya magari yanaoingiza na kutoa mizigo bandarini, Kamati inashauri mchakato huo sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maeneo ya maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika.
104. **Mheshimiwa Spika**, Ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi; Kamati inashauri Serikali kuzingatia ushauri ufuatao:-
 - i) Kwa kuwa Mamlaka hii inatoa mchango mkubwa katika mapato yatoakanayo Na viwanja vya ndege, na kwa kuwa bado kuna changamoto kubwa ya uboreshaji na ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli (*retention*) yatoakanayo na viwanja vya ndege ili kusaidia kuongeza kasi ya shughuli za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini.
 - ii. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kabla ya mwaka wa fedha (2015/2016) kuisha; imalize malipo ya fedha yaliyoidhinishwa kwa kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe, Mtwara na Bukoba;

- iii. Kamati pia inashauri, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kupewa fedha zote zinazotakiwa kwa ajili ya ulipaji fidia ambazo kwa sasa zinafikia takribani **shilingi bilioni 70** kwa viwanja vya ndege vya Julius Nyerere International Airport-JNIA, Mwanza, Bukoba, Omukajunguti, Msalato, Kigoma, Shinyanga, Songwe, Sumbawanga, n.k.
- iv. Serikali itoe fedha zote zinazodaiwa na makandarasi kama madeni kwa miradi iliyosisimama na inayoendelea ambapo madeni haya kwa sasa yanafikia takribani TShs 90 bilioni;
- v. Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuharakisha kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu (*Termina III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa yaani Disemba 2017. Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi;
- vii. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro; Kamati inashauri kiwanja hiki kirejeshwe kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA ili kuongeza ufanisi, tija na mapato ya Taasisi ikizingatiwa "shares" zote zimenunuliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania- TAA ambayo bado hadi sasa inalipa mkopo wa ununuaji wa "shares" hizo;
105. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inapata Hati Miliki za Mali zake zote kwani Kamati ilibaini viwanja vingi vya ndege nchini havina Hati Miliki isipokuwa Viwanja vya Arusha, Moshi, Dar es Salaam, Musoma na Tanga. Kuwa na Hati Miliki na kuweka mipaka kwa mfano uzio au nguzo kutaepusha migogoro na wananchi wanaishi kando kando ya Viwanja vya Ndege na kuzuia uvamizi.
106. Sambamba na hilo; Kamati pia ilibaini tatizo la wamiliki binafsi katika maeneo ya viwanja vya ndege ambao wana hati miliki; Kamati inashauri Serikali kuhakikisha hakuna mgongano katika utendajii kazi.
107. Vilevile, Kamati inashauri Mamlaka ya viwanja vya Ndege iwezeshe Kisheria kuwa Mamlaka Kamili badala ya Wakala wa Serikali kama ilivyo sasa. Hii itawezesha taasisi kupitia Bodi yake kufanya maamuzi yanayohusu kazi na mambo mbalimbali kwa wakati.
108. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Ndege ya Tanzania- ATCL, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha **bilioni 5 (5,000,000,000.00)** kwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya ununuzi wa Ndege mpya nne; Kamati inashauri fedha hizi zitolewe kwa wakati ili shirika hili liweze kujiendesha ipasavyo.

3.2 Sekta ya Ujenzi

109. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali imeonesha dhamira ya dhati kwa kutoa fedha kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi kwa zaidi ya asilimia mia moja (100%). Kamati inashauri Serikali iendeleze utaratibu huu mzuri wa kutoa fedha zote kwa sekta hii muhimu ya ujenzi ambayo inabeba sekta nyingine zote.
110. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia Mamlaka yake chini ya *Appropriation Act, 2015/2016*, Kifungu cha 6(1), kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Ujenzi ili kulipa madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2016; Serikali imeshalipa kiasi cha **shilingi bilioni 635.35** kutoka madaai ya **shilingi trilioni 1.2**. Pamoja na juhudi hizo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kulipa madeni hayo na kuhakikisha madeni yote ya nyuma yanalipwa kwani kuendelea kulimbikiza madeni haya kunasababisha hasara mbalimbali kwa Serikali ikiwa ni pamoja na ongezeko la riba, kazi kufanyika kwa muda mrefu ukilinganisha na muda mradi uliowekewa kukamilika na pia bajeti inayopitishwa kuonekana kubwa ilhali kwa asilimia kubwa inatumika kulipia madeni.
111. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kutekeleza Sera yake ya kuunganisha Mikoa kwa barabara za lami (*Trunk Roads*) kama vile Mikoa ya Mbeya –Makete- Njombe; Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora na Kigoma-Kagera. Aidha, miradi ya barabara hizi ambayo inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu.
112. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na barabara zilizotengewa fedha 2016/17; vilevile, Kamati inashauri Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha nchi yetu na nchi zingine (*Boarder Roads*) hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara.
113. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa **shilingi bilioni 30** kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mikoa yote (*Regional Roads*) ya Tanzania Bara pamoja na madaraja. Kamati inaona kwamba fedha hizi hazitoshi kabisa kwa kazi muhimu ya kutekeleza majukumu ya TANROADS katika kuimarisha ujenzi wa barabara katika Mikoa. Kamati inashauri Serikali kuipa TANROADS fedha za kutosha ili kujenga barabara za lami zenye viwango, hivyo kuepusha hasara kubwa inayotokana na ukarabati wa mara kwa mara wa barabara zinazojengwa kwa changarawe ambayo huondoshwa na mvua muda mfupi baada ya kuwekwa hasa wilaya zenye mvua nyingi.
114. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza ushauri huu Serikali izingatie vigezo muhimu kiuchumi, Kijamii, hasa huduma za afya pamoja na ahadi za

Mheshimiwa Rais Mstaafu na Rais aliyepo madarakani wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2015. Mfano barabara za kupewa kipaumbele ni pamoja na barabara ya Muleba-Kanyambogo-Rubya- Nshamba- Muhutwe; barabara ya Runazi- Karambi- Kasindaga; Runazi – Burigi; barabara ya Njombe- Makete- Isyonji; barabara ya Kitulo- Matamba- Chimala; barabara ya Mlangali-Lupila- Ikonda; barabara ya Mpanda- Kigoma; barabara ya Sumbawanga-Mpanda; barabara ya Masasi-Nachingwea-Ruangwa; barabara ya Mtwara-Newala- Masasi; barabara ya Liwale-Nachingwea, barabara ya Morogoro-Mziha- Handeni; barabara Mpanda-Mlele-Nyonga-Sinkenga- Tabora- Uvinza; barabara ya Malagarasi, barabara ya Kibo- Mwese; Manyoni- Kishapu, barabara ya Ngudu; barabara ya Ikwiriri- Masengi; barabara ya Kisarawe- Mlandizi; barabara ya Makofia- Mlandizi- Mzenge; barabara ya Kilema–Mandaka; barabara ya Dodoma- Kondo- Babati na barabara ya Nongwi.

115. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali na kuunga mkono kwa juhudi zake za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam kupitia miradi mbalimbali kwa mfano mradi wa DART chini ya TAMISEMI, ujenzi wa *fly overs*; barabara ya Dar es Salaam- Chalinze expressway na ukarabati, upanuzi na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zinazounganisha maeneo ya Dar es Salaam (*Feeder Roads*) ikiwemo Tabata Dampo- Kigogo (km1.6), Kimara-Kilungule-External (km 9), Mbezi- Malambamawili- kinyerezi- Banana-(km 14), Tegeta-Kibaoni-Wazo Hill- Goba- Mbezi (Morogoro Road) km 20, Tangi bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti- Msewe-Changanyike (km 2.6), Kibamba-Kisopwa-Mlonganzila (km 4.0), Banana- Kitunda-Kivule- Msongola (km 14.7), Kitunda- Moshi Bar (3.2) , Ardhi-Makongo (km 4). Aidha, Kamati inashauri barabara ya Ardhi-Makongo iendelezwe kutoka Makongo CCM hadi shule ya msingi Londa hadi daraja la Kawe ili kufungua njia ya kwenda makaburi mapya Makongo.
116. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu kutunisha fedha za Mfuko wa Barabara, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa tozo la *Road Licence* kupelekwa kwenye Mfuko wa Barabara ili kuiongezea mapato TANROADS hasa kwa kuzingatia mapendekezo yetu kwamba TANROADS haijapangiwa fedha za kutosha kwa barabara za Mikoa na dharura zinazojitokeza na kuhitaji matengenezo ya haraka.
117. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama luninga, magazeti, radio na Simu za Mkononi. Pia vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara aendeleo kukamilisha zoezi la zuri alilolianzisha Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati alipokuwa Waziri wa Ujenzi

kwa kuonesha mipaka ya barabara na hivyo kuepusha uvamizi wa maeneo ya barabara.

118. Serikali kuharakisha kuleta Sheria ya Vyuma Chakavu ili kuweza kusaidia kupambana na watu wachache waliokosa uzalendo ambao wanaiba vyuma zenye alama za barabarani na kuviuza kama vyuma chakavu. Vile vile kuchukuwa hatua kali za kulipa faini kwa magari ambayo yanagonga vibao vya alama barabarani.
119. Kamati inasisitiza matuta ya barabarani kupunguzwa ama kuondolewa kabisa kwani kitaalam yanachangia uharibifu wa barabara. Kamati inasisitiza kuwa watumiaji wa barabara wanaokiuka sheria na kwenda mwendo kasi sehemu za makazi kuchukuliwa hatua kali.
120. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mzani unaopima magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion*) katika eneo la Vigwaza- Kibaha. Kamati inashauri Serikali kufunga mizani ya kisasa kama hii hasa katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari ili kuokoa muda wa msafiri ambao huongeza gharama.
121. Kamati inapongeza Serikali na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii – NSSF kwa kukamilisha ujenzi wa daraja la Mwalim Nyerere (Kigamboni) hatimaye kulizindua rasmi tarehe 19 Aprili 2016. Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kumpa heshima Baba wa Taifa ili daraja hili la kipekee Afrika Mashariki lipewe jina lake. Kamati inashauri na kuhimiza wadau wote wanaohusika na Daraja hili ikiwa ni pamoja na wananchi kutunza vizuri miundombinu ya Daraja hili la kujivunia na pia kuweka mipango mizuri ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji hasa wageni watakaotembelea daraja hilo.
122. Kamati inashauri Serikali kukusanya mapato yatokanayo na malipo ya watu wanaopita katika daraja hili kwa mfumo wa *electronic* ili kudhibiti ubadhilifu wa fedha kwa watu wachache wasio waaminifu unaoweza kutokea.

3.3 Sekta ya Mawasiliano

123. **Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Sekta ya Mawasiliano, Kamati ilibaini katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa Fedha 2015/2016, hadi mwezi Machi, 2016 hakuna kiasi chochote cha fedha za ndani za maendeleo zilizokuwa zimetolewa kwa Sekta ya Mawasiliano. Kwa upande wa fedha za nje za miradi ya maendeleo zimetolewa kiasi cha **asilimia 32**. Hii ni changamoto kubwa ambayo inachangia kutokamilika kwa baadhi ya miradi kama ilivyotarajiwa. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zote zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016 kabla ya

mwaka wa fedha kuisha, kwani haitokuwa na maana kuidhinisha bajeti nyingine mpya wakati fedha za mwaka unaoisha hazitolewi.

124. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya Makampuni ya Simu kwa kutumia mtambo wa TTMS ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu za mkononi. Kuendelea kuchelewa kulitekeleza suala hili kunazidi kuikosesha nchi kodi stahiki kutokana na Makampuni haya kutotozwa kodi stahiki.
125. Aidha, kwa kuwa Kamati ilijulishwa kwamba, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA imeweza kupata takwimu za huduma za “*Mobile Money*” baada ya usimikaji wa mfumo wa “*Mobile Money Monitoring Solution*”; na kwa kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilishawaandikia barua Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA ili ianze kutumia taarifa hizo na kuweza kupata mapato stahiki lakini hadi mwezi Machi Kamati ilipotembelea Mamlaka ya Mawasiliano bado TRA ilikuwa haijaanza kutumia taarifa hizo na kulikosesha Taifa fedha nyingi; Kamati inaitaka Serikali iliambie Bunge lako Tukufu sababu zilizopelekea Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokutumia takwimu hizi muhimu na kuendelea kukosesha nchi mapato.
126. Aidha, Kamati inashauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao.
127. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kupitia TCRA ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuishia kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kuisaidia Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya *Cyber Crime* na kuwabana wahalifu.
128. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi nzuri ya Serikali ya kusambaza mawasiliano katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kupitia Mfuko wa Mawasilino kwa Wote- UCSAF. Hata hivyo, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Kamati inashauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (*Corporate Social Responsibility*).

129. **Mheshimiwa Spika**, ili mradi wa anuani za makazi (*postcode*) uweze kutekelezeka kwa haraka na ufanisi, na kwa kuzingatia mradi huu ni mtambuka; Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa.
130. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Shirika la Posta Tanzania; Kamati inasikitishwa na Serikali kuchelewa kulipa deni kiasi cha **shilingi billion 5** ambalo linatishia uwepo wa shirika hili linaloendelea kutoa huduma.
131. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL; Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kununua hisa **asilimia 35** zilizokuwa zinamilikiwa na Bharti Airtel katika TTCL ili sasa Kampuni hii iweze kupata dhamana ya mikopo na kuweza kujiimarisha na kuongeza ufanisi. Aidha, sambamba na hilo Kamati inashauri TTCL kuhakikisha inaboresha makusanyo ya mapato na madeni yanayotokana na huduma za simu ambayo kwa kiasi kikubwa wateja wanaodaiwa ni Serikali na taasisi zake.

4.0 HITIMISHO

132. **Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu.
133. **Mheshimiwa spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani (Mb), pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuhanga (Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Uchukuzi), Prof. Faustine Kamuzora (Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Eng. Dkt. Maria Sasabo. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Makaimu Wakurugenzi ambao muda wote wameonesha ueledi mkubwa.
134. **Mheshimiwa spika** kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wa kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake.
135. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe .Prof Norman Adamson Sigalla King, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb -Mjumbe
4. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb ..
5. Mhe. Mizar Bakari Haji, Mb ..
6. Mhe. James Francis Mbatia, Mb ..
7. Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb ..
8. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb ..
9. Mhe. Saul Henry Amon, Mb ..
10. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb ..
11. Mhe. Quambalo Willy Qulwi, Mb ..
12. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb ..
13. Mhe. Hawa Abdallah Bulembo, Mb ..
14. Mhe. Chuachua Mohamad Rashid, Mb ..
15. Mhe. Mery Deo Muro, Mb ..
16. Mhe. Ritha E. Kambati, Mb ..
17. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb ..
18. Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassym, Mb ..
19. Mhe. Bhagwanji Maganilal Meisuria, Mb ..
20. Mhe. Dua William Nkurua, Mb ..
21. Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb ..
22. Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb ..
23. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb ..
24. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb ..
25. Mhe. Emmanuel Mwakasaka, Mb ..

136. **Mheshimwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge. Dkt Thomas D. Kashililah pamoja na Sekreterietu ya Kamati ikiongozwa na Ndg. Msigwe D. Bisile, Ndg. Hosiana John, Ndg. Richard Masuke na wafanyakazi wote kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii. Mwisho namshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha kazi hii.

137. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/17 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

138. **Mheshimiwa spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Prof. Norman Adamson Sigalla King (Mb)
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

17 Mei 2016

SPIKA: Sasa naomba nimwite Msemaji Rasmi wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Namwona Mheshimiwa James Mbatia anakuja. *(Makofi)*

MHE. JAMES F. MBATIA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba nitoe maoni hayo chini ya Kanuni ya 99(9), Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie fursa hii nitoe shukrani zangu za dhati kwa kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge, kwa kunituua kuwa Msemaji wa Wizara hii. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Willy Qambalo, Naibu Waziri Kivuli na Mbunge wa Karatu kwa ushauri na maoni yake yaliyofanikisha kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Vunjo kwa kunichagua kwa zaidi ya asilimia 73 kuwa Mbunge wao; nawahakikishia utumishi wenye kuzingatia misingi ya kukuza utu wao na Taifa kwa ujumla. Kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kutoka moyoni kwa familia yangu, ndugu, jamaa na marafiki na wote kwa msaada wa hali na mali wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, katika Kitabu chake cha Binadamu na Maendeleo ukurasa wa 29 aya ya pili, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anayafafanua maendeleo kama ifuatavyo:-

“Maendeleo maana yake ni maendeleo ya watu, barabara, majumba, kuongeza mazao na vitu vingine vya aina hiyo, siyo maendeleo, ni vyombo vya

maendeleo. Barabara mpya inampanulia mtu uhuru wake kama ataitumia kusafiri. Kuongeza idadi ya majengo na shule ni maendeleo kama majengo hayo yanaweza kutumika kuongeza ujuzi wa elimu ya watu. Maendeleo yasiyokuwa ya watu, yanaweza yakawapendeza wataalam wa historia wa mwaka 3000 lakini kwetu hayana maana, kwani hayahusiani na maisha ya kesho tunayoyajenga."

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikitaja kwa mbwembwe kilometa za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami, wakati ambapo wananchi wengi wanakumbana na adha ya usafiri kutokana na ubovu wa barabara hizo. Kwa mfano, wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao na kupeleka sokoni; akinamama kufariki njiani wakati wa kwenda kupata huduma za matibabu au kujifungua; kuongezeka kwa vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara za lami zilizojengwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 kwa kiwango cha lami ni wastani wa asilimia 16 tu ya barabara zote nchini zenye urefu wa zaidi ya kilometa 35,000. Kwa kasi hii italigharimu Taifa na Chama hiki cha Mapinduzi miaka zaidi ya 62 ijayo kukamilisha ujenzi wa kilometa 29,432 ambayo ni sawa na asilimia 84 ya barabara zote zilizosalia kujengwa katika kiwango cha lami licha ya kujumlisha barabara zinazofanyiwa upembuzi na usanifu wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi ambaye kwa sasa ndiye Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwasilisha hotuba yake katika Bunge la Kumi, kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, alikiri hapa Bungeni kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika Awamu ya Nne ilishindwa kutekeleza ilani zake kikamilifu za uchaguzi kwa mwaka 2005 mpaka mwaka 2015, kwa kujenga barabara nchini kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 5,568 sawa na asilimia 31 tu kwa lengo walilojiwekea la kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilometa 17,762. Sehemu ya Hotuba yake nimeinukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya Awamu ya Tano kutoa maelezo ya kina mbele ya Bunge hili ina mipango gani ya uhakika na endelevu ya kukamilisha ujenzi wa barabara hizo kwa viwango vinavyokubalika Kimataifa na kwa kuzingatia vipaumbele kwa misingi ya kitaalam, badala ya ahadi nyingi zisizotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TANROADS imebainika kuwa na utendaji ambapo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alibaini juu ya usimamizi mbovu katika mikataba ya ujenzi wa barabara na madaraja ambapo ilikuwa chini ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi katika Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TANROADS wakati wa kipindi hicho, iliitia hasara Serikali ya jumla ya Shilingi bilioni 5.6 kutoka kwenye riba inayoongezeka siku hadi siku. TANROADS kuchelewa kuwalipa Makandarasi 11 kati ya kipindi cha mwaka 2012 na mwaka 2015 kwa mujibu wa ripoti ya CAG ya Hesabu za Serikali Kuu akikagua taarifa ya fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2015 iliyotolewa mwezi Machi ukurasa wa 134 na 135.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajuliza kama Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kazi yake kwa haki, uadilifu, uwazi na usawa kwa wote na hasa kwa kile kinachojulikana kama utumbuaji majipu; swali hapa ni nani amfunge paka kengele? Au mkuki mtamu kwa nguruwe, mchungu kwa binadamu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji na utunzaji wa barabara nchini (*Super Single Tyre*), utafiti unaonesha matairi haya yanaharibu barabara. Matairi haya yameanza kutumika takribani miaka mitano iliyopita na mizigo iliyokuwa inabebwa na matairi 24, sasa inabebwa na matairi 12. Matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa barabara.

Uamuzi wa kuruhusu matairi haya haukuwa na busara maana barabara zetu hazijabuniwa kuhimili shinikizo la uzito (*excessive pressure*) linalotokana na matairi haya. Serikali izuie mara moja matumizi ya matairi haya ili kuzinusuru barabara zetu, lakini pia kuokoa fedha za walipa kodi zinazotumika kurekebisha mara kwa mara barabara hizo na kunyima fursa maeneo mengine kupata barabara kwa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo Tanzania ndiye mhusika mkuu katika kuhakikisha nyumba za Serikali zinakuwa katika hali nzuri kwa watumishi wa Serikali kuishi. Katika muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inalikumbusha Bunge kwamba kati ya mwaka 2002 mpaka 2004, Serikali iliiza jumla ya nyumba zipatazo 7,921 na mpaka mwaka 2008 Serikali ilikuwa imejenga nyumba 650 tu.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu za Bunge zinaonesha kwamba Serikali ilitoa taarifa ndani ya Bunge hili kuwa kuna Kamati iliundwa kuchunguza mchakato wa mauzo ya nyumba ya Serikali na Kamati ilitegemea kumaliza kazi yake Februari, 2007, lakini hadi Bunge la Tisa na la Kumi kumaliza uhai wake, hakuna taarifa iliyotolewa na Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali ya Awamu ya Tano irejeshe nyumba hizo mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *Hansard* ya tarehe 25 Aprili, 2008, Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha Nne, Bunge kwa kauli moja baada ya mjadala mkubwa wa hoja binafsi iliyowasilishwa na aliyekuwa Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Aloyce Kimaro iliyohusu Serikali kurejesha nyumba zake zilizouzwa kienyeji na hivyo kuisababishia Serikali hasara kubwa; na hoja hiyo

iliungwa mkono na Bunge ikapitishwa azimio; naomba kunukuu azimio hilo. “Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, itekeleze mara moja bila kusita, Agizo la Rais wa Awamu ya Nne, wakati huo Mheshimiwa Kikwete, kurejesha nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu na kwa watu ambao hawakuwa Watumishi wa Serikali wakati huo na vilevile nyumba ambazo hazikupaswa kuuzwa kama zile zilizopo kwenye maeneo ya Utawala wa Serikali; Irejeshe kwenye umiliki wake nyumba hizo zilizouzwa kinyume na utaratibu; Itoe orodha ya nyumba zake ambazo zilikuwa kwa watu ambao sio Watumishi wa Serikali kinyume na utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za Watumishi wa Serikali wanaostahili kutumia; na ichukue hatua kwa wale ambao hawajalipia na mikataba yao ya kuuziwa nyumba irejewe kuhakikisha kuwa malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao kufutwa na nyumba kurejeshwa kwenye miliki ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutekeleza azimio hilo la Bunge na kwa njia hiyo ile kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu, iweze kutafsiriwa kwa vitendo. Tunajua uuzwaji wa nyumba hizo ulisimamiwa na Wizara ya aliyekuwa akiiongoza yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais wa sasa na kwa uwezekano mkubwa kwamba alisimamia maamuzi ya Serikali kwa pamoja sasa atekeleze ili tuone usafi wake katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tuhuma kwamba mtu ambaye alikuwa dalali katika mchakato mzima wa kujenga *Terminal 3*, Uwanja wa Mwalimu Nyerere, katika mazingira tatanishi. Dalali alifanikiwa kupata asilimia 30 ya mkopo huo kama Kamisheni yake inayofikia takriban Dola za Kimarekani milioni 100, zaidi ya shilingi bilioni 200 za Tanzania. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa undani na kuleta taarifa hapa Bungeni au kwenye Kamati husika ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Dar es Salaam kwenda Bagamoyo ni jipu ambalo limeiva kwa viwango vyote vya sasa na linatakiwa litumbuliwe mara moja. Ni dhahiri kuwa kivuko cha Dar es Salaam kwenda Bagamoyo kilichonunuliwa na TEMESA chini ya uongozi wa Waziri wa Ujenzi wa Serikali ya Awamu ya Nne ambaye ndiye Rais wetu wa sasa wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika hesabu za Serikali Kuu akikagua taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2015 iliyotolewa mwezi Machi, 2016 ukurasa wa 132 na 33, alibaini ununuzi wa boti feki na mbovu uliofanywa na TEMESA na kugharimu Dola za Marekani milioni 4.9 sawa na zaidi ya shilingi bilioni 7.9 kupitia mkataba, namba ya mkataba imetajwa, uliosainiwa tarehe 25 Aprili, 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini masuala makuu mawili kuhusu ununuzi huo wa kivuko feki na kibovu cha Dar es Salaam kwenda Bagamoyo. Jambo la kwanza, CAG alibaini kasi ya kivuko hicho ni tofauti na kasi inayotakiwa kuwepo. Jambo la pili, ni kuwa cheti cha kukikubali kivuko hicho kilikuwa hakijatolewa, kinyume na kanuni ya 247 ya Manunuzi ya Umma. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji tabibu wa kutumbua jipu hili yuko wapi? Narudia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, tabibu wa kutumbua jipu hili yuko wapi? Au msemu usemao kuwa mganga hajigangi unatumika hapa? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji mtazamo mpya wa kisasa na wa uwepo miaka zaidi ya 50 ijayo. Tunahitaji reli ambayo itaendana na mazingira tuliyonayo ya ukubwa wa nchi na fursa tuliyonayo ya nchi zinazotuzunguka. Suala kubwa la kuzingatia ni mwendo kasi na uwezo wa kubeba uzito mkubwa. Ndiyo maana ya hoja ya kwa nini Tanzania inahitaji reli ya kisasa, yaani *standard gauge* sasa na siyo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuna mtazamo kuwa reli ya kisasa tunahitaji chuma cha reli chenye uzito wa paundi 90 hadi 100 au zaidi ya matarajio kwa miaka 50 ijayo. Tukumbuke kwamba uwekezaji wa reli ni uwekezaji mkubwa na hivyo unahitaji ulenge muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji reli ijengwe kwa mtazamo wa mbali wa zaidi ya miaka 50 ijayo. Tuanze na reli moja sambamba na reli iliyopo, lakini mpango uwe kuwa na zaidi ya reli moja ambapo baadaye itawezesha usafirishaji katikati ya Tanzania na hasa reli ya kati na nchi jirani kuwa za muda mfupi zaidi ili kuzivutia nchi jirani kuona reli yetu ndiyo ya pekee ya kuwasafirishia mizigo yao kwa muda mfupi na kwa usalama zaidi ikiwepo sababu za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *standard gauge* uendane sambamba na kuimarisha mawasiliano katika kuendesha shughuli za reli ili kuongeza ufanisi. Kuchelewa kwetu kujenga reli mpya sasa kutaligharimu Taifa hili na vizazi vijavyo. Itafanya tushindwe kufaidika na bandari zetu ipasavyo. Hata tukija kuamua baadaye gharama zitakuwa kubwa kuliko ilivyo hivi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili kufupisha muda wa ujenzi tuwe na wakandarasi ambao watapewa vipande vidogo vidogo takriban kilometa 200 ambavyo vitajengwa kwa wakati mmoja ili kuwezesha reli yetu ikamilike kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili TAZARA iweze kujiendesha kibiashara inatakiwa isafirishwe zaidi ya tani laki sita za mzigo kwa mwaka (*breakeven point*). Hata hivyo, TAZARA kwa muda mrefu imekuwa ikisafirisha mizigo chini ya tani laki moja za mizigo kwa mwaka kutokana na changamoto kadhaa.

Ucheleweshwaji wa mizigo bandarini, miundombinu chakavu, muda mrefu wa usafirishaji wa mizigo. Ni dhahiri TAZARA haitaweza kujiendesha kwa faida kama mabadiliko makubwa ya kiutawala hayatafanyika. Ni aibu na fedheha kwa Serikali kulipa mishahara ya watumishi wa shirika ambalo lilikuwa na uwezo mkubwa. TAZARA ina uongozi usiozingatia utawala. Ni vizuri Serikali ikaiangalia TAZARA kwa jicho la kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa ukiongeza ufanisi wa bandari zetu ni lazima kuimarisha miundombinu ya reli na barabara zinazozunguka bandari ili kuongeza mizigo inayosongamana bandarini kwa haraka na ufanisi. Aidha, Mamlaka ya Bandari (TPA) na Mamlaka ya Mapato (TRA) zinatakiwa kuwekeza kikamilifu kwenye mifumo ya kielektroniki ili kupunguza muda wa usafirishaji wa mizigo na hasa ile ya nchi jirani ambapo hivi sasa ni mkubwa kutokana na mizani na vituo vingi vya ukaguzi vilivyoko barabarani. Kupunguza muda wa usafirishaji kutavutia watu wengi zaidi katika kutumia Bandari ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa Kituo cha Ukusanyaji wa Mapato ya Pamoja chenye ufanisi na utaalum unaokubalika Kimataifa ili kupunguza ucheleweshaji na usumbufu wa kuondoa mizigo kutoka bandarini na kurahisisha ukusanyaji wa mapato na kufanya kazi kwa saa 24 wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuna mwekezaji alishafanya mawasiliano na Serikali hii kutumia eneo la Soga kujenga bandari kavu. Eneo hilo lipo katikati ya reli ya TAZARA na inayosimamiwa na Mamlaka ya Reli (RAHCO) na hivyo ingekuwa rahisi kuchukua mizigo kutoka bandarini kupitia reli ya TAZARA na reli ya kati. Hii ingefanya mizigo yote ya ndani na ya nje iweze kuchukuliwa eneo hili la Soga na hivyo kuondoa msongamano wa malori ya mizigo Jijini Dar es Salaam na bandarini. Aidha, TAZARA na TRL zote zinufaike na mpango huu ikiwa ni pamoja na TRA kuweza kukusanya kodi zake kwa ufanisi pamoja na kupunguza uzito kandamizi katika barabara zetu mjini.

Mheshimiwa Spika, kupitia fursa ya bomba la mafuta la nchi ya Uganda kupitia bandari ya Tanga ni wakati sasa Serikali iwekeze katika bandari hii ili tufungue ukanda wa kiuchumi wa kaskazini. Bandari hii inaweza kutumika zaidi kwa ajili ya mizigo iendayo Uganda, Kenya, Congo, Burundi, Rwanda na Sudani ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya ukanda huu wa kusini mwa Tanzania ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji kwa kuwa ukanda huu utafungua fursa nyingine sana za kiuchumi na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, shehena ya mafuta yaliyosafishwa hadi hivi sasa yanafikia tani milioni 3.6 kwa mwaka ukizingatia kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, mahitaji ya mafuta yatazidi tani milioni sita kwa mwaka kwa kipindi kisichozidi miaka 10 ijayo.

Mheshimiwa Spika, hii inaleta uhitaji mkubwa wa Bandari ya Mtwara kuwa kituo kingine kikuu cha kupokea mafuta yaliyosafishwa ili kuhudumia ukanda wa Kusini pamoja na nchi jirani kama Malawi, Zambia, Uganda na Kenya; kuwa na kituo kikubwa cha kushushia na kuhifadhi mafuta itasaidia pia kuwa rahisi kuhudumia nchi kama Shelisheli na Comoro pamoja na mikoa iliyoko pembezoni mwa bahari ya Hindi yaani Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara na nchi ya Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Spika hali ilivyo sasa, kituo cha kupakulia na kujaza mafuta kwenye malori kilichoko Kurasini kinazidiwa siku hadi siku, kwa hiyo, ni wakati muafaka wa kuwa na kituo kingine. Hii ina maana kwamba kufunguliwa kwa kituo hiki itasaidia mambo yafuatayo:-

Kutapunguza msongamano wa magari yanayokuja kuchukua mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam yapatayo malori 5,000 mpaka 6,000 kwa mwezi; utapunguza muda wa usafirishaji wa bidhaa hiyo na gharama za usafirishaji zitakuwa chini. Hii itachochea pia nchi za jirani kutumia zaidi bandari hii. Unafuu wa mafuta utawanufaisha wawekezaji wanaofanya utafiti wa uchimbaji wa gesi, wawekezaji kwenye viwanda kwa mfano vya saruji – Dangote, itapunguza msongamano wa malori ya mafuta ambao umezoeleka hivi sasa katika Jiji la Dar es Salaam na barabara kuu ya Morogoro, itachangia katika kuongeza fursa za ajira, kuchochea uchumi katika ukanda huu wa Kusini, itaokoa mamilioni ya shilingi ambayo Serikali inalazimika kupoteza kwa kusubiri kwa muda mrefu kupakua mafuta kwenye Bandari ya Dar es Salaam, kuimarisha usalama wa nchi, *National Security* na hili ni kubwa sana kwa kuwa kituo kikuu kikubwa cha pili cha kupakua mafuta ambacho kitasaidia kama kutakuwa na tatizo lolote lile kwenye Bandari ya Dar es Salaam, basi tuna bandari mbadala ya kupakua mafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulianzishwa na Serikali na Sheria namba 11 ya mwaka 2006 ambayo ilipewa jukumu kupeleka mawasiliano vijijini. Malengo ya Mfuko kama yalivyocainishwa na sheria ni kama ifuatavyo:-

Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu; kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali katika utoaji wa huduma ya mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mjini yenye mawasiliano hafifu, kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na

maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu; kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano, huduma rahisi zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika ushindani wa soko; kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha teknolojia, habari na mawasiliano yanapatikana vijijini na sehemu za mjini zenye mawasiliano hafifu na bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba Makampuni ya Simu yanavyofanya shughuli zake hapa nchini ndiyo wachangiaji wakubwa wa Mfuko kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Mfuko huo. Hivyo basi, kitendo cha kutokuchangia au Mfuko kushindwa kukusanya michango hiyo ni kosa kisheria. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa nini Mfuko umeshindwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 3.5 toka kwa Makampuni ya Simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pato la kawaida la mtumiaji, *(average per user)* linapungua kutoka dola 10 miaka 15 iliyopita hadi kufikia dola mbili. Hii pia imechangiwa na kodi kubwa zinazotowazwa na Serikali na kuzipunguzia kampuni za mawasiliano kuwekeza zaidi. Ikumbukwe kuwa Tanzania ni nchi ya pili baada ya nchi ya Gabon kutoza kodi nyingi kwa makampuni ya mawasiliano ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, athari hizi zimesababisha baadhi ya kampuni za simu kuachana kabisa na uwekezaji na kuendeleza minara ya mawasiliano. Wameuza minara kwa kampuni nyingine binafsi na wao kuzikodisha kutoka kwa kampuni hizo kwa lengo la kupunguza matumizi. Kwa kuwa kampuni hizi zinazouziwa minara zipo zaidi kibiashara, itakuwa vigumu kuwekeza kwenye sehemu kama vijijini ambazo hakukuwa na maslahi makubwa ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Makosa ya Mtandao Na.11 ya mwaka 2015 tarehe 1 Aprili, 2015. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipinga kupitishwa kwa sheria hiyo, kwani kulikuwa na vifungu ambavyo vilikuwa vinanyima uhuru wa utoaji na upokeaji wa taarifa kwa njia ya mtandao na baadhi ya Wabunge wake waliwasilisha majedwali ya marekebisho kwa ajili ya kufuta au kurekebisha vifungu kandamizi. Kwa wingi wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi walipinga marekebisho hayo, *Hansard* ya tarehe hiyo tajwa inaonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaendelea kuamini kuwa sheria hiyo ya makosa ya kimtandao kama haikufutwa, basi inatakiwa kufanyiwa marekebisho makubwa ili iweze kukidhi malengo yake badala ya kuwa kikwazo kwa utoaji na upatikanaji wa habari kwa njia za kimtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo kila dalili zinazoonesha kuwa sheria hiyo kandamizi ilitungwa kwa mashinikizo ya Chama Tawala kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kutokana na kasi ya vijana ambao wengi wao ndiyo watumiaji wa mitandao ya kijamii nchini ambao wengi walikuwa wakiunga mkono Upinzani.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kumalizika uchaguzi ushindani unaonesha kuwa sheria hii mbaya ilitungwa kwa makusudi ya kuwabana Watanzania ambao wako tayari kukosoa utendaji mbovu wa Serikali ya Awamu ya Tano ambapo viashiria vinaonesha unaleta utawala wa kiimla na wa kidikteta katika Taifa hili changa ambalo mpaka sasa halijafanikiwa kuwa ni Taifa la uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha MCC kuiondoa Tanzania kama mnufaika wa misaada yake, kinatokana na tamko la uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa MCC iliyotolewa tarehe 28 Machi, 2016 kuwa mojawapo ya sababu za Tanzania kuondolewa katika MCC ni uwepo wa Sheria ya Makosa ya Mitandao ambayo imetumika kama mojawapo ya njia za kuminya uhuru wa mawazo, ikiwemo kukamatwa kwa baadhi ya watu kwa makosa yanayohusiana na mitandao kipindi cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tamko hilo lilielekeza zaidi mazingaombwe ya marudio ya uchaguzi wa Zanzibar ya tarehe 20 Machi, 2016 na sheria kandamizi za makosa ya mitandao vinakinzana na azma ya uwepo wa demokrasia ya uchaguzi huru na wa haki. Hivyo MCC ikatangaza kuvunja utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa MCC kwa kushirikiana na Tanzania. Mojawapo ya sekta zilizokuwa zikipokea fedha za MCC ni Sekta ya Ujenzi wa Miundombinu baadhi ya miradi iliyokuwa inafadhiliwa na MCC kwa Sekta ya Ujenzi nchini Tanzania ni pamoja na mradi wa barabra Kilometa 67 kutoka Songea – Namtumbo ambayo sasa umeondolewa, Mtwara corridor, Tanga – Horohoro, Tunduma na Mafia Island Airport. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kusema hayo, naomba kuhitimisha kwa kusema kuwa, kinachofanywa sasa na Serikali ya Awamu ya Tano ya kukimbizana barabarani na kwenye vyombo vya habari na mfumo wa kifisadi, yaani kutumbua majipu, ni matokeo ya kulea mifumo mibovu miaka mingi iliyopita bila kuzingatia ushauri ambao tumekuwa tukiutoa katika Bunge hili. Ni vyema Serikali ya Awamu ya Tano ikaanza kuweka mifumo endelevu inayojali na kukuza utu wa mama Tanzania. Dhambi ya kutumikia mfumo ni dhambi ya mauti kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia, naomba kuwashukuru tena kwa kunisikiliza. Nina muda mrefu sikuwepo hapa Bungeni, nilikuwa Jimbo la Vunjo, kulikuwa na mafuriko lakini nawashukuru *Bonite Bottlers* kwa mchango mkubwa

walioutoa, nawashukuru Said Bakhresa kwa mchango mkubwa walioutoa na wananchi wote wa Vunjo bila kumsahau Baba Askofu Mkuu Dkt. Fredrick Shoo na Seminari ya Agape kwa kazi kubwa waliyofanya katika mafuriko hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
MHESHIMIWA JAMES FRANCIS MBATIA (MB) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA WA
2016/2017 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge,
Kanuni ya 99(9), toleo la mwaka 2016)*

1.0UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KRUB), kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii nitoe shukrani zangu za dhati kwa kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe(Mb) kwa kuiteua kuwa msemaji wa wizara hii. Aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa Willy Qambalo(Mb) Naibu Waziri Kivuli na mbunge wa Karatu kwa ushauri na maoni yake yaliyofanikisha kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa nawashukuru wapiga kura wa jimbo la Vunjo kwa kunichagua kwa asilimia 73 kuwa Mbunge wao, nawahakikishia utumishi wenye kuzingatia misingi ya kukuza utu wao na Taifa kwa ujumla. Kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kutoka moyoni kwa familia yangu, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa msaada wa hali na mali wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

2.0SEKTA YA UJENZI NCHINI

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) imekabidhiwa majukumu ya kutekeleza Mipango ya msingi ya ujenzi, matengenezo ya barabara, vivuko, nyumba na majengo ya serikali lakini kwa bahati mbaya, Serikali hii imeshindwa kutimiza ahadi zake ipasavyo na badala yake jamii ya Kitanzania sasa inashuhudia ongezeko la msongamano wa magari hususani katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya; Ucheleweshaji wa kumalizika miradi ya ujenzi pamoja na ongezeko

la gharama za miradi ambazo kwa kiasi kikubwa hutokana na uwepo wa masilahi binafsi ya wachache katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia tumeshuhudia barabara nyingi za vijijini hasa kipindi hiki hazipitiki kabisa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha au ujenzi wa barabara usiokidhi viwango. Ubovu wa barabara hizi unasababisha adha kubwa kwa watanania hasa waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu chake cha Binadamu na Maendeleo Ukurasa wa 29 aya ya pili, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anafafanua maana ya maendeleo.

“maendeleo maana yake ni maendeleo ya watu. Mabarabara, majumba, kuongeza mazao, na vitu vingine vya aina hii siyo maendeleo; ni vyombo vya maendeleo. Barabara mpya inampanulia mtu uhuru wake kama ataitumia kusafiri. Kuongeza idadi ya majengo ya shule ni maendeleo kama majengo hayo yanaweza kutumika, kuongeza ujuzi na elimu ya watu.

...Maendeleo yasiyokuwa maendeleo ya watu yanaweza yakawapendeza wataalamu wa historia wa mwaka 3000; lakini kwetu hayana maana kwani hayahusiani na maisha ya kesho tunayoyajenga.”

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imekuwa ikitaja kwa mbwembwe kilometa za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami, wakati ambao wananchi wengi wanakumbana na adha ya usafiri kutokana na ubovu wa barabara hizo. Kwa mfano; wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao kupeleka sokoni, kina mama kufariki njiani wakati wa kwenda kupata huduma za matibabu au kujifungua, kuongezeka kwa vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani n.k.

Mheshimiwa Spika, barabaraza lami zilizojengwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 kwa kiwango cha lami ni wastani wa asilimia 16 tu ya barabara zote nchini zenye urefu wa zaidi ya kilometa 35,000. Kwa kasi hii italigharimu Taifa zaidi ya miaka 62 ijayo kukamilisha ujenzi wa kilometa 29,432 ambao ni sawa na asilimia 84 ya barabara zote zilizosalia kujengwa kwa kiwango cha lami nchini bila kujumulisha barabara mpya zinazosanifiwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi ambaye kwa sasa ni Rais wa serikali ya awamu ya tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwasilisha hotuba yake katika bunge la 10, kuhusu mapato na matumizi ya wizara ya ujenzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, alikiri hapa bungeni kuwa Serikali ya CCM katika awamu ya nne ilishindwa kutekeleza ilani zao kikamilifu za uchaguzi za mwaka 2005 mpaka mwaka 2015, kwa kujenga barabara nchini

kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 5,568 sawa na asilimia 31 kwa lengo walilojiwekea la kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 17,762.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kunukuu sehemu ya hotuba hiyo;

“Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha serikali ya awamu ya nne, serikali imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 17,762 zimekuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 5,568 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 3,873 zimeendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 4,965 zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na serikali inatafuta fedha za kuzijenga kwa kiwango cha lami. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye jumla ya kilometa 3,356 unaendelea”

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali hii ya awamu ya tano, kutoa maelezo ya kina mbele ya bunge hili ina mipango gani ya uhakika na endelevu ya kukamilisha ujenzi wa barabara hizo kwa viwango vinavyokubalika kimataifa na kwa kuzingatia vipaumbele kwa misingi ya kitaalamu, badala ya ahadi nyingi zisizotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa bajeti ya wizara kwa mwaka 2016/17, Sekta ya Ujenzi fungu 98 imetengewa jumla ya **shilingi 2,176,204,557,000/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni ya kimkakati na isiyo ya kimkakati. Na kati ya fedha hizo **shilingi 1,831,365,922,000/-** ni fedha za ndani na zilizobaki ni kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa mwaka 2015/16;

“Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri kuacha mbwembwe nyingi bali aeleze kuwa madeni hayo ya Billioni zaidi ya 800 yanatoka kwenye barabara zipi? Yatalipwaje? Na riba ni kiasi gani?”

Mheshimiwa Spika, hata kwa mwaka huu wa fedha, bajeti ya maendeleo ni 890,572,000.00 kwa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara huku madeni yakiwa zaidi ya Bilioni 800. Hivyo hakuna uhalisia kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa na madeni husika”.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya ujenzi fungu **98** ni sawa na **asilimia 18.41** ya bajeti nzima ya maendeleo, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inamtaka Waziri atoe mchanganuo hapa bungeni kati ya fedha hizo ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kulipia madeni ya wakandarasi, kiasi gani ni kwa ajili ya kuanzisha miradi mipya na ni kiasi gani ni kwa ajili ya ukarabati wa barabara na madaraja?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeomba kupewa takwimu hizo, kwani taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa miradi ya kimkakati inahusu ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja na vivuko. Hii itasaidia bunge hili kutekeleza wajibu wake kikatiba wa kuisimamia serikali kwa niaba ya wananchi ambao ndiyo walipa kodi.

2.1 HASARA YA SHILINGI BILIONI 5.6 ILIYOSABABISHWA NA TANROADS

Mheshimiwa Spika, TANROADS imebainika kuwa na utendaji mbovu kama ambavyo Mdhifiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alivyobaini juu ya usimamizi mbovu katika mikataba ya ujenzi wa barabara na madaraja ambapo ilikuwa chini ya iliyokuwa wizara ya Ujenzi katika Serikali ya awamu ya nne.

Mheshimiwa Spika, TANROADS wakati wa kipindi hicho, iliitia hasara Serikali ya jumla ya **Shilingi 5,616,652,051** kutoka kwenye riba (interest) inayoongezeka kila siku kutokana na TANROADS kuchelewa kuwalipa wakandarasi 11 kati ya kipindi cha mwaka 2012 na mwaka 2015 kwa mujibu wa Ripoti ya CAG ya Hesabu za Serikali kuu akikagua taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 iliyotolewa mwezi Machi 2016 (Ukurasa wa 134 na 135).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajjuliza kama serikali ya awamu ya tano inafanya kazi yake kwa haki, uadilifu, uwazi na usawa kwa wote, na hasa kwa kile kinachojulikana kama utumbuaji majipu, swali hapa ni nani amfunge paka kengele? au mkuki mtamu kwa nguruwe mchungu kwa binadamu?

2.2 UBORESHAJI NA UTUNZAJI WA BARABARA NCHINI

'Super Single Tyre'

Mheshimiwa Spika, utafiti unaonesha matairi haya (super single tyres) yanaharibu barabara. Matairi haya yameanza kutumika takribani miaka mitano iliyopita na mzigo uliokuwa unabebwa na matairi 24 sasa unabebwa na matairi 12. Matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa barabara. Uamuzi wa kuruhusu matairi haya haukuwa na busara maana barabara zetu hazijabuniwa kuhimili shinikizo la uzito (excessive pressure) linalotokana na matairi haya. Serikali izuie mara moja matumizi ya matairi haya ili kuzinusuru barabara zetu lakini pia

kuokoa fedha za walipa kodi zinazotumika kurekebisha mara kwa mara barabara hizo na kunyima fursa maeneo mengine kupata barabara za kiwango cha lami.

2.3. WAKALA WA MAJENGO TANZANIA

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ulianzishwa mwezi Mei mwaka 2002 chini ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1997 ya Wakala za Serikali. Lengo la kuanzisha Wakala wa majengo ni kuwezesha kuwa na nyumba bora zaidi za kuishi watumishi wa Serikali wakiwa kazini na baada ya kustaafu kwa kujenga nyumba na kuwakopesha; kujenga majengo ya Serikali kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na kuyatunza; na pia kutoa huduma za ushauri wa kitalaam kuhusiana na majengo.

2.3.1 NYUMBA ZA SERIKALI ZILIZOUZWA

Mheshimiwa Spika, wakala huyu wa majengo ndiye mhusika mkuu katika kuhakikisha nyumba za Serikali zinakuwa katika hali nzuri kwa watumishi wa serikali kuishi. Katika muktadha huo kambi Rasmi ya Upinzani inalikumbusha Bunge kwamba, kati ya mwaka 2002 mpaka 2004 Serikali iliiza nyumba zipatazo 7,921 na mpaka mwaka 2008 Serikali ilikuwa imejenga nyumba 650 tu.

Mheshimiwa Spika, katika biashara hiyo kwa kuuza zilizokuwa mali ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilipata **Sh. 252,603,000/-** sasa inahitaji kusaka nyumba zaidi ya mara dufu ya kiasi hicho kujenga nyumba za fidia. Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge juu ya uuzaji wa nyumba za serikali kinyume cha taratibu, serikali itatumia **Sh. 677,606,000/-** kujenga nyumba mpya ili zirejeshwe kwa Tamisemi, Rejea taarifa ya Serikali Bungeni tarehe 25 April 2008.

Mheshimiwa Spika, Kwa vile hata wale waliouziwa nyumba hizo, kuna taarifa kati yao wapo walioziua nakujipatia faida kubwa kinyume na mikataba ya mauzo hayo, KRUB inapendekeza wanyang'anywe nyumba hizo kwa kukiuka mikataba na malengo ya mauzo.

Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu za taarifa rasmi za Bunge zinaonesha kwamba Serikali ilitoa taarifa ndani ya Bunge hili kuwa, kuna Kamati iliundwa kuchunguza mchakato wa mauzo ya Nyumba ya Serikali na Kamati hiyo ilitegemewa kumaliza kazi mwezi Februari, 2007, lakini hadi Bunge la tisa na Bunge la Kumi linamaliza uhai wake hakuna taarifa iliyotolewa na Serikali. KRUB, inaitaka serikali ya awamu ya tano irejeshe nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hansard ya Tarehe 25 Aprili, 2008 MKUTANO WA KUMI NA MOJA Kikao cha Kumi na Nne Bunge kwa kauli moja baada ya

mjadala mkubwa wa hoja binafsi iliyowasilishwa na aliyekuwa Mbunge wa Vunjo Mhe. ALOYCE BENT KIMARO iliyohusu Serikali Kurejesha nyumba zake zilizouzwa kienyeji na hivyo kuisababishia Serikali hasara kubwa na Hoja hiyo ikaungwa mkono na Bunge likapitisha azimio, naomba kunukuu azimio hilo;

“KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye yafuatayo:

Itekeleze mara moja bila kusita, Agizo la Rais kurejesha nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu na kwa watu ambao hawakuwa Watumishi wa Serikali wakati huo na vilevile nyumba ambazo hazikupaswa kuuzwa kama zile zilizopo kwenye maeneo ya Utawala wa Serikali; Irejeshe kwenye umiliki wake nyumba hizo zilizouzwa kinyume na utaratibu;

Itoe orodha ya nyumba zake ambazo ziliuzwa kwa watu ambao sio Watumishi wa Serikali kinyume na utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za Watumishi wa Serikali wanaostahili kutumia; na ichukue hatua kwa wale ambao hawajalipia na mikataba yao ya kuuziwa nyumba irejewe hakikisha kuwa malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao kufutwa na nyumba kurejeshwa kwenye miliki ya Serikali”.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutekeleza azimio hilo la Bunge, na kwa njia hiyo ile kauli mbiu ya hapa kazi tu, iweze kutafsiriwa kwa vitendo. Tunajua uuzwaji huo ulisimamiwa na Wizara aliyokuwa akiiongoza yeye na kuna uwezekano mkubwa kwamba alisimamia maamuzi ambayo hakuwa na uwezo wa kuyakiuka. Sasa ni muda sahihi Mhe Rais Magufuli kurekebisha kasoro alizozisimamia na katika mchakato huo ili kurejesha imani katika jamii. Tukumbuke kuwa Rais Kikwete alielekeza nyumba hizo zirudishwe Serikalini lakini alikosa uthubutu wa kusimamia kauli yake.

2.0SEKTA YA UCHUKUZI

3.1 UPANUZI WA UWANJA WA NDEGE WA JULIUS NYERERE (TERMINAL THREE)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Bunge lako tukufu lilipitisha bajeti ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere. Upanuzi huo wa kituo cha tatu (Terminal three) unahusishwa na harufu kubwa ya ufasadi.

Mheshimiwa Spika, kuna tuhuma kwamba mtu ambaye alikuwa ni dalali katika mchakato mzima wa Tanzania kupatiwa mkopo wa ujenzi wa uwanja huo, ulihibitwa na mazingira tatanishi, ambapo dalali alifanikiwa kupata asilimia 30 ya mkopo huo kama Kamisheni yake inayofikia takribani dola za Kimarekani milioni 100 zaidi ya shilingi bilioni 200 za Tanzania , hivyo basi, Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa undani na kuleta taarifa hapa Bungeni, au kwenye kamati husika ya Bunge.

3.2. UFISADI KATIKA VIVUKO NA MADARAJA NCHINI

3.2.1. Ununuzi wa Kivuko Kibovu cha Dar es Salaam –Bagamoyo

Mheshimiwa Spika, Kivuko kutoka Dar es Salaam kwenda Bagamoyo ni jipu ambalo limeiva kwa viwango vyote na sasa linatakiwa litumbuliwe mara moja. Ni dhahiri kuwa Kivuko cha Dar es Salaam kwenda Bagamoyo kilichonunuliwa na TEMESA chini ya uongozi wa waziri wa Ujenzi wa serikali ya awamu ya nne ambaye ndiye Rais wa Tanzania wa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika Hesabu za Serikali kuu akikagua Taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 iliyotolewa mwezi Machi 2016 (Ukurasa wa 132 na 133), alibaini ununuzi wa boti feki na mbovu uliofanywa na TEMESA na kugharimu Dola za Marekani 4,980,000 sawa na shilingi **7,916,955,000** kupitia mkataba namba AE/006/2012-13/HQ/G/CN-39 uliosainiwa tarehe 25 April 2013 kati ya TEMESA kwa niaba ya Serikali na Mzabuni M/s Johs.Gram-Hanssen Bergensgade.

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini masuala makuu mawili kuhusu ununuzi huo wa kivuko feki na kibovu cha Dar es Salaam – Bagamoyo. Jambo la kwanza CAG alibaini kasi ya kivuko hicho ni tofauti na kasi iliyotakiwa kuwepo, jambo la pili ni kuwa cheti cha kukikubali kivuko hicho kilikuwa hakijatolewa kinyume na Kanuni ya 247 ya Manunuzi ya Umma. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, tabibu wa kutumbua jipu hili yuko wapi? Au msemu usemao kuwa “*mganga hajjgangi*” unatumika hapa?

3.3 HALI YA RELI NCHINI

3.3.1. Kuimarisha Reli ya Kati na matawi yake

Mheshimiwa Spika, reli ya kati ya Tanzania ikiboreshwa, ina nafasi ya pekee ya kutawala soko la usafirishaji wa abiria na mizigo ya ndani na kwa nchi jirani kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo - DRC, Burundi ,Rwanda na Uganda na kuongeza pia mapato ya Bandari ya Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji mtazamo mpya wa kisasa na wa upeo wa miaka 50 ijayo. Tunahitaji reli ambayo itaendana na mazingira tuliyonayo ya ukubwa wa nchi na fursa tuliyonayo ya nchi zilizotuzunguka zinazotegemea bandari zetu. Swala kubwa la kuzingatia ni mwendo kasi na uwezo wa kubeba uzito

mkubwa. Na ndio maana hoja ya kwanini Tanzania inahitaji reli ya kisasa 'standard gauge' sasa na siyo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuna mtazamo kuwa na reli ya kisasa tunahitaji chuma cha reli chenye uzito wa pound 90 hadi 100 au zaidi kwa matarajio ya miaka 50 ijayo. Tukumbuke kwamba uwekezaji wa reli ni uwekezaji mkubwa na hivyo unatakiwa ulenge muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tunashauri reli ijengwe kwa mtazamo wa mbali wa zaidi ya miaka 50 ijayo, tuanze na reli moja sambamba na hii iliyopo, lakini mpango uwe kuwa na zaidi ya reli moja hapo baadaye ili kuwezesha usafirishaji katikati ya Tanzania na nchi jirani kuwa wa muda mfupi zaidi, ili kuzivuta nchi jirani kuona reli yetu ndiyo ya pekee ya kuwafikishia mizigo yao kwa muda mfupi na kwa usalama zaidi, ikiwepo sababu za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa 'Standard Gauge' uende sambamba na kuimarisha mawasiliano katika kuendesha shughuli za reli ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwetu kujenga reli mpya sasa italigharimu taifa hili na vizazi vijavyo; Kwanza. itafanya tushindwe kufaidika na bandari zetu ipasavyo, hata tukija kuamua kujenga baadaye gharama zitakuwa kubwa mno kuliko hivi sasa, na si ajabu ikawa ngumu kupata wawekezaji, na hata kama tutafanikiwa bado tutakuwa na kazi ya kuwapata wateja ambao watakuwa wameshazoea kupitisha mizigo yao sehemu nyingine. Wakati wa kufanya uamuzi ni sasa na gharama ya kushindwa kufanya uamuzi sasa ni kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, ili kufupisha muda wa ujenzi, kuwe na wakandarasi ambao watapewa vipande vidogo vya takribani kilomita 200 ambavyo vitajengwa kwa wakati mmoja ili kuwezesha reli hii ikamilike kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa thamani ya dola na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia duniani kunasababisha pia gharama za ujenzi wa reli kupanda, kadri taifa linavyochelea kufanya maamuzi ya ujenzi wa reli ya kisasa basi hata gharama zitakuwa kubwa mno kuliko hivi sasa, na si ajabu ikawa ngumu kupata wawekezaji wenye unafuu, na hata kama tutafanikiwa bado tutakuwa na kazi kubwa ya kuweza kukabiliana na ushindani hasa kwa nchi jirani ambazo nazo zimeanza na nyingine zinakaribia kukamilisha ujenzi wa reli za kisasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri tufanye maamuzi sasa kwa masilahi endelevu ya mama Tanzania.

3.3.2. Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

Mheshimiwa Spika, Reli ya Tazara iliyojengwa miaka ya 1970 ikitokea Dar es Salaam hadi New Kapirimposhi Zambia, uwezo wake wa kusafirisha mizigo na abiria umeshuka sana kutokana na sababu kama zile zile za Reli ya Kati.

Mheshimiwa Spika, Reli hiyo yenye uwezo wa kubeba tani milioni tano kwa mwaka, hivi sasa inaweza kubeba tani 100,000 tu kwa mwaka, sababu kubwa ni uchakavu wa miundombinu kama vile njia ya reli, injini na mabehewa.

Mheshimiwa Spika, ili TAZARA iweze kujiendesha kibiashara inatakiwa isafirishe zaidi ya tani 600,000 za mizigo kwa mwaka (break even point), hata hivyo Tazara kwa muda mrefu imekuwa ikisafirisha mizigo chini ya tani 100,000 za mizigo kwa mwaka kutokana na changamoto kadhaa;

- i. Ucheleweshaji wa mizigo bandarini
- ii. Miundombinu chakavu
- iii. Muda mrefu wa usafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri TAZARA haitaweza kujiendesha kwa faida kama mabadiliko makubwa ya kiutawala hayatafanyika. Ni aibu na fedheha kwa Serikali kulipa mishahara ya watumishi wa shirika ambalo lilikuwa na uwezo mkubwa. Tazara ina uongozi usiozingatia utawala bora, uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, miaka michache iliyopita wafanyakazi wa Tazara waliibua tuhuma nzito dhidi ya Mameneja waandamizi saba (7) ndani ya Tazara. Aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Omar Nundu aliwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi. Katika Mazingira yenye utata Mheshimiwa Harson Mwakyembe alipokabidhiwa wizara hiyo aliwarudisha kazini watendaji hao akidai kuwachukulia hatua za kisheria lakini hadi leo hatua hizo hazijawahi kuchukuliwa, watendaji wako kazini na shirika linaendelea kuporomoka. KRUB, inajiuliza ni kwa nini kunakuwa na hali ya kutunishiana misuli baina ya Mawaziri? Kwani jambo kama hilo pia lilitokea kwenye Bodi ya Mamlaka ya Bandari, Mhe Harrison Mwakyembe aliivunja bodi aliyoikuta na kuteua mpya, Mhe. Samuel Sitta alipoingia akaivunja hiyo bodi na kuteua mpya. Kuna nini hapa ambacho ni siri ya Mawaziri?

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali ina nia ya dhati ya kupiga vita ubadhirifu inakuwaje watu waliotuhumiwa kwa kuchota kiasi kikubwa cha fedha wanalindwa na wale wanaotakiwa kuwachukulia hatua. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri aliangalie vizuri suala hili la uongozi wa Tazara.

3.4 HALI YA BANDARI NCHINI

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaamini kuwa ili kuongeza ufanisi wa bandari zetu ni lazima kuimarisha miundombinu ya reli na barabara zinazozunguka bandari ili kuondoa mizigo inayosongamana bandarini kwa haraka na ufanisi. Aidha, Mamlaka ya Bandari (TPA) na Mamlaka ya Mapato (TRA) zinatakiwa kuwekeza kikamilifu kwenye mifumo ya kieletroniki, ili kupunguza muda wa usafiirshaji wa mizigo na hasa ile ya nchi jirani (Transit goods), ambao hivi sasa ni mkubwa kutokana na mizani na vituo vingi vya ukaguzi vilivyopo barabarani. Kupunguza muda wa usafirishaji, kutavutia watu wengi zaidi kutumia bandari za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa na kituo kimoja cha ukusanyaji wa mapato (Single point tax collection) cheye ufanisi na utadalamu unaokubalika kimataifa ili kupunguza ucheleweshwaji na usumbufu wa kuondoa mizigo kutoka bandarini na kurahisisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya kazi kwa saa 24 kwa siku kwa mamlaka zote zinazohusika.

3.4.1 BANDARI KAVU YA SOGA

Mheshimiwa Spika, kuna mwekezaji aliyeshafanya mawasiliano na Serikali kutumia eneo la Soga kujenga bandari kavu. Eneo hilo lipo katikati ya Reli ya Tazara na Reli inayosimamiwa na Mamlaka ya reli (RAHCO) na hivyo ingekuwa rahisi kuchukua mizigo kutoka bandarini kupitia reli ya Tazara na Reli ya Kati. Hii ingefanya mizigo yote ya ndani na nje (transit goods) iwe inachukuliwa eneo hili la Soga na hivyo kuondoa msongamano wa malori ya mizigo jijini Dar es Salaam na bandarini. Aidha, Tazara na TRL zote zingenufaika na mpango huu, ikiwa ni pamoja na TRA kuweza kukusanya kodi zake kwa ufanisi (single point of tax collection) pamoja na kupunguza uzito kandamizi katika barabara za mijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida zote hizi, bado Serikali inaonekana kuwa na kigugumizi na kusitasita kana kwamba muda unatusubiri. Serikali ifanye maamuzi ya haraka kwa vitu ambavyo vina manufaa kwa nchi. Subiri subiri hii itakuja kuigharimu Serikali, kama ambavyo imekuwa kwa miradi mingi ambayo Serikali ilichukua muda kufanyia maamuzi.

3.4.2 BANDARI YA DAR ES SALAAM

Uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam dhidi ya Bandari shindani kwa mfano Bandari ya Mombasa iliyoko nchin Kenya

Bandari ya Dar Es Salaam	Bandari ya Mombasa
-----------------------------	-----------------------

Tani kwa Mwaka	Milioni 13	Milioni 22
Ujazo wa Kontena kwa Mwaka	600,000	800,000
Gati (Birth) zilizopo	11	19

Chanzo: www.tanzaniaports.com; [https://en.wikipedia.org/wiki/port of Dar es Salaam](https://en.wikipedia.org/wiki/Port_of_Dar_es_Salaam); www.kpa.co.ke

3.4.3 BANDARI YA TANGA

Mheshimiwa Spika, kupitia fursa ya bomba la mafuta la nchi ya Uganda kupitia bandari ya Tanga, ni wakati sasa Serikali iwekeze katika bandari hii na ifungue ukanda wa kiuchumi wa kaskazini. Bandari hii inaweza kutumika zaidi kwa ajili ya mizigo iendayo Uganda, Kenya, Kongo, Burundi, Rwanda na Sudan ya Kusini.

3.4.4 BANDARI YA MTWARA NA MTWARA CORRIDOR

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya ukanda huu wa kusini mwa Tanzania ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji kwa kuwa ukanda huu utafungua fursa nyingi sana za kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo.

Bandari ya Mtwara kama Kituo Mbadala cha Kupakulia na Kupakia Mafuta.

Mheshimiwa Spika, shehena ya mafuta yaliyosafishwa hadi hivi sasa yanafikia tani 3.6 milioni kwa mwaka. Ukizingatia kasi ya ukuaji wa uchumi wetu mahitaji ya mafuta yatazidi tani million 6 kwa mwaka kwa kipindi kisichozidi miaka 10 ijayo. Hii inaleta uhitaji mkubwa kwa bandari ya Mtwara kuwa kituo kingine kikuu cha kupokea mafuta yaliyosafishwa ili kuhudumia ukanda wa Kusini pamoja na nchi jirani kama Malawi, Zambia, Msumbiji na Kongo. Kuwa na kituo kikubwa cha kushusha na kuhifadhi mafuta, itasaidia pia kuwa rahisi kuhudumia nchi kama Shelisheli na Komoro pamoja na mikoa iliyopo pembezoni mwa bahari ya Hindi kama vile Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara na nchi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa kituo cha kupakulia na kujaza mafuta kwenye malori kilichopo Kurasini (Kurasini Oil Jet – KOJ), kinazidiwa siku hadi siku, kwahiyo ni wakati muafaka wa kuwa na kituo kingine. Hii ina maana kuwa kufunguliwa kwa kituo hiki kitasaidia mambo yafuatayo;

- Kutapunguza msongamano wa magari yanayokuja kuchukua mafuta bandari ya Dar es salaam, zaidi ya malori 5,000 hadi 6,000 kwa mwezi.

- Kutapunguza muda wa usafirishaji wa bidhaa hiyo, kwasababu hivi sasa inachukua takribani siku 4 kwa lori moja kuweza kujaziwa mafuta kutoka Kurasini - KOJ kwa sababu ya msongamano na foleni ya kupakia.
- Gharama za usafirishaji zitakuwa chini kwa sababu ya umbali ambao unakatwa kwa kuwa na kituo kikuu cha mafuta katika bandari ya Mtwara na hivyo kusababisha bidhaa hii kupatikana katika mikoa ya kusini kwa bei sawa na Dar es salaam, kwa wastani wa shilingi 400 chini ya kiwango wanachonunulia mafuta hivi sasa. Hii itasababisha mikoa ya kusini kuokoa takribani shilingi billioni 1.2 kwa mwezi.
- Hii itachochea pia nchi za jirani kuitumia zaidi bandari hii, katika kuagiza na kuhifadhi bidhaa hii kutokana na unafuu utakaokuwa unapatikana.
- Unafuu wa mafuta utanufaisha uwekezaji kwa mfano viwanda vya sementi unaofanywa kwenye ukanda huo. Bidhaa kama sementi inayozalishwa na kiwanda cha Dangote itakuwa bei nafuu , kama bidhaa za mafuta ya petroli zitachukuliwa moja kwa moja kutoka Mtwara badala ya Dar es Salaam.
- Itawanufaisha pia wawekezaji wanaofanya utafiti na uchimbaji wa gesi katika ukanda huo.
- Itapunguza msongamano wa malori ya mafuta ambao umezoeleka hivi sasa jijini Dar es Salaam na barabara kuu ya Mororogoro.
- Itachangia katika kuongeza fursa za ajira na kuchochea uchumi katika ukanda huu wa kusini.
- Itaokoa mamilioni ya shilingi ambayo Serikali inalazimika kupoteza kutokana na Meli kusubiri kwa muda mrefu kupakua mafuta kwenye SBM1 (Sub Marine Point 1).
- Kuimarisha usalama wa nchi (National Security) kwa Kuwa na kituo kikuu kikubwa cha pili cha kupakulia mafuta, ambacho kitasaidia kama kutakuwa na tatizo lolote lile kwenye kituo cha Dar es salaam (KOJ au SBM1), nikiyaja tu faida zake kwa uchache.

3.0SEKTA YA MAWASILIANO

4.1. KAMPUNI YA SIMU YA TAIFA-TTCL

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu na kukua kwa sekta ya mawasiliano nchini bado ni ajabu leo hii Kampuni ya Simu ya Taifa letu (TTCL) ni sawa na kichwa cha mwendawazimu. Katika maoni yetu mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilitoa hoja nyingi zilizohitaji majibu kuhusiana na utendaji na

hujuma zinazofanywa ili kuikwamisha Kampuni ya Simu ya Taifa kuendelea kutekeleza majukumu yake na kukabiliana na soko la ushindani katika utoaji wa huduma za mawasiliano nchini na barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2015/16 sehemu ya hotuba alitoa maoni yafuatayo;

"Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania TTCL ilianzishwa kwa mujibu wa sheria Na.20/1993 na kusajiliwa kwa Hati Na. 24490 kuwa ni Kampuni ya Umma (Parastatal Organization) mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23/2/2001, Serikali ilikodisha hisa za Kampuni ya Simu Tanzania TTCL kwa Kampuni ya Mobile System International (MSI) ya Netherlands. Hisa zilizokodishwa ni 35% kwa kulipiwa shilingi bilioni 111 sawa na Dolar za Marekani Milioni Sitini (\$ 60milioni) kwa wakati huu, malipo hayo ni sawa na hisa 17.5%; lakini serikali ikawapa MSI kuongoza Kampuni. Vile vile MSI hawakulipa pesa yote kwa mujibu wa Mkataba, lakini walipewa umiliki wa ukodishaji wa hisa 35% za hisa za TTCL.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Msingi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Waziri alieleze Bunge na Watanzania wote ni kwa vipi HISA zinaweza kukodishwa? Hili la Tanzania kukodisha hisa kwa anayelitwa mwekezaji ni maajabu katika tasnia nzima ya uchumi na uhasibu".

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 26.05.2015 wakati wa kuhitimisha hoja yake aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, wakati wa Bunge kukaa kama kamati ya matumizi alishindwa kujibu hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhusu Serikali kununua hisa zake asilimia 35 kwa thamani ya shilingi bilioni 14.9.

Mheshimiwa Spika, Bunge kwa kusikiliza na kutathmini hoja zilizotolewa, aliyekua Spika wa Bunge la 10 Mheshimiwa Anne Makinda (Mb) aliunda kamati ndogo ya Bunge ikiongozwa na Mheshimiwa Zarina Madabida kufanya kazi ya kiuchunguzi kuhusiana na hujuma zinazofanyika kwenye Kampuni hiyo ya simu. Taarifa hii inapatikana kwenye HANSARD ya tarehe tajwa hapo juu. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua iwapo taarifa ya Kamati hiyo ndogo ya iliyokuwa kamati ya Miundombinu iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Spika? Ikiwa taarifa hiyo haikuwasilishwa mpaka Bunge la 10 linafikia ukomo wake basi ipo haja sasa ya Bunge hili kuchunguza kwa umakini matatizo ya mikataba iliyoingjiwa na Serikali kwa niaba ya TTCL na makampuni binafsi juu ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge hili kuunda kamati maalum sambamba na kuangalia utendaji na mikataba ya TTCL na makampuni mengine ya simu pamoja na ushiriki wa TTCL kwenye mkongo wa Taifa, umiliki wa mkongo huo na mkataba wa TTCL na kampuni ya SEACOM katika uendeshaji au utoaji wa huduma kwa wateja.

4.2 MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE-UCSAF

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya mwaka 2006 ambayo ilipewa jukumu kuu la kupeleka mawasiliano vijijini.

Malengo ya Mfuko kama yalivyoainishwa na sheria ni kama ifuatavyo:-

1. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;
2. Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;
3. Kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;
4. Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;
5. Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa teknolojia ya habari na mawasiliano inapatikana vijijini na sehemu za mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu; na
6. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za wote kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utoaji wa huduma za mawasiliano vijijini ni pamoja na ukosefu wa umeme wenye uhakika katika maeneo ya vijijini. Hivyo basi wakala huyu anashirikiana vipi na wakala wa Umeme vijijini (REA) katika kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika unapatikana kwa wakati na hivyo lengo lake la uwepo wa mawasiliano rahisi na ya uhakika linafikiwa?

Mheshimiwa Spika, kinyume cha hapo ni dhahiri kwamba fedha za Mfuko wa Mawasiliano (UCSAF) zitazinufaisha zaidi kampuni za simu binafsi wakati lengo lake la msingi litashindwa kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba makampuni ya simu yanayofanya shughuli zake hapa nchini ndio wachangiaji wakubwa wa mfuko kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha mfuko huo, hivyo basi kitendo cha kutokuchangia au Mfuko kushindwa kukusanya michango hiyo ni kosa kisheria. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwani Mfuko umeshindwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 3.5 toka kwa makampuni ya simu?

4.3. HALI YA HUDUMA ZA MAWASILIANO YA SIMU NCHINI

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa mawasiliano ya huduma ya simu yamezalisha takribani shilingi trillion 2 kwa mwaka 2015 peke yake. Kwa kiasi kikubwa mawasiliano ya simu yamekuwa yanaendeshwa na makampuni binafsi nchini.

Pamoja na sekta hii ya mawasiliano hasa ya simu kuchangia kwa mapato makubwa, juhudi za serikali kuhakikisha mawasiliano ya simu za mikononi yanapatikana mpaka vijijini zimekuwa ndogo sana. Aidha, makampuni binafsi na serikali zimeshindwa kuwekeza kwenye minara na hivyo kusababisha mawasiliano kuwa ya shida au hamna kabisa katika baadhi ya maeneo nchini hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu za mikononi yanahitaji uwekezaji mkubwa katika minara. Tanzania yenye eneo la mraba la kilometa za mraba 945,087 ni kubwa kwa makampuni binafsi pekee kuweza kuweka minara. Ni dhahiri kuwa kampuni hizi hujenga minara katika maeneo ambayo yana faida kwao kibiashara na kuacha maeneo mengine yasiyo ya kifaida kwao bila ya minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pato la kawaida la mtumiaji yaani 'average revenue per user' [ARPU] limepungua kutoka dola 10 miaka 15 iliyopita hadi kufikia dola 2, hii pia imechangiwa na kodi kubwa zinazotozwa na Serikali na kuzipunguzia kampuni za mawasiliano kuwekeza zaidi. Ikumbukwe kuwa Tanzania ni nchi ya pili baada ya nchi ya Gabon kutoza kodi nyingi kwa makampuni ya mawasiliano ya simu za mikononi.

Mheshimiwa Spika, athari hizi zimesababisha baadhii ya kampuni za simu kuachana kabisa na kuwekeza na kuendeleza minara ya mawasiliano. Wameuza minara kwa kampuni nyingine binafsi na wao kuzikodi kutoka kampuni hizo, kwa lengo la kupunguza matumizi. Na kwa kuwa kampuni hizi zinazouziwa minara zipo zaidi kibiashara, itakuwa vigumu kuwekeza kwenye sehemu kama vijijini ambazo hakuna masilahi makubwa ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa iwapo TTCL itanunua, kuwekeza na kuendesha minara ya mawasiliano na kuikukodisha kwa

kampuni za simu kama Tigo, Vodacom, Airtel, Zantel, Smile nk. Badala ya kuacha kampuni nyingine za binafsi kufanya shughuli hiyo TTCL itaongeza tija na kuweza kujiendesha bila hasara.

Aidha, iwapo Serikali itawekeza vya kutosha katika minara ya mawasiliano, itarahisisha mipango ya kuanzisha na kusambaza mawasiliano hata katika maeneo ambayo yanaonekana kwa sasa, hayana mvuto wa kibiashara. Kwa kufanya biashara hii ya minara kutakuwa hamna tofauti na kama TTCL inavyofanya sasa, kununua njia za mawasiliano ya 'internet' na kuziua kwa makampuni ya ndani, au kama ambavyo walivyojenga mkongo wa mawasiliano (fibre optic), karibia kila wilaya ya nchi hii na kukodisha mkongo huo kwa makampuni mengine ya simu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Serikali ya Rwanda imejenga minara maeneo ya vijijiini na kuikodisha hiyo minara kwa kampuni za simu. Uwekezaji huu ni wa faida kubwa kwa nchi, kwa sababu itasaidia kuwa kichocheo kwa kampuni za simu kueneza wigo wao kufikia kila mwananchi na kuongeza ushindani wa kuboresha ubora wa mawasiliano. Tanzania ina kila nafasi na uwezo wa kuweza kuboresha sekta ya mawasiliano ya simu na kuyasambaza kwa wananchi wake kwa gharama nafuu zaidi.

4.4. SHERIA YA MAKOSA YA MTANDAO NAMBA 14 YA MWAKA 2015

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kwamba wakati Bunge la Jamhuri ya Muungano linapitisha sheria hiyo tarehe 1.4.2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipinga kupitishwa kwa sheria hiyo kwani kulikuwa na vifungu ambavyo vilikuwa vinaminyu uhuru wa utoaji na upokeaji wa taarifa kwa njia ya mtandao na baadhi ya wabunge wake waliwasilisha majedwali ya marekebisho kwa ajili ya kufuta au kurekebisha vifungu kandamizi, lakini kwa wingi wa wabunge wa CCM walipinga marekebisho hayo. Hansard ya terehe tajwa inaonesha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaendelea kuamini kuwa sheria hiyo ya makosa ya kimtandao kama hakiufutwa basi inatakiwa kufanyiwa marekebisho makubwa ili iweze kukidhi malengo yake badala ya kuwa kikwazo kwa utoaji na upataji wa habari kwa njia za kimtandao.

Mheshimiwa Spika, zipo kila dalili zinazoonesha kuwa Sheria hiyo kandamizi ilitungwa kwa mashinikizo ya Chama tawala kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 kutokana na kasi ya vijana ambao wengi ndio watumiaji wa mitandao ya kijamii nchini ambao wengi walikuwa wakiunga mkono upinzani. Mara baada ya kumalizika uchaguzi mkuu, ushahidi unaonesha kuwa Sheria hii mbaya ilitungwa kwa makusudi ya kuwabana watanzania ambao wapo tayari kukosoa utendaji mbovu wa awamu ya tano na kuleta utawala wa kiimla na kidikteta

katika taifa hili changa ambalo mpaka sasa halijafanikiwa kuwa taifa la uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha MCC kuiondoa Tanzania kama mnufaika wa misaada yake kinatokana na tamko la uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya MCC iliyotolewa tarehe 28 Machi 2016 kuwa mojawapo ya sababu za Tanzania kuondolewa katika MCC ni uwepo wa Sheria ya Makosa ya Mitandao ambayo imetumika kama mojawapo ya njia za kuminya uhuru wa mawazo, ikiwemo kukamatwa kwa baadhi ya watu kwa makosa yanayohusiana na mitandao kipindi cha uchaguzi. Zaidi, tamko hilo lilieleza kuwa mazingaombwe na marudio ya uchaguzi wa Zanzibar tarehe 20 Machi 2016 na Sheria kandamizi ya Makosa ya Mitandao vinakinzana na azma ya uwepo wa demokrasia na uchaguzi huru na wa haki. Hivyo MCC ikatangaza kuvunja utekelezaji wa mpango wa pili wa maendeleo wa MCC kwa kushirikiana na Tanzania. Mojawapo wa sekta zilizokua zikipokea fedha za MCC ni sekta ya ujenzi wa miundombinu. Baadhi ya miradi iliyokuwa inafadhiliwa na MCC kwa Sekta ya Ujenzi nchini Tanzania ni pamoja na;

- Mradi wa Barabara, Kilometa 67 kutoka Songea – Namtumbo
- Mtwara Corridor
- Tanga – Horohoro
- Tunduma
- Mafia Island airport

5. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuhitimisha kwa kusema kuwa kinachofanywa sasa na serikali ya awamu ya tano ya kukimbizana barabarani na kwenye vyombo vya habari na mfumo wa kifisadi (kutumbua majipu), ni matokeo ya kulea mifumo mibovu miaka mingi iliyopita bila kuzingatia ushauri ambao tumekuwa tukiutoa katika Bunge hili. Ni vema Serikali ya awamu ya tano ikaanza kuweka mifumo endelevu inayojali na kukuza utu wa mama Tanzania. Dhambi ya kutumikia mfumo ni mauti kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

James Francis Mbatia (Mb),

Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani –Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

17 Mei 2016

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

Sasa kuna baadhi ya wageni tulipokuwa tunatangaza walikuwa bado wako nje ikiwa ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mbunge wa Jimbo la Mlimba ambao ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji, Ndugu Lenifrid Magundula; naomba usimame hapo ulipo. Ahsante, karibu sana, lakini pia Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkangawalo Ndugu Gundram Ligonja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea na uchangiaji, nimepata wachangiaji orodha ya CCM, upande huu bado kimya sina wachangiaji wao, natumaini iko njiani inakuja. Kwa hiyo, tunaanza kidogo kidogo. Msiwe na wasiwasi watani zangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Raphael Chegeni kama yupo angekuwa mchangiaji wa kwanza. Katika orodha hii ukikaa kaa nje huko ukikosekana ndiyo basi tena, umeliwa! *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na wanaofuata nitawataja muda siyo mrefu.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia sekta hii muhimu sana ya uchukuzi, barabara, reli na kadhalika. Kwanza niwape hongera sana timu ya Profesa na mwenzake kwa kazi mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze katika mambo matatu. Suala la kwanza ni suala la kisera. Tumeshakubaliana na kwa mujibu wa Sera za Chama cha Mapinduzi kwamba tutajenga barabara za lami kuunganisha mkoa na mkoa, ndivyo tulivyokubaliana. Nilikuwa najaribu kuangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hiyo sera hamuizingatii. Mnaanza kuhamisha rasilimali na resources kuhangaika na barabara za Kata kwenda Kata na Wilaya kwenda Wilaya. Kwa nini tusianze kujenga barabara za kuunganisha mikoa kwa mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sisi Mkoa wa Kigoma, nashukuru nimeona kuna juhudi inafanyika kwa barabara yetu ya Tabora – Kigoma kwamba kuna vipande vipande bado vinafanyiwa kazi na nimeona kuna mweleko mzuri. *Hopefully flow* ya fedha itakwenda vizuri ili barabara ile ikamilike; lakini bado sisi hatujaunganishwa na Tabora, hatujaunganishwa na Katavi, haijaunganishwa na Kagera, haijaunganishwa na Mwanza, haijaunganishwa na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha anieleze, kwa nini wanatapanya resources wakati tumeshakubaliana kwamba mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano iunganishwe kwanza kabla ya maeneo mengine? Hilo ni jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nizungumzie suala la uwiano. Jamani hii nchi ni yetu wote. Hakuna wa Tanzania bora kuliko Watanzania wengine, Watanzania wote ni sawasawa. Ukiangalia mtandao wa barabara za TANROADS na unaweza ukaenda tu ukapata picha ukurasa 279, ukiangalia zile barabara za changarawe kwa mfano, inakupa picha ya moja kwa moja kwamba kuna mikoa ambayo ina mtandao mkubwa kuliko mikoa mingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ni mpya katika awamu hii na bahati nzuri Jimbo lake ni Ikulu, hana Jimbo la uchaguzi, naomba waanze kwenda na utaratibu kuwe na uwiano, ikibidi wa-employ concept ya *slow match* na *quick match*. Wale waliotangulia sana, wasubiri wenzao. Haiwezekani unakuwa na mkoa una mtandao wa kilometa 300 wengine wana mtandao wa kilometa 600 wengine 900 wengine 800; *that is very unfair*. Twende kwa utaratibu mzuri (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, sisi Mkoa wa Kigoma tumeomba barabara kupandishwa hadhi kutoka barabara za Wilaya, Halmashauri, kuwa barabara za Mkoa kwa maana ya TANROADS. Tunaomba Mheshimiwa Waziri alizingatie hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kule Kasulu kuna barabara muhimu sana, inatuunganisha kati ya Kasulu, Kabanga, Msambala, inakwenda Mwanga mpaka Wilaya mpya ya Buhigwe, kwenda *border* yetu na Burundi. Barabara hiyo tunaomba, Mheshimiwa Waziri kwa kibali chake tumeshapitisha kwenye RCC, inangoja timu yake ile na Kamati yake ili barabara hiyo waweze kuipandisha hadhi. Tutaomba sana! Siyo hiyo tu, ziko barabara tatu, nne za Mkoa wa Kigoma ambazo tumeomba zipandishwe hadhi na hiyo tafsiri yake itatuongezea mtandao wa barabara angalau za changarawe. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni barababara yetu ya kihistoria ya muda mrefu nimeona imetengewa fedha, shilingi bilioni 70 Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi, Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 32 ameeleza vizuri kwamba kipande cha Kidahwe – Kasulu kuna mkandarasi yuko pale na kimetengewa fedha; na kipande cha Kabingo - Nyakanazi, nacho kimetengewa fedha, lakini hapo katikati, kuna kilometa zaidi ya 200 za Kabingo – Kibondo – Kasulu - Manyovu Border na Burundi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameandika kwenye kitabu chake kwamba kilometa 258, amezungumza kwenye kitabu chake kwamba hiyo inafadhiliwa na fedha za *African Development Bank*. Sasa tungependa kujua, ameishia hapo tu na akaweka na nukta kubwa, maana yake nini? Hizo

barabara zinaanza lini? Kwenye vitabu vyake vyote viwili haonyeshi bajeti au hizo fedha za ADB zitatoka lini na ni kiasi gani kwa barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, hiyo maana yake nini? Maana yake ni kwamba, hiyo barabara kubwa ya kihistoria ya Kigoma - Kidahwe - Nyakanazi itakuwa haijakamilika, kama hicho kipande hakijakamilika, sisi tunaotoka Kidahwe, Kasulu itakuwa imekamilika. Nilimshukuru Mheshimiwa Waziri, nilimwona akiwa Kijiji cha Kasangezi anahangaika na barabara ile. Yule Mkandarasi juzi nimemuuliza mwenyewe akaniambia amepewa fedha. Hiyo ni *assurance* ya watu wa Kigoma, kwamba hiyo barabara ya kihistoria sasa inajengwa. Tunaomba *flow* ya fedha iendeleo, barabara hiyo ni muhimu sana, kwa sababu ni barabara ya kihistoria na ni barabara ya siku nyingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo naomba pia nizungumzie barabara ambayo ameitaja kwenye kitabu chake, hii barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi, shilingi bilioni 77. Sasa nataka kujua Mheshimiwa Waziri, hii barabara maana yake kutoka Sumbawanga ukaja mpaka Katavi - Mpanda, ukaja mpaka Uvinza - *Border*, ukaja mpaka Kanyani - Kasulu kwenda Nyakanazi, hiyo ni barabara ndefu sana. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tuelewe, hizi fedha ambazo wamezitenga, shilingi bilioni 77 zinajenga sekta ipi? Maana yake ukitoka Mpanda mpaka Uvinza, unazungumza habari ya kilometa 600 ni mbali sana! Sasa napenda kujua, hizo shilingi bilioni 77.5 zinajenga sekta ipi katika barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kulikuwa na mkakati wa kujenga barabara itoke Katavi kwa maana ya Mpanda kuja Uvinza *border*, ije mpaka Kanyani - Kasulu - Nyakanazi inakuwa ina-*link* ile barabara. Sasa tungependa kujua hizi fedha huyo mkandarasi atakuwa anaanzia wapi, anaanzia Kanyani kwenda Uvinza au anaanzia Uvinza kwenda Mpanda, kwa maana ya Mkoa wa Katavi? Mheshimiwa Waziri ningependa kuelewa kwa sababu hiyo ni barabara ndefu sana na inapewa jina refu sana, kilometa zaidi ya 600, ni barabara ndefu na ningependa kupata maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine dogo tu, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 75 amezungumza ujenzi wa *block train* kwenda Kigoma na Mwanza kwa kuhudumia wafanyabiashara wa Kigoma – Mwanza – Tabora – *DRC* - Burundi - Uganda na kadhalika. Amezungumza habari ya vichwa vya treni, kuundwa. Yeye unajua Kiswahili; yeye ni mtu wa Zanzibar, kuundwa maana yake nini? Wanaunda vichwa vya treni au wananunua vichwa vya treni? Sijui kama ni lugha maana wanazungumza kuunda vichwa vya treni, sasa kuunda maana yake nini? Kama wanaviunda, basi napenda *clarity* tu, labda ni lugha, lakini ninachojua kama wanachozungumza ni kununua vichwa vya treni naweza nikaelewa. Naomba hilo jambo aliweke makini.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 72 nafikiri nayo ni *error*, anazungumza habari ya ujenzi wa reli ya Arusha – Musoma, lakini anazungumza habari ya matawi yake ya Tabora – Mwanza. Mheshimiwa Waziri hiyo jiografia imekosewa; hakuna ujenzi wa reli ya Arusha – Musoma ukawa na matawi ya Tabora kwenda Mwanza. Halafu anazungumza habari ya tawi la kwenda Minjingu na matawi ya kwenda Engaruka, angalieni jiografia hiyo msije mkajichanganya katika utekelezaji wa miradii hii ya reli, hiyo iko ukurasa wa 72.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Kengele ya kwanza?

MBUNGE FULANI: Ya kwanza. Endelea!

SPIKA: Ni kengele ya pili kaka.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Kengele ya pili?

SPIKA: Ndiyo!

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, juhudi ni nzuri, Mheshimiwa Waziri endelea, tuna matumaini makubwa na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko Mbunge wa Kasulu. Taarifa zinazonifikia mezani zinasema Kigoma huko kumekucha! *(Makofi)*

Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Sevelina Mwijage.

MHE. SVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu niweze kuchangia hotuba hii. Kwanza nichangie suala moja linaloniudhi na kuniletea kichefuchefu, barabara ya kutoka Mlandizi kuja Chalinze; barabara ambayo ina matuta utafikiri wanapanda viazi, inanikera. Ni barabara ambayo tunaitegemea wote, Maraisi wanapita pale, Mawaziri wanapita pale, ile barabara ni mbaya sijui kama Mheshimiwa Waziri ameweza kuitengea fedha kwa sababu wote tunapita pale, tunaiona hiyo barabara ilivyo. Ukipita pale kwa *speed* lazima upate mweleka.

Mheshimiwa Spika, Wakandarasi wanaopewa shughuli zote za barabara, sijui wanakuwa wametoa rushwa mimi sielewi, kwa sababu barabara inatengenezwa siku mbili, tatu imeshaharibika, unakuta mashimo. Ni kwa nini wasitafutwe Wakandarasi ambao ni wasomi, wana uelewa wanajua

kutengeneza? Kwa sababu ukiangalia barabara zote zinazotengenezwa Tanzania nzima, ni miezi miwili, mitatu tayari ina mashimo. Naona Wakandarasi hawa huwa wanatoa rushwa ndiyo maana wanapata hizo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye usafiri wa Ziwa Victoria. Nina majonzi makubwa sana kwa Wanakagera. Tumeanza kupata meli ya kwanza mwaka 1961 kwenye uhuru; *Victoria*, tukapata meli ya Usoga, tukapata Butiama, tukapata MV. Bukoba, lakini meli zote hizo unazosisikia zimeshakuwa chakavu na *Victoria* kila mwaka mnatenga bajeti ya kukarabati. Ni lini mtatuletea meli mpya? Kwa sababu tunapata ahadi kutoka kwa Marais na Rais kila anapoingia kwenye mchakato wa kampeni, anaahidi meli moja au meli mbili mpya; mpaka leo hii sasa naona mnaweka fedha za kukarabati. Hatutaki tena kukarabatiwa meli zikaja kuwaua watu, hatukubali tena kwa sababu kile kitendo cha MV - Bukoba kuendelea kuiweka ndani ya Ziwa Victoria imeua watu; mpaka mmekuja kusema kwamba irudi hiyo meli ya MV *Victoria*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali, watu wa Mkoa wa Kagera pamoja na wa Kanda ya Ziwa siyo watu wa kuwategeshea ili wakarabati siku mbili, tatu unakuta imezama, inakwenda Kemondo imezama, inakwenda kwenye Bandari ya Bukoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza, Bandari ya Kemondo na Bandari ya Bukoba Mjini hazijawahi kufanyiwa ukarabati toka kwa mkoloni mpaka sasa hivi. Ukiangalia hizo bandari, zilikuwa zinatumiwa kupeleka mizigo Uganda, inatumia meli ya Umoja, inatoa mizigo pale Bukoba Mjini inapeleka Uganda, inatoa Uganda inapeleka Kemondo, inatoka Kemondo inapeleka Musoma. Mpaka leo hii wananchi wa Bukoba pamoja na wa Kanda ya Ziwa wamekuwa maskini kwa sababu hawana sehemu ya kusafirishia, kupata uchumi katika mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye barabara. Sisi tuna barabara ambazo zinaunganisha nchi zetu jirani. Tuna barabara ya kutoka Mushaka kwenda mpaka Kyerwa mpaka Uganda. Hiyo barabara nafikiri miaka nenda rudi haijawahi kutengewa fedha au kusema katika orodha kwamba inatengenezwa au imewekewa fedha, sijawahi kusikia. Ni mashimo, kutoka Mushaka kwenda mpaka Kyerwa mpaka Mlongo. Ni barabara ambayo tunaweza kufanya biashara na watu wa Uganda kwa sababu ni njia ya karibu ya kuunganisha na Karagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Mushaka kwenda mpaka Benako - Ngara ni barabara ambayo inatuunganisha kwenda Rwanda na Burundi, lakini ni mbaya na majambazi wanatuteka mle mara kwa mara, kwa sababu barabara ni mbaya. Sijawahi kusikia Serikali inaiongelea au kusema kwamba

kuna kipindi ambacho itatengenezwa au wameitengea fedha kadhaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye barabara tena. Kuna barabara ya kutoka Kanazi inakwenda Kafunjo, kuna daraja Kafunjo pale linaitwa Kalebe kabla hujafika Ibwela. Hilo daraja ni bovu sana. Kinachonishangaza ni kimoja na kila Mbunge wa Mkoa wa Kagera akisimama hapa anaeleza hiyo barabara, ni mbaya sana na tunaitegemea, mtu akitoka Kanazi anakwenda Ibwela akitoka Ibwela anaenda Kafunjo, akitoka anaunganisha, yuko Kyaka, tayari ameshaingia Uganda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoomba, Mkoa wa Kagera ukiangalia hata kwenye bajeti za Mawaziri wote sijaona bajeti ambayo inatugusa Wanakagera, naomba sana kwa Mheshimiwa Waziri, wawe wanatukumbuka, nasi ni wananchi wao. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye viwanja vya ndege. Kiwanja cha Ndege cha Bukoba Mjini kimefanyiwa ukarabati, lakini tuna ahadi ya miaka nenda rudi Kajunguti. Kajunguti ina ahadi ya miaka mingi. Sisi tuna zao la ndizi Bukoba tuna mazao ya matunda; tungekuwa na uwanja ambao ni mkubwa na sisi tungekuwa tunasafirisha hata matunda yetu kupeleka nje, kwa sababu unakuta ndizi zinasafirishwa kupeleka Uganda, Uganda wanasafirisha kupeleka nje, lakini sisi wenyewe hatuna. Ni kitu cha kukuza uchumi katika Mkoa wetu wa Kagera. Naomba sana na sisi wawe wanatukumba ni Watanzania wenzao. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, narudi tena hapo hapo kwenye uwanja wa Bukoba. Uwanja wa Bukoba ni mfinyu sana. Kila wanapopanga fedha, wanapanga fedha ambazo ni kidogo kwa sababu unakuta huku kuna wananchi na huku kuna wananchi. Wanapanga fedha kidogo! Kwa nini isitengwe fedha ambayo ni kubwa angalau watu wote wa upande mmoja wakaondolewa, wakabaki wa upande mmoja, ukapanuliwa, tukawa tunasubiri hizo fedha za Kajunguti zitengwe. Hata juzi ndege imeleta matatizo ni kwa sababu ya hali ya hewa ya pale Bukoba.

Mheshimiwa Spika, naomba sana hali hiyo hiyo, michango hiyo inayochangia kuhusu barabara kuhusu na uwanja wa ndege tuna masikitiko makubwa, ni kwa sababu na sisi tuna uchumi ambao tunaweza kufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukipata uwanja wa ndege mkubwa, tukipata barabara za kuunganisha na sisi tungekuwa tunajivunia Mkoa wetu wa Kagera, urudi kama Kagera ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, tunazalisha kahawa; utapeleka wapi kahawa? Naomba sana Mheshimiwa Waziri akija hapa aweze kutueleza sisi Wanakagera wanatuweka upande gani? Upande wa kukosa kabisa bajeti ya Serikali au upande wa kuwekewa kiporo au upande wa kutokukumbukwa kabisa? Tuelewe, hata sisi tujue kwenye bajeti ya Serikali, hatukumbukwi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, barabara za Bukoba Mjini. Nasikitika, barabara za Bukoba Mjini ukiangalia na kipato cha Halmashauri yetu ni kidogo sana kwa sababu hatuna kipato chochote pale Bukoba na ni kwa sababu ya maunganisho ya hizo barabara nilizozisema. Ni mbovu ni mbaya, hatuna Stendi, hatuna Soko, hatuna nini; ni watu ambao tunakaa kwa kukaa kufikiria tufanye nini.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mchango wangu huo, nina majonzi makubwa, naomba Serikali itoe macho iangalie Mkoa wa Kagera na sisi tuweze kupata kipato, tupate hata kale kasungura tulikonako kadogo, kaende Mkoa wa Kagera. Naomba kuishia hapo. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Savelina Mwijage. Mheshimiwa Joseph Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Chegeni jiandae.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema asubuhi, muda mrefu sikuwa hapa Bungeni kwa sababu nilikuwa na kesi ya uchaguzi. Namshukuru Mwenyezi Mungu amenirejesha Bungeni salama na nawashukuru wananchi wangu wa Rombo kwa kuniunga mkono wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikuwepo, iko michango mingi sana ambayo ilitolewa hapa Bungeni tangu wakati wa kuchangia mpango na kadhalika, basi kama nitarudia kwenye eneo ambalo wenzangu waliligusa naomba ionekane tu kwamba nami nataka niweke rekodi katika mambo yaliyotokea katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa nilizungumze ni ujumbe ambao nimetumwa na wapiga kura wangu na baadhi ya viongozi hasa viongozi wa dini tuliokutana kwenye mazishi, akaniomba nikifika Bungeni niuseme, nao ni kuhusu matangazo haya kutokwenda hewani kama ilivyokuwa zamani. Wamenituma niseme ifuatavyo: kwamba Bunge kuna kujichanganya kwa hali ya juu ambapo watu wanahoji, Bunge hili lina wasomi au sote tumegeuka kuwa vilaza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasema hivi, mwanzoni ilisemekana Bunge ndilo linalohusika na kuzuia matangazo, lakini kadri siku zilivyokuwa zinakwenda, Serikali imejitokeza kuwa msemaji wa Bunge. Sasa wanashangaa, ni Bunge au ni Serikali? Katika Serikali kuwa msemaji wa jambo ambalo wanasema linahusu

Bunge, Waziri wa Habari anasema kwamba hili linatokana na gharama, lakini Waziri Mkuu anasema ni ili wananchi wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wanajjuliza, hivi hii Serikali ni moja? Mambo yanaamuliwa kwenye Baraza la Mawaziri au mnaamulia kwenye chai? Kwa hiyo, wananchi wanataka kujua, jambo hili hatma yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nataka niwaambie kuna faida kubwa ya kukaa nje ya Bunge, Mbunge wakati Bunge linaendelea.

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Serikali, msifikiri jambo hili linawaleta umaarufu, linawachanganya kweli kweli kwa sababu wananchi walichoshikilia ni kwamba mnazuia wananchi wasione kile ambacho wanapaswa kuona kwa sababu mnaogopa kukosolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami ninachokiona ni kwamba yako mambo Bungeni hapa yanafanyika mazuri na Wapinzani, yanafanyika mazuri na upande mwingine, ni kwa sababu gani mnakataa wananchi wasipate haki yao ya kuona nini kinachoendelea? Kama sasa hivi katika bajeti hii, wananchi wanauliza, wao wanalipa kodi; Bunge hili la bajeti ndilo linalogawa mafungu ya zile kodi zao, kwa nini mnawakimbiza kulipa kodi lakini wasiwe na haki ya kuangalia ile kodi yao inavyogawanywa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tuseme ili ibaki kwenye rekodi, kwa sababu tumekuwa tukiwashauri, lakini hamtaki kupokea ushauri, nitoe mfano wa ushauri ambao tumekuwa tukiwapa. Tarehe 27 Mei, 2015 katika Bunge hili Mheshimiwa Esther Matiko alishika shilingi katika Wizara hii kuhusu boti ya Dar es Salaam Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, alichosema Mheshimiwa Esther wakati ule ndicho CAG ambacho sasa hivi ame-*confirm* kwamba boti ile ilikuwa chini ya kiwango, kwamba gharama za kununua boti ile zilikuwa kubwa. Sasa sisi hatushauri kwa maslahi yetu, tunashauri kwa maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umezuka mtindo katika Bunge hili Wizara ya Uchukuzi ikiguswa kwa sababu, Rais alikuwa Waziri hapa, kuna hisia za kuzuwiazuwia Wizara hii watu wasiseme maneno! Hatusemi kwamba, Rais akiwa Waziri alifanya ufisadi, inawezekana ni Katibu Mkuu, inawezekana ni watu wake! Na sisi tunamwambia kwa sababu, ya umahiri wake wa kutumbua atumbue hawa ambao walihusika katika kuharibu fedha za wananchi. Hili ni jambo ambalo kila mtu mwenye akili na anayeipenda nchi ataniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitoka huko nenda kwenye barabara zetu. Mheshimiwa SavelinMwijage amezungumza hivi hakuna mtu anayeiona

barabara ya Chalinze – Vigwaza mpaka Mlandizi? Hii barabara Mawaziri wanapita, Rais anapita na kila mtu anapita! Hivi haiingii kwenye fikra kwamba, hapa ni ufisadi umefanyika? Hapa ni wizi umefanyika? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa haya yanazuiwa na yanapozuiwa mnafikiri kwamba, ni kusaidia Serikali, hapana! Serikali inaumizwa kwa kiasi kikubwa sana. Ujenzi wetu wa barabara lazima uangaliwe, kuna ufisadi na wizi mwingi sana unatokea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya kutoka Mwika – Mkuu kwenda mpaka Tarakea, Jimboni kwangu; ile barabara haina miaka mitatu, leo kuna mashimo! Sasa hivi tumeanza viraka, ni nini kimetokea? Feeder roads hazijatengenezwa! Kuna eneo moja linaitwa Mengwe, Keni na Mkuu; zile feeder roads tuta la barabara liko juu mtu anapanda na pikipiki kule haoni gari linapita kule! Matokeo yake watu wanauawa kila siku!

Mheshimiwa Spika, nilisema mwaka jana na mwaka huu nasema tena! Isifikiriwe kwamba, Serikali itapendwa kwa kuambiwa halafu haitekelezi! Ninyi mmeficha wananchi wasitusikie, sisi haya tunakwenda kuwaambia! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, barabara ile ilijengwa na Wakandarasi wawili. Mkandarasi wa kwanza alipeleka vifaa akaviweka kwenye eneo la kiwanja cha michezo cha watoto wa shule pale Mengwe, mpaka leo hii miaka 10, matingatinga yako pale! Magari yanaozea pale! Watoto hawana mahali pa kuchezea! Tumeshahangaika kila mahali yale yaondolewe, hayaondolewi! Sasa mimi sijui Serikali ya Hapa Kazi Tu ningefikiria kwamba, haya mambo ambayo yamelalamikiwa miaka iliyopita ndio ingeyachukua sasa iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo katika barabara hiyo, wamejenga mto unapita juu ya barabara, Kikelelwa kule! Sasa hivi hapa jinsi mvua zilivyonyesha, maji yote yanaenda kwenye majumba ya watu. Watu wanateseka! Tumesema na tunaendelea kusema. Sasa huwezi hata siku moja ukawaridhisha wananchi wakati kero zao hazishughulikiwi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua muda unaniishia, lakini niseme sisi tumepata mafuriko mwaka huu kule Rombo. Kati ya mtandao wa barabara za Halmashauri, kilometa 285, kilometa 167.7 zimebomoka zote. Fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Halmashauri katika bajeti ya 2015/2016 mpaka robo tatu ya mwaka wa fedha tulikuwa hatujapata hata shilingi moja! Naiomba Serikali ituletee hizo fedha kwa sababu, sasa hivi wananchi katika vijiji vyote, katika Kata zote hakuna jinsi, barabara zimevunjika na kwa hiyo, wanategemea sana wapate fedha hizi ili waweze kurekebisha barabara maisha ya wananchi yaende kama ambavyo wanataka yawe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, yapo maeneo korofi maana maendeleo yakija yanakuja na tabu zake; yapo maeneo korofi ambayo tulishaomba yawekewe matuta. Kwa mfano, kuna eneo moja linaitwa Mamsera, juzi nimerekodi mtu wa 22 kuuawa kwa sababu ya speed kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda TANROADS Mkoa wa Kilimanjaro mara chungu nzima, Baraza la Madiwani, Halmashauri iliyopita na hii ya sasa hivi wamekwenda wameomba jamani pale pawekwe matuta watu wanakufa! Hivi ndiyo niseme kwamba, Serikali inapenda kusikia watu wake wanauawa?

Mheshimiwa Spika, juzi uso kwa macho, nimeona mweyewe mtu wa 22 ameuawa! Eneo la Tarakea, eneo la Kikelelwa, eneo la Keni, ni maeneo ambayo ni korofi! Mimi ni mmoja kati ya watu ambao tunapinga matuta, lakini wakati mwingine lazima tuyaombe kwa sababu ya wakorofi wachache. Naomba sana Waziri awaagize watu wa TANROADS Mkoa wa Kilimanjaro waweke matuta eneo la Mamsera, eneo la Keni, eneo la Holili na eneo la Tarakea.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, moja kati ya vitu vinavyochangia hizi barabara kuharibika, niliwaambia yapo magari yanabeba *pozzolana* kutoka Holili na mengine yanabeba mizigo mizito yanapita kwenye ile barabara inakwenda Kenya, wekeni mizani hata ya kamba! Ni leo, ni kesho, ni leo, ni kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ya Awamu ya Nne imekwenda imekuja sasa Serikali ya Hapa Kazi Tu, wekeni basi hiyo mizani! Huu nao ni ushauri tunawasaidia kwa sababu, ile barabara inavunjika. Barabara zinatengenezwa kwa pesa nyingi, lakini wakorofi wachache wanasababisha zivunjike. Sasa tuseme namna gani, ili mtuelewe? Maana tukisema kwa kutetea rasilimali hamuelewi! Tukisema kwa kelele mnasema sisi tunapayuka, tunapiga kelele.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwamba, haya niliyoyasema Wizara iyafanyie kazi. Nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Selasini kwa mchango wako. Ni kweli, ulikuwa muda mrefu haupo, karibu sana Bungeni, lakini ile ajenda yetu moja ya Rombo ile haukutueleza kidogo! Yale mambomambo ya Rombo yale! Bado yapo au yamekwisha? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe! Mheshimiwa Chegeni jiandae!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, leo na kesho tunajadili bajeti ya Wizara ambayo inabeba asilimia 46 ya Bajeti yote ya maendeleo ya nchi yetu.

Yaani katika fedha za Bajeti ya Maendeleo ambazo zinaombwa na Serikali mwaka huu, trilioni 10.5, trilioni nne *point* nane ni ya Wizara inayoongozwa na Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Naamini kabisa kwamba, wakati tunapanga siku za kujadili hatukuwa tumezingatia hili, ilipaswa Wabunge wapate muda mwingi zaidi kwa kuwa na siku nyingi zaidi za kujadili Wizara hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara hii inaongoza taasisi ambayo kwa mujibu wa Taarifa ya *PPRA* ndio taasisi ya pili kwa thamani ya manunuzi nchini, *TANROADS*, baada ya *TANESCO*. Kwa hiyo, ni Wizara ambayo ni nyeti sana na naamini kabisa kwamba, Waheshimiwa Wabunge wataitendea haki na Serikali itaweza kutoa majibu yanayostahili kwa ajili ya hoja mbalimbali ambazo Wabunge wataweza kuzi-raise. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda nisisitize hoja ambazo Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Waziri Kivuli wa Miundombinu, amezi-raise ziweze kupatiwa majibu na hasahasa hoja ya *MV Dar-es-Salaam* kwa sababu, ni hoja ambayo inakimbiwakimbiwa na ni muhimu tuweze kuona suala la *MV Dar-es-Salaam* likichukuliwa hatua, ndiyo tutaamini kweli kuna nia ya dhati ya kupambana na ufisadi katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nsanzugwanko na Wabunge wengine wa Kigoma watakaopata nafasi watazungumzia barabara za Mkoa wa Kigoma. Tuna kilometa 258 ambazo zitaunganisha Nyakanazi na Manyovu kwa maana ya kutokea Kabondo – Kabingo – Kibondo – Kasulu mpaka Manyovu, kilometa 258.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri wa Fedha walitwambia kwamba, mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Katika vitabu vya bajeti hatuoni, siyo tu ni lini mradi huu utaanza, hatuoni fedha zimetengwa kiasi gani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, kuna *confusion* ya *project number* kwa sababu, barabara iliyokuwa inatoka Sumbawanga mpaka Nyakanazi ilikuwa na *Project Number* hiyo. Sasa hivi *project number* nyingine kwa Nyakanazi mpaka Manyovu kwa maana ya kwamba, Wizara ya Ujenzi bado haijarekebisha jambo hili. Kwetu sisi Kigoma, mkoa pekee ambao haujaunganishwa na mkoa mwingine wowote kwa lami moja kwa moja, barabara ya Nyakanazi ni barabara muhimu, ni barabara ya kimkakati na ndiyo siasa za Kigoma. Kwa hiyo, naomba jambo hili Waziri aweze kulitolea ufafanuzi wa kina, hasa hasa inaanza lini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Tabora na Kigoma kuna takribani kilometa 200 pale kama 204 hivi ambazo bado hazijakamilika. Kwa hiyo, naomba Waziri aweze kutueleza taratibu, tumeona Urambo – Kaliua

itaanza mwaka huu, lakini pale Kazirambwa mpaka Chagu hatujajua inaanza lini. Kwa hiyo, naomba mambo haya Waziri aweze kuyatazama ili Mkoa wa Kigoma uweze kuunganishwa. Pili, barabara ya kutokea Uvinza kwenda Mpanda na barabara ya kutokea Uvinza kwenda kwenye Daraja la Malagarasi, tunaomba tupate *commitment* hapa ya Serikali, inaanza lini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hasa tumeambiwa kwamba, barabara ya Mpanda mpaka Uvinza inaanza kilomita 30 kuanzia Mpanda. Naomba nimshauri Waziri kwamba, tuwe na Mkandarasi ambaye ataanzia Mpanda kuja Uvinza na tuwe na Mkandarasi ambaye ataanzia Kanyani mpakani kwenye njipanda ya kwenda Uvinza mpaka Uvinza ili tuweze kuhakikisha kwamba, barabara hii inakamilika vizuri kwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la reli. Kama ilivyo kwa barabara, reli kwa Kigoma ndiyo siasa na siyo Kigoma peke yake, kwa mikoa yote ambayo inategemea reli ya kati, reli ni kiungo muhimu sana cha usafiri. Hapa napenda nirejee maoni ambayo yalitolewa asubuhi kama swali na Mheshimiwa Sabreena na baadaye tukawa tumeyazungumza na majibu ambayo Waziri ameyatoa; kuna haja kubwa ya kuchukua hatua za haraka kuondoa ulanguzi wa tiketi katika Stesheni ya Reli, Kigoma. Ni jambo ambalo linaumiza sana watu, watu wanatoka mbali na njia pekee ni njia ya uwakala. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata ukisema tunatumia *digital*, tunatumia simu, bado simu zitatumia mawakala kwa sababu, ni lazima *TRL* iweze kukubaliana kuingia makubaliano na kampuni binafsi kama zile ambazo zinatumika kwa ajili ya uwakala, kwa hiyo, huwezi kukwepa uwakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba jambo hili watu wa *TRL* waweze kulitazama, lakini jambo la msingi sana katika eneo hili, lazima sasa tufahamu kwamba, *RAHCO* ndiyo *TANROAD* ya reli. *RAHCO* inapaswa kuachia *assets* zote ambazo hazihusiani na ujenzi wa reli, kuiachia *TRL* ili *TRL* iweze kuwa na *balance sheet* iliyo nzuri kwa kuweza kupata fedha za uendeshaji wa reli, kwa hiyo, naomba jambo hili liweze kutazamwa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, tuangalie namna gani ya kutumia Stesheni za Reli kama maeneo ya biashara; stesheni zetu za reli zote kuanzia Dar-es-Salaam mpaka Kigoma zimelala! Hamna shughuli yoyote inayofanyika! Kwa hiyo, naomba *TRL* waweze kupewa kibali maalum cha kuendeleza Stesheni za Reli ambazo sasa hivi ziko chini ya *RAHCO*. Kwa hiyo, naomba mabadiliko hayo yaweze kutazamwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ya Serikali kuhusu kipande cha reli kutokea Kigoma kwenda Tabora na Uvinza – Msongati kwa ajili ya *standard gauge* kwa sababu, naona sasa hivi mwelekeo wa Serikali ni kupeleka

reli Isaka mpaka Kigali na mmesahau kabisa suala zima la Uvinza – Msongati na jambo hili kwetu ni siasa kwa sababu, tunataka Uvinza iwe ni *hub* kwa ajili ya maeneo ya Maziwa Makuu. Kwa hiyo, naomba jambo hilo liweze kutazamwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza, naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kuhusu Uwanja wa Ndege wa Kigoma kwa sababu, tulizungumza na alikuja Kigoma na aliona. Ametenga fedha, lakini naomba nifahamu kiwango gani ambacho kinakwenda kupanua *runway* na kiwango gani ambacho kinaenda kujenga jengo la abiria kwa sababu, kwenye bajeti yake hakufafanua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo ambayo yame-*miss* katika bajeti; la kwanza, ni Bandari ya Ujiji kwa sababu tulishakubaliana na Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa Bandari Ndogo ya Ujiji na Mamlaka ya Bandari Tanzania wamesema wanaanza mwaka huu. Sasa sijaiona hiyo kwenye bajeti! Sasa ni kwa sababu, iko kwenye Bajeti ya Maendeleo ya Mamlaka ya Bandari ama namna gani? Naomba nipate maelezo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ni suala zima la Bandari ya Kigoma. Bandari ya Kigoma ndiyo Mji wa Kigoma! Bandari ya Kigoma ikilala mji unalala kwa sababu, biashara zinakuwa hazipo! Sasa hivi Bandari ya Kigoma inaendeshwa na Mamlaka ya Bandari, lakini huwezi ukafanikiwa kuiendesha Bandari ya Kigoma kama huna biashara kutokea Kongo, kama huna biashara kutokea Kalemii. Kwa hiyo, Serikali inapaswa kuwa *strategic* kuhusu Bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Kigoma inapaswa kuendeshwa na taasisi ambayo inao uwezo wa kupata mzigo kutoka Kongo. Kwa hiyo, Waziri naomba jambo hili alitazame, tulilizungumza Kigoma, tulijadiliana Kigoma, lakini sasa hivi kuna ushindani mkubwa sana, vinginevyo reli tunayojenga itakuwa haina maana yoyote kwa sababu, haitapata mzigo kutokea Kongo. Kwa hiyo, naomba jambo la uendeshaji wa Bandari ya Kigoma waweze kulitazama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, *MV Liemba*, naomba jambo hili tuweze kulimaliza, tumelizungumza muda mrefu sana. Waziri Mwakyembe anakumbuka, tulizungumza mpaka na watu wa Ujerumani, alikutana na Waziri wa Usafirishaji kutoka Ujerumani wakati akiwa ni Waziri wa Wizara hii. Jambo hili la *MV Liemba* yasije yakatokea mambo yaliyotokea kwa *MV Bukoba*! Kwa hiyo, naomba *MV Liemba*, kama meli ya kihistoria, iweze kutazamwa na iweze kushughulikiwa kwa namna ambavyo inatakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, nami napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Awali ya yote, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Hasna Mwilima baada ya kupata ushindi usiokuwa na shaka na Mahakama imetenda haki. Hii imeonesha jinsi ambavyo kwa kweli, kesi nyingi zinafunguliwa hazina mashiko yoyote ndiyo maana Sheria inaposimama CCM inachanua. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Chegeni, Spika hajakusikia! Hebu weka vizuri! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, najua hujasikia na wala hukuona kwa sababu, Wagogo mna sifa ya kutokuona na kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwa michango ya wenzangu, wamesema mambo mazuri, wakati mwingine ushauri kama huu lazima Serikali iusikilize. Ushauri ambao unakuwa na tija, ushauri ambao unakuwa na mwelekeo wa kujenga Serikali yetu na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, niwatoe hofu ndugu zangu wanaposema yatumbuliwe majibu sijui wapi! MV Dar-es-Salaam na kadhalika. Jamani, msubiri! Mbona mnakuwa na haraka! Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati ya kuweza kusafisha Serikali yake na kuunda nchi hii ili iweze kuwatumikia Watanzania wote, kwa hiyo, msiwe na haraka, kila kitu kitakwenda hatua kwa hatua. Haiwezekani leo hii ukaanza kutembea na ukaanza kukimbia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika Hotuba hii naona Mheshimiwa Waziri hajazungumzia suala la mikoa mipya na wilaya mpya, kwa sababu, wilaya hizi na mikoa mipya ina miundombinu ambayo kwa kweli, ni kama haipo. Sijaona kwenye bajeti mkakati mahususi kwamba, ni kwa vipi barabara hizi zitaimarishwa ili kuifanya mikoa hii na wilaya hizi ziweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Simiyu hata kwenye Hotuba haujaunganishwa na barabara ya kwenda Singida wala Arusha! Ningeomba katika Hotuba hii Mheshimiwa Waziri, hebu tuainishie kwamba, hata usanifu au upembuzi yakinifu ni lini utafanyika kuiunganisha Simiyu na Singida? Leo hii kuna barabara, lakini haijatajwa Mheshimiwa Waziri, ningeomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika barabara ya kutoka Maswa kwenda Bariadi, kilometa 50, hata hazijatajwa Mheshimiwa Waziri hapa, lakini barabara kutoka Maswa kwenda Mwigumbi inawekewa lami na Mkandarasi

yupo! Sasa ni kitu cha kushangaza, unanza kujenga unaacha kipara katikati! Tunafanyaje kazi namna hii? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri katika kuhitimisha hotuba yake, ningependa kusikia mkakati kwamba, zile kilometa 50 za kutoka Maswa kwenda Bariadi, Makao Makuu ya Mkoa. Sisi watu wa Simiyu tuliamua wenyewe kwamba, Makao Makuu yawe Bariadi tena kwenye RCC na Mikutano yote ya hadhara, wananchi wakaunga mkono na hatuna ubishi na hilo. Kwa hiyo, ningepomba sana hili liweze kuzungumzwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kingine tunataka kuimarisha uchumi wetu. Hivi unaimarisha vipi uchumi kama Dar-es-Salaam Bandari yenyewe imefungamana? Hata namna ya kusafiri kutoka nje ya Dar-es-Salaam haiwezekani! Magari, mlundikano na hata namna ya kupenyeza mizigo inakuwa ni tatizo! Tumepata wawekezaji wako tayari kuwekeza zaidi ya Dola milioni 200 kujenga Bandari Kavu pale katika Kijiji cha Soga, Kibaha.

Mheshimiwa Spika, leo ni miaka miwili na nusu, wanakwenda, wanarudi, Serikali imeshindwa kutoa maamuzi. Hivi kwa nini Mheshimiwa Waziri akiwa mwenye dhamana hii asione kwamba leo Mheshimiwa Rais anatafuta wawekezaji, wawekeze katika nchi hii na Dar es Salaam aweze kuifungua, haya malori ya mizigo hayapaswi kuingia Dar es Salaam, yakwamie huku bandari kavu.

Mheshimiwa Spika, hata barabara Waheshimiwa wamezungumza kwamba barabara ya Chalinze kuelekea Dar es salaam imekuwa kama chapati, ni kwa sababu gani? Kwa sababu mizigo mikubwa inatokea sehemu moja inapita sehemu moja. Lazima tuziokoe barabara zetu, ningepomba sana Mheshimiwa Waziri anapohitimisha mjadala huu anipe maelezo ni kwa nini tunachelea kupata wawekezaji ambao wako tayari. Kama ni suala la kuzungumza mnaweka *terms and condition*, mnakubaliana ili tuweze kuifungua Dar es Salaam, mizigo isianzie Bandari ya Dar es Salaam, mizigo ianzie mahali ambapo kuna *dry port* na tuweze kuokoa uchakavu wa barabara zetu. Katika hili ningepomba sana Mheshimiwa Waziri atupatie majibu.

Mheshimiwa Spika, kingine, unapokuwa na TRL halafu mwenye *assets* ni RAHCO, hivi inawezekana namna gani? TRL ha-own any asset zaidi ya zile TRL *commutative* peke yake. Sasa anakuwa na uwezo gani hata wa kukopa? Hawezi kukopesheka huyu, lakini huyu mwenye RAHCO yeye ndiye mwenye mtandao wote, lakini hana uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ningepomba Mheshimiwa Waziri, suala la Reli na RAHCO aunganishe, aache reli asimamie *assets* zote zile aweze ku-*transact* vizuri, aweze kukopesheka na tuweze kuona reli. Naomba sana hii ndiyo njia

pekee inayoweza kufufua uchumi wetu, tunaimba uchumi hatuwezi kufufua uchumi wetu kama hatuwezi kuwa na fikra za namna hii na naomba majibu ya subiri, tuachane nayo. Mheshimiwa Rais anasema kwamba, hapa ni Kazi tu, naomba na nyie Waheshimiwa Mawaziri sasa muwe hapa kazi tu, mambo ya kuchelewa kufanya maamuzi tuachane na biashara hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakuja katika suala la uwanja wa ndege wa Mwanza, uwanja wa ndege wa Mwanza una kila sababu za kiuchumi, kimaendeleo na hata za Kikanda. Ukisimamia uwanja wa ndege wa Mwanza zaidi ya mikoa 10 umeihusisha na nchi jirani. Naomba upewe kipaumbele, uwanja huu uweze kukamilika, uwe uwanja wenye hadhi ya Kimataifa ili tuweze kuifungua Kanda ya Ziwa na Mikoa pamoja na nchi jirani kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hii tunazungumzia kuongeza Pato la Taifa. Ukifungua uwanja wa ndege wa Mwanza ukawa wa Kimataifa, ukawa *Serengeti International Airport*, tayari ile *Serengeti corridor* yote umeifungua, tayari umeweza kuvutia wawekezaji, watalii na ndiyo maana uchumi ambao tunauhitaji leo kutoka Mwanza kwenda Entebbe ni dakika 30, Kigali dakika 45, Kinshansa masaa matatu, lakini ukitokea Arusha, Dar es Salaam ni mbali zaidi. Kwa sababu hakuna ndege inayotoka Mwanza kwenda huko kwenye nchi nilizozitaja hizi, naomba sana Waziri anapohitimisha mjadala huu atuambie ni lini uwanja wa ndege wa Mwanza sasa utakamilishwa kwa kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busega, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi, barabara ya Dutwa-Ngasamo-Nyashimo ni kilometa 46, alisema itajengwa kwa kiwango cha lami. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, kwamba barabara hii sasa iwekwe kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais, aliahidi kwamba itajengwa kiwango cha lami na kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, barabara ile ilikuwa barabara ya mkoa lakini ina-link barabara mbili za TANROAD. Kwa hiyo, ina maana kwamba inaelemewa na uzito wa mizigo ya magari yanayopita pale, kwa hiyo, *automatically* lazima ipandishwe hadhi iwekwe kwenye kiwango cha TANROADS, barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna kipande cha Mkula, pale Mkula ndiyo mzungumzaji anapotoka. Mheshimiwa Rais alitoa zawadi akasema kwamba kwa sababu barabara imepita pembeni na ule Mji wa Mkula ambapo anatoka mzungumzaji na wenyewe uwekwe lami, kilometa 1.45, alitoa ahadi hiyo. Naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha aniambie kama ahadi hii ameshairekodi vilevile.

Mheshimiwa Spika, cha mwisho, ni namna ya kuboresha usafiri majini. Kweli wenzetu wa Mkoa wa Kagera, naomba nizungumze, ahadi ya meli imekuwepo kwa muda mrefu, lazima tufike mahali Serikali i-respond.

Haiwezekani tukarudia matukio kama mwaka 1996 kwa sababu ya uchakavu wa meli. Leo hii MV Victoria imeshachakaa hakuna usafiri *reliable* kati ya Mwanza na mikoa jirani kama Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani wenzangu wa Kanda ya Mwanza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Wiliam Mgaya, sikuoni.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, nipo, nashukuru kwa kunipa nafasi naomba nami sasa nianze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano. Nianze kwa kusema kwamba Mkoa wetu wa Njombe ni mkoa mpya, sitoacha kusema hivyo, kwa sababu tunahitaji maendeleo ili mkoa uweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya barabara ambazo zimeshafanyiwa usanifu ndani ya Mkoa wa Njombe ni pamoja na barabara ya Njombe - Makete inayopita Mbunga ya Kitulo kwenda kutokezea Isonja, Mkoa wa Mbeya. Barabara hii iliwekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi namba moja, lakini vilevile barabara hii iliwekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 mpaka mwaka 2010 iliwekwa tena upya. Hiyo haitoshi, barabara hii Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati anakuja kuomba kura za Urais kule Makete na Wilaya ya Wanging'ombe alisema kwamba barabara hii ndiyo ya kwanza ambayo itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais, barabara hii ina umuhimu mkubwa sana kwa sababu, barabara hii kama itatengenezwa kwenye kiwango cha lami itainua uchumi wa Taifa, katika zao la Pareto, lakini vilevile katika masuala ya utalii. Sisi kule Makete kuna Mbuga ya Kitulo kwa sababu barabara hii imepita kwenye mbuga ya Kitulo, sasa hivi watalii wanashindwa kwenda kwa wingi kwenye ile mbuga ya Kitulo kwa sababu barabara ile haipitiki. Hasa kipindi cha mvua ndiyo haipitiki kabisa. Kwa hiyo, naiomba Serikali izeze kujenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kule katika barabara ile pia kuna mazao ambayo yanasafirishwa ya mbao, viazi mnavyokula Dar es Salaam vinatoka Makete. Barabara hii ina umuhimu mkubwa, naiomba Serikali izeze kujenga

barabara hii. Vilevile ndani ya Mkoa wa Njombe bado kuna barabara nyingine ambayo imefanyiwa usanifu, barabara ya Njombe-Mdandu-Iyayi ambayo nayo inakwenda kukutana na Mkoa wa Mbeya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, barabara hii wakazi wa Wanging'ombe wanaolima mazao ya alizeti pamoja na mbao wanashindwa kusafirisha kwa urahisi kupeleka Mbeya, lakini vilevile wanashindwa kusafirisha kwa urahisi kuja Njombe ili kwenda mikoa mingine kama Ruvuma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuna barabara nyingine ambayo imefanyiwa usanifu, barabara ya Njombe - Ludewa, Manda – Itoni. Barabara hii ni muhimu kwa sababu kule Ludewa kuna makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma. Naiomba pia Serikali ikamilishe barabara hii kwa kujenga kwa kiwango cha lami barabara yote ili kuweza kusafirisha makaa ya mawe kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, pia tuna barabara ya kibena - Lupembe-Madete ambayo inaunganisha Mkoa wa Morogoro, tunaomba pia barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. Nakumbuka asubuhi Mheshimiwa Hongoli aliuliza swali na Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami mwaka 2016 - 2017. Ukienda kwenye hotuba ukurasa wa 37 inasema kwamba Lupembe-Madete Kilometa 125 taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu zinaendelea. Nimwambie tu Mheshimiwa Waziri, stage hii ilishapita, nilitegemea sasa hivi watatuambia kwamba labda tender inatangazwa kwa ajili ya kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nina ombi moja kwa Serikali kuhusiana na Jimbo la Lupembe. Lupembe kuna barabara ambayo inatoka Lupembe-Lukalawa, inapita Ikonda kutokea Makambako. Barabara hii ni *business road*, kuna wakulima wanasafirisha sana mbao, maharage, pamoja na chai. Naomba sasa barabara hii itoke katika ngazi ya Halmashauri ipelekwe iwe barabara ya TANROAD, ili iweze kujengwa kwenye kiwango cha lami kwa uharaka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitoke kwenye barabara niende kwenye kiwanja cha ndege. Mkoa wetu wa Njombe kiwanja chetu cha ndege cha Njombe kina hali mbaya sana. Kwa nini naomba kiwanja hiki? Ruvuma hakuna kiwanja cha uhakika cha ndege, lakini kama tutakarabati kiwanja kile cha ndege cha Njombe na kuweka kwenye kiwango cha lami ina maana ndege nyingi sana zitakuja. Kwa hiyo, Mkoa jirani wa Ruvuma watafaidika na kiwanja kile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, istoshe kule Njombe tunalima zao la maua haya, tunalima maua mazuri sana, kuna roses nyingi sana kule, tunashindwa kusafirisha kufikisha Dar es Salaam zikiwa *fresh* kwa sababu hatuna kiwanja cha ndege cha uhakika, hakuna ndege zinazokuja mkoani pale. Hivyo inasababisha kulega lega kwa kilimo hiki cha maua. Naiomba sasa Serikali ione

umuhimu wa kiwanja hiki, wakarabati katika kiwango cha lami ili na sisi tuweze kusafirisha maua kwa wingi kuja Dar es Salaam na kwenda nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwa mradi wa DART, mabasi yaendayo haraka. Naipongeza Serikali kwa kuweza kutengeneza mradi mkubwa kama huu ambao umegharamia takribani bilioni 322. Hata hivyo, katika mradi huu bado kuna upungufu mwingi sana, kitu cha kwanza nilichokuwa naiomba Serikali ihakikishe kwanza lile suala la hisa. Suala la hisa halijakaa vizuri kwenye mradi huu, Serikali irudi iende ikaangalie kwa umakini jinsi gani ya utaratibu wa hisa. Vilevile nashangaa kwa nini mradi huu hauanzi? Mradi umetumia gharama kubwa sana, bilioni 322, uanze kufanya kazi ili wananchi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna vituo ambavyo havijakamilika katika mradi huu, kituo cha Kimara pale mwisho, kuna kituo cha Ubungo *Terminal*, kituo cha Morocco, kituo kule Posta ya zamani. Vituo hivi viko wazi, ni hatari kama mradi utanza ina maana watu watakuwa wanaingia kwenye mabasi bure. Naiomba Serikali sasa iangalie umuhimu wa kukamilisha vituo hivi na Serikali iwape fedha huu mradi uweze kukamilika ili uweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya, tulikuzoea unakaa upande huu sasa kumbe umesogea kidogo.

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba leo asubuhi Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago aliomba mwongozo kuhusu utaratibu wa wageni wanaoingia hapa Bungeni na ningeomba Waheshimiwa Wabunge wote fuelewane kwa sababu tunaleta wageni wanaotutembelea jambo ambalo ni zuri, ni kwamba kanuni zetu zinamtaka Mpambe wa Bunge kuongoza na kusimamia shughuli za wageni wanaoingia katika eneo lote la Bunge.

Kwa hiyo, ameweka utaratibu kwamba wageni wanaokuja wakifika pale langoni watapewa kitambulisho cha Bunge, lakini wanapopewa Kitambulisho cha Bunge wao nao wanaacha kitambulisho chao pale langoni ili kuhakikisha kwamba wanapotoka wanakabidhi kile kitambulisho cha Bunge pia.

Kwa hiyo, kitambulisho ambacho unatakiwa kuwa nacho ni chochote kile kama vile kitambulisho cha kazi, leseni ya udereva, kitambulisho cha mpiga kura, hata kitambulisho cha bima ya afya au kitambulisho kingine cha aina yeyote. Kama huyo mgeni hana kitambulisho chochote ndiyo anaombwa aache simu yake pale halafu atakapotoka ataipitia simu yake kwa kurudisha kitambulisho cha Bunge.

Kwa hiyo, naomba tuwaeleze wageni wetu mapema wanapokuja wasisahau kuja na vitambulisho vyao, basi wakikosa wanaacha simu yao pale halafu wanapoondoka wanaichukua. Ni masuala tu ya ulinzi na usalama, naomba tutoe ushirikiano, kama bado kuna malalamiko tutayajadili kwenye vikao vyetu vingine vya ndani, tuwaambie Makamishna wetu.

Tangazo la Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa Makamu wa Mwenyekiti, anaomba niwataarifu Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Wabunge Waislam.

Naomba nirudie tena, Mheshimiwa Mchengerwa Makamu Mwenyekiti anaomba Wabunge wote ambao ni wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Wabunge Waislam kukutana saa tisa pale katika kumbi ndogo ndogo mojawapo za Msekwa *hall*. Kwa hiyo, ni Kamati ya Utendaji tu siyo Wabunge Waislam wote, hapana.

Mheshimiwa Boniphace Mwita, Mbunge wa Bunda, anaomba Wabunge wote wanaotokana na wafugaji mkutane Ukumbi wa Msekwa mara baada ya shughuli hizi. Wabunge wanaotoka maeneo ya wafugaji mkutane Msekwa *hall*.

Pia Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Mheshimiwa Upendo Peneza, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni vijana wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa, leo tarehe 17 Mei, 2016, saa saba hii.

Waheshimiwa Wabunge, kikao hicho ni cha kujadili na kupitia Katiba ya Umoja huo. Wabunge vijana mnaombwa mkutane pale Msekwa na *definition* yao Mbunge vijana uwe na umri chini ya miaka 40.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na shughuli zetu saa 10. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea)

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, jioni hii tutaanza na Mheshimiwa Willy Qulwi, baadae atafuata Mheshimiwa John Heche, na baadae tutaendelea na Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Muda wangu nitagawana na jirani yangu Mheshimiwa Japhary, kama atawahi, asipowahi nitaendelea mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo jioni hii ya leo. Tunapoongelea uchumi wa viwanda, ni jambo la kufurahisha kwamba bajeti tunayojadili jioni hii ina mchango mkubwa sana katika kutufikisha kwenye uchumi huo wa viwanda. Naomba nijielekeze katika eneo la kwanza la upembuzi yakinifu, mara nyingine usanifu wa kina na wakati mwingine wanapenda kutumia maneno Mhandisi Mshauri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua sana umuhimu wa zoezi hilo la kabla ya miradi kutekelezwa, lakini niseme kwamba, zoezi hili limekuwa ni kichaka cha kujifichia kwenye Wizara hii, Mawaziri wakijibu asubuhi maswali utaambiwa mradi huo uko kwenye upembuzi yakinifu; baadaye utaambiwa uko kwenye usanifu wa kina; baadaye utaambiwa Mhandisi Mwelekezi anaendelea. Kwa hiyo, nataka kushauri, wananchi wetu kule nje wanachotaka kuona, ni miradi inatekelezwa. Pamoja na kwamba hatua hii haiepukiki na ni muhimu sana, nashauri hebu tupunguze muda wa mazoezi haya, ili hatimaye tuingie kwenye masuala ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingine mazoezi haya yamechukua miaka ya kutosha miaka mitano, upembuzi yakinifu siku nyingine miaka mitano, usanifu wa kina na kadhalika, kwa hiyo, mradi utakuja kutekelezwa baada ya miaka 10, 15 mpaka 20. Tuna mfano hapa uwanja wa ndege wa Msalato, ukienda pale Msalato hadi leo ni pori tupu, lakini miaka kadhaa iliyopita mazoezi haya yalifanyika, yakatumia mabilioni ya fedha zetu. Pia baadaye zoezi kama hilo hilo likafanyika, kwa hiyo, ni kama *duplication* ya jambo hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la pili, la madeni ya wakandarasi, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake, bado Serikali inadaiwa. Huwa najisikia vibaya sana napodaiwa, wanasema dawa ya deni ni kulipa, kwa nini Serikali hii isivalipe hao Wakandarasi? Miradi mingi iliyotekelezwa huko nyuma tunadaiwa, iwe kwenye maji, iwe kwenye eneo hili la ujenzi na kadhalika na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali ili kulinda heshima yake ikwepe jambo hili na tunaingia kwenye matumizi ya ziada ya kulipa fedha za hawa wakandarasi kwa kuwa tumekaa na fedha zao. Kwa hiyo, nashauri kama Serikali hii kweli iko makini, kama Serikali hii ni Serikali ya "Hapa Kazi" hebu tuwalipe wakandarasi ili pia pale wanapokosea tuwe na nguvu ya kuwasukuma na kuwasahihisha. Wakati mwingine hawa wakandarasi wanaishia kufanya kazi zetu vibaya kwa sababu tu wanatudai. Kwa hiyo, nataka kushauri, hebu haya madeni ya wakandarasi tuyalipe kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni eneo la zile barabara zilizoko kwenye ngazi ya Halmashauri. Barabara hizi ziko nyingi sana na barabara hizi zinahitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo, lakini fedha tunazopelekewa ni kidogo, hazitoshi. Nimesikia hapa ndani Waziri amesema yapo maombi zaidi ya 3,000 ya kupandisha hizi barabara. Nashauri hebu maombi haya yafanyiwe kazi ili hizi barabara kweli ziweze kuchukuliwa na TANROAD ambao wana nguvu kubwa kuliko sisi Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la kuunganisha mikoa, hili ni jambo la kisera na kwa kuwa ni jambo la kisera linahitaji kuwa ni jambo la kutekelezwa. Iko mikoa mingi ambayo mpaka sasa hivi bado haijaunganishwa; ukiwa Arusha ukitaka kwenda Musoma, inabidi upite nchi ya jirani; ukiwa Arusha ukitaka kwenda Mwanza inabidi upite barabara ndefu ya kupitia Singida na Shinyanga, lakini zipo barabara ambazo unaweza kupita ukafika mapema.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante, dakika tano hizo, mwenzio Mheshimiwa Raphael.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii na namshukuru Mbunge mwenzangu kwa kunipa fursa hii ya kuchangia dakika zake tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili tu, la kwanza ni suala linaloendelea hapa Bungeni mara kwa mara, Wabunge wengi wakichangia na hasa wa maeneo ya Kusini wanajaribu kuonesha kwamba Kaskazini kumeendelea sana. Sasa hofu yangu dhana hiyo inaweza ikapoteza mwelekeo wa Serikali katika kupanga keki ya Taifa, kwa kuamini kwamba Kaskazini kumeendelea kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukizungumzia Kanda ya Kaskazini unazungumzia Tanga, ukienda kwenye Majimbo ya Tanga kuhusu barabara utapata shida, sasa ikioneshwa kwamba Kaskazini kumeendelea, maana yake ni kwamba hayo Majimbo yote yana barabara nzuri za lami, yanapitika vizuri, kitu ambacho siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda Manyara ni Kaskazini, maeneo ya Wamasai, hayapitiki; kwa hiyo, hoja ya kwamba Kaskazini kumeendelea pia siyo ya ukweli kama inavyozungumzwa hapa Bungeni. Ni jambo jema kufikiri kwamba kama kuna maeneo hayajaunganishwa mkoa kwa mkoa

likatekelezwa hilo, kwa sababu ni sera ya Serikali. Yale ambayo yalishaunganishwa mkoa kwa mkoa yaunganishwe wilaya kwa wilaya, yale ambayo Wilaya zilishamalizika yataunganishwa Kata kwa Kata na hatuwezi kwa pamoja katika nchi hii, kuendelea kwa kiwango cha aina moja kwa wakati mmoja, tunapogawa *resources* za Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tukubaliane tu kwamba kwenye Bunge hili, sote katika nchi hii kama walipa kodi na wachangiaji wa Pato la Taifa tunapaswa kugawana keki ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kaskazini reli ya Tanga mpaka Arusha, hapa ni wimbo, ukijiuliza ni kwa nini reli hiyo mpaka sasa iko katika hali ile, wala kabla hatujafikia upembuzi yakinifu bado ile reli ingefaa kutumika na ikainua sana uchumi wa Kanda ya Kaskazini. Hata hivyo, reli ile mpaka sasa haifanyi kazi, lakini bado kuna dhana kwamba Kaskazini kumeendelea. Ukienda kule Kilimanjaro ukienda Upareni utasikitika, bado unaambiwa Kilimanjaro kumeendelea au Kaskazini kumeendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hilo ili kuweka rekodi sawa, kwamba Taifa hili lina uhitaji unaofanana katika mahitaji yote ya barabara, mahitaji ya reli na mahitaji mengine yoyote yanayohusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alivyoleta bajeti yake, ni lazima aiangalie Kaskazini kama anavyoiangalia Kusini na Magharibi na Mashariki mwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee suala la pili kuhusu *TRL* na *RAHCO*. Mpaka mwaka 2002, Shirika la Reli (*TRC*) lilikuwa na uwezo wa kufanya kazi yake vizuri. Mpaka mwaka 2002 Shirika la *TRC* lilikuwa na vichwa 68, mpaka mwaka 2002 Shirika la *TRC* lilikuwa na mabehewa 1,500 mpaka mwaka 2002 Shirika la *TRC* lilikuwa na uwezo wa kusafirisha tani 1,500,000; kwa hiyo, mgawanyiko kati ya *TRC* na *RAHCO*, ndiyo umeleta shida katika Shirika la Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ni makosa ya Serikali kuingia kwenye mkataba ambao haukuwa mzuri, kati yake na kampuni ya wenzetu wa India, ndiyo uliosababisha hali hii iliyojitokeza. Sasa rai yangu kwa Serikali, ni lazima hapa leo tutoke na azimio katika Bunge lako Tukufu la kuunganisha *RAHCO* na *TRL*, ni lazima tutoke na tamko hilo, vinginevyo maeneo mengi yaliyokuwa yakifanya vizuri kipindi cha *TRC* yatakuwa ni magofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRC* ilikuwa na karakana nzuri, ilikuwa inahudumia reli yake vizuri, lakini leo maeneo yote hayo hayafanyi vizuri kwa sababu ya *TRL* kunyimwa nguvu na Shirika la *RAHCO* ambalo ukiangalia kwa nini lipo hupati majibu yaliyokamilika. *TRL* haina uwezo wa kukopa, kwa sababu

haina dhamana, lakini TRL ndiyo inayoangalia mabehewa yake, vichwa vyake na reli kwa wakati mwingine, naomba sana, muunganishe TRL na RAHCO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Raphael Japhary. Tunaendelea na Mheshimiwa John Heche na baadaye Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy ajiandae.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia kwa niaba ya watu wa Tarime. Kwanza nimesoma hiki kitabu cha bajeti na hotuba ya Waziri na niseme tu kwa niaba ya watu wa Mkoa wa Mara, nina masikitiko makubwa sana, na watu wa Mkoa wa Mara, hawataunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba Rais alichohadi wakati wa kampeni akiwa Mkoa wa Mara mzima, aliahidi uwongo, kwa sababu nimesoma kitabu hiki, Mkoa wa Mara mzima umepewa 0.8 kilometa za lami, haikubaliki; watu wa Mkoa wa Mara ndiyo wenye mbuga kubwa kuliko zote, Mbuga ya Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mkoa wa Mara ndiyo waliokuwa na mgodi wa Buhemba, ambao umechimbwa umekwisha madini pale, wana mpaka wa Sirari, wana Ziwa Victoria wanatoa samaki pale, wana Mgodi wa Nyamongo ambao unaendelea kuua watu. Halafu inapofika kwenye maendeleo, hamuwapelekei pesa haikubaliki, haitakubalika kwa viwango vyovyote vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitamtaka Waziri aje atujibu hapa na nimesoma kitabu cha Mpango hiki hapa, Mheshimiwa Waziri amepeleka kiwanja cha ndege Geita Wilaya ya Chato; kutoka Geita Mjini kwenda Chato kwanza ni kilometa zaidi ya 100 na kitu, sijui amepeleka kwa kujipendekeza kwa Rais au ni Rais mwenyewe amemwagiza akipeleke nyumbani kwake sijui hilo atatujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwangu hapa ni kwamba, Mkoa wa Mara ambao una mbuga ya wanyama ya Serengeti, ina ziwa pale Musoma tunashindwa kujenga uwanja wa Mkoa wa Mara, uwanja wa ndege na kuuboresha uwe wa Kimataifa, wazungu washuke pale waleta uchumi kwa watu wa Mkoa wa Mara. Tunachukua mikoa mipya ambayo imeanza juzi, tunaitengea mabilioni ya pesa kwenda kujenga viwanja ambavyo havina muunganiko wowote wa kiuchumi, ni viwanja vya watu kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu wa Mkoa wa Mara tunauhitaji kwa kweli; naomba sana Waziri anapokuja kuzungumza hapa azungumze hili, kwa sababu ni aibu kwa watu wa Mkoa wa Mara ambapo Mwalimu Nyerere anatoka kule na kila siku mnamsifia, lakini kutendea watu hawa haki hamfanyi hivyo. Hivi kweli watu ambao tunachangia madini yetu mnachukua, samaki wetu mnachukua, kila kitu mnachukua pale, wanyama mnachukua. Jana Mheshimiwa Maghembe alikuwa anasema hata kuchunga hataki tuchunge, anasema ng'ombe wetu ni tatizo, kwenye ardhi ya kwetu wenyewe, ng'ombe anasema ni shida; tunachoambulia na mbuga ile ni ng'ombe wetu kupigwa risasi, ni watu wetu kubaki vilema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukubali hali hii, unapofika wakati wa kutuletea pesa, hospitali ya Kwangwa pale imekuwa wimbo. Haya ni matusi na nitaomba Waziri aje atuambie ni lini mnakwenda kujenga uwanja wa ndege wa Mkoa wa Mara ili kuunganisha watalii waje Serengeti na sisi tuna ziwa pale, watalii wanapenda *beach*, sisi tuna *beach* pale, watakuja kuogelea pale, mtuunganishie mtuletee uchumi, hilo ni la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu barabara. Barabara ya kutoka Tarime kwenda Serengeti ni barabara muhimu. Wote mnajua watu wa Serengeti chakula wanachokula kinatoka Tarime na hii barabara bahati nzuri inapita kutoka Tarime Mjini inakwenda inapita Nyamongo, mnakochukua mawe ya pesa, lakini mnataka wale watu waendeleo kufa na vumbi, wakati dhahabu yao mnachukua, na kila siku wanapigwa risasi na jana walipigwa risasi pale, hata kuwapelekea barabara, hamuoni aibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarime nzima hakuna hata mita moja ya lami ambayo mmetujengea pale, wakati madini yanatoka pale. Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri aje atujibu, hii barabara ndiyo inalisha watu wa Musoma, ndiyo inalisha Bunda, ndiyo inaleta ndizi Mwanza, tofauti na zile zinazotoka Kagera. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kujibu atuambie na hili siyo la kwangu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati akihutubia Nyamwaga na wakati akihutubia Nyamongo, aliwaahidi watu hawa barabara hii ya lami ya kutoka Tarime mpaka Serengeti. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vingine vinafanyika unashangaa, nimeona hapo mnafumua barabara ya lami hapa Dodoma, yaani watu wengine wanalala porini siku hata 10 hawana hata barabara mbovu, hiyo mnafumua eti imetoboka, mnaweka lami mpya. Hivi haya maamuzi mnayafanya mkiwa wapi? Kwa nini mnafanya maamuzi ya aina hii? Tunahitaji mje mtuambie majibu hapa, ni kwa vipi watu hawa wanapata barabara nzuri ya kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Ndege; nchi hii ni miongoni mwa nchi zinazotia aibu kweli kweli, karibu kwenye kila kitu, leo Rwanda nchi ambayo hailingani hata na Mkoa wa Mara, ina ndege zinaruka dunia nzima. Sisi ndege yetu ni *Fast Jet* ambayo hata Waziri anajua ukienda hata na begi unalipishwa. Nimelipishwa begi shilingi 200,000 kwenye ndege, Taifa halina hata ndege ya kuruka ndani kwa ndani hapa, acha kwenda Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 55 ya uhuru hatuna ndege, sasa Waziri anakuja kutuambia hapa kwamba watanunua ndege, mtazitunza vipi, wakati watu wanahujumu, wanauza ndege ambazo zingefanya kazi wanauzia *trip ma-fast jet*, sijui wanahongwa. Kuna watu wako pale *Air Tanzania* wanakaa kwenye ofisi asubuhi mpaka jioni wanasubiri mshahara, halafu hawafanyi kazi, aibu, yaani hawarushi ndege hata moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mhasibu, kuna *Engineer* sijui kuna *pilot* sijui wanarushwa popo mle ndani? Labda kuna popo wanaendesha mle, wanaruka mle ndani, ndiyo ma-*pilot* wa hao popo. Ya kwanza au ya pili?

WABUNGE FULANI: Ya kwanza.

MHE. JOHN W. HECHE: Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, anapokuja hapa utoe majibu kwa Watanzania, ni kwa vipi au wana mpango gani wa kwenda kufufua Shirika la Ndege na lirushe ndege kwa nchi nzima. Kwa nchi ambayo tuna Maziwa tuna kila kitu, ndege haiwezi kuwa anasa kwa Watanzania kusafiria. Haya ni majibu ambayo Watanzania wanahitaji na tunahitaji kuyasikia hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana bajeti ya nchi yetu imekuwa ni *formality* tu; watu wanakuja hapa wanapiga kelele, mwaka baada ya mwaka, kuwa Serikalini, liwe jipu ni la CCM, uwe usaha ni wa CCM, viwe vyombo vya kutumbulia ni vya CCM, hatuna sababu yoyote ya kutetea majipu, yaani haipo kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema, ni kwa nini mpaka sasa watu wa *TANROADS* ambapo hata mtoto anajua wamejenga barabara ambazo ni sawasawa na zile sahani tunazotumia kwenye hoteli zile *disposable* yaani barabara ukipiga teke hivi lami inaruka juu. Wamejenga barabara za kiwango kibovu cha aina hiyo, lakini mpaka sasa hatujasikia hata mtu mmoja ametumbuliwa kutoka *TANROADS* au ni kwa sababu mkubwa ambaye mmesema asiguswe humu alikuwa hapo? Hivi anashindwa vipi kuungamanishwa na hilo? Leo mmetumbua mpaka watu wa nyuki lakini watu wa *TANROADS* hatujaona wakitumbuliwa. Hatuwachochei mtumbue, tunataka mtumbue waliokosea. (Makofi/Kicheko)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Heche muda wako umeisha.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa anafuatia Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud ajiandae.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi. Kwanza mimi natoa pongezi sana kwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wote. Kusema kweli tunachotaka sasa ni Serikali kuipa fedha zote Wizara hii ili ikatekeleze mipango kama ilivyo kwenye bajeti yao. Mimi katika mkoa wangu wa Rukwa hasa Wilaya ya Nkasi nimeshukuru sana, miaka sita barabara yetu toka Sumbawanga - Mpanda ilikuwa haijakamilika kwa bajeti hii naona barabara Disemba itakuwa lami tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilikuwa napiga kelele sana kuhusu shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kwenda kukamilisha Bandari ya Kipili. Leo naona kwenye bajeti kuna pesa ya kutosha kwa ajili ya kutengeneza barabara mpaka Bandari ya Kipili. Naipongeza sana Serikali na Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe masikitiko yangu makubwa, alipokuwa hapa ndani, leo ni Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli alikuwa Waziri wa Ujenzi, aliniahidi barabara ya kutoka Kirando - Kazovu - Korongwe na shahidi ni Alhaji Iyombe alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na alikubali kunisaidia. Wakati wa kampeni zake tena alipokuwa Namanyere aliniahidi hii barabara atanisaidia. Vilevile aliahidi kwamba Namanyere Mjini atanipa pesa za kilometa tatu za barabara ya lami, lakini sikuona humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusu usafiri *Lake Tanganyika*. Awamu ya Nne tuliahidiwa meli mbili, Awamu ya Tano hakuna cha meli, ni utengenezaji wa Liemba kwa shilingi bilioni 5.6. Ndugu zangu, tuliahidiwa meli moja leo hamna meli ni matengenezo, tuna meli kule MV Mwongozo haitajwi kabisa, ilikuwa pacha pamoja na ile iliyozama kule Bukoba, zilitengenezwa siku moja...

MBUNGE FULANI: MV Bukoba.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Ndiyo MV Bukoba, lakini sisi ile meli tunayo mpaka sasa, haina matengenezo haina chochote imekaa pale Kigoma kazi yake kukodishwa na wafanyabiashara kidogo kidogo haijulikani inafanya kazi gani. Tunaomba Serikali kama haina pesa za kutosha ya kununua meli mpya

iifanyie ukarabati wa hali ya juu MV Mwongozo ili iweze kuwahudumia wananchi wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kibaya zaidi ni kuhusu wafanyakazi wa Liemba, hii *Marine Service* inatesa watumishi. Mpaka leo mshahara wa mwezi wa nne wafanyakazi wa Liemba hawajapata, hawana bima ya afya, hawana hela ya likizo hata waliostaafu hawajalipwa mafao yao mpaka leo. Hata meli ya mtu binafsi ungesikia kelele, hii siyo meli siyo chochote na wakati wowote inaweza kutokea ajali maana hata *engine* zake zinazimika mara kwa mara ndani ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru sana Serikali, nilipiga kelele tokea bajeti ya kwanza kuhusu Bandari ndogo ya Kabwe lakini kwenye bajeti hii nimeona kwamba itaanza kutengenezwa mwezi Julai. Naomba Mheshimiwa Waziri hicho kipindi cha mwezi Julai itakuwa Bunge hapa hakuna na mimi nitakuwa Kabwe, nataka nihakikishe huo mwezi Julai bandari ya Kabwe imeanza kutengenezwa kama ulivyoahidi kwenye bajeti yako. Maana bajeti ya mwaka 2015/2016 zilitengwa shilingi bilioni moja kwenye bajeti kwa ajili ya Bandari ndogo ya Kabwe lakini sikuona chochote mnasema tu vifaa vimeshawasili Dar es Salaam. Mmesema bandari ya Kabwe na Lagosa zitaanza kujengwa mwezi Julai na kipindi hicho Mheshimiwa Waziri tutakuwa huko, nitakuwa kwenye jimbo langu nihakikishe bandari ya Kabwe imeanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Serikali ni yetu wote, kuna mikoa hapa inapendelewa siyo uongo na ni mikoa ambayo iko mbele ukienda utafikiri uko Durban au uko Johannesburg na sisi wengine hata barabara za vumbi hatuna. Kuna watu wanadai viwanja vya ndege, kuna watu wanadai barabara za lami, sisi tunataka barabara za vumbi. Katika hayo maombi 3,000 watu walioomba kuhamisha barabara kutoka halmashauri kwenda *TANROADS*, lazima tufikirie mikoa mingapi ina lami, mingapi ina barabara za *TANROADS* ili tuinue mikoa ambayo iko nyuma kabisa. Kuna mikoa mingine iko kama peponi, leo unakuja kusema hapa maneno ya ajabu ajabu sijui kisungura na kadhalika, tuangalie mikoa hii.

Ndugu zangu, nchi hii tumetembea kila kona, labda ninyi hamjakwenda mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma mkaangalia jinsi tulivyokuwa nyuma katika suala la barabara...

MBUNGE FULANI: Na Simiyu.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Nendeni Simiyu, ninyi mnataka mpaka lami ziwafikie kwenye majumba yenu binafsi, hilo Mheshimiwa Waziri hatutalikubali. Ni

lazima tuangalie upya mkoa upi una kilometa nyingi za lami, una kilometa nyingi za TANROADS ili na sisi mkoa mingine bajeti iende kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wilaya nyingine zina lami mpaka kwenye mitaa, miji yao ina lami makao makuu ya Wilaya...

MBUNGE FULANI: Sema.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Lakini Wilaya nyingine hazina lami hata kilometa moja. Ni kweli, mwenzangu ametoka kuzungumzia hapa, utashangaa, unabandua lami unabandika lami wakati zina mashimo, sisi wengine za vumbi hatuna. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa, toka Kirando kwenda Kazovu kuna vijiji zaidi ya sita mpaka Korongwe, tangu uhuru hawajaona hata bajaji. Wananchi wanapata taabu, Ziwa Tanganyika likichafuka mitumbwi inazama, akina mama wanakufa hawana njia nyingine ya usafiri ni kwa mguu au kwa mitumbwi, *Lake Tanganyika* wimbi lake ni la ajabu utashangaa mwenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Waziri aachane na wanaoomba viwanja vya ndege ndugu zangu hata abiria hakuna, wanapanda Wabunge, nilizungumze hapa, wanapanda Wabunge baada ya Ubunge kuisha hata tiketi hawakati, leo wanaomba viwanja vya ndege kila Wilaya atapanda nani. Akina mama na bibi zetu wanapanda magari, wanapanda treni, leo mnakwenda kuchukua mabilioni ya hela, tuchukue mfano kidogo wa uwanja wa ndege wa Mpanda nani anautumia? Tuseme ukweli nani anautumia uwanja wa ndege ya Mpanda, kuna ndege ya abiria inayokwenda Mpanda? Nimekwenda Tabora na ndege hakuna abiria anayepanda wala anayeshuka, Tabora hapo ndiyo mji mkubwa, leo unaomba kiwanja wakati abiria hakuna. Watu wa Tabora wanataka reli, watu wa Mpanda wanataka reli siyo viwanja vya ndege. Tusiwe tunadanganyana hapa, tugawane sawa hiyo keki. Mnabandua lami, mnabandika lami wengine hawajaona hata lami, ndugu zangu tunakwenda wapi, tuoneane huruma. Wengine nchi hii mpaka leo wanatembea kwa mguu hawana barabara, wewe unaomba kiwanja cha ndege, ndugu zangu, huoni hata aibu! Unakuja kuzungumza uwanja wa ndege mbele ya Bunge, mbele ya nchi hii wakati wenzako hawana barabara! (Kicheko/Makofi)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Aah, utajua mwenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Keissy, naomba ukae. Mheshimiwa Heche taarifa.

TAARIFA

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Keissy kwamba huu uchumi wa viwanda wanaousema na wazungu kuja hapa, watapanda hizo bajaji anazosema kwenda kule Rukwa? (Makofi)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi ninaosema reli ndiyo itakayotuletea uchumi, siyo ndege. Hayo makontena ya vifaa vya viwanda itapakia ndege? Wewe mwenyewe umelalamika ndege wanatoza shilingi 200,000 sanduku, ndege gani si unadanganya Bunge hapa, hakuna kitu kama hicho. *FastJet* bei yake ni rahisi kuliko ndege zote hapa leo unataka kuwapakazia *FastJet* begi shilingi 400,000 begi gani hilo jeneza? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari, bandari yetu inatuletea msongamano mkubwa Dar es Salaam inatumiwa na nchi nyingi. Tuliomba bandari ya nchi kavu na kuokoa msongamano, reli ichukue mizigo mpaka Kibaha kule mbali au Chalinze ili magari yote ya kutoka nchi jirani yabebe mzigo kwenda nje. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Sawa sawa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Kwa kufanya hivyo, tutaondoa msongamano katika Jiji letu la Dar es Salaam. Hizi *flyovers* mnazoweka, sijui mnapanda mabasi yaendayo kasi haitasaidia kama bado mizigo inakwenda kuchukuliwa bandarini na magari makubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mafuta lazima kuwe na mpango ili bomba la mafuta liende mbali kidogo na Dar es Salaam ili magari yote yakachukulie huko mafuta kwenda nchi za nje. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Sawa sawa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Bila kufanya hivyo msongamano utaendelea kuwa pale, magari kutoka bandari kupitia *Mandela road* ni foleni ya ajabu, saa tatu mpaka nne ni foleni, ndugu zangu tunapoteza muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri fanya kazi yako, wewe ni Waziri mzuri unafanya kazi, usitishwe na mtu yeyote, endelea kusaidia sehemu ambazo hazina barabara, hazina mawasiliano, lakini kusema mimi nataka

uwanja wa ndege achana na viwanja vya ndege, achana kabisa havina maendeleo kwa nchi yetu bado changa vilivyopo vinatosha. Tuendeleo na viwanja vya Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Kigoma pembezoni kule vinatosha lakini vingine vya katikati ndugu zangu ni kupoteza wakati hakuna abiria, nimefanya utafiti hakuna abiria. Sisi wa kule Sumbawanga kiwanja cha Mbeya kinatosha sana, tusidanganye. Tunakwenda na ndege *FastJet* asubuhi abiria hawajahi, leo unataka kiwanja kijengwe Sumbawanga, Mpanda, Mbozi, Kibaha, ndugu zangu hela zitatoka wapi? Tuendeleo kujenga barabara na reli ili nchi yetu itoke katika uchumi huu uende uchumi wa mbele, tusidanganyane! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani unakuwa Mbunge hapa unasema Morogoro wanataka kiwanja cha ndege, Tabora uwanja wa ndege, dai gauge Tabora reli itakusaidia. *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Tarime.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Tarime uwanja wa ndege, utapanda wewe peke yako Mbunge? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri ahadi ya Rais alipokuwa Waziri alinahidi hapa akatuma na wataalam kwenda kukagua barabara kilometa 35 tu, alinahidi atanisaidia alipokuwa Waziri na alipokuwa Rais, nakuomba itekelezwe. Shahidi ni Mheshimiwa Mzee Lukuvi alikuwa anaambatana naye na yuko humu alinahidi kujenga hiyo barabara. Kwa hiyo, naomba hiyo barabara tafuta hela popote ikatengenezwe kusaidia watu wa Kazovu na Korongwe.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ujumbe wangu umefika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Keissy. Tunaendelea na Mheshimiwa Kanali Masoud na Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae.

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri inayoonesha mwelekeo mzuri wa kuletea

maendeleo Taifa letu. Pia nimpe changamoto kwamba ajitahidi kwa sababu Wizara hii ndiyo Wizara ambayo iko kwenye kioo cha kila mtu. Kwa hiyo, akifanya kweli ataonekana na asipofanya ataonekana hata kabla ya kuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuchangia kuhusu hali ya anga la Tanzania. Kwa uono wangu kimataifa tunajulikana Tanzania tuna anga la Tanzania, hakuna anga la Zanzibar wala anga la Tanzania Bara. Hivyo basi, ni muhimu tunavyotoa huduma za anga tuzijenge kulenga kufanikisha kwa sifa ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na mawasiliano ya muda mrefu kati ya TCAA na Mamlaka ya Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar. Kiwanja hiki kwa muda mrefu hakijafungwa kifaa cha *Instrument Landing System (ILS)* ambacho kilikuwa kifungwe kipindi cha miaka minne, mitano iliyopita, kila siku ahadi inakuwa kitakufungwa. Kweli huduma za ndege zinaendelea lakini hiki ni kifaa muhimu kinachowasaidia marubani kutua wakati wa usiku, mawingu na mvua kwa uhakika na usalama zaidi.

Niombe basi Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie kama hili jukumu si la TCAA, ni bora watoe kauli dhahiri inayosema kwamba hiki kifaa hawatakiunga na hakiwahusu ili sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iweze kuchukua jukumu la kutafuta hicho kifaa na kukifunga kwenye uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vizuri vitu kama hivi vikawa vinatupwa kama mpira. Ni bora kuambizana ukweli ili kila mtu afahamu jukumu lake, lakini litekelezwe ili kuleta ufanisi wa kazi tunazozifanya za kila siku. Tukipata sifa ya anga, nasema mara ya pili, ni sifa ya Tanzania na likitokea tatizo bado mamlaka hizi zitahusika na kutakiwa kujibu maswali ambayo kwa kweli nahisi hayatakuwa muhimu na ya msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nichangie hilo lakini nimkumbushe Mheshimiwa Waziri akisaidie kiwanja hiki cha ndege cha Zanzibar. Nakumbuka lilitolewa jibu lakini nimsisitize tu awasaidie kulipwa lile deni lao la shilingi milioni 230 na ATC. Tunasikia au tumeambiwa madeni yatahamishiwa Hazina, lakini nimuombe tu alipe uzito ili kuwasaidia wenzetu hawa kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba dakika tano na nahisi zimenitoshwa kwa kuchangia jambo hili muhimu sana. Na mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kanali Masoud. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi na nianze na kumshukuru Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Rais alipokuja kutafuta kura moja ya jambo alituhidi pale ilikuwa ni barabara ya Mwandiga - Chankele – Kagunga. Naomba atakapokuja kujibu hoja utuambie *status* ya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Rais alipokuwa Simbo alisema atatupa kilometa kumi za lami kutoka Simbo – Ilagala. Naomba Waziri atakapokuja kujibu hoja napo utusaidie *status* ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mheshimiwa Rais aliongelea suala la kuwalipa fidia wale ambao hawakulipwa kwenye barabara ya Mwandiga - Manyovu. Nalo naomba kujua *status* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nataka nipate *status* ya gati la Kagunga na watu wanaolipwa fidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ambalo leo nadhani nitatumia muda wangu mrefu ni suala la viwanja vya ndege na ATC pamoja na reli. Reli ndiyo inayoweza kukuza uchumi wetu kwa haraka sana. Mimi naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kama kuna jambo ambalo Rais Magufuli ataenda kwenye historia ya miaka 100 ni kujenga reli kwa kiwango cha *standard gauge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la reli ni *legacy* ya Rais Magufuli. Mimi namuomba Waziri, *unless* hataki tuandike *legacy* ya Mheshimiwa Rais Magufuli, naomba tujenge reli ya kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Mwanza, kutoka Tabora kwenda mpaka Kigoma, kutoka Isaka kwenda Keza, kutoka Kaliua kwenda Mpanda, Mpanda kwenda Karema na Uvinza kwenda Msongati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tubadili tabia, tukienda kwa hali hii tutaongea tutamaliza miaka mitano hatujaanza kujenga. Nchi zinazotuzunguka za Afrika, Kenya ilikuwa ni jambo la siku mbili, tatu leo wanajenga reli yao, Uganda nao wanajenga, Ethiopia wamejenga, Senegal wamejenga na wote hawa wamekwenda China kuchukua fedha. Naomba sana Mheshimiwa Waziri najua atasema ameweka shilingi trilioni moja, trilioni moja huwezi kujenga reli hii. Ni matarajio yangu shilingi trilioni moja hii ni sehemu ya fedha ya Serikali kama mchango wetu kwenye huo mpango mkubwa zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawaombeni watu wa Wizara, Rais Magufuli tutamtofautisha na Marais wote tukijenga reli. Akijenga barabara na

Kikwete alijenga, Marais wote walijenga barabara. Tunachotaka Rais Magufuli fanyeni kila mnaloweza tuache longolongo tujenge reli kwa *standard gauge*. Naomba Waziri unapokuja kujibu hapa atuambie jambo ambalo linaeleweka. Kama anakuja anasema anataka watu washindane, naombeni tusiwe wafungwa wa sheria zetu, hili suala ni la uchumi, ni la maendeleo, naomba tujenga reli ya kati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ndege, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri ameanza kutengeneza ndege, lakini naomba tuseme tunataka kujenga *airline* ya namna gani? Kama tunataka kujenga *airline* kwanza lazima tuje na Shirika la Ndege ambalo ni imara. Wengine wanasema hamna wapanda ndege, ngojeni niwaambieni, tukiweka viwanja vya ndege mikoa yote, bei za ndege zitashuka na watu wote watapanda ndege. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena mimi nachosema mikoa ambayo imeanza juzi ya Geita, Simiyu, Katavi, Songwe tujenge viwanja vya ndege. Viwanja vya Bukoba, Kigoma, Tabora, Singida, Dodoma vyote vijengwe. Tukishakuwa na viwanja tukawa na *network*, hilo shirika letu la ndege la ATC likawa lina-*fly* mikoa yote, kitakachotokea bei zitashuka, watu wengi watapanda ndege na shirika hili litapata faida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikoa lazima tujenge viwanja vya ndege, hiyo mikoa mipya ya wenzetu, Shinyanga tujenge, kiwanja cha Mwanza ni muhimu sana, tupanue kiwanja cha Kigoma na tupanue kiwanja cha Tabora. Kwa kufanya hivyo, tunayo hakika hili shirika tunalotaka kutengeneza litakuwa na maana na litatupeleka mbele tutapata faida. Kama unaleta shirika la ndege unataka ukashindane na mashirika yaliyoanza muda mrefu umeanza na kushindwa. Lazima tuanze kwanza ndani ili kama walivyosema wenzangu, leo unakwenda unapanda *FastJet* kweli inaonekana bei rahisi lakini ukiwa na begi unalipa shilingi 100,000 au shilingi 200,000 inawezekanaje? Siyo ndege rahisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tiketi yenyewe wanakuambia labda ni shilingi 90,000, unakuta tiketi za bei hiyo ni nne au tano nyingine zote ni za shilingi 400,000 mpaka shilingi 500,000, ni kwa sababu hatuna ushindani. Anayeweza kuleta ushindani ni shirika letu la ndege. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la minara vijijini. Nimesoma hapa suala la UCSAF naona Wazri sasa hivi halichangamkii sana. Tulianzisha sheria hapa, tukasema tuweke huko ili UCSAF wapeleke minara vijijini. Haiwezekani minara tukaletewa na hawa Halotel, Halotel ni wafanyabiashara kama yalivyo makampuni mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni kama Serikali tuendeleze mipango yetu ya kuhakikisha tunawapa fedha watu wa UCSAF ili kasi ya kuleta minara iwe kubwa. Mheshimiwa Waziri anajua kuna vijiji vyangu vya Kata ya Ziwani, vijiji vyote saba hakuna minara na tumelisema hili, tunaomba sasa lifanyiwe kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la bandari ya Dar es Salaam. Kuna kitu kinaitwa VAT kwenye *transit cargo*, Waziri najua atajibu atasema VAT haitozwi lakini kwenye sheria ipo, tuliipitisha mwaka jana kwenye *Finance Act*. Kwa sababu tuliipitisha mwaka jana, yule anayetaka kutumia bandari ya Dar es Salaam anachukua sheria, una muda gani kwenda kumwambia hatutozi. Tuitoe kwenye sheria ili wajue hakuna VAT kwenye *transit cargo*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ni ushindani, naombeni sana tuiache bandari ya Dar es Salaam ifanye biashara kama biashara zingine zozote duniani. Kama kuna sehemu tunatakiwa tusiweke siasa ni kwenye bandari ya Dar es Salaam. Tumecheza na siasa, tulianza mwaka 2008 tunaongelea habari ya gati 13 na 14 leo ni mwaka 2016 hatujajenga. Tulikwenda China na watu wa Mombasa, Mombasa wameshamaliza kujenga wanaanza kwenda Lamu, sisi bado tunajiliza tu tutumie *modal* gani. Nadhani muda umetoshwa, nakuomba sana Waziri umefika wakati tuache siasa kwenye suala la bandari ya Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ya Dar es Salaam lazima itafute masoko, lazima waende huko kwenye masoko wakaiuze bandari. Naombeni muondoe urasimu ili watu wa masoko waende huko, ndiyo kazi yao kwa sababu tunashinda, mzigo wenyewe siyo mwingi sana duniani. Ni kweli sasa hivi kuna *downturn* ya *economy* duniani, mzigo umeshuka lakini sisi hata kama mzigo umeshuka duniani lazima kuwe na sababu za kwetu, kama sisi hatutekelezi majukumu yetu kwetu utashuka zaidi na Mungu ametupa bandari hii tuitumie kwa maendeleo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri atakapokujibu hoja atuambie kwa uhakika tuweze kumwelewa lini tunaanza ujenzi wa reli ya kati? Lini tunaanza kuandika historia ya Rais Magufuli ya miaka 100 ijayo ya kujenga reli ya *standard gauge*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Serukamba. Sasa hivi anafuata Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea machache kuhusu bajeti iliyokuwa mbele yetu. Naomba niingie moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanategemea reli hususani mkoa wangu wa Katavi na Wilaya ya Mpanda. Alikuwepo Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Arfi, alikuwa anatetea sana reli ya kutoka Tabora - Mpanda. Mimi kila siku najiuliza Wabunge humu ndani wanazungumza kuhusu reli, lakini utekelezaji wake haupo. Mheshimiwa Arfi alivyokuwepo humu ndani alikuwa anazungumza kila siku, reli ya Mpanda - Tabora siyo salama. Mpaka leo reli ya Mpanda - Tabora ina *pounds* 40 na reli hiyo inabeba mizigo mingi, inaiitea pesa nyingi Serikali na wananchi wa Mpanda wanategemea reli lakini mpaka leo reli ile wala hajishughulikiwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unasikia kuna sehemu reli zinang'olewa zinapachikwa *pound* nyingine. Sasa najiuliza zile *pound* zinatoka zinakwenda wapi? Hivi karibuni walizing'oa *pound* 60 Tura, sasa zile zilipelekwa wapi? Badala ya kutolewa pale na kupelekwa sehemu ambapo kuna *pound* ndogo ili reli yake iweze kuimarishawa lakini ndugu zangu hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku wananchi wa Mpanda tunalalamika kuwa hatuna barabara, tunategemea reli na ndiyo maana Wabunge wengi wanasema RAHCO na TRL waunganishwe hili shirika lingine life kwa sababu hawana faida. Kuna *pound* zingine wameziacha pale makao makuu, *pound* 80 zimekaa hawajui kama wananchi wengine wanahitaji hizo *pound*, sasa wana maana gani? Hii RAHCO tunaomba Serikali sheria ilikuja Bungeni na ikaunganisha RAHCO na TRL, sasa sheria hiyo ije tena tutenganisha Shirika la RAHCO pamoja na TRL, sheria hiyo ije tena tupangue tuunganishe hili shirika liwe moja. Kwanza ukiangalia wanapewa hela nyingi halafu vitu vyake havieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka mnasikia Godegode kuna matatizo, treni inaanzia Dodoma, ina maana Serikali mpaka leo haina ufumbuzi wa tatizo la pale Godegode? Kila siku Godegode treni imeishia Dodoma, Godegode treni imeishia Dar es Salaam, Godegode kuna mafuriko. Mnajua kabisa Godegode tatizo, kwa nini msichukue hatua za kurekebisha kwa sababu treni inayotoka Dar es Salaam – Mwanza – Kigoma - Mpanda inabeba abiria wengi sana na wananchi wengi maskini wanategemea reli, kwa nini hapo Godegode hapashughulikiwi, kila siku Godegode shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwanza Kaimu Mkurugenzi mpya, nashangaa kwa nini hawampi ukurugenzi, amethubutu safari hii, wananchi wamekwama njiani na treni amechukua chakula yeye kama yeye kuwapelekea wananchi. Tunaomba hawa Wakurugenzi ambao wanao

uthubutu wapewe ukurugenzi. Kitu cha kushangaza, mimi naomba niseme, leo hii mashirika yote makubwa, bandari Mkurugenzi Kaimu, uwanja wa ndege Mkurugenzi Kaimu, TRL Mkurugenzi Kaimu, wapeni ukurugenzi kamili ili waweze kufanya kazi nzuri, wameweza kuthubutu hawa wapeni basi ukurugenzi waweze kufanya kazi vizuri. Mnavyowaacha na ukaimu wanafanya kazi kwa wasiwasi, wapeni mamlaka ili waweze kutekeleza yale mliyowakabidhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri akija hapa aniambie kabla ya *standard gauge* haijaanza maana haya ni majaliwa, Mbunge ametoka hapa kusema hayo ni majaliwa, tunaomba kujua reli ya kutoka Tabora - Mpanda mtatubadilishia lini zile *pound* 40 iwe angalau tu 60 ili ile reli iweze kuwa *stable*. Kwa sababu wananchi wa Mpanda wapo rehani huku barabara ikiziba huku treni wasiwasi. Kabla *standard gauge* haijaanza tunaomba uimarishaji wa reli ya kutoka Tabora - Mpanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaenda kwenye *standard gauge* na tumesema inafika mpaka Karema, Karema tunategemea bandari, lakini hatujaona mwamko wowote wa bandari Karema. Naomba hii mikakati ianze ili wale wananchi wa Karema waone kama na wenyewe wapo Tanzania kwa hii bandari inayopelekwa huko kwa ajili ya *standard gauge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja darala la Kavuu; kuhusiana na barabara ya kutoka Inyonga – Majimoto, hii ni Wilaya mpya. Wananchi kutoka Mpimbwe huko Majimoto, Kibaoni, Usevya, Kasansa mpaka wafike makao makuu yao ya Wilaya Inyonga wanatembea siku mbili. Mtu anatoka Kasansa aje Mpanda alale kesho yake aondoke aende Inyonga, hiyo ni Wilaya au kitu gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge wengine hapa wamesema kuhusu masuala ya barabara, hili daraja la Kavuu limechukua miaka saba. Hebu jamani mtuangelie watu wa mkoa wa Katavi, kila siku tunazungumza, tunaomba hili daraja liishe ili wananchi wa upande wa Kibaoni, Usevya, Kasansa waweze kufika kwenye makao makuu yao ya Wilaya siku moja. Tunaomba chonde Waziri akija hapo atuambie daraja la Kavuu litaisha lini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza ile barabara ya kutoka Stalike - Mpanda na nikasema pale Mpanda kuna shimo, lile shimo linaisha lini? Ni kero kwa wananchi wa Mpanda, kila siku ajali zinatokea. Nilizungumza Januari lakini mpaka leo hakuna mkandarasi, hakuna kitu chochote, kila kitu kipo vilevile. Tunazungumza mpaka lini? (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante muda wako umeisha.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Joseph Mkundi ajiandae.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia afya na uzima na kuweza kupata nguvu ya kuweza kuwawakilisha wananchi wangu wa Jimbo Mtwara Vijijini na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla na Watanzania.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya kwa sababu Wizara hii ni zaidi ya Wizara tatu kama tulivyozoea kuziona, lakini nina imani kabisa kwamba ataweza kuzimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kile kitendawili chetu cha wananchi wa mkoa wa Mtwara kuhusu barabara yetu ya uchumi angalau mwaka huu tunazona kilometa 50 zikiwa zimetengewa pesa. Ametuhakikishia kwamba kilometa hizo 50 kutoka Mtwara mpaka Mnivata ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2016/2017. Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa ningependa tu kusisitiza, Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati anaomba kura alituhidi akishinda zile kilometa 159 zinazobaki kutoka Mtwara - Newala - Masasi watagaiwa wakandarasi kilometa zote ili ujenzi uweze kukamilika kwa wakati. Mheshimiwa Waziri nitapenda wakati unatoa ufafanuzi utuelezee utaratibu uliopo kwa zile kilometa ambazo zimebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda pia nilizungumzie ni kuunganisha barabara zetu za mkoa na mkoa lakini pia kuunganisha nchi na nchi. Mheshimiwa Waziri tunazo barabara zetu zinazotuunganisha Mtwara na majirani zetu wa Msumbiji, kutoka Mtwara - Kilambo na kutoka Mtwara - Msimbati kimekuwa kilio cha muda mrefu, tumekuwa tukiomba zijengwe kwa kiwango cha lami kama ambavyo mipaka mingine yote inaungwanishwa. Kwa hiyo, nitataka kusikia ni lini mkoa wa Mtwara utaunganishwa na Msumbiji kupitia kivuko cha Kilambo na Msimbati kwa kujengwa kwa kiwango cha lami hasa ukizingatia kwamba Msimbati ndiko ambako gesi inatoka na tuna vitega uchumi vyetu vingi kule vya thamani ambavyo kwa kweli lazima tujenge

barabara ya uhakika ambapo tutaweza tukaenda wakati wowote bila kujali mvua au jua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni bandari. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 tuliambiwa kwamba majadiliano na wawekezaji upande wa Mtwara yamekamilika kwa ajili ya kujenga gati nne katika bandari ya Mtwara, leo Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba majadiliano yale ambayo tuliambiwa yamekamilika hayakufanikiwa na badala yake inataka kujengwa gati moja yenye mita 350, hatukatai sawa lakini lengo lilikuwa ni gati nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utafiti wa gesi unaoendelea kule; zao letu la korosho na viwanda vingi ambavyo vinakwenda kule ikiwemo vya mbolea na hivyo vya kina Dangote kwa bandari iliyopo sasa hivi haitoshelezi na wakati mwingine inaleta usumbufu mkubwa sana hasa katika kusafirisha zao letu la korosho. Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Waziri atuambie gati zingine tatu zilizobaki mpango ukoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunalo eneo la Kisiwa na Mgau ambapo eneo lingine tumempa Mheshimiwa Aliko Dangote ili ajenge bandari kwa ajili ya kusafirisha saruji na eneo lingine bandari yenyewe iliamua kuchukua kwa ajili ya kujenga bandari yake. Tathmini imeshafanyika, sasa hivi imebaki ni hadithi kesho, kesho kutwa. Amekuja Mheshimiwa Waziri Mkuu kule tuliambiwa baada ya siku tano fidia awamu ya pili italipwa. Lile eneo ambalo Dangote amepewa fidia ilishalipwa imekamilika, eneo ambalo bandari wamechukua kwa nini hamlipi? Dangote ameshalipa, wananchi wameshatumia pesa zao lakini wale ambao wanapaswa kulipwa na Mamlaka ya Bandari imebaki danadana. Sasa mnawagombanisha, kwa nini upande wa Dangote walipwe na upande wa bandari hamtaki kuwalipa?

Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri aje aseme ni lini watalipwa kwa sababu kila siku maelezo ni kwamba wanasubiri Bodi ya Bandari iundwe ili iweze kuridhia zile pesa kwa sababu pesa za kulipa fidia zipo shilingi bilioni 13, hiyo Bodi ya Bandari inaundwa lini ili mambo yaende? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulichangia ni kuhusu reli ya kutoka Mtwara - Songea - Mbamba Bay. Nimeona katika hotuba kwamba upembuzi yakinifu na usanifu umekamilika Februari 2016. Napenda kufahamu ujenzi wa reli hiyo ya kutoka Mtwara - Mbamba Bay na matawi yake ya kwenda Liganga na Mchuchuma utanza lini? Kwa sababu uwekezaji unaofanyika kule Liganga na Mchuchuma, makaa ya mawe yaliyoko Ngaka bila kuwa na reli mradi ule Mheshimiwa Waziri itakuwa ni hadithi. Naomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie ujenzi wa reli kutoka Mtwara - Mbamba Bay na matawi yake yanayokwenda Liganga na Mchuchuma utakamilika lini kwa

ajili ya kusafirisha makaa ya mawe na chuma kwenda katika bandari yetu ya Mtwara huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ukarabati wa uwanja wa ndege wa Mtwara. Iliwekwa katika bajeti lakini mpaka sasa hivi hakuna fedha iliyotoka hata kidogo. Pia tuliambiwa uwanja ule utawekewa taa, mpaka sasa hivi taa hakuna. Tunachofanya pale ni kuazima taa za muda za wenzetu wa BG, hivi siku BG wakitukakatalia tunafanya nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutonana na utafiti na uchimbaji wa gesi na mambo yanayoendelea kule Mtwara, kwa kweli ni lazima ule uwanja upate taa na ukarabatiwe. Uwanja ule ulijengwa mwaka 1965, hata mimi sijazaliwa na nimeshafikia mahali ambapo kama ni umri naweza nikasema zaidi ya nusu labda au nusu nimeshamaliza uwanja ule haujakarabatiwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri anapokuja aje atuambie uwanja unakarabatiwa lini na unawekewa taa lini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, tunayo makampuni ya mitandao ya simu na kila mara wamekuwa wakidai kwamba wanalipa kodi ya huduma (service levy) katika Halmashauri, lakini Halmashauri zetu nyingi hazipati ushuru huu na badala yake unalipwa katika Halmashauri chache. Niiombe Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia taasisi zake ikusanye ushuru huu makao makuu na ugawanywe katika Halmashauri zote bila kujali ukubwa wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Hawa Ghasia. Sasa hivi ni zamu ya Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Magdalena Sakaya pamoja na Mheshimiwa Ezekiel Maige wajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii. Mchango wangu utakuwa kwenye maeneo kama matatu hivi. Nilitamani niongelee suala la reli lakini watu wengi wameliongelea, kwa hiyo sitaelekea huko, nitaelekea kwenye maeneo yanayohusu Jimbo langu la Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wengi mnavyojua Ukerewe inaundwa na visiwa zaidi ya 30. Mategemeo makubwa ya wananchi zaidi ya 300,000 wa Ukerewe kuunganishwa na mji wa Mwanza na maeneo mengine ni kupitia meli. Bahati mbaya usafiri wa meli kutoka Mwanza kwenda Ukerewe umekuwa na matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona hapa kuna pesa zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya meli ya MV Butiama. Suala la MV Butiama limekuwa ni wimbo wa muda mrefu sana, miaka takribani mitano usafiri ni wa shida kweli kweli kwenye eneo lile. Sijui kama Serikali inafurahi muda wote iwe inatoa rambirambi kwenye mazingira kama haya, si jambo jema sana. Yametokea maafa pale Zanzibar, yametokea maafa ya MV Bukoba, sitamani sana jambo kama lile litokee kwenye eneo la Ukerewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna meli moja MV Clarias, napenda kuwapongeza kampuni binafsi ya Nyehunge, wanatoa huduma ya usafiri pale, lakini meli zile zinazotoa usafiri bado hazitoshi, wananchi wanataabika sana kwa usafiri wa meli. Kama kwenye bajeti mmetenga hii pesa kwa ajili ya kutengeneza hii meli ya MV Butiama, itengenezwe iweze kuhudumia wananchi wale. Si hiyo tu, hata meli iliyopo sasa hivi ya MV Clarias haiwezi kumudu muda mrefu, imekuwa ni meli ya muda mrefu sana kila wakati inasumbua, inaharibika. Kwa hiyo, pendekezo langu, pamoja na kutengwa kwenye bajeti shilingi bilioni tatu na *point* kwa ajili ya marekebisho ya MV Butiama, Wizara iangalie uwezekano wa kutengeneza meli nyingine mbadala wa MV Clarias ambayo ni ya muda mrefu na imechoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niombe Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuangalia suala la uwekezaji katika visiwa hivi. Ukerewe ni eneo ambalo linaweza kutumika kwa shughuli za utalii, naomba kama kunaweza kufanyika ushawishi ufanyike au Wizara yenyewe itengeneze *speed boat* kwa ajili ya huduma za usafiri kuunganisha Mwanza na visiwa vya Ukerewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuongelea ni eneo la vivuko. Kama nilivyosema Ukerewe inaundwa na visiwa na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kwa mwaka 2015/2016 kuna vivuko kadhaa ambavyo vimefanyiwa marekebisho kikiwemo kivuko cha MV Nyerere. Sawa, lakini kuna maeneo ambayo wananchi wanataabika sana kama kwenye visiwa vya Ilugwa, Izinga na maeneo mengine, niombe Wizara itengeneze vivuko vingine kwa ajili ya kusaidia wananchi wa maeneo yale ambao wanataabika sana na usafiri kutoka kwenye visiwa vile wanavyoishi kuja kwenye kisiwa kikubwa cha Ukerewe na hatimaye kutafuta mazingira ya kusafiri kwenda Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hiki kivuko cha MV Nyerere ambacho kinafanya kazi kwenye eneo la Bugolola na Bwisa kisiwani Ukala, hivi kunakuwa na tatizo gani, kwa mfano Wizara ndiyo inayohusika na vivuko hivi na meli kutoka Mwanza kuja Nansio, ni kwa nini kusiwe na *matching* ya ratiba kwamba wasafiri wanaotoka Mwanza waweze kuingia Nansio lakini wakawahi vilevile

usafiri wa Bugolola kwenda Kisiwa cha Ukala? Sasa hivi wananchi wanataabika sana, wanatoka Mwanza wanakaa Nansio pale zaidi ya saa sita wakisubiri ratiba ya ferry ya kutoka Bugolola kwenda Ukala.

Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri, inawezekana akatoa maelezo ni kitu gani kinaweza kufanyika lakini litakuwa jambo jema sana kwa maslahi ya wananchi wa Ukerewe, hususan kwenye visiwa vya Ukala ratiba hii itawekwa sawa angalau iweze kuwiana na ratiba ya kutoka Mwanza kwenda Ukerewe.

Vilevile uangaliwe uwezekano kutengeneza vivuko vingine kwa ajili ya kusaidia wananchi kwenye visiwa vidogo vidogo vinavyounganisha Ukerewe na maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu ambalo nilitaka nigusie ni suala la barabara.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ninyi mbona hamsikilizi?

MBUNGE FULANI: Sikilizeni ninyi Mawaziri.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mnaongea ongea tu.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo sera ya Serikali hii ya kuunganisha mikoa yote ya Tanzania Bara kwa barabara za lami, kuna barabara ya kutoka Bunda – Kisolya - Nansio ambayo kimsingi inaunganisha mkoa wa Mara na Mwanza kupitia Ukerewe. Kwenye hotuba inaonekana kuna mpango wa kuendelea kujenga kati ya Bunda - Kisolya, lakini kuna kipande hapa cha kilometa 11 kutoka Lugezi kufika Nansio, ni kwa nini kipande hiki kisiunganishwe mradi huu ukakamilika wote kwa pamoja? Ni kilometa chache sana hizi, kwamba sehemu moja itengenezwa halafu hizi kilometa 11 zibaki zitafutiwe fedha nyingine au mradi mwingine ndipo ije ikamilike na barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Tunasema tunatengeza Tanzania ya viwanda, ni muhimu basi tujenge mazingira ya kiuchumi ya wananchi wetu. Kwa wananchi wa Ukerewe, kama barabara hii itatengenezwa kwa kiwango cha lami itasaidia sana mawasiliano na hasa kiuchumi kati ya wananchi wa Ukerewe, Bunda na Mwanza Mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe vilevile Wizara hii, ninaamini si eneo la Ukerewe tu, maeneo mengi barabara nyingi zimeharibika. Sasa niombe fedha za Mfuko wa Barabara ziwe zinatolewa mapema na kwa kiwango kile ambacho kinaweza kikasaidia ili Halmashauri zetu ziweze kurekebisha barabara zile zinazokuwa zimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kutokana na barabara zetu kutokuwa katika hali nzuri, Halmashauri ya Ukerewe tuliomba kununuliwa greda kwa ajili ya kutengeneza barabara na Wizara ikale greda kwenye Halmashauri ya Ukerewe. Niombe Mheshimiwa Waziri kama anaweza kunisaidia hili, lile greda Halmashauri ya Ukerewe imekuwa haina mamlaka nalo sana kiasi kwamba ikitaka kulitumia liweze kurekebisha barabara za Wilayani Ukerewe inakuwa ni shida kweli kweli kulipata wakati kimsingi Halmashauri hii ndiyo iliyo-process mpaka greda hilo likapatikana. Ni kwa nini sasa kama Wizara msitoe mamlaka, kwa sababu Halmashauri hii ndiyo iliyoanzisha mchakato mpaka greda hili kununuliwa, kwa nini lisikabidhiwe kwenye Halmashauri ile? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Ukerewe ni ngumu sana, msifananishe na maeneo mengine. Mkifanya hivi mtakuwa mmelisaidia sana eneo la Ukerewe kuboresha barabara zake na inawezekana ikapunguza gharama nyingini ambazo zingekuja kwenu Wizarani. Kwa hiyo, niwashauri kama Wizara, likabidhini greda hili kwenye Halmashauri hii ilisimamie. Kama kuna masharti na taratibu nyingine muhimu basi waelekezwe lakini greda lile liwekwe pale Halmashauri lifanye shughuli za kuboresha barabara za Ukerewe hatimaye basi mazingira ya Ukerewe yawe bora angalau ukilinganisha na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiendelea kuisitiza, niombe tafadhali, kwenye hii barabara ya Bunda – Kisolya – Nansio, haina sababu kilometa 11 hizi kuziacha, ziunganisheni. Pia kulikuwa na mpango wa kujenga daraja kati ya Lugezi - Kisolya, sijui imefikia wapi Mheshimiwa Waziri nitaomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Joseph. Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye hotuba iliyoko mbele yetu na kwa sababu ya muda nienda *straight* kwenye hoja zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tumekuwa tunatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kujenga miundombinu ya barabara, nyingine za nchi na nyingi pia za jasho la walipa kodi. Kwa bahati mbaya sana barabara hizi zimekuwa zikichukua muda mfupi sana kwa sababu kwanza viwango vya ujenzi ni dhaifu, utunzaji wake ni dhaifu lakini pia tunatumia makandarasi ambao baadhi yao hawana viwango vya kuweza kujenga barabara kwa uhakika. Badala ya kutengeneza barabara angalau tumalize miaka kumi ili tuhame kutoka eneo moja twende eneo lingine tunarudi mle mle huku maeneo mengine hayana barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge wanazungumzia juu ya kubandua barabara za lami kujenga nyingine wakati mikoa mingine wako kwenye udongo. Miaka 54 ya uhuru tunabandua lami na kurudisha lami pale pale wakati wengine wako kwenye udongo hawajui ni lini watapata barabara za lami. Kwa hiyo, tatizo kubwa ni kwamba hatusimamii vizuri barabara zetu. Ifike mahali tuwe na *standards* za ujenzi wa barabara nchi nzima. Tuamue kwamba mkandarasi ambaye anashindwa kukidhi vigezo vya matengenezo tunayoyataka asipate kandarasi. Kwa sababu ya kubeba wakandarasi mtu anaharibu huku anapelekwa kule, matokeo yake tunaingiza hasara kubwa kwa Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwenye barabara nyingi, niseme kabisa barabara zilizotengenzewa ndani ya miaka kumi ya uongozi wa Awamu ya Nne zote ziko kwenye hali mbaya. Nyingi zina mashimo mengi, nyingi zina migongo, nyingi zinaanza kuchimbika kuanzia pembeni, Awamu ya Nne barabara zote zimeharibika. Pamoja na kuwa anasifika kwamba alitengeneza barabara nyingi lakini kaziangalieni, nimefanya utafiti barabara nyingi za uongozi wa Kikwete ziko kwenye hali mbaya kwa sababu usimamizi ulikuwa mbovu. Hatuwezi kuwa na barabara za lami za kutosha kama tunashindwa kuweka *standards* kwa ajili ya barabara zetu za lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tumekuwa tunatoa fedha kidogo kidogo kwenye ujenzi wa barabara matokeo yake tunaweka vyombo vya ujenzi barabarani kwa muda mrefu na tunalipa wakandarasi waelekezi kwa muda mrefu, tunapoza fedha nyingi sana za walipa kodi kwa kitu ambacho hakitakiwi. Tunapotengeneza barabara miaka minne, mitano haijakamilika lakini vyombo vinalipiwa, mkandarasi mwelekezi analipwa, *how much are we wasting?* Ni pesa nyingi sana tunapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na utaratibu, tunapopanga kutengeneza barabara tuitengee muda, ndani ya mwaka mmoja, miwili ikamilike ili tuokoe fedha na faini tunazolipa kwa ajili ya kuweka vyombo barabarani wakati huo hatutoi fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara zile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la reli. Suala hili ni uchumi wa Taifa. Ni jambo la ajabu kwa nchi inayotegemea kilimo kwa zaidi ya asilimia 80, leo tuna reli kwanza sio za *standards*, zinabomoka kila siku, lakini kwa kiwango kidogo, ni aibu mpaka leo. Sambamba na kwenda kwenye uchumi wa viwanda, sambamba na kwenda kwenye uchumi wa kati, suala la reli halikwepeki. Kwa hiyo, katika mawazo yote ya Serikali ili tuweze kwenda pamoja lazima suala la reli lipewe kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nilianza kuumizwa na Waziri wa Fedha. Kwanza alikuja na mpango wa kwanza kwamba lazima tutengeneze reli ya kati kwa *standard gauge*, tulipokwenda Dar es Salaam kwenye semina anasema kwamba tunatafuta wabia na nchi ambazo tuna-*share* matumizi ya reli hiyo, hatuwezi kutegemea watu wa nchi nyingine, pengine kwao reli si *priority* lakini ndani ya nchi yetu reli ni *priority*. Kwa hiyo, ni lazima tujipange sisi wenyewe kuhakikisha kwamba tunajenga reli zetu? Leo tunategemea Burundi, Burundi kwake pengine reli si *priority*, au Rwanda, *it is not their priority*, au Kenya, sisi kama sisi tunafanyaje?

Kwa hiyo, suala la reli ya kati na matawi yake ina-cover karibu mikoa 15 ya nchi hii. Wengi wamezungumza kwa msisitizo tunaomba wakati wa ku-*wind up* kesho tuambiwe tarehe ya kuanza na kumaliza kujengwa reli ya kati na kwa *standard gauge*, halikwepeki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la upungufu wa mabehewa. Kuna shida kubwa ya upungufu wa mabehewa ya abiria. Reli yote hii ya kati mabehewa ni machache sana matokeo yake imeleta matatizo makubwa. Leo Wabunge walikuwa wanazungumzia suala la bei kwenda juu pamoja na kuwepo kwa walanguzi, shida kubwa ni mabehewa machache. Leo ndani ya Wilaya ya Kaliua kwenye *stop station* ya Kaliua kwa siku moja, kwanza treni ni siku mbili tu kwa wiki, lakini hiyo siku mbili eti siku kumi, *can you imagine?* Watu kumi kwenye kituo kwa wiki mara mbili! Reli iko kwenye wilaya yao, wengi hali ya uchumi ni mbaya, hawana uwezo wa kutumia 50,000, 60,000 kwa basi angalau reli ndicho chombo chao wanaambiwa siti kumi. Matokeo yake watu ambao si wasafiri na wanakwenda na vitambulisho wananunua wanakwenda kuziua mitaani kwa wale wasafiri. Matokeo yake mtu badala ya kununua tiketi shilingi 23,000 ananunua shilingi 40,000 na huwezi kuzuia kwa sababu mabehewa ni machache. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Waziri, amesema ameongeza mabehewa, lakini mengi ni ya mizigo, mabehewa ya mizigo kutoka 530 mpaka 704, lakini suala la mabehewa ya abiria ni shida kubwa. Pia tuongeze angalau *route*. Kwa kweli ni jambo la ajabu kuambiwa kwamba Wilaya ya Kaliua reli yote ya kati kituo kimoja, kwa wiki moja wasafiri watu 20, kwa kweli inasikitisha sana. Hatuwezi kukwepa suala la kuendelea kulanguliwa kwa tiketi kama hatuongezi mabehewa lakini pia kama hatuongezi angalau *routes* za treni tuweze kusaidia wananchi ambao treni pia ni tegemeo lao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyeki, suala lingine ni la mafao ya watumishi wa iliyokuwa TRC waliohamia RITES. Mwaka 2007 walipohama kutoka TRC kwenda TRL waliambiwa watalipwa mafao yao leo ni karibu miaka kumi hawajawahi kulipwa. Tunaomba Waziri wakati ana-*wind up* atuambie wale watumishi

waliohamishwa kutoka TRC kwenda TRL mwaka 2007 mpaka leo hawajalipwa haki zao wanalipwa lini haki zao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye barabara za Tabora. Mkoa wa Tabora mpaka tunapoongea umeunganishwa na mkoa mmoja tu, Mkoa wa Singida. Mwanza moja kwa moja mpaka Tabora bado, Mbeya bado, Shinyanya bado, Kigoma bado. Tunaomba sana, kuna barabara hii ya Nyahuwa – Chanya, ni kipande kidogo tu pale, kilometa 85.4 imetengewa fedha kidogo. Ni yale yale ninayoyasema, tukitenga fedha kidogo kidogo tunaleta gharama zaidi. Hebu tuhakikishe kwamba tunaweka fedha za kutosha barabara hii ikamilike ili angalau tuunganishe Dodoma na Tabora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini barabara nyingine ni barabara ya Urambo - Kaliua. Ni barabara muhimu kweli kweli, imetengewa shilingi bilioni tano tu, sasa hizi ni za uchambuzi au za kufanya nini? Barabara ile ni fupi, kilometa 28, tunaomba Mheshimiwa Waziri aweke fedha ya kutosha angalau ikamilike. Leo ukienda pale una mimba changa inatoka, barabara hali ni mbaya sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni ya Kazilambwa - Chagu. Tunashukuru angalau kwa kipande kidogo imekamilika, kutoka Kazilambwa kuja Kaliua tayari, Kazilaumbwa kwenda Chagu kwa maana ya kuunganisha Tabora na Kigoma bado. Fedha iliyowekwa ni kidogo sana labda ni kwa ajili ya uchambuzi, sijui. Naomba barabara hii na yenyewe iweze kutekelezwa ndani ya bajeti hii ili angalau tuunganishe Mkoa wa Tabora na Kigoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni ya kuunganisha kutoka Mpanda – Ugala – Kaliua, Ulyankhulu – Kahama. Ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Kaliua, Mpanda na Kahama. Barabara hii imewekewa fedha kidogo ya uchambuzi, tunaomba kwa bajeti ya mwaka wa kesho ihakikishe inajengwa kwa lami, ni barabara nzuri sana kwa ajili ya uchumi wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la viwanja vya ndege. Kiwanja cha Tabora ni matatizo, leo ni mwaka wa nne tangu kimetengewa fedha ya ukarabati, hakikamiliki kwa nini? Nashangaa Wabunge wanaosema kwamba ndege ni anasa, ndege siyo anasa, tunataka uchumi wa kati, tunataka wawekezaji. Leo unamtoa Mchina kutoka Dar es Salaam aingie kwenye makorongo afike Tabora saa ngapi? Angetaka apande ndege *straight* afike Tabora aangalie eneo la kuwekeza, arudi kwenye shughuli zake. Kwa hiyo, viwanja vya ndege ni uchumi wa nchi hii. Tunaomba Mheshimiwa Waziri akija atuambie kiwanja cha Tabora lini kitakamilika kwa *gauge* kubwa, kipanuliwe kiweze kuwa kiwanja ambacho kinaingiza ndege kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja kile ndege kubwa haziingii. Ndege ndogo, nauli kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora ni shilingi 450, 000 nani mwenye uwezo huo? Gharama ni kubwa, wananchi wengi hawawezi. Kuna Mbunge kasema hapa tukiweza kuwa na viwanja vikubwa, ndege nyingi zikatua, zenye upana mkubwa hata gharama zinapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kidogo kuhusiana *FastJet*, Wabunge wanasema kwamba *FastJet* ni rahisi, *FastJet* ni gharama kuliko maelezo, ni aibu. Kwanza mimi niseme *FastJet* ni wezi, ni wezi kabisa. Leo unachangishwa begi shilingi 200, 000, maji nusu lita shilingi 3,000 hii ni aibu, ni wizi wa hali ya juu. Anakwenda kuchukua maji kwa jumla jumla shilingi 300 kwa nusu lita anakuja kuuza shilingi 3,000 huu ni wizi, hakuna gharama ya unafuu wa aina yoyote. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Magdalena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji na sasa ni Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Flatei Massay wajiandae.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwanza kwa ushindi mkubwa alioupata lakini kwa kazi kubwa anazofanya hadi hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hayo, moja ya eneo kubwa ambalo limekuwa likileta shida sana katika mambo ambayo sisi wana-CCM tumekuwa tukiahidi ni utengaji wa fedha kwa ajili ya sekta ya miundombinu. Kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais amekuwa kwenye ofisi hiyo na tumeshuhudia shilingi trilion zaidi ya nne zimetengwa kwa ajili ya miundombinu. Naomba nimpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba nionyeshe masikitiko yangu kwenye baadhi ya maeneo. Baadhi ya Wabunge wamezungumzia, ninaamini kwamba fedha hizi zingeweza kufanya kazi nzuri sana katika utekelezaji wa Ilani yetu ya CCM, lakini ninavyoona kuna hatari kubwa ya kutapanya fedha hizi kwenye maeneo mengi na mengine ambayo wala hayaendani kwa kiasi kikubwa na *Vision 2020 - 2025* na mengine wala hayawiani na ahadi ambazo tulizitoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la reli. Reli ya kati iko katika Ilani ya CCM, ukisoma Ilani yetu tuliahidi ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge*. Si

kwamba tutaanza, si kwamba tutafanya *feasibility study* au tutafanya kitu kingine chochote. Mimi kama Mwenyekiti wa Wabunge wanaotoka kwenye ukanda unaopitiwa na reli ya kati, tumekuwa na mazungumzo kwa nyakati kadhaa na Mheshimiwa Waziri tukizungumzia suala hili na hata tunapokuja kwenye bajeti yake tulikuwa hatujakutana kuzungumza na kuweka mkakati na Wabunge wenzangu kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekuwa akituhakikishia mipango aliyoweka kwenye bajeti yake itahakikisha reli inajengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba Waziri ametu-betray kwa sababu upembuzi yakinifu na mambo mengine ya awali kabla ya ujenzi kuanza yalikuwa yameshakamilika na tulichokuwa tunategemea kwa hatua ya sasa ni kutafuta fedha na kuanza kujenga. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote ambao tunatumia reli ya kati, ambao wananchi wetu wanaumia kimaisha kutokana na ughali wa bidhaa zote tuliangalie suala hili. Kwa mfano, mabati, nondo, cement zote zinatoka Ukanda wa Pwani, viwanda vyote vya cement viko Ukanda wa Pwani lakini ujenzi unafanyika mpaka Kigoma. Mfuko wa cement Kigoma ni zaidi ya shilingi 20,000/=, mfuko wa cement Dar es Salaam ni shilingi 12,000/=, shilingi 8,000 anayolipa mwananchi wa Kigoma ni adhabu anayopewa kwa sababu tu Mheshimiwa Waziri hajachukuwa hatua za kujenga reli ya kati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hatua hazichakuliwa kwa sababu ukisoma ukurasa, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuchukuwe vitabu vya hotuba ya Waziri, muangalie ukurasa wa 72, ile libara ya 127. Ukisoma ile ibara inasema, mpango uliokuwepo mwanzo ulikuwa ni wa kujenga reli kwanza kwa kujenga sisi wenyewe lakini pia kwa kutumia mpango wa PPP, Serikali imiliki reli, sekta binafsi iendeshe. Waziri anasema mpango huo umekwama na sasa wamefuta mwezi Februari baada ya kukutana na Mawaziri wenzake wa Rwanda na Burundi sijui wanachangia shilingi ngapi katika ujenzi wa reli ya kwenda Mwanza, mbaya zaidi wamefuta na sasa wanasema utajengwa kwa utaratibu mwingine unaitwa Sanifu, Jenga, Endesha, Kabidhi. Utaratibu huu utaanzia kwenye *design* ambayo inaonyesha kwamba itakamilika baada ya miezi 24. Ukihesabu miezi 24 kuanzia sasa *obvious* itakwenda zaidi ya mwaka 2019 na ilani yetu ya CCM ilisema tutajenga reli kabla ya mwaka 2020, tutakuwa tumeiba kura za wananchi kwa kuahidi reli ambayo haitakuwepo. (Mkaofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza naomba niseme maelezo ya Waziri hayajaniridhisha kwenye suala hili. Kwa maana hiyo nilikuwa naomba endapo Waziri katika majumuisho yake hatasema ni nini kitafanyika kuanza kujenga reli wala siyo maneno yaliyoko kwenye ukurasa wa 72 nilioonyesha, mimi binafsi na Wabunge wenzangu nitawashawishi sana wote tunaotumia reli ya kati tusikubaliane na jambo hili hadi tutakapohakikisha reli inajengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siko tayari mimi kuhukumiwa kwa kuiba kura, nimesimama Isaka niwaambia reli inajengwa sikuwaambia kwamba tunaanza kujenga kwa utaratibu tofauti, sikuwaambia kwamba tunaanza upembuzi yakinifu, tulisema tunaanza kujenga reli. Naomba reli ijengwe, bila kufanya hivyo Wabunge wote tunachimbiwa shimo, Mheshimiwa Mwakasaka hutarudi na rafiki zangu wote hamtarudi kwa sababu reli haitajengwa na hata Mheshimiwa Genzabuke hautarudi. Mpango wa ujenzi wa reli hauridhishi na hauendani na ahadi tulizotoa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia suala hilo, naomba nizungumzie suala lingine la barabara na hapa nizungumzie barabara yangu ambayo kimsingi inakidhi vigezo vyote. Mbunge mmoja amesema kwamba tunataka barabara zinazounganisha mikoa na mikoa ndipo twende kwenye barabara zinazounganisha wilaya na wilaya na baadaye kata na kata. Wote ni Watanzania na wote tunalipa kodi, tumekuwa tukizungumza toka mimi nimekuwa Mbunge mwaka 2005 kuunganisha mkoa wa Shinyanga na Geita. Tunasema kuunganisha, kwanza ni kuunganisha mkoa na mkoa lakini baya zaidi maeneo haya yana uchumi mkubwa unaoendesha uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kahama kuna migodi miwili, Mgodini wa Bulyanhulu na Mgodini wa Buzwagi, Geita kuna Mgodini wa Geita. Si mara moja wala mara mbili mimi nimezungumza na wenye migodi ile na bahati mbaya kanuni haziruhusu lakini ningeomba kama utaruhusu tutengue kanuni tumkaribishe Injini Dabalize aliyekuwa Mhandisi wa TANROADS Mkoa wa Shinyanga, tulishazungumza na watu wa Mgodini wa Bulyanhulu, tulishazungumza na watu wa Mgodini wa Geita wanasema wako tayari kushiriki katika ujenzi wa barabara ya Kahama - Geita kwa kiwango cha lami, upembuzi yakinifu umeshakamilika. Kwenye hotuba ya Waziri barabara hiyo wala haijatajwa, wala hajaonyesha nia yoyote ya kuzungumza na hawa wawekezaji ambao wako tayari kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kahama, Msalala, Geita siyo kwamba tu wanahitaji barabara hiyo kwa sababu ya umuhimu wake wa kibiashara lakini wanahitaji pia kwa sababu ya masuala mazima ya afya.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu hii barabara kwa wale ambao hamjaipitia, inapitisha malori yenye kusomba mafuta kupeleka mgodi wa Bulyanhulu, inapitisha malori yanayosomba mchanga wa dhahabu kutoka mgodi wa Bulyanhulu kwenda nje ya nchi na kwa wastani kwa siku zinapita semi trailer zaidi ya 200. TANROADS Shinyanga na Geita wamejaribu kuwa wanakarabati barabara hii lakini haiishi zaidi ya miezi miwili imeshaharibika. Sasa niulize, hivi nini kinakwamisha kuanza ujenzi wa barabara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa Waziri wa Ujenzi miaka ya nyuma, alisema na akahakikisha kwamba barabara hii itaanza kujengwa *immediately* baada ya kuwa ameshaingia madarakani kama Rais.

Ninaamini jambo hili Mheshimiwa Rais halifahamu na naomba Mheshimiwa Rais huko uliko ufahamu kwamba Mheshimiwa Profesa Mbarawa hajaanza kuweka mpango wa kujenga barabara ya Kahama - Geita kama ulivyoahidi ulivyokuwa unahutubia wananchi wa Kahama. Ninaamini amefanya hivyo kinyume cha dhamira yako, kinyume cha matakwa ya Watanzania wanaoishi Kahama na Geita. Naomba Mheshimiwa Waziri tafuta fedha ujenge hii barabara, upembuzi yakinifu umekamilika, wawekezaji wa hiyo migodi wako tayari kuchangia ili mradi Serikali ikubaliane nao namna ya kurekebisha masuala ya kodi, kufanya *tax rebate* kwa miaka ya mbele kutokana na uchangiaji watakaokuwa wamefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimepigwiwa kengele nimalizie kwa kuomba sana kwamba Kanda ya Ziwa tunategemea uwanja wa ndege wa Mwanza uwe wa Kimataifa kwani utafungua ukanda wetu ule ili tuweze kupata watalii. Nimeona kuna fedha zimetengwa lakini ningepomba tu Waziri atuambie hivi ni lini uwanja wa ndege wa Mwanza utakamilika kujengwa kwa kiwango cha kimataifa na utakuwa *International Airport* ili wageni waingilie uwanja wa ndege wa Mwanza, waingie Serengeti watokee KIA au waingilie KIA waje watokee Mwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona bado kuna dakika chache, nimalizie kwa kusema jambo lingine kwamba ili kupunguza msongamano wa malori Dar es Salaam kumekuwepo na pendekezo la kuweka *dry port* nje ya Dar es Salaam hasa eneo la Kibaha. Naomba Wizara hii ilichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili, tujenge bandari kavu eneo la Kibaha ili malori yasiwe yanaingia Dar es Salaam hasa kwa kuangalia misongamano na ajali zinazotokea ambazo kwa kwa kweli hazina maana yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Niombe kwa dakika chache zilizobaki *feasibility study* ya barabara ya kutoka Kahama - Mwanza kupitia Bulige na Solwa ianze. *Feasibility study* ya barabara ya kutoka Kahama - Msalala - Nyang'hwale - Busisi ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais walipokuja Nyang'hwale pale kwenye mkutano Karumwa walihidi barabara ya kutoka Busisi - Sengerema - Nyang'hwale - Karumwa - Msalala - Kahama nayo itajengwa kwa kiwango cha lami. Ni barabara inayounganisha mikoa mitatu na ina sifa zote za kujengwa kwa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ezekiel. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Flatei Massay ajiandae.

MHE. EMMANUEL P. JOHN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninalopenda kuzungumzia ni juu ya reli hii ambayo imepangwa kujengwa lakini napenda kushauri kwamba ujenzi wa reli hii uwe kwa awamu kwa sababu kila anayesimama anazungumzia reli, lakini reli haiwezi kujengwa kwa wakati mmoja, nafikiri tujenge reli kwa awamu kama ni Dar es Salaam - Tabora, kama ni Dar es Salaam – Mwanza. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuna barabara ya kutoka Handeni - Kibirashi - Kijungu - Kibaya - Njoro nimeiona kwenye mpango. Barabara hizi kujengwa ni gharama kubwa kwa Serikali na ukiangalia gharama na jinsi zinavyotakiwa kwa maana kwamba kila mtu anaomba barabara, ningeshauri mambo yafuatayo:-

Naomba Mheshimiwa Waziri safari hii ajenge barabara kutoka Handeni - Kibirashi aishie hapo, mwakani ajenge Kibirashi – Kibaya - Kiteto aishie hapo, mwaka unaofuata ajenge Kibaya - Chemba aishie hapo, mwaka unaofuata ajenge Chemba – Singida, ndiyo njia pekee inayoweza kusaidia barabara hizi kuisha. Hizi barabara unaweka upembuzi, pesa inaingia, *feasibility study* baada ya muda fedha zikikosekana mnaanza upya tena, hizi zote ni gharama kwa Serikali na tunapata hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba kushauri barabara zijengwe kipande kidogo kidogo na kwa awamu. Barabara itakayopata mfadhili wa nje kama ni kilometa 400, 500 akiianza amalize yeye mwenyewe lakini kama ni fedha za ndani tujenge kidogo kidogo ili na maeneo mengine yapate na fedha nyingine zitumike kujenga barabara hizi za vumbi na changarawe katika maeneo mengi ikiwa ni sehemu ya kufungua barabara zetu za vijijini. Hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo la tatu, naomba kushauri kama inawezekana tubadilishe mfumo wa manunuzi itusaidie kwenye mambo haya yafuatayo; hizi fedha zinazotengwa kwenda kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya barabara hebu toeni asilimia 20 tukopesheni vifaa kwa ajili ya barabara. Mkoa mzima wa Manyara kama umetengewa shilingi bilioni tatu au shilingi bilioni nne, asilimia 20 Serikali tukopesheni vifaa, weka *government guarantee* tupate katapila na vifaa vingine vya ujenzi wa barabara, sisi wenyewe tu-fuel halmashauri zetu kutokana na *collection* za ndani, tutumie gharama nafuu

kutengeneza barabara zetu za halmashauri vinginevyo ni gharama kubwa kwa Serikali. Tusipobadilisha hii sheria hatuwezi kupata hiyo *guarantee* na kuweza kununua vifaa vyetu. Najua hii inaokoa fedha nyingi za Serikali lakini kama kuna mikono ya watu wanaotafuna haiwezi kupita. Naomba Wabunge mniunge mkono kwa hili tuweze kuwa na vyombo vyetu vya kutengeneza barabara zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Arusha – Kibaya - NARCO, nimekuwa namwambia Mheshimiwa Spika barabara ya NARCO - Kiteto mbona huizungumzii anasema nimebanwa. Sasa Mheshimiwa Waziri useme leo umembanaje Spika, kwa nini hutengenezi barabara hii? Barabara hii ni ahadi ya Serikali, ni ahadi ya Mheshimiwa Kikwete mwaka 2013 mpaka leo imeshindikana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, jenga barabara ya NARCO – Kongwa na NARCO - Dosidosi tu. Jenga Kongwa kwa mwaka huu mwaka unaofuta jenga Dosidosi mpaka Kibaya kilometa 39, kidogo kidogo mwisho wa siku utafika Oljoro, Arusha. Mimi naomba tujenge barabara kwa awamu ili hii barabara itengenezeke, lengo ni kufungua barabara hii ili mazao yaweze kutoka. Kiteto ndiyo inayolisha Tanzania kwa maana ya Dar es Salaam, ndiyo inayolisha Kanda ya Kati, kwa nini hamfungui barabara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa pili ndani ya barabara ile zimeanguka gari saba kwa siku moja zikipeleka chakula cha msaada. Sasa kwa nini msifungue hii barabara tukaweza kupita, ni zaidi ya kilometa 91 tu. Nadhani jitihada za makusudi hazijachukuliwa kukamilisha ujenzi wa barabara hii. Barabara ya Oljoro - NARCO iliwahi kutengewa shilingi milioni 900 mwaka 2013 za upembuzi mpaka leo hatujui zilienda wapi. Tunaomba hii barabara iangaliwe na itengenezeke, tutaamini kama Thomas tutakapoona wakandarasi wako *site*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya ndege, ndege tunazihitaji, tunahitaji Watanzania watembe lakini kuna jambo nataka kushauri. Viwanja vyote vya ndege ambavyo sasa vina vumbi, vimekwanguliwa hebu suburini kwanza, jengeni hivi viwanja vyote ambavyo mmeanza vya Dar es Salaam, Arusha, KIA, Mwanza ili vimalizike, tujenge kwa awamu na tutakapomaliza tuanze kiwanja kimoja kimoja kwani kushika miradi mingi kunatupotezea mambo mengi. Bajeti ya nchi ni ndogo, fedha zinazokusanywa ni kidogo, tufanye jambo liishe tukirudi hapa tuseme liliisha. Kila siku unazungumzia habari ya kiwanja cha Mwanza, miaka 10 unahangaika na nini kama kimetushinda kiacheni! Jenga Dar es Salaam ukimaliza hamia Arusha, ukimaliza hamia Mwanza, ukimaliza hamia Kigoma, ukimaliza hamia Kagera, maliza kwanza kimoja ujue kwamba kiliisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege. Rwanda ina ndege mpya 14 na ni nchi ndogo, ATC imebaki alama, kwa nini? Mmeonyesha mpango wa kununua

ndege lakini kama tunanunua ndege, niwashauri Wabunge wenzangu tukubaliane tutafute CEO wa kampuni au shirika hilo kutoka nje, siyo Mtanzania watalifuta, litaliwa! Watafunaji ni wengi na kwa sababu hakuna anayeionga mkono Serikali, leo tunalalamika ndege, ndege, tumeuwa wenyewe, tunatafuna wenyewe, kilichoko kinaliwa, mashirika kutoka nje yanatutafuna, tuna-sign wenyewe, mnahangaika na nini? Tu-import wataalam watufanyie kazi tuwalipe ili tuokoe vinavyowezezana. Naomba kushauri hizi ndege zitakazonunuliwa punguzeni watumishi wote wa ATC bakiza wachache, zitembee ndege chache, zifanye kazi, wakope wanunue nyingine ziweze kutembea ndani ya nchi yetu *at least* kwa hesabu tukijua kwamba wamekopa watalipa, wakishindwa magereza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge mmoja amesema barabara za lami wanabandua wanabandika, ndiyo! Kitaalam lami *life span* yake ni miaka 15, ikiisha biashara imekwisha lazima ubandue. Ukiona imedemadema mkandarasi alikuwa mzuri, unashukuru Mungu. Leo hii reli ya kati *life span* yake ilishaisha, ukiona inademadema Mungu ametusaidia. Mimi naomba watu wazungumze kwa *data*, tuone ni jinsi gani tunatakiwa tutoke hapa, hizi barabara nyingi kushindikana kwake ni kwa sababu hata wakandarasi wetu wengi wamekuwa wachakachuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri leo, kama leo Dangote Mtwara simenti inaweza kuwa shilingi 8,000; kwa nini tusijenge barabara za zege? Kama tunaweza kupasua mawe, tukachukua simenti ya gharama nafuu, mwaga zege barabara toka Mtwara kwenda Songea, kwenda Ruvuma pasua huko kote, una haja gani ya kuhangaika? Kama tuna kiwanda Tanga, jenga barabara ya zege kutoka Handeni njoo mpaka Singida watu watambae huko. Una haja gani ya kuagiza lami Ulaya ambayo tunatoa pesa za nje wakati pesa hizo hatuna? *Internal collection* yetu, simenti ni yetu, mawe ni yetu, mwaga zege barabarani wakandarasi tunao ili barabara ziweze kupitika kwa muda ambao sisi tumekusudia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kushukuru na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Papian. Tunaendelea na Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Charles Tizeba ajiandae.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niseme machache. Kwanza namshukuru Mungu kunisaidia kusimama hapa mbele na kuchangia hotuba hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu JPM, maarufu sana mzee wa kutumbua majipu. Mheshimiwa Magufuli

amefanya mambo mengi na lazima tumuunge mkono. Nataka niseme leo hili, mimi namuombea kwa Mungu na namuombea kwa sababu anakutana na changamoto nyingi ambazo kimsingi sisi Wabunge tunazona. Kutumbua majipu siyo kazi rahisi, anapotumbua majipu kuna wengine wanaumia, wengine wanalia lakini wengine tunafurahi hasa sisi ambao tunatoka katika mazingira duni, sasa tunaanza kuona ukweli na uhalisia wa Serikali inavyozidi kuwajibika. Kwa nini nimeshukuru haya. Nimeshukuru haya kwa sababu tunaona sasa walau Serikali inaanza kuchukua hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi na kumshukuru Rais, namwambia aendele. Inawezekana wapo wengine wanabeza hali hii, tulitaka Rais mkali, tulisema yule mpole, sasa amekuja mkali tumuungeni mkono jamani! Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mimi namuombea kwa Mungu na kila siku nitasali kwa ajili hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, katika Wizara hii ya Miundombinu, napenda kuchangia eneo moja kubwa na kwa kweli hili nimetumwa na wananchi wangu. Kwa kuwa tunakuja huku kwa kura, naomba niseme hili kwamba katika swali namba 76 lililoulizwa kwenye Mkutano wa Pili wa mwezi Februari, Mheshimiwa Waziri alinjibu akasema barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom - Singida itajengwa na walau itawekwa kwenye mpango wa upembuzi yakinifu kwenye bajeti hii ya 2016/2017.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimeiona kwenye ukurasa wa 152 na ndiyo maana naona kweli walau Serikali inafanya kazi. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, huu upembuzi yakinifu basi usiendele kwa muda mrefu sana kwamba mwaka huu mpaka mwakani upembuzi bado unaendelea. Barabara hii ni muhimu sana kwani pia imehidiwa na Rais aliyetangulia. Juzi wakati anaomba kura Mheshimiwa Magufuli ameahidi tena barabara hii na wananchi wamempa kura na tuna imani kwamba barabara hii itaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu halafu baadaye iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu Mbulu na Mbulu Vijijini ni wilaya ya siku nyingi sana, nimeshawahi kusema hapa imezaliwa 1905. Tukifanya kitu kinachoitwa *research* hapa tutakuta kuna Wilaya nyingine ambazo zimezaliwa hivi karibuni, kimsingi naamini Mbulu inapaswa kupata haki hii. Mbulu imeweza kuiza Hanang, leo Hanang kuna kaafadhali kidogo, imezaa Babati na imezaa Karatu. Kwa hiyo, naomba niseme leo wilaya hii imekuwa bibi na kwa kuwa imekuwa bibi hebu muoneni huyu bibi basi awe kama kijana aweze kupatiwa hii miundombinu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi huwezi kutoka Mbulu ukafika makao makuu ya mkoa ambayo ni Babati, uko mlima unaitwa Magara, wakati Mkapu amekuja miaka 11 iliyopita kwenye kona za Magara alishaanza kusema mke

wangu mnampeleka wapi kwa sababu zile kona zinaonyesha kama zinarudi. Kuna daraja pale linaitwa daraja la Magara, ukiitwa kikao kama unatokea Mbulu, Mheshimiwa Lukuvi naona unacheka, ina shida ile barabara, nafikiri ulipata kizunguzungu ulipopita pale, kufika Babati kuna daraja kubwa pale. Kwa hiyo, naomba ndugu zangu wapendwa muone na Wizara iangalie daraja hili ili liweze kuwekwa kwenye mpango ujao, daraja litengenezwe na ule mlima urekebishwe ili tuweze kufika makao makuu ya mkoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutoka pale kuna barabara ya kutoka Dareda - Dongobesh, hii barabara imewekwa kwenye Ilani ya CCM na mimi naamini huu ndiyo wakati mzuri wa kusemea sasa. Barabara nyingine ni kutoka Haydom – Katesh. Barabara hizi zinasaidia sana wananchi wetu kutoka katika maeneo yao kwenda kwenye Hospitali ya Haydom. Barabara hii haishii hapa inakwenda mpaka Sibiti inapitia Mkalama na Kidarafa inafungua Mkoa wote wa Manyara kwenda Singida, itahudumia maeneo yote mpaka Simiyu kule. Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge wa maeneo haya niliyoyataja, nafikiri ndiyo wakati wa kueleza Serikali sasa kuifanya barabara hii ipitike na iweze kuleta kitu kinachoitwa maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri sisi tunalima vitunguu saumu kule, mpunga na mazao mengi ambayo kimsingi sisi ndiyo tunaolisha viwanda. Ukieleza habari ya uchumi wa viwanda, Arusha hawawezi kuendelea bila kuwa na barabara iweze kupeleka mazao ghafi au malighafi katika viwanda vya Arusha. Kwa hiyo, barabara hii ikitengamaa na mkajialia kuipangia bajeti katika mwaka wa fedha ujao baada ya huo upembuzi, hakika mambo yatakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Mungu kwamba Waziri kwenye majibu yake ya mwanzo amesema kwamba Benki ya KfW, Benki ya Ujerumani imekubali kufadhili barabara hii. Niombe sana, Mheshimiwa Waziri siku akiwa na kikao na hao wanaoitwa KfW tuite basi na sisi tuweze kushauriana nao tuweze kuweka hoja zetu ili barabara hii itoke Karatu – Mbulu - Sibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu najua muda ni mdogo sana, naomba nishauri mambo machache kwenye mawasiliano. Mawasiliano ni taabu katika maeneo yetu mengi sana hasa kwenye kata za Ari, Tumati, Mangisa, Yaeda Ampa, kule sisi tuna shida hiyo na ninaamini hii inasikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala kubwa sana la kitu kinachoitwa barabara za Wilaya kupandishwa hadhi kufikia kuwa barabara za TANROADS. Manyara tuna miaka minne barabara hazijapanda hadhi. Kwa hiyo, niombe Wizara iangalie Manyara kwa jicho la pekee na kuipandisha ile barabara hadhi maana sasa hivi Mkoa wa Manyara barabara zake zimekuwa scattered, hatuwezi kutoka wilaya kwa wilaya. Ukitoka Kiteto kuja Babati ni tatizo, ukitoka

Babati kwenda Hanang ni shida hasa kutoka Mbulu kwenda pia Babati, niombe haya, naamini Wizara inasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kubwa katika Sheria ya Manunizi, naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika alete mabadiliko ya Sheria hii ya Manunuzi, tufanye mabadiliko ya sheria hii hapa ili walau tuweze kujenga barabara zetu sisi wenyewe.

Halmashauri ziwezeshe kununua vitu vinavyoitwa *caterpillar*, *grader* ili tuweze kujenga barabara zetu wenyewe. Niombe Mheshimiwa Waziri anayehusika, hizi *caterpillar* zinapoingia hapa zisamehewe kodi hasa sisi tukileta maombi kama wa halmashauri ili tuweze kujitengeneza barabara zetu wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimshukuru sana Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri na kuweka barabara zetu hapa. Nachoamini ni kwamba barabara zilizoko kwenye Ilani zitakuwa za kwanza kutengewa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kuchangia haya tu, nasema naunga mkono haja. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Flatei. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Tizeba na Mheshimiwa Marwa Chacha ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Kwa sababu za wazi kabisa nitajikita katika sekta ya ujenzi na mawasiliano na ile sekta nyingine nitaiskip kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kupongeza Baraza zima la Mawaziri, mmeanza vizuri sana na kwa kweli fikisheni salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais kwamba anaendelea kufanya vizuri na ninyi mnaomsaidia tunawaomba kila lililo la kheri. Kwa kutambua kwamba hii ndiyo bajeti yenu ya kwanza basi sisi wenzenu tuna matumaini makubwa sana na ninyi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekipitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri na kwa kweli kwa kiwango kikubwa kimekaa vizuri sana, kime-capture maeneo mengi muhimu na ya msingi. Wasiwasi wangu tu ni kama yote yaliyoandikwa yatatekelezwa kama yalivyoandikwa. Kwa sababu limekuwepo tatizo la muda mrefu tu kwamba mpango huu tunaupitisha ukiwa mzuri sana lakini utekelezaji ukianza mambo mengi yale yaliyoandikwa yanaachwa yanatekelezwa mengine pia ambayo hata hayakuwa yameandikwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natafiti kwa nini hili linatokea, nimejifunza tu kwamba katika ile *Appropriation Act* tunayoipitisha hapa, kipengele kile cha sita (6) kinatoa mwanya kwa Waziri mwenye mamlaka kufanya mabadiliko au kuhamisha pesa, wataalam wa haya mambo wanaita *budget leakage*. Napenda sana niseme haya Mheshimiwa Dkt. Mpango akiwa hapa kwa sababu yeye hasa ndiye mwenye kuweza kuruhusu hizi *leakages* kutokea. Nina hakika *leakages* zisingekuwepo katika bajeti hakuna Mbunge angekuwa analalamika sana hapa kwa sababu mambo tunapitisha wote na kwa hiyo tungekuwa tunatumaini yatatekelezwa kama tulivyoyapitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ifike wakati tukiangalie hicho kipengele cha sita (6), tukipe masharti ili mabadiliko hayo ya fedha kutolewa fungu moja kwenda lingine yafanyike, basi ziwepo sababu za msingi na kama inawezekana angalau Kamati ya Bunge ya Bajeti iwe imeridhia mabadiliko hayo. Kwa namna hii, tutakuwa tumezua sana au tume-ring fence mpango mzima kama tunavyokuwa tumeupitisha hapa ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuzungumzia ni *Road Fund*, lakini naomba nianze na barabara yangu. Mheshimiwa Mbarawa, hii barabara siyo ya kwangu tu, inaanzia mkoa wa Geita inaishia Mwanza. Kwa vigezo vya kiuchumi na kadhalika vyote inakidhi na kwa umuhimu huo ndiyo maana ipo katika Ilani. Mimi nisiseme mengi, nikuombe tu Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha anipe *commitment*, mwaka huu potelea mbali, lakini naomba *commitment* ya mwaka kesho na anipe kwa maandishi mzee siyo kwa mdomo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili eneo la *Road Fund*, katika kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu nilitoa maoni kwamba umefika wakati Sheria ile ya *Road Fund* iangaliwe upya. Yakatolewa majibu hapa kwamba Serikali inaangalia utaratibu wa kuanzisha kitu kinachoitwa *Tanzania Rural Roads Agency* lakini kwenye kitabu humu hakuna. Kama kwenye mpango wa mwaka huu hauzungumzii chochote kuhusu hiyo *agency* kuanzishwa basi tuangalie kwanza tulichonacho tukifanyie marekebisho ili malalamishi ya Wabunge kuhusu barabara za vijiji na za wilaya kutokuwa na *appropriate funding* liishe. Leo tukiendelea hivi kwa matumaini ya *Tanzania Rural Roads Agency* kuanzishwa, sisi tunaokaa katika vijiji huko tutaendelea kuathirika kwa matumaini. Tubadilishe hii sheria, mgawanyo uwe mwingine, itakapanzishwa hiyo *agency* basi ita-fit in katika hili ambalo tutakuwa tumelianzisha na kulifanyia mabadiliko sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge katika majimbo ya vijijini, ninyi mnajua suala la fedha ya barabara zetu kwenye Halmashauri ilivyo kidogo. Tunaendelea kuomba barabara zipandishwe hadhi, zitapandishwa hadhi ngapi? Suala ni kupeleka hela huko huko barabara

zinakotengenezwa na siyo kuomba zipandishwe hadhi. Mmoja alikuwa anasema sijui kuna barabara elfu kumi na tatu na mia ngapi zinasubiri kupandishwa hadhi, halafu mwaka kesho tena elfu ishirini na ngapi, mwisho wake nini? Kwa hiyo, niombe sana suala hili la ama kubadilisha Sheria ya Mfuko wa Barabara au kuanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini basi tuambiwe haya yote yapo katika hatua gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia hicho kitabu, barabara inayoanzia Sengerema – Nyehunge - Nkome imepewa fedha za matengenezo katika *sections* mbalimbali. Nimestaajabu sana kipande cha Sengerema - Nyamazugo hakimo! Tutatengeneza barabara hii kwa *style* gani kwamba kipande hicho kisipopata matengenezo barabara hii haipitiki na kipande hicho ni kibaya kweli, Mheshimiwa Ngeleja anajua, hakina fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye vivuko. Ukurasa wa 211, Mheshimiwa Waziri fungua uone pale, zimetengwa fedha za kununua vivuko viwili, kimoja Kigamboni na kingine Busisi. Hata hivyo, juzi tu mmezindua daraja la Kigamboni, ndani ya kitabu hiki mmetenga fedha shilingi milioni 800 na zaidi za kuanzisha usanifu kwa ajili ya daraja la Busisi, sasa unafanya lipi? Mara unaendelea kununua vivuko pale Kigamboni huku daraja limeanza kufanya kazi. Wale watu wanatoza pale, tusiwa-sabotage kwa kuendelea kununua vivuko huku. Busisi tunataka daraja pale, habari ya kununua *ferry* mpaka ije ikamilike na daraja umeanza kujenga, *why?* Maana *ferry* hii siyo kibiriti kwamba utakwenda dukani utanunua kesho, utaanza tena na yenyewe michoro kuja kufikia kuipata na daraja umeanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka mliangalie upya suala hilo ili zile fedha za Busisi mpeleke Kome. Pale Kome kivuko kile sasa hivi ni kidogo na hakifai, wanapandisha huku na huku, *SUMATRA* hawataki kufanya kazi yao vizuri tu, wangeshakizuia kile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni gharama za ujenzi wa barabara. Naomba tu nitoe ushauri katika hili, Mheshimiwa Waziri, hebu zitazame upya. Pamoja na Sheria ya Manunuzi isiyofaa lakini nadhani zimekuwa *exaggerated* sana. Haiwezekani hapa Tanzania ndiyo tunajenga barabara zenye gharama kubwa kuliko dunia nzima, *why?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, DSTV, Star times, Azam na kadhalika, hawa watu wawekeeni sheria ya kuwabana. Jamani ukinunua *airtime* ni mpaka uongee ndiyo fedha yako itumike, lakini kwa hawa watu wa ving'amuzi ukilipa hata usifungue mwisho wa mwezi fedha imekwisha. Imekwenda wapi na mimi sijafungulia king'amuzi? *Software* za ku-*bill* zipo, kwa nini hawa watu wa ving'amuzi hawawekewi hizo taratibu? Tuombe tu, kwa sababu watu wanalalamikia mengine lakini na hili eneo, *TCRA* mko hapa mnasikiliza, kitu gani

kigumu kuwaambia hawa mtu akiwasha *decoder* ndiyo ianze kusoma matumizi ya fedha yake? Mna mgao huko, sidhani kama mna mgao huko, basi tusaidieni tu wafunge na wao *software* hiyo ambayo mtu akianza kutumia king'amuzi chao ndiyo kweli aanze kuwa *billed* lakini vinginevyo jamani inatumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unalipia DSTV Dodoma hapa mnakaa wiki mbili ukiondoka ukija kurudi hiyo ilishakwisha uanze tena kulipa upya, utakuwa na hela kiasi gani. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Kengele?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Tizeba.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Marwa Chacha na baadaye Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya wananchi wa Serengeti naomba nichukue nafasi hii kuchangia Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nianze na Mawasiliano. Katika Wilaya ya Serengeti tuna maeneo mengi sana ambayo mitandao ya simu hakuna na tunavyoongelea Serengeti, ndiko kwenye mbuga ambayo inaingiza fedha nyingi katika nchi hii, yaani ndiyo mbuga ambayo inasaidia ku-*finance* watumishi wa TANAPA kwenye mbuga nyingine kama Mikumi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mbuga hii kuna maeneo mengi ambayo hayana mawasiliano. Kwa mfano Robo ambako kuna Hoteli ya Robo hakuna mawasiliano kabisa, Bilila iko shida. Mheshimiwa Waziri nikuombe wakati wa ku-*wind up* hebu njoo na jibu la kueleweka kwamba sasa hoteli ambazo ziko ndani ya hifadhi watapata minara kwa ajili ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni barabara. Sasa naomba niseme kuhusu barabara ya Makutano – Nata – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu. Aliyeanza kuwa na maono ya kujenga barabara hii ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wakati huo ikiitwa Makutano – Nata – *Ikoma Gate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye alipokuja Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ndipo wakaanza kuiweka kwenye Ilani ya CCM. Mkapa akaondoka, katika miaka yake kumi hakujenga barabara hii. Akaja Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ikawekwa kwenye Ilani ya CCM, wakati huo Mheshimiwa John Pombe Magufuli akiwa ndiye Waziri wa Wizara ya Ujenzi. Ikapita miaka kumi wala hakuna chochote kilichofanyika. Sasa amekuja ambaye alikuwa Waziri wa wizara hiyo, Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni barabara pekee inayounganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha. Wakati mwingine watu wa Mkoa wa Mara wanalalamika hawanufaiki na utalii, hawanufaiki na fursa zilizopo za utali, ni kwa sababu barabara hii haijafunguka kuunganisha mkoa wa Mara na mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu sana, barabara hii mwaka 2013 ilitengewa fedha kwenye bajeti ili ianze kujengwa na mwezi wa tatu mwaka 2013 ujenzi wa barabara ukaanza, ambapo wakandarasi wa ndani ndio waliokuwa *awarded tender* ya kujenga barabara hii. Na bahati nzuri mmoja wa wakandarasi anaitwa Steven Makigo, rafiki yake sana Magufuli, akapewa kazi ya kujenga barabara hii. Yeye na wenzake *contractors* kumi, tangu mwaka 2013 mwezi wa tatu mpaka leo ninavyoongea wamepewa shilingi bilioni 14 hawajajenga hata mita moja ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia; waliopewa kujenga barabara hii ya lami, Makutano – Nata – Mto wa Mbu ni *contractors* wa ndani wakiongozwa na Kampuni ya Mayanga ambayo Mkurugenzi wake ni huyu Steven Makigo, wako *contractors* kumi. Wakaisajili kwa jina moja wanasema *Mbutu Bridge Contractors*; ni wa kwetu ni wazawa. Tangu 2013 wamepewa shilingi bilioni 14 hata mita moja ya lami hakuna halafu mnasema hapa kazi tu, hapa kazi kwa *issue* gani? Kama mmewapa bilioni 14 wameshindwa wanyang'anyeni, watumbueni majipu wale, anzeni na huyu mkandarasi, yaani hakuna chochote anachofanya lakini munampa mahela tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nimeuliza swali hapa Mheshimiwa Waziri hakulijibu na hiyo wamepewa kujenga 50 kilometers kuanzia Makutano mpaka Sanzate. Sasa hivi ninavyoongea mkataba wa kujenga barabara ile uliisha mwaka 2015 mwezi wa tano, baadaye wakaomba *extension* wakaongezewa mpaka Machi 2016, hivi huu ni mwezi gani? Mpaka leo bado hawajajenga hata mita moja, bado tunaendelea ku-*entertain* watu wa namna hii, si afadhali mtuwekee pale Mchina ajenge ile barabara ikamilike haraka. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae, kuna utaratibu, kuhusu utaratibu Mheshimiwa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Soma kanuni kwanza.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mimi najua Kanuni wewe.

MHE. MARWA R. CHACHA: Soma.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(2) na hususani ile fasili ya (1) ambayo inahusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, na ninaomba nisiisome kwa kuokoa muda wa kiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maudhui ya kusimama kwangu ni kumtaka Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kwa mujibu wa Kanuni hii asitaje jina la Rais vibaya kwa nia ya kujenga hoja. Anaweza akajenga hoja yake kwa namna nyingine yoyote ile akaeleza ubovu uliojitokeza kwenye utekelezaji wa mradi huo lakini hawezi kuhusisha, kwa sababu ni jambo lisiloruhusiwa kwa mujibu wa Kanuni, jina la Rais na hoja yoyote ile anayojaribu kujenga ili kulishawishi Bunge lifanye vinginevyo na kwa muktadha wa Kanuni hii ninaomba utumie mamlaka uliyonayo kumtaka ayaondoe maneno yote yanayohusisha jina la Rais na utekelezaji hafifu wa mradi huo kwa sababu si katika mambo yanayoruhusiwa ndani ya Bunge. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mjifunze utaratibu wa kuvumilia, wengine mmesoma sheria mmesoma sheria wapi? Jengeni hoja kwa kutumia kanuni, hili ni Bunge tunaongozwa na kanuni.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Wewe ukitaka kunitukana mimi najua kutukana zaidi yako, tuheshimiane tu. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumia dakika mbili, naomba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa Chacha, naomba urekebishe kauli hiyo haraka kwa mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 5(3).

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo, kwa kanuni aliyoisoma; inasema hatatumia jina la Rais kwa dhuhaka katika mjadala au kwa maudhui ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani kwani mimi nimewashawishi? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hapo sasa, Hilooo!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naombo niendeleo.

MBUNGE FULANI: Endelea baba!

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi simuungelei Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, namuungelea yule aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu, kama watu wamepewa shilingi bilioni 14 hata mita moja ya lami hawajajenga halafu unaniambia niongee, *I have to talk*. Nimeletwa hapa kama Mbunge wa Jimbo la Serengeti niongee kwa niaba ya wananchi wa Serengeti. Tunachokiongea hapa si mambo ya chama, hata kama ingelikuwa kwako wewe wametumia shilingi bilioni 14 hawajajenga kilometa moja ya lami utasikia vizuri, au huyo malaika akiguswa mnasikiaje? Tulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni yenyewe sasa hivi wanajenga daraja la Mto Kiarano, hata *structural engineer* hawana, *material engineer* hayupo! Hivi hii Wizara ikoje hii?

MBUNGE FULANI: Jalala!

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haina watu wa kwenda kukagua pale waone kwamba kuna *structural engineer, material engineer?* wataalamu wa namna hii hawapo? Sasa unajenga barabara ya kuunganisha mkoa na mkoa *key personnel are not there*, ninyi vipi? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Majipu!

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka Waziri anapokuja atuambie hii barabara itakamilika lini? Kwa mwendo huu ndiyo mtatuambia hapa kazi tu, hakuna cha kazi hapa tunadanganyana. Na kama kweli Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli anaipenda nchi hii, anawapenda wananchi wa Mkoa wa Mara, anawapenda wananchi wa Serengeti, aanze ku-*deal* na huyu mkandarasi. Kama mtu anaweza kutumia shilingi bilioni 14 halafu hakuna chochote alichofanya halafu watu wanaona sawa tu eti usimguse nitakugusa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara tumesema ni mkoa ambao ni *very potential*, una mbuga ya wanyama, una migodi ya Nyamongo, tuna watalii na watalii wengi kama mnavyojua wanatokea uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta – Nairobi, wanapita Sirali, Tarime wanakuja Serengeti. Ninavyoongea kwa sasa barabara zote Serengeti zimekatika na tunaelekea kwenye *high season*, sijui hata hayo mapato tunayoyategemea kutokana na utalii tutayapata wapi kama barabara zimekatika inakuwa ni *chaos* kwa watalii?

Mheshimiwa Maghembe uko hapo unafahamu, watalii wengi wanatokea Nairobi, sasa kama hatutaki kujenga hata barabara ya Tarime - Mugumu watalii watakata tamaa. Kuna Barabara ya Musoma – Sirori Simba, Magange Ring’wani ya kuingia Mugumu, barabara zote hizo hazina hata lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Serengeti ndiyo wilaya pekee ambayo mtoto anaweza akazaliwa akasoma Shule ya Msingi Ring’wani akaenda sekondari ya Ring’wani akamaliza akaenda *form six* pale Nata sekondari, akasoma Chuo cha Kisare hajawahi kuona hata lami. Ni Wilaya pekee ya kitalii ambayo haina hata mita moja ya lami... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ...

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi namuomba Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umemalizika Mheshimiwa Marwa!

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado bwana wewe vipi?

MWENYEKITI: Tayari jamani.

MHE. MARWA R. CHACHA: Alaa.

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke na baadaye Mheshimiwa Kiteto Koshuma ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti. Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kigwangalla naomba ukae tuendelee kwanza, tuendeleo na mchangiaji jamani. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, tunaendelea. *(Makofi)*

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, namshukuru Mungu kwa kunijalia afya kwa mara nyingine kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hasna Mwilima kwa kushinda kesi ya uchaguzi katika Jimbo la Uvinza. Kwa niaba ya wanawake wa mkoa wa Kigoma ninampongeza sana na ninamshukuru Mungu kwa kuweza kutenda maajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana CCM tulikuwa tunaitwa wapinzani, lakini kwa utekelezaji mzuri wa Sera za CCM Mkoa wa Kigoma waliamua kuachana na upinzani wakarudi kukitendea haki Chama cha Mapinduzi. NCCR Mageuzi wakati ule walikuwa wanasema wao ndio Chama Tawala sasa Kigoma Chama cha NCCR Mageuzi kwisha kabisa, chali cha mende, nyang'anyang'a. Tumbaki na ...

MBUNGE FULANI: Changia hoja!

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kuzungumza hayo...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa! Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Genzabuke, endelea.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti niliwahi kuwaambia, kwa mambo makubwa yaliyofanyika Kigoma..

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, anatukana vyama vya watu.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mambo yalifanyika Kigoma wananchi wa Kigoma waliamua wakasema, sasa NCCR basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo za kumpongeza Hasna, naomba nianze kuchangia. Mkoa wa Kigoma tutaendelea kumkumbuka Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kufungua mkoa wa Kigoma akiwa na Waziri wa Ujenzi ambaye ndiye Rais wetu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya matendo makubwa sana, amejenga barabara za lami tunazopita, wana CCM na wapinzani wote ni mashahidi, zilijengwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema barabara zimeharibika. Kumbukeni mvua zikinyesha barabara zinaharibika, magari makubwa yakipita barabara zinaharibika, kwa hiyo ndugu zangu ambao mnasema Mheshimiwa Rais hajafanya chochote; mwaka jana wakati anawasilisha bajeti yake akiwa Waziri wa Ujenzi kwa kumbukumbu zangu nakumbuka kabisa Wabunge wote tuliipitisha bajeti ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kura za ndiyo bila kupinga bajeti ile, wote tunaamini ni mchapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mwaka wa jana tulipokwenda kwenye uchaguzi hatukuhangaika kumnadi Mheshimiwa John Pombe Magufuli, alijiuzwa mwenyewe kwa sababu ya utendaji wake uliotukuka.

Ninaomba kusema, kwa barabara ambazo tayari zimeshafunguka, naomba sasa barabara ya Kigoma – Nyakazi, Kigoma – Kasulu kilometa 50, Nyakanazi – Kibondo, kilometa 50, nashukuru kwa kutengewa pesa. Ninaomba sasa barabara ya kutoka Kibondo – Kasulu mpaka Manyovu nayo iweze kutengewa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumekuwa tukisifika kwa kuwapokea wakimbizi, lakini watu wanaobeba mzigo mkubwa wa kuwapokea na kuwabeba wakimbizi ni watu wa Kigoma. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri ambaye mwaka huu kabla ya bajeti hii ulitoka Kibondo, Kasulu mpaka Kigoma ukaone kile kipande cha kilometa 258 ambacho ndicho kimebaki

hakijatengewa pesa. Kipande kile ndicho kinachotumika kupitisha wakimbizi wanapotokea Burundi kupita Manyovu, kuja Kasulu kwenda mpaka Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipande hicho kitengewe pesa mara moja ili na chenyewe kiweze kukamilika.

Ninaomba kipande cha kutoka Uvinza mpaka daraja la Kikwete kiweze kutengewa pesa ili kikamilike ikiwa ni pamoja na kipande cha Chagu mpaka Kazilambwa na chenyewe kiweze kujengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye reli. Huu ni mwaka wangu wa 11 nikiwa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muhuri ya Muungano wa Tanzani. Mimi kwa kushirikiana na Wabunge wa mkoa wa Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Mara, Rukwa Katavi na Kagera kilio chetu kikubwa kimekuwa ni reli. Tunaomba basi mipango ya ujenzi wa reli inayowekwa iwe ni ahadi inayotekelezeka, isije kuwa ni ahadi isiyotekelezeka. Ipangwe kujenga kwa *standard gauge* ili wananchi waweze kunufaika na matunda ya nchi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa mkoa wa Kigoma, na mikoa yote hiyo niliyoitaja wanapata shida sana kutokana na ukosefu wa usafiri wa uhakika wa reli. Akina mama wanapata shida, wanateseka, wanafunzi wanapokwenda shuleni wanapata shida sana. Tunaiomba Serikali, iweze kutekeleza ahadi ya kujenga reli ili kuwaondolea shida wananchi wanaoishi ukanda huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nimeangalia katika kitabu hiki sijaona kama imetengewa pesa kwaajili ya ukarabati wa bandari ya Kigoma. Ninaomba tunapokwenda kujenga reli na bandari ya Kigoma nayo itengewe pesa kwa ajili ya kutengenezwa. Kwa sababu mizigo ikisafiri kupitia reli ni lazima itafika bandarini, ikifika bandarini itasafirishwa kwenda DRC na Burundi. Kwa hiyo sambamba na kutengeneza reli tunaomba na bandari nayo iweze kuangaliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli ya Liemba ina miaka 100; meli ile ipo kabla ya uhuru, naomba iwekwe meli nyingine ya kusaidia meli ile. Tunapoteza mapato mengi sana kwa sababu meli tuliyonayo imechoka, imezeeka, kwa hiyo tunaomba tupatiwe meli nyingine. Lakini vilevile tunaweza hata tukapewa boti hizi za *fiber boat* kusudi ziweze kusaidia kusafirisha mizigo kutoka Kigoma kupeleka Burundi na DRC. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kiwanja cha ndege cha Kigoma. Ninaomba kiwanja hicho kiweze kutengewa pesa, kipanuliwe ili ndege ziweze kutua na kuruka. Ndege kubwa haziwezi kuruka kwa sababu uwanja ule

maeneo ya kuruka ni kidogo. Naomba kipanuliwe ili ndege kubwa ziweze kuruka. Kwa sababu kiwanja kile kikiweza kutengenezwa kikawa na maeneo ya kuruka na kutua ndege kubwa watu wataweza kufanya biashara muda wote, tofauti na ilivyo sasa ndege ikienda asubuhi ikifika kule mchana hakuna ndege nyingine inayoweza kutua jioni au usiku.

Kwa hiyo, naomba kiwanja kile kiweze kutengenezwa. Lakini vile vile kule kwetu kuna hifadhi ya Gombe watalii wataweza kuja kwa wingi kutoka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma naomba kitengewe hela. *(Makofi)*

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Koshuma na baadaye Mheshimiwa Mdee ajiandae. Kama hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

Kwanza nimshauri tu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, usiige utamaduni wa mtangulizi wako wa kutuletea vitabu vikubwa ambavyo mtu akisoma *between the lines* kuna maneno mengi kuliko uhalisia.

Ushauri wangu kwako tu, inawezekana huu ni mwaka wa kwanza bado una mihemko ya aliyekutangulia, kuanzia mwaka ujao uje na kitabu ambacho kinaeleza tumepanga nini na tutatekeleza nini kwa huo mwaka, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili watu ambao mnaongea sana, sijui Mheshimiwa Magufuli alivyokuwa Waziri kafanya nini, mwaka jana mwenyewe amekiri hapa, katika miaka kumi ya Ilani ya CCM, 2005 – 2015 ameweza kutekeleza asilimia 31 ya kile mlichotakiwa mkifanye. Sasa hivi nyie mtoto akifanya mtihani akipata 31 chini ya 100, hivi huyo amefeli amefaulu?

MBUNGE FULANI: Amefeli!

MHE. HALIMA J. MDEE: Kwa hiyo, tuache kujikomba, unafiki, tusaidie Serikali ndilo jukumu letu kama Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina barabara zangu Jimboni, najua kuna wengine huko wanapata shida na barabara zao zimechokachoka, sisi wa town tuna nafuu kidogo. Lakini nimeahidiwa hapa, miaka mitatu iliyopita na Mheshimiwa Waziri, naomba utoe majibu. Kuna barabara za kupunguza foleni mkoa wa Dar es Salaam; barabara ambazo zinaunganisha Jimbo la Kibamba na Jimbo la Kawe; barabara ya Goba – Tanki Bovu; Goba – Wazo Hill –Tegeta, Gao – Goba – Makongo – Mlimani City.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mkiwa mnanijibu hapa, msiniambie ujenzi umeanza, ninajua hizi ni barabara tatu tofauti zinazounganishwa na kipande kimoja. Sasa nataka leo msiniambie kwa sababu ukiangalia vitabu vya bajeti, na ndio maana nawaambia Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasoma, tukiwa hatusomi Mawaziri hawa wanakuja wanatudanganya. Miaka mitatu mfululizo hizi barabara zimetengewa fedha, kipande cha kuunganisha Jimbo la Kibamba na Kawe, Goba – Mbezi, Goba – Wazo Hill, Goba – Mlimani City, lakini leo ni mwaka wa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kuna hela zimetengwa hapa, zipo, kama ambavyo mwaka wa jana Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa maneno haya haya kama ya kwako zilikuwepo lakini mwaka mmoja baadaye hakuna barabara. Sasa Waziri kesho ukiwa unajibu naomba uniambie kwa uhakika wananchi wa Kawe wasikie, kwa sababu wewe ni mwananchi wangu pia na Mbunge wako nikiwa nazungumza lazima usikilize hizi barabara zinakamilika lini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa juzi, wakati wanajenga hii barabara ya Mwenge – Tegeta – Kibaoni niliishauri Serikali nikaiambia wakati wa mvua kuna kiwango kikubwa cha maji kinachotoka ukanda wa Wazo huku juu Goba na ili barabara iweze kudumu kuna maeneo ambayo lazima mapokeo na matoleo ya maji yawe makubwa ili tuweze kuelekeza maji baharini. Leo barabara imejengwa, mvua ikinyesha ukiwa pale Afrikana, Goigi ni majanga, hii barabara itakatika miaka mitano haitimii, kuna faida gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi namuomba Mheshimiwa waziri akiwa anajibu, kwa sababu niliandika barua kama Mbunge nikiwaomba; mkasema ooh! huyu mjapani ambaye tumepewa msaada ana masharti tutatumia fedha za ndani kujenga mapokeo ya maji makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo naomba niambiwe maana mvua ikinyesha yakitokea maafa Mheshimiwa Jenista Mhagama huyo, halafu mvua ikikauka na yeye anasepa, barabara iko vilevile. Sasa leo nataka mniambie mna mikakati gani, dhahiri, shahiri, kuweza kuokoa ile barabara ya mabilioni ya shilingi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Rais ambaye watu tunaambiwa tusimtajetaje, tutamtaja tu kama alichemsha, msitutishe. Wakati tunapitisha bajeti ya barabara ya Mwenge – Tegeta ya shilingi bilioni 88 tuliambiwa hii barabara itajengwa vipande viwili, kwa matukio mawili. Moja ni Mwenge kwenda Tegeta ya pili ni Mwenge kwenda Morocco, bilioni 88. Sasa leo kuna uchafu unaendelea pale, kutoka Mwenge kwenda Morocco sijui mnatengeneza kichocho, sijui mnatengeneza kitu gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka nijui zile shilingi bilioni 88 ambazo Mheshimiwa John Pombe Magufuli, katika Bunge hili akiwa Waziri alisema kazi yake ni kujenga hizi barabara mbili, ziko wapi? Nataka majibu. Na ule uchafu mnaojisifia sijui fedha za Uhuru, sijui fedha za nini, ile barabara ilikuwa na pesa; kwa hiyo msitafute ujiko kwa kuwa mmezitafuna zile pesa mnatuletea uchafu. Si hadhi ya Dar es Salaam kujengwa ibarabara zile na kama mnatuambia mnajenga kwa muda, hilo pia ni tatizo linguine, *misuse of resources*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuriko. TANROADS walifanya upembuzi yakinifu sijui mnavyoita ninyi, wakatengeneza na michoro kwa ajili ya mfereji mkubwa kuzuia mafuriko ukanda wa Kunduchi, miaka minne imepita. Mwaka juzi alienda Mheshimiwa Pinda, akaambiwa mchoro huo upo, wakati wananchi wanaelea kwenye bahari ya mafuriko, mkasema itajengwa, itatengewa fedha, hakuna kilichofanyika, naomba nipate majibu kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Serikali. Naomba niseme hivi, haya majipu yanayotumbuliwa tutaona huyu bwana mkubwa ana maanisha akitekeleza Azimio la Bunge la mwaka 2008. Bunge lilisema nyumba ambazo zilipewa watu ambao si sahihi zirejeshwe, nyumba ambazo zilikuwa za maeneo ya kimkakati ya watumishi zirejeshwe. Sasa kuna maneno mengi ya mtaani yanasemwa kuhusiana na watu waliopewa nyumba hizi. Sasa tukiona bwana mkubwa anashindwa kufanya utekelezaji yale maneno ya mtaani tutaanza kuyaamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka hatua zichukuliwe, ukaguzi ufanyike kwa kina, CAG aagizwe ili hizi nyumba 7,921 zilizouzwa, tujue mbivu zipi, mbichi zipi, na kama kuna watu walipewa kinyume na utaratibu nyumba zirejeshwe (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana Mheshimiwa Samuel John Sitta akiwa Waziri nilizungumza juu ya nyumba za TAZARA zilizouzwa kinyemela, kinyume na utaratibu. Kuna *audited report* ya mwaka 2014 aliniomba nakala nikampatia; nyumba zaidi ya 500 ziko hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa nyie kawaida yenu mnaendana na mihemko, maana kipindi kile aposhinda Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ari mpya, kasi mpya, yaani kila mtu akija hapa ni swaga tu za ari mpya, maisha

kwa Watanzania yamekuwa *fresh*. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ameenda na ya kwake, Mheshimiwa John Pombe Magufuli ametengeneza asilimia 31 tunakuja huku, hapa kazi, *story* tu, yaani ninyi ni watu wa mapambio. Sasa mimi nitakupatia hii *audited report* ili umuulize na Mheshimiwa Samuel John Sitta aliifanyia nini, ili kesho unipe majibu juu ya hizi nyumba zilizouzwa. Kwa mtindo ule ule wa nyumba zile za Serikali utaratibu wake uko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru, lakini niwaombe Wabunge wenzangu mtanikumbuka miaka mitano ikiisha. Pitieni vitabu vya ujenzi mtanikumbuka maneno yangu. Ninyi kaeni, mnaona majina yenu hapa mnacheka cheka tu, itakula kwenu *big time*. Asanteni sana Mheshimiwa. (Makofi)

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa Mdee, tunaendelea na Mheshimiwa Pudensiana Kikwembe, na baadaye Mheshimiwa Hassan Elias Masala atafuata. Mheshimiwa Pudensiana kama hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Elias Masala. Yupo?

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii.

Kwanza kabisa napenda niwapongeze walioandaa hotuba hii, na sisi kuweza kutupatia nafasi kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na viwanja vya ndege. Ni kweli Serikali imejitahidi kupanga bajeti kwa ajili ya viwanja vya ndege, na tunaomba basi, kwa namna ambavyo mmeweza kupanga, muweze kuvitekeleza, tumekuwa na mipango mingi ambayo hatuiwezi. Napenda kuishukuru Serikali kwa kuweza kutenga kiasi fulani cha fedha kwa kiwanja cha ndege cha Mpanda, mmetenga karibu shilingi milioni 700. Sasa hizi shilingi milioni 700 sijajua zinaenda kutengeneza visima vya mafuta, kuweka taa, ama *extension* ya zile kilometa mbili. Kwa hiyo, nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri, utakapo kuja uweze kunipatia majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niende kwenye suala moja la daraja langu la Kavuu kwenye Jimbo la Kavuu. Sipendi sana kulaumu napenda niseme litekelezwe. Daraja hili la Kavuu si chini ya miaka nane linapangiwa bajeti. Kila bajeti nikisoma ni shilingi bilioni mbili ambazo sijazona, kila mwaka naona shilingi bilioni mbili ambazo sijui zinapelekwa wapi. Ninaomba Waziri uniambie daraja hili linakwisha lini? Na ningependa liishe mwaka huu na ninapenda pesa hizo zitakapotoka uniambie ili nizifuatilie daraja hilo niweze kulisimamia mwenyewe naona Serikali imeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba kabisa Waziri pesa hizo pindi zinapotoka uniambie ili niweze kuzifuatilia na wakandarasi wa nchini wapo wanaoweza kufanya kazi nzuri, tunaweza tukakuelekeza; wengine wako Mbeya na Sumbawanga, wanafanya kazi vizuri sana, hasa katika mkoa wa Katavi ambao wanaufahamu na udongo wa kule wanaufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo napenda pia nijue kiwango cha lami kitajengwa lini kutoka barabara ya Kibaoni mpaka Kilamatumu kupitia Inyonga, kutoka Inyonga mpaka Ilunde. Ninaongea haya akina mama, watoto, wagonjwa wana teseka kweli kweli; hawafiki maeneo ya matibabu kutokana na ubovu wa barabara. Hakuna magari kwa sababu maeneo yale karibu eneo kubwa ni mbuga na ni hatari kwa kina mama kwa kupanda pikipiki na magari kwa sababu tu ya barabara.

Ninaomba barabara hizo zitengenezwe ili wananchi wa maeneo hayo nao waweze kupata ahueni hasa katika suala zima la kufuata matibabu; ukizingatia kwamba mkoa wetu bado ni mpya na hauna hospitali ya Mkoa wala ya Rufaa, ni lazima twende Bugando, Tabora ama Mbeya. Kwa hiyo lazima tupite hizo barabara na tunapita kwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sana ili na sisi tuweze kupata matunda ya nchi yetu kwa sababu tunalipa kodi kama watu wengine wanavyoishi mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye suala la bandari, naongelea gati la Karema. Gati hili limekuwa ni wimbo, meli ya MV Liemba imetoka kuongelewa hapa, katika bajeti iliyopita ukurasa wa 38 wa kitabu kile mmeongelea ile meli sasa inawekwa kwenye makumbusho, lakini leo humu ninasoma mnasema mmekubaliana na Ujerumani kwamba mnakuja kuitengeneza. Kipi ni kipi wananchi wale wachukue, kwamba meli ile ni nzima ama ni mbovu inafanyiwa marekebisho ama inawekwa makumbusho inaletwa meli nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tuweke maisha ya Wananchi wa Ikola, Karema, Kala, Kirando, Kabwe mpaka Kigoma tuyaweke rehani kwa ajili ya meli hii? Kama ni mbovu meli hiyo wekeni, leteni meli mpya wananchi wanataka maendeleo. Ile ni *corridor* ya biashara, tunaenda Congo, Burundi, Zambia, kama mnaona tatizo kwamba meli kutoka Mpanda mpaka Karema inashindikana, tukarabati barabara/tutengeneze barabara ya kwenda Kasesha, Karema mpaka *Kasanga Port* ili tuweze kupata na kufanya biashara na wananchi wa mkoa wa Katavi na Rukwa waweze kuuza mazao yao kwa urahisi, ili waweze kujiongezea kipato na waweze kukuza uchumi wao kama Serikali inavyosema, kutoka kima cha chini kwenda kima cha kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nafikiri unanisikia, unanielewa, umetoka Katavi juzi na umeona hali halisi ya kule naomba utekeleze hilo hasa daraja la Kavuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja barabara ya kutoka Kibaoni – Kasansa – Buze – Kiliamatundu na ya Majimoto – Inyonga mpaka Ilunde, ninaomba majibu ya barabara hizo. Tumekuwa tukisema kila siku, na ninapenda nirudie kama wenzangu waliokwisha tangulia kusema kuwa hatuna sababu ya kusema tunasubiri barabara fulani ipandishwe daraja, tunapadisha daraja kutoka lipi kwenda lipi? Wananchi ni wale wale, wa *level* ile ile, haki yao ni sawa. Wote tuna haki ya kupata barabara bora, maji salama na huduma za msingi kwa wakati mmoja bila kujali huyu ni wa kijijini au wa mjini.

Ninaomba sasa kama Sheria hiyo ya Bodi ya Barabara au ya kwenu, inaleta matatizo tunaomba muilete hapa, ile siyo msahafu wala biblia kwamba haibadiliki. Leteni hapa tutafanyia marekebisho watu waweze kuapata maendeleo sawa kwa sawa na mgawanyo uwe sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja barabara ya kutoka Kawajense – Ugala – Kaliua mpaka Kahama. Barabara hii tumekuwa tukiiiongelea sana sambamba na ujenzi wa daraja la Ugala, tumekuwa tukiiiongelea sana, itamsaidia mwananchi kutoa mazao yake kutoka Mbeya, Sumbawanga, Katavi, Kahama na hatimaye kwenda Musoma na na hata kwenda Darfur wanakopigana kila siku hawana chakula. Tumekuwa tukiongelea umuhimu wa barabara hii; na barabara hii ilikuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2005 na haijatengewa hata hela ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sipendi sana kuilaumu Serikali lakini tufike mahali tuwe *realistic*, kila siku tunaongea hapa haipendezi mtu kila siku ukalisema neon moja, ukisema neno moja kila siku unaumia. Sasa tusianze kupeana *pressure* humu maisha ni mazuri hata kama magumu. Lakini tunahitaji tunapoongea tunajua tunaongea na Serikali ni watu wazima, wenye akili timamu, tusikilize shida za wananchi na zitekelezwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongelea suala la reli ya kati, reli ya kati imeongelewa sana, kwa kweli itakuwa ni aibu kama kila siku tutakuwa tunaongelea suala hili ifike mahali tuchukue maamuzi tufanye kwa vitendo sasa. Matokeo makubwa sasa si pesa, ni pale unapokuwa na tatizo na ukali-solve tatizo mara moja, hayo ndiyo matokeo makubwa na si pesa kutoka sehemu nyingine. Niwaombeni sana tatizo la reli tunalo, sasa ni wakati muafaka wa kulitatua. Tutakapo litatua ndipo tutakapokuwa tumefika kwenye matokeo makubwa sasa.

Kwa hiyo, niwaombe kabisa na Serikali inisikilize na *standard gauge* iwe ni kipaumbele, si suala la kung'oa mataruma ya reli ya Tura mkayapeleka Katumba ama mkapeleka Mpanda hapana, tunataka reli sawa sawa na maendeleo ya sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongelea suala la kurudisha, vinaitwa nini vile?

MBUNGE FULANI: Viberenge.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: *Not viberenge, magenge.* Tulisema yale magenge yatasaidia sana katika kulinda reli zetu na pia katika kuongeza ajira. Sasa mimi sielewi kwa nini yaliondolewa. Ndiyo maana mnaona kila wakati yale mataruma yanang'olewa na wananchi kwenda kuuza chuma chakavu, tunaona kwenye tv magari yanavyobeba. Ni vyema sasa mkafikiria mahali na mkafika wakati wa kurudisha; sambamba na kwenye barabara tuliposema kwamba turudishe *Public Work Department* kwa ajili ya matengenezo ya kila mara ya barabara, kwa ajili ya kuhakikisha barabara zetu zinapitika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala la mitandao au suala la mawasiliano. Ninashukuru sana Serikali yangu kwa kutupatia mitandao hasa vijijini kupitia Halotel, hawa ndugu zetu wa Vietnam, wanafanya vizuri nashukuru. Tatizo langu kubwa na hawa watu ni namna wanavyotoza zile tozo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Haiwezekani wakatoa kwenye mnara shilingi 30,000 kwa mwezi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umeisha.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza. Mimi hilo nalikataa ninaomba kabisa Serikali iangalie namna itakavyo toza hizo tozo tozo hizo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae muda wako umemalizika.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Haiwezekani shilingi 30,000 kwa mwezi huo ni uonevu na ni wizi hata kama wanapewa huduma wanafanya biashara...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae muda wako umemalizika tafadhali. Naomba ukae muda wako umemalizika.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Wapewe hela kufuatana na huduma wanayotoa.

MWENYEKITI: Tunaendelea na mwingine, Mheshimiwa naomba ukae muda wako umemalizika.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Elias Masala baadae Mheshimiwa Kepteni Geogre Mkuchika na ajiandae mwingine Mheshimiwa Zuber Kuchaua.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ambayo imesomwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie maeneo manne yale yanayogusa Jimbo la Nachingwea ambalo natokea, lakini yapo ambayo yatagusia ukanda mzima wa kusini mwa Tanzania na yale yanayohusu Taifa letu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa hotuba nzuri nimeipitia hotuba yake vizuri sana, naomba nimpe hongera kwa kazi nzuri na tunamtakia kila la kheri katika kutimiza ahadi ya yale yote ambayo yamezungumzwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo na pongezi hizo naomba sasa nijielekeze kwenye hoja zinazohusu barabara zetu. Uchumi wetu kwa sehemu kubwa unategemea barabara ambazo lazima ziwe katika kiwango cha lami ili tuweze kuleta maendeleo ambayo tunayakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano lakini pia kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Serikali ya Awamu ya Nne imefanya kazi kubwa, mimi natoka mkoa wa Lindi na wale wanaotoka mkoa wa Mtwara watakubaliana na mimi. Miaka kumi iliyopita tulikuwa tunatumia zaidi ya wiki moja kuifikia Dar es Salaam, lakini sasa hivi tunatumia saa nne au tano; unatumia gari ndogo hata taxi kufika Mtwara na Lindi. Hii yote ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo kwanza ilianza kufanywa wakati wa Mheshimiwa Magufuli akiwa Waziri na sasa hivi

ndiye Rais wetu, kwa hiyo, hatunabudi tumshukuru na tumpongeze kwa kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya Wabunge hapa wanachangia mimi nashangaa na nitashangaa sana, kupitia bajeti hii mtu anasimama hapa anasema tunapewa vihela vidogo hivi wakati kuna maeneo ambako wanatafuta pesa hizo waweze kujengewa miundombinu waweze kupata huduma. (Makofi)

Mimi nafikiri ifike wakati sasa tunapokwenda kutekeleza bajeti hii baadhi ya maeneo ambayo hawaoni umuhimu wa hizi kazi tunazozifanya hebu tuachane nao tuelekeze nguvu zetu sasa kwenye yale maeneo ambayo Watanzania wanahitaji kuona miundombinu bora na wanahitaji kuboresha huduma zao badala ya kukaa na kuja hapa kusema maneno ambayo kimsingi hayana mbele wala nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba sasa nirudi kwenye barabara ambayo kwa muda mrefu imekuwa inazungumzwa. Mheshimiwa Waziri Mbarawa nafikiri unakumbuka ulikuja Nachingwea mwaka jana kama sio mwanzoni mwa mwaka huu, umeona hali ya barabara ya kutoka Nachingwea kwenda Masasi na kutoka Nanganga kwenda Nachingwea. Nashukuru kupitia bajeti hii imeorodheshwa na imesemwa kwa kilometa 91; zipo kazi ambazo wakati unakuja kuhitimisha ningeomba unipe ufafanuzi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba maandalizi yanafanyika kwa ajili ya barabara hii, sasa sijajua maana kama ni *feasibility study* tayari kazi hii imeshakamilika kwa mujibu wa taarifa nilizonazo. Hapa nimeangalia imetengwa shilingi bilioni moja, sijajua hii shilingi bilioni moja ni kwa ajili ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana ndani ya mkoa wetu wa Lindi leo tunajadili shughuli za kiuchumi, kwenda kuweka viwanda kwa ajili ya mihogo, kuona namna gani tunaboresha mazao yetu ya korosho na ufuta lakini bado hatujawa na miundombinu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika na Serikali yetu bado nimuombe Mheshimiwa Waziri atakaposimama awaeleze wananchi wa Jimbo la Nachingwea ambao wanapakana na wananchi wa Jimbo la Ruangwa, Masasi na Liwale; lazima haya maeneo yote tuelezwe katika bajeti hii Serikali imejipanga vipi kuhakikisha tunajenga hizi barabara kwa kiwango cha lami badala ya kufanya *periodical maintenance* ambayo kila wakati tunalazimika kuingia gharama kubwa na barabara hizi bado zinakuwa zinaleta usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni lile ambalo linagusa barabara zinazounganisha mkoa wetu wa Lindi. Tunayo barabara inayotoka Nanganga kwenda Nachingwea. Barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami inaenda kuunganika na mkoa wa Ruvuma kupitia njia ya Kilimarondo. Kwa muda mrefu barabara hii imekuwa ni muhimu sana kiuchumi katika maeneo yetu.

Kwa hiyo, ningepomba kupitia Wizara Mheshimiwa Waziri tuione barabara hii ili tuiweke katika mipango yetu tuweze kujenga kwa kiwango cha lami tuunganishe na mkoa wa Ruvuma ili tuweze kuunganika na mkoa wa Mtwara na tufungue maendeleo ya mikoa ya Lindi Mtwara pamoja na Ruvuma ambayo kwa muda mrefu kidogo tumekuwa nyuma katika shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumza nje ya barabara ni eneo la viwanja vya ndege. Wapo baadhi wamezungumza kutoona umuhimu wa viwanja vya ndege. Mimi naomba niseme viwanja vya ndege ni muhimu, kwa nchi yetu hapa ilipofikia inahitaji kujenga viwanja katika maeneo yake. Hapa katika orodha ya viwanja ambavyo vitakarabatiwa kipo kiwanja cha Lindi kimetajwa hapa, kiwanja hicho kina hali ngumu

sana kwa sisi watu wa Mkowa wa Lindi. Lakini kwa Nachingwea, leo viongozi wote wanatua Nachingwea ndipo wanakwenda katika maeneo mengine. Kwa muda mrefu Mheshimiwa Benjemini Mkapa ametumia uwanja wa Jimbo la Nachingwea kwenda Masasi, na sasa hivi hata Waziri Mkuu anapokwenda Ruangwa lazima atue Nachingwea; na bado mahitaji ya watu wa Nachingwea kuweza kutumia ndege na viwanja vyake bado ni makubwa sana. Kwa hiyo wakati Mheshimiwa Waziri anakiangalia kiwanja cha Lindi bado kiwanja cha Nachingwea tungependa kuona hata ukarabati unafanyika kwa sababu ndicho kiwanja kikubwa ndani ya mkoa wa Lindi ambacho kinaweza kikaruhusu kutua kwa ndege na kuweza kufanya safari kuelekea maeneo ya pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la mawasiliano ya simu. Naomba nipongeze Wizara, ipo kazi kubwa imefanyika lakini pia kupitia kitabu ambacho ninacho hapa Mheshimiwa Waziri naomba nikupongeze. Ninazo Tarafa za Kilimarondo, Ruonda kule kwangu Nachingwea. Tarafa hizi kwa sehemu kubwa zimeshapata mitandao ya simu na hasa mtandao wa *TTCL*, hata katika orodha ya vijiji na Kata ambazo zina maeneo haya mmeorodhesha. Lakini bado mtandao wa *TTCL* kwa wananchi au wakazi wa haya maeneo ambayo nimekutajia Mheshimiwa Waziri bado hawajapata mawasiliano ya uhakika zaidi, wanashindwa kupata huduma za fedha kwa sababu *TTCL* hawajaingia katika biashara hiyo. Kwa hiyo, tungeomba mitandao kama ya Vodacom, Airtel; na orodha hii tayari

tumshaleta Wizarani, tungependa katika awamu hii uweze kutoa msukumo ili tuweze kupeleka mawasiliano wananchi wale waweze kuunganika na watu wengine wa maeneo mengine ya Wilaya ya Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na waliotangulia kusema juu ya suala la uuzaji wa nyumba za Serikali. Mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao siungi mkono utaratibu ambao ulitumika kuuza nyumba za Serikali. Utaratibu ule hauna tija kwa Taifa letu. Leo hii viongozi wanateuliwa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, baadhi ya Mawaziri wanakwenda kukaa katika nyumba za wageni badala ya kwenda kukaa kwenye nyumba za Serikali. Hii ni hasara kwa Taifa letu na haya maamuzi kimsingi bado hatujachelewa, kupitia Serikali ya Awamu ya Tano naomba niishauri Serikali yangu, kwa heshima na taadhima hebu ifanye maamuzi ambayo ni magumu ya kurejesha nyumba zote ambazo ziliuzwa bila utaratibu ili watumishi wetu waweze kuzitumia na tuweze kuona namna bora ya kuweza kuboresha watumishi wetu na watu wa kada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa ufupi ATC. Naomba nipongeze jitihada ambazo Mheshimwia Waziri amezitungumza za ununuzi wa ndege japo ni ndege chache, tumechelewa na kimsingi tunapaswa tukimbie sasa kwa sababu idadi ya ndege tulizonazo ni chache na ni aibu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaunga mkono bajeti hii lakini tunaomba watu wa Wizara wawe *active* waweze kuona wenzetu ambao wameendelea kwenye nchi mbalimbali ukienda kama Dubai - Emirates kule, ukiangalia katika maeneo ya Qatar, wana ndege nyingi, walitumia njia gani? Sisi tunao wasomi ambao wanaweza wakaishauri Serikali yetu na Wizara wakaona namna ya kuweza kuongeza idadi ya ndege kutoka hizi mbili ambazo leo tunazitungumza na tukawa na ndege nyingi ambazo zinaweza zikatua katika maeneo mengi ndani na nje ya nchi yetu. Kwa kufanya hivyo nafikiri tutakuwa tunatafsiri kwa vitendo uchumi ambao tunauzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimisha kwa kuzungumzia reli ya Mtwara, Mbamba Bay pamoja na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umeisha naomba ukae.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika, na baadae Mheshimiwa Zuber ajiandae.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema na kwa sababu katika Bunge hili ni mara yangu ya kwanza kuzungumza. Nataka niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Newala Mjini kwa kunirejesha tena katika jengo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mengi ya kusema kabla sijaenda mbali. Nikiwa ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa Klabu ya Yanga nataka kuipongeza klabu yangu ya Yanga kwa kuchukua ubingwa. Vijana wetu tunawapongeza, mmefanya yale tuliyowatuma mfanye, tunataka mfanye hivyo na nchi za nje pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza maraisi waliotokana na Chama changu kwa kushinda uchaguzi. Tupo awamu ya tano ya maraisi, na faraja niliyonayo kwamba wote waliopokezana vijiti wametoka Chama cha Mapinduzi.

Nampongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kushinda, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, Mabaraza ya Mawaziri yote ya Muungano na lile la Baraza la Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna kazi moja tu ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri chapeni kazi. Ukimsikia mtu anakuambia mnakwenda kasi muulize nilipoapishwa niliambiwa niende speed gani? Kwa hiyo, mimi nataka kupongeza sana. Lakini wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Ndugu zangu uongozi wa nchi ni kupokezana. Kabla ya Magufuli tulikuwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kafanya mambo mengi nchi hii. Mimi nataka niwape mfano ambao ni *my personal experience*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimaliza shule *form four* mwaka 1967 wengi mlikuwa hamjazaliwa. Shule inaitwa *St. Joseph College Chidya*, nikapelekwa kwenda Ilboru, kwa sababu ya matatizo ya mawasiliano ya Mtwara na Arusha mimi nilikuwa natembea wiki nzima kwa gari katika barabara ya vumbi kutoka Newala, Nachingwea, Tunduru, Songea, Njombe, Iringa, Morogoro nikifika Chalinze napanda basi kwenda Arusha; wiki nzima niko njiani, hatukuwa na barabara ya lami. Akaja Mzee Mwinyi akatuanzishia daraja, Mzee Mkapu akatujengea daraja, Jakaya akatuwekea lami. Leo unatoka Newala kwa gari saa nane mchana na saa mbili jioni upo Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amefanya kazi nzuri, ametuwekea sekondari kila kata, amejenga barabara za lami nchi hii, kama ilikuwa ni kushindana ndiye anayeongoza kwa kujenga barabara za lami nyingi kuliko waliomtangulia. Kigoma mlikuwa mnalalamika tupo gizani, ameondoa tatizo la umeme, amewawekea daraja mto Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwanza tunampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ameiongoza nchi salama miaka kumi amemaliza, kijiti amemkabidhi Mheshimiwa John Pombe Magufuli, sasa sikilizeni kazi ya Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya miezi sita tu vijana wanasoma bure toka *fstandard one* mpaka *form four*, ndani ya miezi tu. Ndani ya miezi sita amesema ile Mahakama ya Ufisadi mliyokuwa mnaidai tarehe 01 mwezi Julai inaanza. Miezi sita bado...

(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila kutumia vipaza sauti)

MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mtu mzima naongea mambo ya kuzomea zomea wakati hujaruhusiwa, mtu mzima anaongea. Mimi nilidhani mnawafanyia vijana wenzenu hata mimi size ya mzee wenu? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hajafundwa huyo, hajafundwa.

MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii *disturbance* iliyotokea utaniongozea muda. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo nasema nchi ipo salama. Ametoka Rais wa CCM amemkabidhi kijiti Rais wa CCM, ilani ya uchaguzi iliyokuwa inatekelezwa sasa Mheshimiwa John Pombe Magufuli amechukua pale alipoacha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ndiyo maana nchi ipo shwari, haijashikwa na watu wababaishaji, imeshikwa na watu makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo niseme mengine. Kwanza nataka niombe sana Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli ana nia nzuri na nchi hii, Mawaziri wake wana nia nzuri na nchi hii, hebu tuwape ushirikiano ili Tanzania pawe mahala pazuri pa kuishi. Mbona kila nchi nje huko wanatupongeza? Wanawashangaeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo nataka kwenda kwenye barabara. Nataka niishukuru Serikali yangu ya CCM Serikali sikivu, watu wa Mtwara tumeomba barabara ya lami kutoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi. Hotuba ya Waziri inasema bajeti ya mwaka huu kuanzia tarehe 1 Julai, 2016 barabara inajengwa. Naomba watu wa Tandahimba,

Newala, Masasi, Mtwara, kazi mliyotutuma tumeifanya majibu ya Serikali ndio hayo, barabara itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili barabara ya mkoa. Mheshimiwa Waziri Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mtwara tumeomba barabara ya mkoa kutoka Newala – Nyambe – Ndanda ichukuliwe na mkoa kwa sababu, watu wa Tandahimba na Newala Hospitali yetu ya Rufaa ni Ndanda. Tunaomba ombi hilo lichukuliwe barabara iwe ya mkoa ili iweze kutengenezwa vizuri kwa sababu, Halmashauri zetu uwezo umekuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Newala tulikuwa na uwanja wa ndege ambao umetumika sana wakati wa vita vya Msumbiji. Bahati mbaya nyumba zimejengwa karibu sana mpaka uwanja wa ndege ule umefutwa, lakini Halmashauri imeomba ipewe barua rasmi ya kuufuta uwanja wa ndege wa Newala, hilo jambo halijafanyika, tunaomba lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Wilaya tumetafuta eneo la kuweka uwanja wa ndege, Waziri uliwatuma wataalam kuja kuona, wametuambia shughuli gani tufanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba suala la ujenzi wa uwanja wa ndege Newala, utakapokuwa unajibu, watu waliozoea kuwa na uwanja wa ndege tangu enzi ya mkoloni sasa inapokuwa hatuna uwanja wa ndege tumerudi nyuma. Tutapenda kusikia kauli ya Serikali kuhusu lini mnaanza kujenga uwanja wa ndege wa Newala, lakini kwa hatua za awali tunaomba wale watu wafidiwe eneo lile mlíchukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Newala tuko mpakani na Mto Ruvuma; nimeona hapa hotuba kivuko hapa, kivuko hapa, sisi tuna mawasiliano ya karibu sana na Msumbiji. Kuna daraja kule la Umoja, kuna daraja la Kilambo, lakini Tandahimba na Newala pale tuna vivuko vingi na nafikiri ndio tunaingiliana zaidi na watu wa Msumbiji kwa sababu ya kupakana, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, Wizara iangalie uwezekano wa kutuwekea kivuko katika Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko barabara inaitwa barabara ya Ulinzi, hii ni barabara inatoka Mtwara inaambaa ambaa kandokando ya Mto Ruvuma mpaka Tunduru mpaka mkoa wa Ruvuma. Barabara hii haijatengenezwa miaka yote na Serikali kuu, muda mrefu mmeaicha kuitengeneza, tunapata tabu kusomba korosho kwa sababu ya hali ya barabara na korosho za Mtwara nyingi zinatoka katika bonde la Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nilikuletea barua, bado uko mgeni Wizarani kwamba, vijiji vya bonde la Ruvuma Wilaya yangu ya Newala, hawana mawasiliano ya simu. Walikuwa wanatumia simu za Msumbiji ambazo

dakika moja tu shilingi 1,000, lakini haraka haraka ulituma watu wako, watu wa Halotel wakaja, bonde la Ruvuma leo Halotel ni Halotel kweli kweli. Tatizo lile la watu wa Newala, watu wa Tandahimba kutumia simu za Msumbiji umetuondolea tuko ndani ya Halotel ndani ya nchi yetu. Mheshimiwa Waziri, mimi nataka nikushukuru sana kwa uharaka wako. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mkuchika, nimeshakuongeza robo dakika.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru, lakini kwa kumaliza uwanja wa ndege wa Mtwara uwe uwanja wa Kimataifa wa Mtwara. Ninakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi na baadaye Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Mwakasaka wajandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo na mimi nitoe mchango kwenye Wizara hii. Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi kusimama jioni hii ya leo nikiwawakilisha Wanaliwale, nikifikisha vilio vyao Wanaliwale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda huko naomba nitoe utangulizi kidogo maana nasikia watu wanalalamika reli, reli, reli, reli. Mbona haijengwi, mbona haijengwi. Nataka niwape faida moja, tatizo la Serikali yetu ni kutanguliza mipango kabla ya nia au dhamira. Sisi kwenye uislamu tunaamini kwamba, mtu unatakiwa utangulize nia, kwanza nia iwepo utende jambo; haiwezekani katika karne ya 21 Tanzania unasafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa gari! Unasafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara kwa gari! Bandari Mtwara ipo haiwezekani! Hivi Wajerumani wakati wanajenga ile reli tuliwaona wendawazimu? Wamechukua tu nchi wakajenga reli, sisi leo karne ya 21 tunategemea malori, miaka 54 ya Uhuru hapa hatuendi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakandarasi mnaowapigia kelele, mnawalalamikia wanajenga barabara, maana gari likipiga kona na barabara nayo inapiga kona! Hawa tutaendelea kuwalaumu, hata aje malaika ajenge hiyo barabara kwa malori yale yanayopita kwenye hizo barabara haziwezi kudumu, cha msingi tubadilishe *mindset* zetu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalalamika kwamba, wenzetu sijui Kenya, sijui Rwanda, sijui nani, wameamua kufanya kazi! Wale wameamua kufanya kazi wametoka maofisini wanafanya kazi. Ndugu zangu Watanzania leo hii Mtanzania ukikabidhiwa mradi cha kwanza ni kutafuta kiwanja, cha kwanza ni

kuagiza gari, tunakwenda wapi? Hatuwezi kwenda! Tena basi kama wewe ni Meneja wa Mradi, mradi unakwisha huna nyumba, huna gari, jamii inakucheka, unaonekana wewe fala! Tubadilishe *mindset* zetu, tuondoe ubinafsi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka niwaambie reli hii kama Waziri huyu aliyekuja leo anadhamira ya kujenga mimi nitaiona. Huwezi kupingana na hawa wafanyabiashara wa malori, mtu ana malori 2000, 3000, 5000, hivi unayapeleka wapi? Nani atakubali reli ijengwe? Tuache kubabaishana, turudi kwenye uhalisia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye viwanja vya ndege. Mheshimiwa Waziri mimi sielewi Mzee Kawawa aliacha usia gani kwa Wilaya ya Liwale, ile miradi yake yote iliyokuwepo yote imefutwa. Sijaelewa kabisa, kabisa tatizo ni nini! Pengine Waziri atakapokuja atanieleza pengine kuna maagizo *special* Mzee aliyaacha ile Wilaya muisahau kwa kiwango hicho. Sisi Liwale kulikuwa na kiwanja cha ndege leo hii kuna miti unaweza kuchuma hata matunda ule uwanja wa ndege haupo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye upande wa mawasiliano ya simu. Mawasiliano ya simu kwa Wilaya ya Liwale jamani tunaomba mtotoe kisiwani. Mimi namuomba Mheshimiwa Waziri kwa heshima na taadhima muitoe Liwale kisiwani, Liwale kuna tatizo la barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Rais aliyepo madarakani, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, amekuwa muadilifu. Aliulizwa hapa habari za barabara Nangurukulu – Liwale akasema haiko kwenye mpango wa kujengwa kwa lami na kwa kulikumbuka hilo alipokuwa anaenda kuomba kura Liwale hakuja, alijua kwa sababu wameshakataa kwamba hiyo barabara hatowajengea kwa kiwango cha lami na kweli hakujenga na alipoenda kuomba kura hakuenda Liwale kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshukuru pengine angekuja nisingekuwa hapa sasa hivi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna barabara mimi naomba Mheshimiwa Waziri utotoe Liwale kisiwani. Tuna barabara ya Nachingwea – Liwale, kilometa 120, sijaiona kwenye hotuba yako yote. Kuna barabara ya Nangurukulu – Liwale kilometa 230 sijaiona kwenye mpango wako wote, tunakosa nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa jinsi Liwale ilivyo na rasilimali za kutosha, tunazo mbuga za wanyama, tunayo mazao ya misitu, tunao wakulima wanalima ufuta, wanalima korosho. Tungekuwa na barabara Liwale

tusingekuwa walalamikaji kama tunavyolalamika leo upande wa afya, tunaolalamika upande wa elimu, tungeweza kujenga hospitali zetu. Hizi zahanati tungeweza kuziwezesha kwa mapato ya Halmashauri, leo Liwale imefungwa, Halmashauri inapata wapi mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuomba Waziri atusaidie, atuokoe, atuondoe kisiwani. Nimeona kwenye mpango kuna barabara inatoka Mtwara – Newala – Masasi – Nachingwea inarudi Nanganga; nikupe umbo la hiyo barabara ina “U”, chini ya hiyo “U” ndio kuna Liwale, hebu muone Liwale ilivyotengwa. Yaani umechora “U”, umetoka huku umekwenda ile “U” chini ndio kuna Liwale, wameiacha huko chini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi watu wale wakiona kwamba CCM haiwataki, wana haki au hawana haki? Mmetengeneza “U”, inatoka Mtwara – Newala – Masasi – Nachingwea inarudi Ruangwa – Lindi, Liwale iko chini! Tunawatendea haki watu wale na tunawahitaji? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hapana.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba kwa heshima na taadhima uiondoe Liwale kutoka kisiwani. Tatizo kubwa ninaloliona hapa, tatizo kubwa, Chama cha Mapinduzi tangu Uhuru mnaongoza hii nchi, lakini hii nchi kila siku inazaliwa upya! Kila tunapobadilisha uongozi nchi inazaliwa upya. Kwa maana ya kwamba, kila Rais anayekuja ana vipaumbele vyake, hatuwezi kufika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja Mheshimiwa Mkapa na *Mtwara Corridor*, Mheshimiwa Mkapa kaondoka na *Mtwara Corridor* imekufa. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wameiua.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama ipo tena? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hawaiiaki.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuja huyu na lake, mimi nafikiri, sijui tuseme waongoze milele, sijui kama Rais mmoja abaki tu, sijui tufanyaje? Maana kila tunapobadilisha pamoja kwamba chama ni kile kile, watu ni walewale, lakini mikakati yao ni tofauti kabisa. Utafikiria aliyekuja ni tofauti yaani utafikiri ni chama kingine na nchi ni nyingine...

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tena kwa kujisifia kabisa kwamba Tanzania inazaliwa upya! Inazaliwa upya kwa kuyaacha yale ambayo yalipangwa awali.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MBUNGE FULANI: Kaa chini wewe.

MBUNGE FULANI: Endelea, endelea.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MWENYEKITI: Naomba ukae, Mheshimiwa Zuberi. Mheshimiwa Mhagama, Taarifa.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu mzungumzaji kwamba *Mtwara Corridor* haijafa. Barabara inayojengwa toka mkoa wa Ruvuma na kuunganisha mikoa ya Mtwara yote ndio *project* ya *Mtwara Corridor*. Na katika hotuba ya Waziri imefafanuliwa vizuri miradi hiyo ikiwemo miradi yote ya reli pamoja na miradi yote ya Mchuchuma na Liganga. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi unapokea taarifa hiyo?

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo sijaipokea kwa sababu zifuatazo; amesema *Mtwara Corridor* bado ipo, anaweza kuniambia *Mtwara Corridor* ilikuwa ni mradi wa miaka mingapi? Na uliishia wapi? Na ulitengewa fungu kiasi gani? Na ni kwa miaka mingapi? Na utekelezaji wake leo umefika wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mtwara Corridor* ilikuwa inatuunganisha sisi mpaka Msumbiji, leo hii huyu mchangiaji aliyetoka hapa anaongelea suala la kutuunganisha na Msumbiji. Eti mtu anakuja anasema Mtwara kule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hili ni tatizo la watu kutokujua jiografia ya Tanzania. Watu jiografia ya nchi hii hawaijui na ndio maana leo hii ukiongelea barabara ya Kusini mtu anakwambia daraja la Rufiji! Mimi nataka niwaambie daraja la Rufiji halina tofauti na daraja la Ruvu kwa sababu mtu leo anadai barabara ya Kigoma unamwambia daraja la Ruvu, inaeleweka? (Makofi/Kicheko)

MBUNGE FULANI: Haieleweki.

MHE. ZUBEIR M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio hicho mnachokifanya! Maana tukiwaambia jamani tunahitaji barabara ya Kusini, aah, ninyi Kusini sijui mmetengenezewa daraja la Mkapa. Daraja la Mkapa ndio nini sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuanzia leo hii Kigamboni nako wamepata daraja lile huku Kimbiji, Gezaulole, nani, hawaitaki tena barabara kwa sababu, wanadaraja la Nyerere. Tunakwenda wapi? Mbona tunakuwa wavivu wa kufikiri? Mbona tunakuwa wavivu wa kufikiri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tunahitaji kufanya kazi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kufanya kazi nchi hii, tunahitaji watu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, muda wako umeisha, naomba ukae tafadhali.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Sio ya kwanza hiyo?

MWENYEKITI: Ya pili hiyo Mheshimiwa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Siungi mkono hoja.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, wamekubaliana na Mheshimiwa Mwakasaka watatumia dakika tano tano.

Karibu Mheshimiwa Zedi!

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na moja kwa moja nitaanza na mitandao ya simu katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kubaini kwamba, makampuni ya simu za mikononi yamekuwa *reluctant* kujenga minara katika maeneo ya vijijini kwa sababu maeneo hayo hayana mvuto wa kibiashara Serikali kwa nia njema kabisa iliamua kuanzisha Mfuko Maalum wa Mawasiliano kwa Wote

(UCSAF) ili uweze kutumia fedha za mfuko huo kujenga minara katika maeneo ya vijijini. Lakini mpaka sasa nimeona kuna jitihada fulani zimefanyika, lakini bado maeneo mengi ya vijijini hayana huduma hii muhimu ya simu za mikononi. Mimi mwenyewe kwenye jimbo langu katika huu mfumo wa UCSAF ni kata za Isagehe na Semembela na Kamahalanga ndizo ambazo ujenzi wa minara ya simu umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ombi langu kwa Serikali ni kwamba, kwa kuwa bado makampuni haya ya simu ya Airtel, Vodacom na Tigo tukiyaachia yenyewe yajenge minara kwenye maeneo ya vijijini hayataweza kufanya hivyo kwa sababu, hakuna mvuto wa kibishara. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwenye maeneo mengi ya Vijijini bado mfuko huu wa UCSAF utalazimika kujena minara hata kwa kutoa ruzuku kwa asilimia mia moja. Tukiyaachia haya makampuni ya simu hayataweza kujenga kwa sababu maeneo hayo mengi hayana mvuto wa kibiashara na makampuni haya *motive* yake kubwa ni faida tu hayataweza kwenda huko. Kwa hiyo, tunahitaji mfuko wa UCSAF ujenge minara maeneo ya vijijini, maeneo mengine uwe tayari kujenga hata kwa asilimia mia moja kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu tatizo la upelekaji wa fedha katika Halmashauri zetu za Wilaya hasa Mfuko wa Barabara na fedha za ruzuku (LGCDD), ili kuhudumia barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri za Wilaya. Kuna tatizo kubwa sana la kwamba fedha tunazopanga kwenda kuhudumia barabara zetu za Halmashauri mwisho wa mwaka unapofika ni asilimia ndogo mno ya fedha inakuwa imekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Nzega, mwaka 2014/2015 kwenye Mfuko wa Barabara tulitenga takribani milioni 700 kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Nzega inamtandao wa barabara wa karibu kilometa mia sita na kitu. Kwa hiyo, tulitenga na tulipanga shilingi milioni 700 ziende kuhudumia barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, lakini mpaka mwisho wa mwaka unafika ni shilingi milioni 300 tu zilikuwa zimekwenda na hivyo kufanya barabara nyingi kukosa huduma. Lakini hali ilikuwa mbaya sana kwenye mfuko wa LGCDD ambako tulipanga zipelekwe shilingi milioni 700, lakini mpaka mwaka unaisha ni shilingi milioni 49 tu zilikuwa zimekwenda kwa hiyo...

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja na tulikubaliana na Mheshimiwa Mwakasaka atamalizia dakika tano nyingine, asante sana.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Mwakasaka na badaye atajiandaa Mheshimiwa Lucy Magereli na mwisho atajiandaa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza nimshukuru Mbunge mwenzangu kwa kunipa nafasi hii ya dakika tano, lakini naomba pia nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano pamoja na Uchukuzi kwa hotuba yake nzuri. Mimi naomba niongee suala moja ambalo hili limekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa kampuni hii ya kuhodhi mali ya reli (*RAHCO*) iliundwa kisheria atulettee muswada hapa Bungeni ili tuweze kufanya marekebisho waweze kuungana. Kuna tatizo kubwa sana la hii *RAHCO*. *RAHCO* ni moja ya tatizo katika uendeshaji wa Shirika la Reli Tanzania na ushahidi upo. Hawa *RAHCO* ndiyo waliokuwa wanauza hata mabehewa yale ambayo waliuza kwa chuma chakavu ni hawa *RAHCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, kuna tatizo la *conflict of interest* (mgongano wa maslahi) kati ya *RAHCO* na *TRL* unafanya lile shirika lisiende vizuri. Naomba labda nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba achunguze vizuri ile Godegode imesemwa sana na Gulwe; yale mabilioni yanayopelekwa pale kila siku na *RAHCO* yanakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRL* inashikilia reli, inaangalia reli na kinachopita juu ya reli. *RAHCO* wao wanaangalia reli tu, wafanyakazi karibu asilimia 95. Hata wa *RAHCO* wenyewe wako Shirika la *TRL* kwa hiyo, ili kuondoa huu mgongano wa kimaslahi haya makampuni ni vizuri yaunganishwe. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho kesho kwa kuwa huu pia ni msimamo wa Kamati ya Miundombinu kwamba haya Mashirika yaunganishwe aweze kutupa majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kuna suala la mishahara. Hawa *RAHCO* ndiyo wanapelekwa pesa zote na wanajilipa mishahara mikubwa kweli kweli tofauti na *TRL*, wakati uendeshaji wao ulikuwa mmoja, hata Mheshimiwa Rais ameongelea sana hili suala la mishahara kupita kiasi kwa watu ambao wanafanya kazi zinazofanana. Sasa lile suala la kwamba *RAHCO* wana hodhi kila kitu lina matatizo sana. Kwa hiyo, ningepomba hii kama tulivyokubaliana hata kwenye Kamati ya Miundombinu, ulete muswada wa kuirudisha *RAHCO* pamoja na *TRL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kuna mkataba ule wa mwaka 2014 ambao ulikuwa umesainiwa kati ya Afrika Kusini na Tanzania kuhusu kutengenezwa vichwa kumi na moja vya treni. Vichwa tisa viko tayari, sasa

ningemuomba Mheshimiwa Waziri sijui hili suala la kulipia vile vichwa tisa, tulipata taarifa ni karibu shilingi bilioni 57 zinatakiwa ili waweze kulifanyia hilo, lakini pia maslahi ya Wafanyakazi ambayo yanafika karibu 7.5 au 6 billion; malimbikizo ya madai yao mbalimbali; haya yanaleta migogoro kila mara katika Shirika la Reli Tanzania.

Naomba Mheshimiwa Waziri wakati unajumuisha majumuisho yako na hili uweze kuliona, ni moja ya matatizo ambayo kila mara yanaleta migogoro katika Shirika letu la Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nizungumzie suala katika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga Mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Magereli na baadae Mheshimiwa Msongozi jiandae.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia jioni ya leo katika Wizara ya Ujenzi, Miundombinu na Mawasiliano.

Kabla sijaenda mbele nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuwepo ndani ya jengo hili, ninamshukuru amejibu ndoto zangu, ingawa ninachokiona haki ya Mungu ninastaajabu. Sikuwahi kufikiri kile chombo kinachoitwa Serikali ambacho tuliamini ni *supreme* haya ndiyo kinayoyafanya na kwa kweli ninasikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea nimpongeze na nimtaje kwa heshima kabisa kiongozi wangu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kamanda, kuwa mpinzani kwa miaka zaidi ya 20 siyo mchezo. Kazi uliyoifanya tumeiona, leo Bunge hili lina watu mahiri sana ndani yake ambao wataisaidia sana Serikali hii na si Bunge hili tu hata Bunge lililopita ndiyo kati ya Mabunge ambayo yaliwaamsha Watanzania wakajua ni nini kinachoendelea kwenye nchi yao na hatimae tuko hapa tulipo na tunafanya tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye suala la daraja la Kigamboni. Nilimsikia Mheshimiwa Tizeba akichangia akisema, eti kwenye bajeti ya Wizara wameweka kivuko kingine cha Kigamboni; sawa sawa kabisa na mkiweke kwa sababu lile daraja mmetengeneza *photo point*, watu

wakapige picha, siyo kwamba mmetengeneza liwasaidie chochote watu wa Kigamboni. Tulikuwa tunahangaika na vivuko vibovu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. LUCY S. MAGERELI: ...habari ndiyo hiyo, tulieni sasa mpate habari zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunahangaika na vile vivuko vibovu *despite the fact* kwamba viko tu kilometa sifuri kutoka Ikulu, lakini huduma tuliyokuwa tunapata pale ni mbovu kabisa na leo Serikali ikaja ikatuahidi ya kwamba tunajenga daraja halafu maisha yetu yatabadilika, hayajabadilika chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile daraja linaendelea kuchajiwa, Watanzania wa Kigamboni wanalipia lile daraja, tena eti mnasema mnaweza kumtenganisha Mtanzania wa Kigamboni na baiskeli na pikipiki na bajaji na *hiace* na gari la mzigo. Hivi mmetenganishaje huyo Mtanzania wa Kigamboni? Mmempaa ahueni gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kivuko ndizo hizo hizo zilizohamishiwa kwenye gharama za daraja la Kigamboni, Mmempaa ahueni gani mama ntilie? Mmempaa ahueni gani yule Mtanzania anayesubiri kununua kifaa cha ujenzi akafanyie shughuli zake za ujenzi? Mmempaa ahueni gani ikiwa lile guta tu ambalo linachukua bidhaa Buguruni na Kariakoo kupeleka Kigamboni linachajiwa gharama ile ile sawa na iliyokuwa inachajiwa kwenye gharama za kivuko? Hakuna mabadiliko, hakuna ahueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kivuko mlituambia mnatuchaji kwa sababu kuna gharama za uendeshaji, *well and good*. Mmeleta daraja tunachajiwa gharama zile zile, eti mnasema anayekwenda kwa mguu tu ndiye amepata ahueni, amepata ahueni gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niko Dar es Salaam nimekwenda mjini kwa shughuli za kikazi nikapigiwa simu nyumbani, mtoto anaumwa. Nimekwenda asubuhi nimelipa shilingi 2,000, nikarudi Kigamboni kumchukua mtoto nikalipa shilingi 2,000, nikarudi hospitali nikalipa shilingi 2,000, baada ya mtoto kutibiwa nikarudi nyumbani nikalipa shilingi 2,000, ni lazima nirudi kumaliza lile jukumu langu mjini nikalipa shilingi 2,000, jioni nilirejea nyumbani nimelipa shilingi 2,000, umenisaidia nini? *And that not only me*, Watanzania wengi wa Kigamboni wanapitia katika hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifikirie upya kuhusu habari ya tozo za daraja la Kigamboni; mmetumia pesa za Watanzania, lazima ziwarejee.

Lazima pesa za Watanzaia zilizotumika kujenga daraja la Kigamboni, mmejenga Malagarasi, mmejenga la Mkapa, mbona lile hamku-charge? Hawa Watanzania wa Kigamboni na wao wanalipa road licence kama ninyi. Zile gharama za barabara tunazokatwa kwenye lita moja ya mafuta na wao wanalipa, mbona mnawa-double charge? (Makofi)

MBUNGE FULANI: (Hakutumia kipaza sauti).

MHE. HALIMA J. MDEE: Unasemaje wewe?

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukubaliane ya kwamba mmewaonea sana watu wa Kigamboni, mmewanyanyasa sana, mmewanyonya mno kwa tukio hilo la kuamua kuwa-charge kwenye lile daraja, lakini tukubaliane pia kwamba, hamjawatendea haki hata kidogo. Utabaki kuwa msimamo wangu na Mheshimiwa Waziri naomba ulichukue hilo ulifanyie kazi utupe majibu, hutaki tutakuachia lile daraja sasa upigie picha tuendelee kupita kwenye Kivuko kwa sababu tunachajiwa kitu kile kile, adha yetu ni ile ile, lakini shukrani kutuongezea kingine basi, ili walau tuendelee kuteseka kwa sababu, sioni kama umekuja na mkakati wa maana sana juu ya kusaidia hatma ya Kigamboni na maendeleo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile eneo la Kigamboni ukishaondoka tu pale darajani, pana njia nyembamba kama mrija wa biki. Kwa hiyo, mlipanda pale juu mkafanya kazi ya kisiasa, mka-celebrate mkaondoka, hamkujua watu wakishaondoka mjini basi kule mliko-cross mkasema cross overs sawa, baada ya kuondoka darajani unarudi Kigamboni, barabara pale iko wapi? Usanifu wa kina mnaoita, sijui na upembuzi yakinifu ulishafanyika, wale matajiri wanaomiliki matenki ya mafuta maeneo yale barabara iliyopangwa kutoka daraja la Kigamboni ilipaswa ipite maeneo yale, leo sijui mmekaa meza gani, mmejadiliana namna gani, wananchi wangu wananiambia mmebadilisha msimamo, eti mmeamua kwenda kupitisha daraja tena eneo la makazi ya wananchi ambao hawakufanyiwa tathmini, mnaendelea kutunyonya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie kwenye suala lingine, suala la Serikali kukopa holela; Serikali yetu eti imepata kimbilio la kwenda kukopa fedha China na wao wamejua kabisa ya kwamba wana ajenda yao. Na mkigonga tu hodi wanasema yes, *what do you want men?* Mmepewa dola milioni 500 kwa ajili ya fedha za maendeleo...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. LUCY S. MAGERELI: ...hizo pesa zikapotea. zikayeyuka.

MBUNGE FULANI: Baby!

MBUNGE FULANI: Huyu hajitambui!

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi wanaofanya miradi ya maendeleo hapa Tanzania, wakandarasi wa Kichina, wamedai fedha zao mlishakula! Mkatumia mwanya mwingine kwa sababu mnajua kukopa kiholela mmerudi Uchina, mmeomba dola milioni 500 zingine. Mlikataa msaada wa Marekani wa MCC mkidai ya kwamba eti hamtaki pesa zenye masharti! Mchina alipowapa dola milioni 500 akawaambia sharti la kwanza lazima wakandarasi wa Kichina wote walipwe, ambao wanaidai Tanzania siyo chini ya dola milioni 365. Mmekataa masharti yapi na mmepokea yapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tukubaliane kabisa ya kwamba, kwenye hili lazima muwe waangalifu kwa sababu kwanza mnakopa fedha nyingi sana kutoka source moja! Hatari hata kwa ustawi wa Taifa, hatari hata kwa usalama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la mizigo bandarini. Naomba nieleze kwa masikitiko kabisa ya kwamba bandari ya Dar es Salaam ina hali mbaya na inekoelekea sijui inakwenda kufa sina hakika, kwa sababu kwa mwezi wa kwanza na wa pili tu kwa takwimu, naomba nirejee, mizigo iliyokuwa inapita kwenye bandari ya Dar es Salaam kutoka Zambia imepungua kwa 42%, container kwa 28%, magari kwa 55%. Mizigo iliyokuwa inakwenda Congo imepungua kwa 9%, container 31%, magari 50%. Mizigo iliyokuwa inakwenda Burundi imepungua kwa 27%, mizigo iliyokuwa inakwenda Malawi imepungua kwa 35.6%, container kwa 11%, lakini mizigo ya Uganda imepungua kwa 77%. Nchi nyingine zikiwa na bandari ndiyo zinazojivunia kwa sababu, ni moja ya mlango wa uchumi... Imeisha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Msongozi.

MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Kwanza kabisa nianze kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali imara, yenye Sera nzuri zinazokubalika na zinazotekelezeka. Niipongeze sana Serikali yangu ya Awamu ya Nne iliyokuwa ikiongozwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Katika Wizara hii ya Miundombinu ilikuwa na Jemedari wetu ambaye sasa hivi ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. John Pombe

Magufuli. Serikali hii imefanya kazi nzuri ya kuhakikisha ya kwamba mikoa yetu inaunganishwa na barabara za lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana hata kama huna masikio, lakini hata macho hayaoni? Amesimama mlevi mmoja hapa, mimi namuita mlevi, amesimama mlevi akisema kwamba eti Serikali ya Chama cha Mapinduzi hamna chochote inachokifanya. Barabara hizi zimejengwa kwa 31% kwa miaka 15! Safari ni hatua, kama imefikia 31% ina maana Serikali inafanya kazi na inaendelea kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumtia moyo Waziri wa Miundombinu na Naibu wake pamoja na *delegation* yake yote, endeleeni kuchapa kazi, sisi tuko nyuma yenu, tunaendelea kuwaomba. Kazi mnayofanya ni nzuri na inaendelea kuonekana kwa hiyo, ungeni pale ambapo Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Dkt. Magufuli walipoishia ninyi endelezeni pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba, hakuna mwanamke yeyote yule atakayeweza kumsifia mke mwenzake hata siku moja. Mke mwenzani ni mke mwenzani tu na kama ikitokea ukamsifia mke mwenzako basi wewe kidogo utakuwa *fuse down*. Hali kadhalika, debe tupu ndilo lenye kelele, debe lililokuwa na ujazo mzuri halipigi kelele. Tunawashukuru wananchi wetu wa Tanzania ambao wameona umuhimu wa kukipa Chama cha Mapinduzi kura za kishindo na wakiwa na imani na Serikali yao kwamba ina sera nzuri na zinazotekelezeka na sasa hivi Chama cha Mapinduzi kiko mtamboni kitaendelea kutekeleza majukumu yake. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye nyumba za Serikali. Nyumba za Serikali zilizokuwa zinasemwa hapa ni nyumba ambazo ziliuzwa wakati wa Rais wa Awamu ya Tatu akiwepo Waziri Mkuu ambaye ndiye mwaka jana alikuwa miongoni mwa watu wa mabadiliko. (Makofi)

MHE. KASUKU S. BILAGO: Kuhusu Utaratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Sumaye ndiyo ambaye alikuwa Waziri Mkuu kwa wakati huo na ndiye aliyesimamia. Kama alifanya kazi mbaya basi muone kwamba mabadiliko mliyokuwa mnaenda kuyafanya ni mabadiliko hovyoo...

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu hata ambaye alipewa ridhaa ya kuipeperusha bendera ya CHADEMA kwa mwaka jana naye ni hovyoy, fisadi aliyepindukia na pia ukija na Mheshimiwa Sumaye naye ni tatizo! Ndiye aliyeuza nyumba hizo kwa mipango mibovu! (Makofi)

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba asinipotezee muda, nina mambo ya msingi sana ya kuchangia hapa. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uendele. (Makofi)

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msongozi endelea tumalize.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisiharibiwe muda kwa sababu sindano zinapoingia na wao watulie kama wao walivyokuwa wanaingiza sindano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua lazima Wananchi watambue wazi kwamba, hata katika suala ambalo kwa mfano tunachangia humu ndani, upande mwingine ni kelele maana yake ni madebe matupu na upande mwingine wanatulia kwa sababu wana hoja. Na niseme tu kwa upande wa wenzetu wa Upinzani kwa wanawake wanaoweza kujenga hoja ni watu wawili, Mama Sakaya na Upendo, lakini wengine *the rest* hamna kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja ya msingi sana. Pamoja na kazi nzuri ambayo inaendelea kufanywa na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, naomba niende moja kwa moja kwenye barabara yenye urefu wa kilometa 124, barabara ambayo inatoka Likuyufusi kuelekea Mkenda. Barabara hii ni ya muda mrefu, Waheshimiwa Wabunge waliopita, Mheshimiwa Jenista Mhagama, dada yangu Stella Manyanya na Marehemu

John Komba na wengineo walisimama imara sana kutetea hii barabara ili iweze kujengwa, lakini mpaka sasa hivi barabara hii haijajengwa, ni barabara ambayo inaunganisha Msumbiji na Tanzania. Naomba Waziri mwenye dhamana, barabara hii iweze kuanza kujengwa kwa kipindi hiki cha mwaka 2016/2017, utakapokuja hapa wakati una-*wind up* tafadhali naomba ueleze bayana barabara hii inaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye barabara ya Morogoro - Ruvuma; mimi hizo kelele hazinibabaishi kwa sababu ninyi kwetu, kwa lugha ya kwetu tunawaita *mazindolo*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambayo inaunganisha mkoa wa Morogoro na mkoa wa Ruvuma, na sisi kwetu hatuna aibu Wangoni hawana aibu hata kidogo kwa hiyo, barabara hiyo inatoka Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha mpaka kufika Songea. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umemalizika, naomba ukae.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

MBUNGE FULANI: *Mazindolo!*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(8) na (11), sasa namkaribisha Mheshimiwa Cosato David Chumi aweze kuwasilisha maelezo yake binafsi.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, Miongozo na Utaratibu nitapokea baadae. Naomba tuendelee kwanza.

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa Kanuni hiyo ambayo umeisoma, nitarejea sehemu ya hiyo kanuni inasema; “Bila kuathiri masharti ya Kanuni hii wakati Spika,” *therefore* Mwenyekiti kwa sasa, “anapotaka kuliahirisha Bunge wakati huo unaweza kutumiwa kama fursa

kwa Mbunge yeyote kutaka ufafanuzi utolewe na Waziri juu ya jambo lolote lililo chini ya madaraka ya Waziri huyo.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni hiyo naomba nipatiwe ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kuhusu kuondolewa (*disqualification*) au kuwa *disqualified* kwa wanafunzi 424 wa Chuo Kikuu cha *Saint Joseph* waliokuwa wanasoma programu ya Shahada ya Elimu kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 Chuo Kikuu cha *Saint Joseph* kilianzisha programu ya miaka mitano kwa nia ya kupata wanafunzi watakao somea Shahada ya Elimu kwa masomo ya sayansi yaani *B.Sc Education in Mathematics, Physics, Chemistry, Biology* na *Computer Science*. Lengo la programu hii iliyopewa jina la *Five Years Integrated Bachelor Degree Program* ilikuwa ni katika jitihada za kukabiliana na uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005, Sehemu ya Pili, inaeleza uwepo wa Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*) na inataja majukumu yake makuu kuwa ni pamoja na Tume hii kuwa na mamlaka ya kusimamia na kudhibiti ubora na usimamizi wa uendeshaji wa vyuo vikuu hapa nchini.

Kwa mantiki hiyo na kwa mujibu wa Sheria kabla ya kuanzisha programu yoyote, chuo chochote kitawasilisha kwa *TCU* mtaala wa masuala yote ya kitaaluma kuhusu programu inayokusudia kuanzisha, baada ya kujiridhisha, *TCU* itaithibitisha ama kutoithibitisha programu hiyo. Aidha, baada ya programu au kozi hiyo kupata uthibitisho au *approval* chuo husika kitadahili wanafunzi ambao pia, orodha yao itawasilishwa *TCU* kwa nia ile ile ya kuwathibitisha wale wenye sifa za kitaaluma kulingana na matakwa ya *program* husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la wanafunzi 424, baada ya chuo kuwasilisha *TCU* mpango wake wa kuanzisha programu hiyo ya *Five Years Integrated Bachelor Degree Program*, *TCU* iliithibitisha programu au kozi hiyo na kukijulisha Chuo cha *Saint Joseph* kukubaliwa kwa programu hiyo kwa barua yenye kumbukumbu namba *TCU/M10/11* ya tarehe 9 Julai, 2013.

Aidha, hata baada ya vigezo, sifa za kitaaluma, kubadilishwa mwaka 2015 *TCU* ilikiandikia chuo barua yenye kumbukumbu namba *TCU/A40/66, Vol. 4* ya tarehe 26 Machi, 2015, kuthibitisha tena kuwa wale wote waliokwihadahiliwa kwa vigezo vya mwaka 2013 hawatahusika kwa vigezo vipya vya Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi (*NACTE*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika hali ya kushangaza na kushtukiza, tarehe 8 Aprili 2016, *TCU* iliwaondoa au iliwa-*disqualify* wanafunzi 424

wa chuo hicho kwa madai kuwa walipodahiliwa hawakuwa na sifa za kitaaluma za kujiunga na programu hiyo. Katika taarifa yake TCU imeonesha orodha ya majina ya wanafunzi 157 kuwa ndiyo pekee wenye sifa za kitaaluma za kuendelea na masomo. Kwa hali hiyo wanafunzi 424 wakawa-*disqualified* kwa madi kuwa hawakidhi vigezo vipya vya Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi (NACTE).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika idadi ya jumla ya wanafunzi 622 waliokuwa wamedahiliwa kwenye programu hii baadhi yao wanaozidi wanafunzi 300 walikuwa wanapata mikopo toka Bodi ya Mikopo. Mikopo hiyo ilijumuisha *school fees* kiasi cha shilingi 1,300,000, *meals and accommodation allowance* kiasi cha shilingi 2,400,000 na *special faculty requirement* kiasi cha shilingi 300,000; kwa jumla kiasi cha shilingi 4,000,000 kilikuwa kinatolewa na Bodi ya Mikopo kwa kila mwanafunzi ambayo ni sawa na shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hawa walioondolewa au waliokuwa *disqualified* walipata udahili:-

(i) Programu hii ya *Five Years Integrated Bachelor Degree* ilithibitishwa na TCU.

(ii) Udahili wa wanafunzi hao ulithibitishwa na TCU.

(iii) Miongoni mwao wapo waliopata mikopo, orodha ya majina yao ili wapate mikopo iliwasilishwa kwa Bodi ya Mikopo na TCU.

Je, katika hali hiyo, ni haki kweli kuwaondoa wanafunzi hao kwa makosa, kama yapo, ambayo si makosa yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili; wanafunzi hao walikuwa wanapata mikopo toka Bodi ya Mikopo, lakini baadhi yao wazazi, ndugu na jamaa walikuwa wanawalipia wale ambao hawakupata Bodi ya Mikopo. Je, hasara hii itafidiwa vipi, ikiwemo hasara ya kisaikolojia, fedha na muda? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; kwa sababu hizo hapo juu na kwa kuzingatia kuwa, lengo la kuanzishwa kwa programu hii ilikuwa ni katika jitihada za kukabiliana na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati. Kwa nini Serikali isiruhusu wanafunzi hawa waendeleo na masomo kwa kuwa udahili wao ulizingatia vigezo vilivyo thibitishwa na TCU? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke wazi kuwa sio kusudio langu kupuuza umuhimu wa kuzingatia sifa stahiki za kuingilia katika vyuo vya elimu ya juu au

vyuo vyovyote vile, bali mimi ni muumini wa elimu bora na sio bora elimu. Na nina amini sifa mojawapo ya kuwa na elimu bora ni pamoja na kudahili wanafunzi kwa kufuata na kuzingatia vigezo vya kitaaluma. Na katika suala hili vigezo vya kitaaluma vilizingatiwa kama ilivyothibitishwa na TCU. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, ninaisihi Serikali iwafungulie kifungo hiki wanafunzi hawa kwa kuzingatia kuwa ni karibia mwezi sasa wako nyumbani wakiwa njia panda, hawajui hatma yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Cosato.

Kwa hali hii, Serikali itabidi mlete kauli Bungeni! Mnasemaje Serikali? Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia na tunapokea hilo agizo lako. Tutajiandaa ndani ya Serikali, ili tuje kutoa maelezo ya nini kilichotokea na tuli arifu Bunge lako ni nini ambacho Serikali imeshafanyia kazi katika jambo hilo. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, nitapokea Mwongozo mmoja.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na nikitumia Kanuni ya 64(1),(a),(f),(g), Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuchangia amesema watu vibaya, ametumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha wengine, alitumia maneno kwamba, kuna mlevi mmoja aliyechangia humu ndani, lakini amesema upande wa upinzani ni debe tupu, ni sawasawa na wake wenza, amewataja viongozi wastaafu waliokuwa Mawaziri Wakuu kwa majina yao...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. CECILIA D. PARESSO: ...amewataja Waheshimiwa Lowassa na Sumaye, akawafananisha ni kama viongozi ambao hawaja-perform na kama ni viongozi wa hovyoy. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako! Mheshimiwa Msigwa jana hapa, alitumia tu neno moja kwamba, wanakodoa macho akatakiwa

afute! Lakini huyu leo anatumia haya maneno, wanamshangilia na Kiti chako kiko kimya!

Kwa hiyo, tunaomba haya ambayo ameyasema kuhusu viongozi wakuu wastaafu athibitisha, lakini hayo ambayo anayasema kuwa kuna walevi humu ndani ayafute na athibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimeshapokea Mwongozo mmoja huku, huku hamna Mwongozo? Hakuna!

Kwa hiyo, Mwongozo nimeupokea na mtapatiwa majibu yake wakati muafaka.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja hapa; Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, ni Katibu wa Umoja wa Wabunge wa Reli ya Kati, anawatangazia wajumbe kikao cha Umoja wa Wabunge wa Reli ya Kati mara baada ya kuahirishwa Bunge, saa 2.00 usiku.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kwa siku ya leo na ninaliahirisha Bunge hadi kesho, siku ya Jumatano, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.49 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano,
Tarehe 18 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*